

**MWINGILIANOMATINI KATIKA *TENZI ZA FUMO LIYONGO, MIKIDADI
NA MAYASA, GILGAMESH NA SIMULIZI YA SAMSONI***

Na

Priscah J. Kiprotich

**Tasnifu Iliyowasilishwa katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za
KiAfrika ili Kutimiza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamifu**

Chuo Kikuu cha Moi

2022

IKIRARI

Mtahiniwa

Hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote ili kutimiza mahitaji ya shahada yoyote.

Sahihi:.....

Tarehe

Priscah J Kiprotich
SASS/D.PHIL/KIS/04/15

Wasimamizi

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa ridhaa yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi:.....

Tarehe

Prof. Samuel M. Obuchi

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za KiAfrika

Chuo Kikuu cha Moi

Eldoret

Sahihi:.....

Tarehe

Dkt. Mwanakombo M. Noordin

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za KiAfrika

Chuo Kikuu cha Moi

Eldoret

TABARUKU

Kwa mjukuu wangu mpendwa, Abby Koech. Nakuhimiza ufuate nyayo na kuipeperusha bendera ya elimu juu zaidi.

SHUKRANI

Ee Mungu nguvu yangu, uzipokee shukrani zangu za kipekee kwa ulinzi, uongozi na maarifa yote uliyonipa tangu mwanzo wa safari hii ya kiakademia. Daima nitakutumikia. Shukrani za dhati ziwaendee wazazi wangu wapendwa Joseph na Mary, kwa ulezi, wosia na maombi ya kila wakati. Mwenyezi Mungu awabariki na awape maisha marefu.

Shukrani za kipekee ziwaendee wasimamizi wangu Prof. Samuel Obuchi na Dkt. Noordin Mwanakombo kwa uongozi na uelekezi katika mchakato mzima wa uandishi wa tasnifu hii. Ingingekuwa kwa msaada wenu usio na kifani nisingekuwa na furaha niliyo nayo kuona mwisho wa kazi hii. Ninawashukuru kwa moyo wangu wote na ninawaomba baraka za Mungu ziwaandame milele. Namshukuru mkuu wa Idara, Dkt. Opijah kwa usaidizi wote alionipa. Mola akubariki. Aidha, nawashukuru wahadhiri wangu katika Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika ikiwa ni pamoja na Prof. Ogechi, Prof. Simatei, Prof. Oduori, Dkt. Muge, Dkt. Iballa na wote ambao sijawataja kwa majina. Asante sana. Shukrani zangu vilevile hazitakamilika pasipo kutaja Prof. Mosol Kandagor na Dkt. Magdaline Wafula kwa kunitia moyo nilipoonekana kulegea katika uandishi wa tasnifu hii. Niliona upendo mkuu na ari yenu ya kutaka kuona mwisho wa kazi hii. Mbarikiwe. Sitasahau kumshukuru Dkt. Magugu ambaye alinifaa zaidi katika kutafsiri *Utendi wa Gilgamesh*. Asante sana.

Nani kama mume wangu? Upendo wa dhati, usaidizi wote ulionipa na wema wako unakumbukwa. Si wa kifedha, si wa kijamii, si wa kiroho...Asante sana na Mungu azidi kupanua mipaka yako. Ninawashukuru watoto wangu; Jinaro, Chelly, Chemwe, Kossy, Chumba na Edu kwa subira na ushirikiano mwema katika kipindi cha masomo yangu. Mlionesha ukomavu wa hali ya juu. Asante sana Edu kwa maswali yako yaliyonitia moyo kila wakati nilipokuwa chuoni. Mungu awape maisha marefu. Sehemu hii haitakamilika pasipo kutaja ndugu zangu ambao walinihimiza kila wakati kukamilisha kazi hii. Mbarikiwe kweli. Aidha, nawashukuru sana Meltus (Moi), Maxwell na Bethwell (Kipkorgot) kwa msaada wa kitarakilishi mlionipa kila nilipokuwa na hitaji. Maombi ya Kasisi Kirui (AIC Utawala), Pasta Tanui (AIC Kipsinende), Pasta Priscah (AIC Kaplut) na wote walioniomba na kunitakia mema yanasalia katika kumbukumbu za moyo wangu. Mbarikiwe.

IKISIRI

Tenzi ni tungo za kale katika historia ya ushairi na Fasihi ya Kiswahili. Aidha, tenzi zinahusisha masimulizi marefu yaliyosukwa kihadithi na hushirikisha wahusika wanaojenga mfululizo wa matukio katika hadithi mahususi. Ingawa kazi zilizoteuliwa katika utafiti huu ziliandikwa katika vipindi tofauti kihistoria, mwangwi fulani unabainika. Utafiti huu ulitathmini vipi mwangwi huu unavyobainika katika matini teule. Tasnifu hii inahusu mwingilianomatini katika *Tenzi za Fumo Liyongo* (UFL), *Mikidadi na Mayasa* (UMM), *Gilgamesh* (UG) na *Simulizi ya Samsoni* (SS). Utafiti ulichunguza mwingiliano wa kimatini kwa kuzingatia vipengele vya mbinu ya usimulizi, sifa za wahusika na kikale cha safari ya shujaa katika kazi teule. Malengo mahususi ya utafiti huu yalikuwa ni: kufafanua mwingiliano wa mbinu ya kisimulizi katika UFL, UMM, UG na SS; kuonyesha mwingiliano wa sifa za wahusika wakuu katika matini teule na kuhakiki maingiliano ya kikale cha safari kama kigezo muhimu kinachodhihirika katika tenzi. Nadharia zilizoongoza utafiti huu ni Mwingilianomatini na Vikale. Mwasisi wa nadharia ya Mwingilianomatini ni Julia Kristeva (1980). Mwingilianomatini inasisitiza kuwa kazi za kifasihi huhusiana na kutegemeana ili kuzalisha maana upya. Nadharia hii ilitumika kuonyesha namna masuala ya mbinu ya usimulizi na sifa za wahusika wakuu zinavyoingiliana na kuathiriana katika matini teule. Aidha, nadharia ya Vikale ilitumika kuhakiki maingiliano ya kikale cha safari katika matini teule. Kwa mujibu wa Campbell (2008), nadharia hii inasisitiza kuwa vikale ni ishara bia zilizoenea hivyo kutambulika katika kazi za kisanii. Inaeleza hatua za safari ya shujaa inayopatikana katika jamii mbalimbali. Nadharia hii ilirejelewa katika uchanganuzi wa hatua mbalimbali za motifu ya safari ya shujaa. Mbinu ya uteuzi wa kimaksudi ilitumika ili kuteua sampuli na kupata data iliyokidhi mahitaji ya utafiti huu. Matini zilizoteuliwa ni: *Simulizi ya Samsoni* kutoka katika *Biblia Takatifu*, kitabu cha Waamuzi, sura ya kumi na tatu hadi kumi na sita, *Utendi wa Fumo Liyongo* uliotungwa na Mohammed Kijumwa kama anavyoeleza Mulokozi (1999), *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* kama anavyoelezwa na Bashir (1972). Aidha, *Simulizi ya Gilgamesh* ilirejelewa kutoka *Utendi wa Gilgamesh*, tafsiri ya Kiingereza ya Kovacs (1998). Utafiti huu ni wa maktabani. Kuhusu ukusanyaji wa data, mbinu ya uchambuzi wa yaliyomo ilitumika. Data ilikusanywa kwa kusoma na kuchuja taarifa muhimu katika matini teule zilizoakisi mada ya utafiti huu. Uchanganuzi wa data ulifanywa kulingana na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia za mwingilianomatini na vikale. Uwasilishaji wa matokeo ya data ni wa kimaelezo katika sura mbalimbali. Lengo la kwanza la utafiti huu lilionyesha ulinganifu katika kazi teule zinazodhihirisha mtiririko wa matukio ya kiajabu kwa kutumia mbinu ya usimulizi wa ki-utendi, usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya tatu na vipengele katika matumizi ya lugha. Kwenye lengo la pili, utafiti ulibainisha kuwa licha ya tofauti za kiusuli, hulka na sifa za wahusika wakuu zinaingiliana katika vipengele vya sifa za ukatili, uongozi, ushujaa, majigambo, tanzia na athari ya mwanamke kama mhusika katika maisha ya wahusika wakuu katika UFL, UMM, UG na SS. Katika lengo la tatu, utafiti umebainisha maingiliano katika motifu ya safari ya shujaa inavyodhihirika katika kazi teule. Utafiti umeonyesha kuwa *Biblia Takatifu* inaweza kutumika kama matini rejea katika uchambuzi wa kazi za fasihi. Matokeo ya utafiti huu yanafaa kwa wanafunzi, walimu na wapenzi wa fasihi. Inabainika kuwa UFL, UMM, UG na SS ni tungo za kale, hivyo utafiti huu unatoa fursa ya kuziangalia kazi hizi upya kwa lengo la kukipa kizazi cha Karne ya Ishirini na Moja mafunzo yanayopatikana katika kazi za kijadi.

ABSTRACT

Epics are ancient works in so far as History and Kiswahili oral literature are concerned. Epics are also connected with lengthy narratives knit as a story and depict characters that build the flow of episodes in the specific story. Although the selected works were written in different historical times, a resounding echo is evident. This study sought to evaluate how this echo is portrayed in the selected texts. The research focuses on intertextuality as depicted in the *Epics of Fumo Liyongo, Miqdad and Mayasa, Gilgamesh* and *Samson's Narrative*. The study seeks to examine and compare the issue of intertextuality with emphasis on elements of narration as a style, characterization and the archetypal monomyth of the Hero's journey. The specific objectives of the study were; to examine how narration as a style manifests intertextually in UFL, UMM, UG and SS, to show the intertextuality of the main characters and their character traits and to critique the intertextuality of the archetypal monomyth as an important criterion evident in epics. The research was guided by Intertextuality and Archetypal theories. Intertextuality theory is accredited to Julia Kristeva (1980) as its founder. It emphasizes that literary works have commonalities and are interdependent of each other as they seek to generate new meaning. Intertextuality theory was used to evaluate manifestations of issues relating to narration as a style as well as characters in conjunction with their character traits in the selected texts. Archetypal theory was used to critique intertextuality of the monomyth as depicted in the texts under study. According to Campbell (2008), the theory emphasizes that archetypes are universal images that result from the common imagination of the collective unconscious thus recognized in literary texts. It explains about the stages of a hero's journey common in different societies. The theory was used to elaborate different stages portrayed in the hero's journey in UFL, UMM, UG and SS. Purposive sampling was used to arrive at the sample size and suitable data used in this study. The selected texts were; *Samson's Narrative* from the *Holy Bible*, the book of Judges, chapters thirteen to sixteen, the *epic of Fumo Liyongo* Mohammed Kijumwa's version as indicated in Mulokozi (1999), *the epic of Miqdad and Mayasa* as explained by Bashir (1972). *Gilgamesh's* narration was referenced based on the *epic of Gilgamesh*, Kovac's English translation (1998). The research is library based. In this research, data collection was done by picking specific data for use. Data was collected by reading and picking specific data fragments relevant to the topic of research. Analysis of data was done based on research objectives and the main tenets of intertextuality and archetypal theories. Research findings have been presented in a descriptive form in different chapters. In relation to the first research objective, similarity is evident in the flow of the story through epic narration, first-person narrative technique, third-person narrative style and use of specific language elements. In the second objective, the study established that despite different backgrounds, behaviour of the main characters exhibited intertextuality as seen in elements of character traits such as inhumanness, leadership, heroism, self pride, tragedy and the effect of woman as a character in the lives of the main characters in UFL, UMM, UG and SS. In respect to the third objective, the study established that the monomyth evident in the texts under study is an indication of universal archetypes found in the world. The research indicates the centrality of the *Holy Bible* as a text that can be used as reference to analyze and enrich literary works. The research findings shall be beneficial to students, teachers and all those who love literature. UFL, UMM, UG and SS are ancient works thus giving the opportunity to re-examine the texts under study with a view to impacting the teachings found therein to the 21st century generation.

YALIYOMO

IKIRARI	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI.....	iv
IKISIRI	v
ABSTRACT	vi
YALIYOMO	vii
MAELEZO YA VIFUPISHO NA MANENO MUHIMU	xiii
SURA YA KWANZA	1
MISINGI YA UTAFITI	1
1.0 Utangulizi	1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti.....	1
1.2 Suala la Utafiti	7
1.3 Malengo ya Utafiti.....	8
1.4 Maswali ya Utafiti	8
1.5 Sababu za Kuchagua Mada ya Utafiti	8
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti	10
1.7 Umuhimu wa Utafiti.....	11
1.8 Hitimisho	13
SURA YA PILI	14
MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA	14
2.0 Utangulizi	14
2.1 Mapitio ya Maandishi	14
2.1.1 Maandishi kuhusu Usimulizi katika Tenzi	14
2.1.2 Sifa za Wahusika Wakuu katika Tenzi	19
2.1.2.1 Tanzania kama Sifa Muhimu ya Wahusika Wakuu katika Tenzi	24
2.1.2.2 Maandishi kuhusu Tanzania.....	24
2.1.2.3 Maandishi kuhusu Tanzania-ramsa	27
2.1.3 Maandishi Kuhusu Vikale	29
2.2 Kiunzi cha Nadharia	30
2.2.1 Nadharia ya Mwingilianomatini	30
2.2.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Mwingilianomatini	35
2.2.2 Nadharia ya Vikale	38

2.2.2.1 Mihimili ya Nadharia ya Vikale	45
2.3 Hitimisho	46
SURA YA TATU	47
MBINU ZA UTAFITI	47
3.0 Utangulizi	47
3.1 Mbinu za Utafiti.....	47
3.2 Eneo la Utafiti.....	47
3.3 Sampuli.....	48
3.4 Ukusanyaji wa Data.....	48
3.4.1 Mwingiliano wa Mbinu ya Kisimulizi katika UFL, UMM, UG na SS	49
3.4.2 Sifa za Wahusika Wakuu katika UFL, UMM, UG na SS.....	50
3.4.3 Maingiliano ya Motifu ya Safari katika UFL, UMM, UG na SS	51
3.5 Uchanganuzi wa Data	52
3.5.1 Mihimili ya Nadharia ya Mwingilianomatini	53
3.5.2 Mihimili ya Nadharia ya Vikale	54
3.6 Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti	55
3.7 Hitimisho	55
SURA YA NNE	56
MWINGILIANO WA KISIMULIZI KATIKA TENZI ZA FUMO LIYONGO GILGAMESH, MIKIDADI NA MAYASA PAMOJA NA SIMULIZI YA SAMSONI	56
4.0 Utangulizi	56
4.1 Dhana ya Usimulizi	56
4.1.1 Utenzi wa Fumo Liyongo.....	59
4.1.2 Utendi wa Mikidadi na Mayasa (UMM)	61
4.1.3 Utendi wa Gilgamesh (UG)	63
4.1.4 Simulizi ya Samsoni (SS)	66
4.2 Mbinu za Kisimulizi katika UFL, UG, UMM na SS	69
4.2.1 Usimulizi wa ki-Utendi katika UFL	70
4.2.2 Usimulizi wa ki-Utendi katika UMM.....	71
4.2.3 Usimulizi wa Nafsi ya Kwanza katika UG	75
4.2.4 Usimulizi wa Nafsi ya Kwanza katika SS	78
4.2.5 Usimulizi wa Nafsi ya Tatu katika UFL.....	79
4.2.6 Usimulizi wa Nafsi ya Tatu katika UMM	81

4.2.7 Usimulizi wa Nafsi ya Tatu katika UG.....	87
4.2.8 Usimulizi wa Nafsi ya Tatu katika SS	88
4.3 Usimulizi Maizi katika SS	93
4.4 Mwingiliano wa Kimuundo katika UFL, UG, UMM na SS	96
4.4.1 Mwingiliano katika Kitangulizi	96
4.4.2 Mwingiliano katika Dhamira	99
4.4.3 Mwingiliano katika Kimalizio	104
4.5 Mwingiliano katika Matumizi ya Lugha	108
4.5.1 Matumizi ya Tashbihi katika UFL.....	108
4.5.2 Matumizi ya Tashbihi katika UMM	110
4.5.3 Matumizi ya Tashbihi katika UG.....	111
4.5.3.1 Matumizi ya Sitiari katika UG.....	111
4.5.3.2 Matumizi ya Sitiari katika UMM	113
4.5.3.3 Matumizi ya Sitiari katika SS	114
4.5.3.4 Maswali ya balagha Katika UFL.....	115
4.5.3.5 Maswali ya balagha Katika UG.....	117
4.5.3.6 Maswali ya balagha Katika UMM.....	118
4.5.3.7 Maswali ya balagha Katika SS	120
4.5.4 Taswira.....	121
4.5.4.1 Taswira katika SS	121
4.5.4.2 Taswira katika UFL.....	122
4.5.4.3 Taswira katika UMM.....	124
4.5.4.4 Taswira katika UG.....	125
4.5.5 Matumizi ya barua katika UFL na UMM	126
4.6 Ulingano na Tofauti katika Mwingiliano wa Kisimulizi Katika UFL, UMM, UG na SS.....	128
4.7 Hitimisho	130
SURA YA TANO	131
MWINGILIANO WA SIFA ZA WAHUSIKA WAKUU KATIKA <i>TENZI ZA FUMO LIYONGO, MIKIDADI NA MAYASA, GILGAMESH NA SIMULIZI YA SAMSONI</i>	131
5.0 Utangulizi	131
5.1 Sifa za Wahusika Wakuu katika UFL, UMM, UG na SS	131
5.1.1 Sifa ya Ukatili katika UFL.....	132

5.1.2 Sifa ya Ukatili katika UMM	133
5.1.3 Sifa ya Ukatili katika UG.....	137
5.1.4 Sifa ya Ukatili katika SS.....	141
5.2 Sifa ya Uongozi katika UFL, UG na SS	144
5.2.1 Sifa ya Uongozi katika UFL	145
5.2.2 Sifa ya Uongozi katika UG	146
5.2.3 Sifa ya Uongozi katika SS	147
5.3 Sifa ya Ushujaa katika UFL, UMM, UG na SS.....	149
5.3.1 Sifa ya Ushujaa katika UFL.....	150
5.3.2 Sifa ya Ushujaa katika UMM	152
5.3.3 Sifa ya Ushujaa katika UG.....	154
5.3.4 Sifa ya Ushujaa katika SS.....	157
5.4 Sifa ya Majigambo katika UMM, UG na SS.....	158
5.4.1 Sifa ya Majigambo katika UMM	159
5.4.2 Sifa ya Majigambo katika UG	161
5.4.3 Sifa ya Majigambo katika SS.....	162
5.5 Sifa za Mwanamke kama Mhusika katika UFL, UMM, UG na SS	163
5.5.1 Hekima ya Mwanamke katika UFL.....	163
5.5.2 Hekima ya Mwanamke katika UMM	166
5.5.3 Hekima ya Mwanamke katika UG.....	171
5.5.4 Unafiki wa Mwanamke katika SS	177
5.6 Sifa ya Tanzania katika UFL, UMM, UG na SS.....	180
5.6.1 Tanzania katika UFL	180
5.6.2 Tanzania katika UG.....	191
5.6.3 Tanzania katika SS	198
5.6.4 Tanzania- ramsa katika UMM.....	205
5.7 Mfanano na Tofauti baina ya Wahusika Wakuu katika UFL, UMM, UG na SS	211
5.8 Hitimisho	213
SURA YA SITA	215
MAINGILIANO YA MOTIFU YA SAFARI KATIKA TENZI ZA FUMO LIYONGO, MIKIDADI NA MAYASA, GILGAMESH NA SIMULIZI YA SAMSONI	215
6.0 Utangulizi	215
6.1 Motifu ya Safari kwa Ujumla	215

6.1.1 Hatua za Mwanzo wa Safari	216
6.1.2 Hatua ya Kivuko cha Kizingiti	217
6.1.3 Hatua ya Tatizo	218
6.1.4 Hatua ya Ufufuo.....	219
6.2 Hatua ya Mwanzo wa Safari katika UFL, UMM, UG na SS	219
6.2.1 Hatua ya Mwanzo wa Safari katika UFL.....	221
6.2.2 Hatua ya Mwanzo wa Safari katika UMM	224
6.2.3 Hatua ya Mwanzo wa Safari katika UG	227
6.2.4 Hatua ya Mwanzo wa Safari katika SS.....	230
6.3 Hatua ya Kivuko cha Kizingiti	232
6.3.1 Kivuko cha Kizingiti katika UFL	232
6.3.2 Kivuko cha Kizingiti katika UMM.....	236
6.3.3 Kivuko cha Kizingiti katika UG	239
6.3.4 Kivuko cha Kizingiti katika SS	242
6.4 Hatua ya Tatizo.....	245
6.4.1 Hatua ya Tatizo katika UFL.....	245
6.4.2 Hatua ya Tatizo katika UMM	248
6.4.3 Hatua ya Tatizo katika UG	250
6.4.4 Hatua ya Tatizo katika SS.....	253
6.5 Hatua ya Ufufuo	256
6.5.1 Hatua ya Ufufuo katika UFL	257
6.5.2 Hatua ya Ufufuo katika UMM.....	258
6.5.3 Hatua ya Ufufuo katika UG	262
6.5.4 Hatua ya Ufufuo katika SS	264
6.5.5 Ulingano na Tofauti ya Motifu ya Safari katika UFL, UMM, UG na SS.....	266
6.6 Hitimisho	268
SURA YA SABA	270
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI.....	270
7.0 Utangulizi	270
7.1 Muhtasari wa Tasnifu	270
7.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti.....	272
7.2.1 Mwingiliano wa Kisimulizi katika <i>Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh</i> na <i>Simulizi ya Samsoni</i>	272

7.2.2 Mwingiliano wa Wahusika Wakuu katika <i>Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh na Simulizi ya Samsoni</i>	275
7.2.3 Mwingiliano wa Kikale cha Safari katika <i>Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh na Simulizi ya Samsoni</i>	278
7.3 Hitimisho	279
7.4 Mapendekezo ya Utafiti.....	280
MAREJELEO	282
Vitabu.....	282
Tasnifu	285
Majarida	286
Mtandao	286
VIAMBATISHO	287
Kiambatisho 1A: Usimulizi katika <i>Utendi wa Fumo Liyongo (UFL)</i>	287
Kiambatisho 1B: Usimulizi katika <i>Utendi wa Mikidadi na Mayasa (UMM)</i>	293
Kiambatisho 1C: Usimulizi katika <i>Utendi wa Gilgamesh (UG)</i>	301
Kiambatisho 1D: Usimulizi Katika <i>Simulizi ya Samsoni (SS)</i>	310

MAELEZO YA VIFUPISHO NA MANENO MUHIMU

K12	Karne ya Kumi na Mbili
K19	Karne ya Kumi na Tisa
Khj	Kama hapo juu
KK	Kabla ya Kuzaliwa Kristo
MA	Matini Asilia
MT	Matini Tafsiriwa
Mf	Mfano
Ub.	Ubeti
SS	<i>Simulizi ya Samsoni</i>
UFL	<i>Utendi wa Fumo Liyongo</i>
UG	<i>Utendi wa Gilgamesh</i>
UMM	<i>Utendi wa Mikidadi na Mayasa</i>
Biblia	Kitabu chenye maandiko matakatifu kinachotumiwa na waumini Wakristo
Utendi	Mtungo wa kishairi ulio na beti nyingi ambao huelezea kisa kimoja ama cha kishujaa au tukio la kihistoria
Waamuzi	Kitabu katika Biblia, Agano la Kale. Jina limetokana na viongozi waliojulikana kama Waamuzi, ambao Mungu aliwainua kuiongoza nchi ya Israeli

SURA YA KWANZA

MISINGI YA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Katika sehemu hii tumejadili masuala ya kimsingi ya utafiti yaliyofaa kuzingatiwa. Kila kipengele kimejadiliwa kwa kuzingatia mada ya utafiti ambayo ni Mwingilianomatini katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni*. Tumbainisha lengo la utafiti, kueleza sababu zilizotufanya kuchagua mada ya utafiti na hatimaye kueleza upeo na umuhimu wa utafiti huu. Simulizi ya Fumo Liyongo ilipatikana katika *Utendi wa Fumo Liyongo* kama inavyoelezwa katika Mulokozi (1999). Simulizi ya Mikidadi na Mayasa ilipatikana katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* (1972). Simulizi ya Gilgamesh ilirejelewa kwenye *Utendi wa Gilgamesh*, tafsiri ya Kovacs (1998) ilhali *Simulizi ya Samsoni* imerejelea *Biblia Takatifu*, kitabu cha Waamuzi sura 13, 14, 15 na 16.

1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Utenzi/utendi ni aina ya ushairi uliotokana na fasihi simulizi katika jamii. Hivyo, ushairi ndio utanzu wa fasihi ulio mkongwe zaidi katika jamii za kilimwengu kuliko tanzu nyingine. Ni utanzu wa fasihi unaobadilika sambamba na ukuaji wa binadamu ulimwenguni (Njogu na Chimera, 1999). Mtunzi wa mashairi ana nafasi ya kuelezea maendeleo ya binadamu kila uchao. Kufikia sasa, ushairi wa Kiswahili umepitia vipindi mbalimbali vya maendeleo. Kuna mitindo ya awali zaidi inayojikita katika kanuni za kiarudhi na kuna mitindo ya baadaye ya washairi iliyozivua kanuni hizo jinsi anavyoeleza Arege (2013). Kwa vyovyote vile, tenzi zinaonyesha utajiri mkubwa wa lugha ya Kiswahili na usanii wa kiwango cha juu.

Katika kurejelea *Tenzi Tatu za Kale*, Mulokozi (1999) anaeleza kuwa tenzi tatu alizozihakiki, ambazo ni *Utenzi wa Fumo Liyongo, Utenzi wa Mwana Kupona* na

Utenzi wa Al Inkishafi ni muhimu katika fasihi ya Kiswahili, kama zana kuu ya kukuza viwango vya fasihi shuleni na vyuoni. Mulokozi anasema kuwa maudhui yaliyomo katika tenzi ni muhimu kwa jamii ya leo si tu kwa kuelezea historia ya Kiswahili na jamii za Pwani, bali pia kwa kuzingatia maadili na maisha ya jamii. Hivyo, tenzi zina umuhimu wake katika ufundishaji wa fasihi katika taasisi mbalimbali za elimu.

Asili ya utanzu wa ushairi andishi ni ushairi simulizi kupitia nyimbo za hafla tofautitofauti katika maisha ya kila siku ya binadamu. Matukio mbalimbali ya kijamii yalisababisha kuwepo kwa vipera kama vile hadithi na ushairi simulizi katika utanzu wa fasihi simulizi. Matini zilizoteuliwa kwa ajili ya utafiti huu ni za kijadi na za asili ya fasihi simulizi. Kwa mujibu wa Mulokozi (1999), *Utendi wa Fumo Liyongo* ulitungwa na Bwana Muhamadi bin Abubakar bin Omari al-Bakry, anayejulikana zaidi kwa jina la Muhamadi Kijumwa, mwaka 1913. *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* ulichapishwa kwa mara ya kwanza 1971. Tenzi hizi mbili zinahusishwa na jamii ya Waswahili. *Utendi wa Gilgamesh* unatoka katika jamii ya Wasumeri. Heidel (1949) anasema kuwa vijisehemu vya utendi huu, vilikusanywa katika Karne ya Saba na mnamo 1872, vibao (Tablets) kumi na moja vilitafsiriwa kwa mara ya kwanza katika lugha ya Kiingereza. Hata hivyo, utendi huu haujatafsiriwa hadi Kiswahili, jambo linalohitaji kutekelezwa.

Utafiti pia ulirejelea *Biblia Takatifu*, kitabu cha Waamuzi sura 13, 14, 15 na 16 ili kupata *Simulizi ya Samsoni*. **Waamuzi** katika Biblia ni kitabu kinachohusu Waisraeli na viongozi wake baada ya kifo cha Yoshua hadi wakati wa Waamuzi kama vile Gideon, ambapo walitenda maovu mengi. Waisraeli walimuasi Mungu kwa njia

nyingi, hivyo Mungu 'akawaacha' wateseke. Moja kati ya wale waliowaokoa dhidi ya utesi wa Wafilisti ni Samsoni, aliyekuwa na sifa maalum za kiungu (Barker, 1973).

Dhana ya utendi imejadiliwa na wataalamu mbalimbali kwa mitazamo tofauti. Ruo (1989) anafanua utenzi kwa kusema kwamba ni maelezo ya tukio fulani refu kwa njia ya kishairi. Anaeleza kuwa mshairi anaweza kuandika beti nyingi kulingana na usimulizi alio nao. Vilevile, Ruo anagawanya tenzi katika vikundi vitatu: tenzi zinazoeleza matukio makubwa katika historia ya jamii kama vile *Utenzi wa Tambuka*, tenzi zinazoeleza matukio mbalimbali ya kidini kama vile *Utenzi wa Adamu na Awaa*, tenzi za kuasa na kutoa maoni juu ya maadili ya kimaisha kama vile *Utenzi wa Mwanakupona*. Matumizi ya tenzi katika jamii za kijadi yanaonyesha kuwa tenzi zilichukua nafasi ya kipekee katika jamii.

Kutokana na maandishi mbalimbali kuhusiana na tenzi, inabainika kwamba tenzi zilitumika hasa katika jamii za kijadi kama njia moja ya kuleta burudani. Hata hivyo, tenzi zilitumika vilevile kuwasilisha ujumbe tofautitofauti kwa jamii. Mulokozi (2002) amezungumzia mgogoro katika tendi za Kiafrika kwa kuyajadili masuala yanayohusu historia, falsafa, ujumi na mitazamo mbalimbali katika *Tenzi za Mugasha, Rukiza, Kachwenyanja* na *Mugangala*. Anaeleza utendi kama shairi refu lenye masimulizi marefu kuhusu mhusika fulani katika jamii husika. Mulokozi anaonyesha umuhimu wa tendi kuwa ni hifadhi kuu ya historia ya jamii. Anaonya kuwa jamii ya karne hii isipochukua hatua madhubuti, sanaa hii muhimu huenda ikapotea. Maelezo ya Mulokozi yanadhihirisha kuwa tendi ni kipengele chenye umuhimu mkubwa katika jamii.

Wamitila (2003) anaeleza utendi kama shairi refu la kisimulizi, linaloeleza kwa mapana na mtindo wa hali ya juu matendo ya mashujaa au shujaa mmoja. Anasema

kuwa utendi huwa na sifa nyingi na huweza kuleta pamoja hadithi kuhusu shujaa, maghani, visasili, historia pamoja na ndoto za taifa fulani. Kwa kuzingatia historia na fasihi ya jamii nyingi duniani, kila jamii ina mashujaa wake ambao wameteteleza mambo fulani yafikiriwayo kuwa ya kishujaa.

Kwa mujibu wa Shitemi (2010), tendi ni tungo za kishairi ambazo hueleza kisa kwa urefu. Anasema kwamba utendi ni hadithi ambayo huelezwa kishairi kwa makini ikiwa na mwanzo, kati na mwisho. Maelezo ya Shitemi kuhusu utendi huendana na maelezo ya wataalamu wengi kuwa utendi ni masimulizi marefu yanayohusu tukio au matukio fulani. Katika hali hii, matukio husukwa na kutiririshwa ili kujenga maudhui. Shitemi amezungumzia ushairi wa Kiswahili kabla ya Karne ya Ishirini. Nakala za baadhi ya tungo za jadi ni rejea muhimu katika utafiti huu. Kazi ya Shitemi inajenga msingi wa kufanya utafiti zaidi kuhusiana na tenzi za jadi za Kiswahili.

Ruo (1989), Mulokozi (2002), Wamitila (2003) na Shitemi (2010) wana maelezo yanayoelekea kufanana kuhusu tendi. Wanabainisha kwamba utendi una sifa ya usimulizi wa kisa kirefu kinachoelezwa kishairi. Mtafiti anakubaliana na wataalamu hao hasa kwa kuzingatia sifa ya usimulizi. Aghalabu, usimulizi huhusishwa na hadithi ambayo ina wahusika wachache wanaochangia mtiririko wa kisa chenyewe. *Simulizi ya Samsoni* ni miongoni mwa tendi zinazopatikana katika Biblia. Davidson (2011), anaeleza kwamba simulizi za Biblia zinaonyesha ustadi mkubwa katika uteuzi wa maneno yenye kuamsha hisia na taswira fulani sawa na miundo ya kazi zozote za kifasihi. Davidson anasema kwamba *Simulizi ya Samsoni* ni moja kati ya simulizi za Biblia zinazochukuliwa kuwa matini za kifasihi. Kwa kurejelea vigezo vya utendi-simulizi wa Kiafrika vilivyoorodheshwa na Mulokozi (1999), *Simulizi ya Samsoni* inaakisi baadhi ya vigezo hivyo na kubainisha kuwa ni miongoni mwa tendi zinazopatikana katika Biblia.

Tenzi mbalimbali zina manufaa ya kihistoria na kifasihi katika jamii. *Utenzi wa Mwanakupona*, kwa mfano, una habari muhimu kuhusiana na majukumu ya mwanamke katika jamii ya Waswahili na masuala ya kidini ya Kiislamu. Kupitia tenzi, vilevile, tunaweza kufahamu utamaduni wa jamii husika, habari kuhusu viongozi na mashujaa wa jamii husika. Kutokana na maelezo ya Ruo (1989), Mulokozi (2002), Wamitila (2003) na Shitemi (2010) kuhusiana na tenzi, inabainika kwamba tenzi ni hazina muhimu ya kifasihi na kihistoria katika jamii yoyote. Ili kufanikisha maudhui na dhamira mbalimbali katika kazi teule, wahusika huwajibika kutekeleza majukumu yao kwa njia inayotarajiwa. Kila mhusika anapaswa kusimama katika nafasi yake kisanii kwa njia ya kushika makini ya hadhira yake. Uigizaji, kama sanaa, unahusisha watu wengi au vikundi vya watu wanaoshiriki katika utendaji. Kwa mujibu wa Mutembei (2012), mhusika hudhihirika katika ushairi wa kingonjera katika utanzu wa ushairi. Mhusika huongoza mchezo na hata kuathiri mwelekeo wake. Mtu mmoja anaweza kushiriki kikamilifu katika onyesho kutokea mwanzo hadi mwisho.

Tenzi zinahusisha masimulizi marefu yaliyosukwa kihadithi na hushirikisha wahusika wanaojenga mfululizo wa hadithi. Matumizi ya mhusika mmoja katika utendaji hubainika katika *Tenzi za Fumo Liyongo* (UFL), *Mikidadi na Mayasa* (UMM), *Gilgamesh* (UG) na *Simulizi ya Samsoni* (SS). Wahusika wakuu ambao ni Fumo Liyongo katika UFL, Mikidadi katika UMM, Gilgamesh katika UG na Samsoni katika SS ni kitovu cha masimulizi yaliyoendelea katika matini teule. Utafiti huu ulichunguza mwingiliano wa wahusika hao ili kubainisha mwingiliano wa kimatini baina yao.

Metzger na Coogan (1993) wameelezea *Biblia* kuwa ni kitabu kitakatifu kinachotumiwa na waumini wa dini ya Kikristo katika mafundisho yanayohusiana na imani yao. Imani hii husisitiza uhusiano mwema baina ya Mungu na binadamu.

Mafundisho katika Biblia hukuza uhusiano mwema baina ya binadamu na Mungu na vilevile binadamu na binadamu mwenzake. Aidha, Metzger na Coogan (khj) wanasema kuwa *Biblia* ni kitabu chenye kufasiriwa kama fasihi. Kazi za fasihi hushughulikia binadamu na mazingira yake. King'ei na Kisovi (2005) wanafafanua kwamba fasihi kama sanaa nyingine ni zao la jamii fulani kwa kipindi fulani katika historia.

Mafundisho katika *Biblia* hukuza maadili na kuhimiza binadamu kuishi maisha ya kumpendeza Mungu, maisha yenye maadili huku yakikashifu matendo maovu. Kidini, *Biblia* ina thamani ya mafundisho ya kimaadili. Maudhui katika fasihi ya Kibiblia ni kuhusu Mungu, binadamu na maadili, mazingira na mahusiano yao. Kwa kuzingatia misingi hiyo, ni muhimu kugundua kwamba masuala ya kifasihi yapatikanayo katika *Biblia* hayajaangaziwa kwa upana. Tungo zilizoteuliwa katika utafiti huu zinadhihirisha masimulizi marefu yanayohusisha matukio mengi. Mtafiti amechambua *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa* pamoja na *Simulizi ya Samsoni* kwa kuzingatia vipengele vya vikale, wahusika na mbinu ya usimulizi kama ilivyotumika na watunzi wa kazi teule. Mbinu ya usimulizi, kwa mfano, imetumika kama njia ya kuwasilisha dhamira mahususi katika simulizi.

Katika fasihi ya Kiswahili, tenzi ni tungo za zamani katika historia ya ushairi wa Kiswahili. Ingawa tenzi nyingi za Kiswahili zina ithibati ya mwingiliano wa kimatini, suala kuwa tenzi hizi huweza kuchunguzwa kimwingilianomatini halijatafitiwa kwa kina. Tafiti zilizotangulia kuhusu tenzi, kama vile Kwame (2013); Gathara (2015); Mningo (2015) na Nabea (2017), zimejikita katika maudhui ya ushujaa miongoni mwa wahusika wakuu. Aidha, ingawa wataalamu wa kidini kama vile Gabel (1996) wameeleza *Biblia* kama mkusanyiko wa vitabu vya kifasihi, baadhi ya sehemu za *Biblia* hazijazingatiwa wala kuhakikiwa kama rejeo muhimu katika kazi za kifasihi.

Eliade (1959) anaeleza kuwa dini zote zinafanana na kwamba jazanda zinazotumiwa na binadamu zinaashiria kuwa na maana sawa. Simba mara nyingi, kwa mfano, huashiria ushujaa wa mwanamume ilhali mwanamke mara nyingi anarejelewa kijazanda kama ua. Licha ya kuwa kila matini husheheni athari ya matini nyinginezo, hakuna uchunguzi wa kimwingilianomatini ambao umeangazia mwingilianomatini katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa* pamoja na *Simulizi ya Samsoni*. Mabadiliko katika jamii yanayoletwa na teknolojia ya kisasa yamesababisha baadhi ya kazi za jadi kama vile tenzi kusahaulika.

1.2 Suala la Utafiti

Ingawa tafiti nyingi zimefanywa kuhusiana na suala la mwingilianomatini, hakuna utafiti tunaoufahamu ambao umechunguza suala la mwingilianomatini katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa* pamoja na *Simulizi ya Samsoni*, matini teule katika *Biblia*. Tenzi ni hifadhi muhimu ya historia ya jamii, hivyo zinafaa kuhifadhiwa kwa kufanyiwa utafiti zaidi ili ziendeleo kufaidi jamii. Kutokana na udurusu wa maandishi uliofanywa na mtafiti, ilidhihirika kwamba matini teule zinawasilisha visa mbalimbali kwa njia ya usimulizi.

Licha ya kuwa matini teule zilitungwa katika vipindi tofauti vya kihistoria na kutungwa pia katika maeneo tofauti kijiografia, kuna mwanangwi fulani unaohisika kisimulizi hivyo kulazimu utafiti huu. Hili ndilo lililozua pengo la kiakademia lililokusudiwa kuzibwa na utafiti huu. Utafiti umezingatia *Biblia* kama matini muhimu ambayo ina wingi wa kazi za kifasihi zinazohitaji kuhakikiwa, mojawapo ikiwa *Simulizi ya Samsoni*.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti ulinuia kutimiza malengo yafuatayo:

- i Kufafanua mwingiliano wa kisimulizi katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni*.
- ii Kuonyesha sifa za wahusika wakuu katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni*.
- iii Kuhakiki maingiliano ya kikale cha safari katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni*.

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo ya utafiti:

- i Mwingilianomatini wa kisimulizi ulivyotumika katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni* unasababishwaje na muktadha wa kijamii ama mtindo wa usimulizi wa watunzi?
- ii Mwingiliano wa sifa za wahusika wakuu umedhibitishwa vipi katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni*?
- iii Ubia wa kikale cha safari umebainishwa vipi katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni*?

1.5 Sababu za Kuchagua Mada ya Utafiti

Katika utafiti huu, mtafiti aliteua mada hii ili kujua jinsi *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni* zilivyoingiliana kimatini. Mtafiti aliteua mada hii ili kuonyesha mwingilianomatini katika tenzi teule za fasihi na *Simulizi ya Samsoni* yenye misingi ya kidini ya Kikristo.

Suala la usimulizi katika fasihi simulizi ni muhimu. Kumekuwa na madai kwamba usimulizi hudhihirika tu katika utanzu wa fasihi simulizi. Hata hivyo, usimulizi teule

huweza kuhifadhiwa kimaandishi ili kufaidi jamii kwa muda mrefu. Katika karne hii, inabainika kwamba kizazi cha leo hakitambui wala kuelewa baadhi ya fasihi simulizi katika jamii zao. Kutokana na hayo, mtafiti alichagua mada ya utafiti huu kwa lengo la kuhamasisha jamii ya sasa kuhusu umuhimu wa simulizi za tenzi za kale.

Uteuzi wa mada hii ulitokana na sababu kwamba tafiti nyingi za awali zimezingatia tanzu za riwaya, tamthilia na hadithi fupi katika fasihi andishi ya Kiswahili. Utanzu wa fasihi simulizi unahitaji kufanyiwa utafiti zaidi. Baadhi ya vipera vya fasihi simulizi vinavyopaswa kutafitiwa ili kuhifadhiwa ni pamoja na hadithi, maigizo, semi na ushairi. Utafiti huu ulinua kuonyesha kuwa utanzu wa ushairi wa Kiswahili unafaa kuangaziwa kuliko jinsi ulivyo sasa. Wapenzi na wataalamu wa mashairi watapanua maarifa yao kuhusiana na masuala mbalimbali katika utanzu huu. Utafiti utawahamasisha wanafunzi kuondoa imani potofu kwamba ushairi ni mgumu.

Tenzi ni hazina kubwa ya historia ya jamii. Kama asemavyo Mulokozi (2002), kuna haja ya kuzichunguza, kuzihakiki na kuzihifadhi tenzi za Kiafrika ili kusitokee mkasa wa kupoteza tenzi hizi za kipekee. Kwa hivyo, imehalisi mtafiti kuteua mada ya utafiti huu ili kuzindua kizazi cha karne ya ishirini na moja kuona umuhimu wa tenzi hata katika enzi hii ya utandawazi.

Biblia kama matini huangazia masuala ya kidini ya Kikristo. Jamii inatilia maanani mafundisho ya kidini *Biblia* ikiwa ni kama mwongozo wa maadili unaopaswa kuigwa na jamii. Aidha, ni muhimu kutambua kwamba ukosefu wa mwongozo bora husababisha mporomoko wa maadili hasa katika Karne hii ya Ishirini na Moja. Hivyo, utafiti huu umetathmini mafundisho katika *Biblia* kwa kuonyesha uamilifu na uyakunifu wake katika jamii ya sasa kwa kurejelea *Simulizi ya Samsoni*.

Sababu nyingine iliyosababisha uteuzi wa mada ya utafiti huu ilitokana na ilhamu, hususan masuala ya ubia wa motifu ya safari katika utafiti. Suala la motifu ya safari limehakikiwa kwa kuzingatia ubia wa vikale katika fasihi. Ilimlazimu mtafiti kuchunguza suala hili kwa lengo la kuonyesha ruwaza ya urudiaji wa kikale cha safari na kwamba vikale katika tenzi ni dhahiri hivyo vinaweza kutafitiwa pia katika utanzu wa ushairi.

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unachambua mwingilianomatini katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni* katika Biblia. Vipengele ambavyo vimeshughulikiwa ni mtindo wa kisimulizi, mwingiliano wa sifa za wahusika na udhihirikaji wa kikale cha safari katika matini teule.

Simulizi ya Fumo Liyongo imetolewa katika muktadha wa kifasihi katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, simulizi ya Gilgamesh imerejelea *Utendi wa Gilgamesh* na simulizi ya Mikidadi na Mayasa imetoka katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Simulizi ya Samsoni imeibuliwa katika *Biblia Takatifu*, kitabu cha Waamuzi sura za kumi na tatu hadi kumi na sita. Ingawa kitabu cha Waamuzi kina sura ishirini na moja, mtafiti aliteua sura 13 hadi 16 kimaksudi kwa sabababu ziliakisi mada na malengo ya utafiti huu.

Utafiti huu umefafanua mwingiliano wa mbinu ya kisimulizi ilivyotumika katika uwasilishaji wa ujumbe katika matini teule. Aidha, utafiti umeonyesha mwingiliano wa sifa za wahusika na vilevile kubainisha urudiaji wa ruwaza ya motifu ya safari katika matini teule. Mtafiti amechunguza matini teule na kuonyesha kuwa ijapokuwa ni kazi za kijadi, jamii ya sasa ina nafasi ya kuyafinyanga upya mafunzo yanayotokana nazo.

Nadharia zilizotumika katika utafiti huu ni Mwingilianomatini na Vikale. Anavyosema Wamitila (2008), nadharia ya Mwingilianomatini huchukulia kwamba kila kazi ya kifasihi inahusiana na kazi nyingine kwa namna fulani. Nadharia hii imetumika kuchambua vipengele vya mbinu ya kisimulizi vilivyoingiliana na kuathiriana. Aidha, nadharia hii imetumika katika uchambuzi wa mwingiliano wa sifa za wahusika katika matini teule. Nadharia ya Vikale inahusu ubia wa ishara na visasili mbalimbali kote ulimwenguni. Nadharia hii ilikuwa muhimu katika uhakiki wa ruwaza ya motifu ya safari ilivyobainika katika UFL, UMM, UG na SS.

Matini teule za utafiti huu zilitungwa katika vipindi tofauti vya kihistoria. Hata hivyo, matini zote zina ukale wa kuanzia Karne ya Sita kabla ya kuzaliwa Kristo ambapo *Utenzi wa Gilgamesh* ulikusanywa, (Heidel, 1949). *Utenzi wa Gilgamesh* ni utenzi wa kale mno ilhali una umuhimu wake wa kifasihi hasa ikizingatiwa kwamba hakuna utafiti wa kina uliofanywa kuhusiana nao. Kwa mujibu wa Barker (1973), *Simulizi ya Samsoni* ilirekodiwa katika Biblia karne ya kumi Kabla ya kuzaliwa Kristo. Hali kadhalika, *Tenzi za Mikidadi na Mayasa* na *Fumo Liyongo* ni kazi za jadi zinazotupa nafasi ya kuona fasihi ya Kiswahili katika kipindi cha kirasimi. Anavyosema Shitemi (2010), urasimi ni kipindi kinachoenda sambamba na fasihi simulizi ya Waswahili iliyohifadhiwa katika kumbukumbu za masimulizi ya midomoni na kunaswa hapa na pale katika kumbukumbu za kutumia hati za Kiarabu. Kwa ujumla, kazi zilizoteuliwa katika utafiti huu ni za kale na hutupatia taswira ya maisha ya mwanadamu wa wakati huo.

1.7 Umuhimu wa Utafiti

Tahakiki nyingi za awali zinazohusiana na ushairi zimechunguza matumizi ya lugha na maudhui pasipo kuzingatia dhana ya usimulizi katika ushairi. Utafiti huu uliazimia kuchunguza suala la mwingilianomatini katika usimulizi wa kishairi na kutambulisha

mbinu za kisimulizi, sifa za wahusika wakuu na udhihirikaji wa motifu ya safari kama baadhi ya vipengele vinavyozua mwingilianomatini katika tenzi. Ni madhumuni ya utafiti huu kuchangia katika kubainisha mbinu za kisimulizi zilizotumika ili kusababisha mwingilianomatini katika UFL, UMM, UG na SS.

Utafiti huu utachangia maarifa katika taaluma ya fasihi andishi na simulizi. Utafiti utawafaidi wataalamu na wasomi wa fasihi katika kutathmini suala la mwingilianomatini katika *Simulizi ya Samsoni* katika *Biblia* na *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh* na *Mikidadi na Mayasa*. Utafiti umechambua mbinu ya kisimulizi ilivyotumika katika matini teule na kuonyesha kuwa tenzi zinaakisi sifa za kisimulizi zinazodhihirika katika usimulizi wa hadithi katika fasihi simulizi.

Kazi hii itakuwa ya manufaa kwa walimu na wanafunzi wanaoenzi taaluma ya ushairi. Watu wengi walio na maoni hasi kuhusiana na ushairi wataweza kuona kwamba ni taaluma inayojikita katika mafundisho muhimu mbali na kuwa na uburudisho kwa jamii. Wanafunzi waliokuwa na maoni hasi hivyo watabadilisha mtazamo wao kuhusu ushairi. Kazi hii basi itatoa changamoto kwa wanataaluma wa fasihi kutoa tathmini mpya kuhusu ushairi.

Utafiti huu unachangia maarifa kuhusu uchanganuzi wa baadhi ya fasihi zinazopatikana katika *Biblia* na kuonyesha kuwa *Biblia* ni mojawapo ya matini inayoweza kuchambuliwa kwa mitazamo ya kifasihi. Mbali na *Simulizi ya Samsoni*, kuna matini nyingi ambazo zinaweza kuchambuliwa katika *Biblia* ili kuchangia maarifa mapya katika taaluma ya fasihi. Hivyo basi, utafiti huu utachochea baadhi ya wanafasihi kufanya utafiti wa aina hii kwa kuzingatia *Biblia* kama matini rejea.

Vikale aghalabu vimehusishwa na utanzu wa riwaya katika fasihi. Utafiti huu unaonyesha kuwa suala hili linaweza kuchambuliwa pia katika ushairi, tenzi

zikiwemo. Suala la vikale katika utanzu wa ushairi halijafanyiwa utafiti zaidi kama ilivyo katika riwaya. Utafiti huu basi utawachochea watafiti wengine kuchunguza suala hili katika tenzi nyingine mbalimbali.

Uchambuzi wa mwingiliano wa sifa za wahusika katika matini teule ulionyesha kwamba wahusika wakuu hasa wanalandana katika misingi ya fasihi linganishi. Utafiti huu hivyo ni muhimu katika taaluma ya fasihi linganishi kwa kuzingatia miktadha ya kidini na fasihi katika matini husika. Kazi hii ni ya manufaa kwa walimu, wanafunzi na wataalamu wa fasihi katika Karne hii ya Ishirini na Moja. Utafiti huu vilevile unaweka msingi kwa ajili ya tafiti nyingine katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili.

1.8 Hitimisho

Sura hii imekuwa msingi wa utafiti huu. Katika sura hii, tumejadili vipengele mbalimbali vinavyoendana na suala la utafiti na malengo ambayo yaliongoza utafiti huu. Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa katika sehemu hii ni pamoja na usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, malengo na maswali yaliyotokana na malengo hayo ya utafiti. Aidha, sura hii imeonyesha sababu za kuchagua mada, ikatoa upeo na mipaka ya utafiti na hatimaye kuangazia umuhimu wa utafiti huu. Sura inayofuata inashughulikia mapitio ya maandishi yanayohusu mada ya utafiti na misingi ya kinadharia.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.0 Utangulizi

Katika sura ya kwanza ya utafiti huu, tuliangazia masuala ya msingi ya utafiti huu. Sehemu hii imehakiki maandishi mbalimbali yanayolingana na mada ya utafiti huu. Watafiti na wasomi tofauti wamezungumzia kwa njia moja ama nyingine mambo yanayohusiana na mada ya utafiti huu. Mapitio ya maandishi hayo yamekuwa ya manufaa kwa sababu yalisaidia kuimarisha hoja za utafiti na vilevile kuonyesha pengo lililoachwa, hivyo kuzua tatizo la utafiti huu.

2.1 Mapitio ya Maandishi

Sura hii imehakiki maandishi mbalimbali yaliyohusiana na malengo ya utafiti huu. Mwanzo, tumechambua maandishi kuhusu usimulizi katika tenzi, pili, mwingiliano wa sifa za wahusika na tatu, mapitio ya maandishi kuhusu tanzia kama kigezo muhimu katika uchambuzi wa tenzi teule na matini ya kidini.

2.1.1 Maandishi kuhusu Usimulizi katika Tenzi

Mbinu ya usimulizi hudhihirika katika uwasilishaji wa ujumbe katika vipengele mbalimbali vya fasihi andishi na simulizi. Ni mbinu ambayo inatumia maneno kiubunifu ili kushika makini ya hadhira yake. Usimulizi huhusisha mtiririko wa simulizi ili kufafanua kisa fulani katika simulizi hiyo. Masimulizi huundwa kwa njia ya kuonyesha usimulizi wa mfuatano wa matukio yenye mahusiano. Genette (1980) katika ufafanuzi wa nadharia ya Naratolojia anasema kwamba katika simulizi, lazima kuwa na utambwaji wa hadithi kwa njia mbalimbali. Aidha, mfuatano wa matukio katika simulizi huweza kuwasilishwa kwa njia tofautitofauti kama vile uelezaji na uonyeshaji. Kipengele cha usimulizi kimeshughulikiwa katika sura ya nne ya utafiti huu.

Njogu na Chimerah (1999), wanafafanua maelezo ya mtindo katika ushairi kupitia kwa baadhi ya maswali yafuatayo: mtunzi amepangaje mishororo yake? Ana takriri (kwa mfano vibwagizo) na endapo vipo, vitasisitiza jambo gani? Waweza kusema nini kuhusu ukwapi na miloto ya shairi hilo? Mtunzi ameumbaje utungo wake? Ameanza na hoja zipi? Amemaliza na hoja zipi? Maswali ya wataalamu hao yanafafanua maelezo ya mtindo hasa katika utanzu wa ushairi. Kwa sababu hii, “utamu” wa kazi teule hutegemea mtindo uliotumiwa na msanii. Utafiti huu ulichunguza mtindo wa kisimulizi ulivyotumika katika matini teule ili kufaulisha ujumbe kwa hadhira lengwa.

Mohochi (2000) ameshughulikia usimulizi kwa kuhakiki Riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*. Anaeleza kuwa baada ya uvumbuzi wa maandishi, kazi nyingi za fasihi zinapatikana katika maandishi na hivyo usimulizi dhahiri haujitokezi katika kazi hizo. Hata hivyo, hatukosi kuisikia sauti ya msimulizi katika akili zetu iwapo si masikio yetu angalau pale tunapoifuatilia hadithi kwa kuisoma. Katika ufafanuzi wa maelezo yake, inabainika kwamba dhana ya usimulizi hudhihirika katika kazi za kimaandishi za kinathari. Kazi ya Mohochi ni muhimu kwa kazi yetu kwa kuwa imetuongoza kujua namna usimulizi ulivyotumika katika riwaya. Hata hivyo, kazi yake inatofautiana na kazi yetu kwa sababu utafiti huu unashughulikia kipengele cha usimulizi katika utanzu wa ushairi. Wamitila (2003) ameorodhesha aina mbalimbali za kisimulizi kwa mfano, usimulizi maizi, usimulizi penyezi, usimulizi sawia, na usimulizi tangulizi. Mbinu zingine alizozitaja ni pamoja na usimulizi wa ki-utendi, usimulizi wa nafsi ya kwanza, pili na tatu. Katika utafiti huu, tumeangazia baadhi ya mbinu za kisimulizi jinsi zinavyotumika katika matini zilizochunguzwa.

Inabainika kwamba fasihi simulizi ni utanzu mkongwe zaidi kuliko tanzu nyingine za fasihi. Dai hili hutokana na sababu kuwa binadamu tangu mwanzo walikuwa wakiwasiliana. King'ei na Kisovi (2005) wanatilia mkazo kuwa fasihi simulizi ilianza mara tu wanadamu wa jamii fulani walipoanza kuwasiliana. Fasihi hii ilianza kushamiri na kustawi pale watu wa jamii moja walipoanza kufanya kazi kwa kujumuika pamoja na kufanya sherehe nyingi tofauti. Ushairi andishi ni zao la ushairi simulizi hivyo basi kuwa na sifa za kisimulizi sawa na kazi nyingine katika fasihi simulizi.

Katika fasihi, mtindo huhusisha msuko wa kazi teule kwa njia fulani maalum. Mtindo huu huweza kufananishwa na ususi ambapo kila msusi ana njia yake ya kusuka nywele. Uwasilishaji wa ujumbe pia huweza kuwa tofauti katika matini za riwaya, tamthilia na ushairi. Katika tendi, mtindo unahusisha zaidi mbinu ya kisimulizi na matumizi ya tamathali za usemi. Aidha, kuna matumizi ya takriri za aina tofauti kama vile za neno, maneno, silabi na matumizi ya jazanda. Wakirejelea uchambuzi wa mashairi, Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kwamba ni muhimu kuchunguza kwa makini vipengele vya kisanaa na kimuundo vilivyotumiwa ili kubainisha ni vipi vinaingiliana na maana ya shairi zima. Uchunguzi wa aina hii unamwezesha mhakiki yeyote kutathmini dhamira ya shairi na hivyo kuelewa hasa lengo la mtunzi.

Gimode (2006) amechambua matumizi ya lugha kanisani na namna yanavyoathiri ujumbe unaopitishwa. Anasema kwamba matumizi ya lugha ya kijazanda huzua hisia kwa waumini na hivyo kuwa na ufasaha katika kushawishi watu wafuate mwelekeo fulani. Usanii wa lugha ni muhimu hasa katika kazi za kishairi. Athari ya dini ya Kikristo ina mchango wake katika kazi za fasihi simulizi ya Kiafrika. Kwa mfano, *Biblia Takatifu* na kitabu maarufu cha Bunyan, *Pilgrim's Progress* ni vitabu vya mwanzo kabisa kutafsiriwa katika lugha asilia za Kiafrika. Waafrika walijifunza fasihi

ya Kimagharibi kupitia vitabu hivyo vya Kikristo. *Pilgrim's Progress* (Sehemu ya kwanza), kwa mfano, imetafsiriwa katika lugha ya Manganga, katika Afrika ya Kati na kutumiwa katika Wilaya ya Ziwa Nyassa. Kihistoria, dini ya Kikristo iliweka msingi wa usomi kwa Waafrika ambao baadaye waliweza kuandika kuhusu fasihi yao ya Kiafrika.

Arege (2012) ameshughulikia usimulizi katika tendi kwa kuchunguza *Utendi wa Rasil Ghuli*. Kwa kutumia nadharia ya Naratolojia, anajadili mbinu ya kisimulizi ilivyotumika katika uwasilishaji wa ujumbe katika *Utendi wa Rasil Ghuli*. Arege anazungumzia mbinu ya kisimulizi kama mtindo unaotumika kwa upana katika tendi. Anaonyesha viwango mbalimbali vya msimulizi na hali kadhalika sauti tofautitofauti za msimulizi. Anapendekeza kuwa utafiti zaidi ufanywe ili kubainisha ufaafu wa mbinu hii katika tenzi mbalimbali. Kazi ya Arege ilikuwa na umuhimu katika utafiti huu kwa sababu ilimsaidia mtafiti kupata maarifa zaidi kuhusiana na usimulizi katika tendi. Hata hivyo kazi yake ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa utafiti huu unachunguza mwingilianomatini katika *tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh*, na *Simulizi ya Samsoni*.

Wanyama, Chimerah na Karisa (2017) wanachambua Muundo wa Utenzi wa Wabukusu wa *Khuswala Kumuse*. Wao wanajadili kwamba mbali na kuelezea majagina wa Kibukusu, utenzi pia unaelezea visa vya Biblia hasa kuhusu uumbaji wa Adamu na Eva na asili ya koo mbalimbali. Utenzi unaendelea kuelezea muktadha wa mbinguni katika uumbaji wa Adamu na Eva na kuelezea nasaba yake. Wasomi hao wanasisitiza kwamba kuna mwingilianomatini katika *Utenzi wa Khuswala Kumuse*, kwamba msanii anatumia nyimbo, ngano, vitendawili na mafumbo katika uwasilishaji wa ushairi wake. Mintarafu ya wasomi hao, ni muhimu kufanya utafiti zaidi kuhusiana na vipengele vingine vya fani kama vile mandhari na wahusika katika

tenzi. Inabainika kwamba *Biblia* ni rejeo ambalo linastahili kuzingatiwa katika tafiti zinazohusiana na tungo za kale kama vile tenzi.

Katika kuujadili mchango wa Mathias Mnyampala kuhusu maendeleo ya Kiswahili, Kyamba (2018) anaeleza kwamba Mnyampala aliibua mitindo mbalimbali kama vile msisitizo na mtiririko katika ushairi. Anasema kwamba Mnyampala alifufua na kuhuisha baadhi ya mbinu kama vile ngonjera na mashairi ya vidato zilizotumika hapo awali na kuzifanya mpya. Utafiti wa Kyamba ulibaini kuwa mbinu za kifani zilizotumika katika kuibua maudhui ya mashairi ya Mnyampala zinaingiliana, zinatagemeana na kukamilishana. Utafiti wake unarejelea nadharia ya Mwingilianomatini kubainisha kuwa kuna mwingiliano wa tanzu za fasihi simulizi, maudhui na mbinu za kifani zinazotumika katika ushairi wa Kiswahili. Hata hivyo, kazi yake ni tofauti na kazi yetu kwa sababu utafiti huu unatumia nadharia ya Mwingilianomatini kuhakiki matini teule UFL, UMM, UG na SS wakati utafiti wake unatumia nadharia hii kuhakiki mashairi ya mtunzi mmoja, Mathias Mnyampala.

Dhana ya usimulizi ni kigezo cha kifani katika fasihi andishi na fasihi simulizi ya Kiswahili. Hata hivyo, kipengele hiki hakijashughulikiwa kikamilifu katika tenzi. Utafiti huu umehakiki usimulizi kama mbinu iliyotumika kuwasilisha ujumbe katika UFL, UMM, UG na SS. Matini hizi zimeonyesha mwingiliano kwa namna ambavyo ‘zinawasiliana’ kisimulizi. Watunzi wa simulizi hizi ni kana kwamba walikulia katika mazingira sawa. UFL, UMM, UG na SS zilitungwa katika vipindi tofauti vya kihistoria na mazingira tofauti kijiografia. Mbinu ya kisimulizi iliyotumika kuwasilisha ujumbe katika matini teule imeibua dhamira mbalimbali zinazojitokeza katika matini. Watunzi wa kazi teule wameonyesha msimulizi kuwa mwenye dhamira au mwelekeo fulani unaofanana ambao anakusudia msikilizaji au msomaji wake kujishirikisha nao katika matini husika.

2.1.2 Sifa za Wahusika Wakuu katika Tenzi

Kwa kutoa ufafanuzi wa wahusika katika tamthilia ya kitanzia, Dorsch (1965) akimnukuu Aristotle, anasema kuwa wahusika na matendo yao wanaweza kuwa wazuri au wabaya. Uzuri au ubaya wa mhusika ndio unaoleta tofauti kati ya futuhi na tanzia. Aidha, uzuri au ubaya wa mhusika husababishwa na kosa au dosari moja tu ambayo baadaye huja kumwangusha. Mhusika kupitia kwa matendo yake huwafanya watazamaji kuvutiwa kwake au kusukumwa mbali kwa sababu ya sifa maalum zinazohusishwa naye. Utafiti huu ulichunguza mwingiliano baina ya wahusika walivyosawiriwa na watunzi wa *Simulizi ya Samsoni* katika misingi ya dini ya Kikristo na *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa*.

Gabel (1996) ameorodhesha mitindo ya fasihi inayopatikana katika *Biblia* kama vile matumizi ya jazanda, ishara, sitiari, uhuishaji, kejeli na ushairi. Chini ya sitiari mwandishi huyu ameonyesha jinsi mtindo huu unavyotumika katika *Biblia Takatifu* ili kuleta maana yenye kueleweka zaidi. Mfano katika *Biblia* unapatikana katika kitabu cha 2 cha Samueli, kifungu cha 12 kuhusu Nathan na Mfalme Daudi. Aidha, Gabel anaonyesha simulizi kama mtindo unaotumika kwa minajili ya kufafanua ujumbe unaokusudiwa bila kupotosha maana. Anaendelea kusema kuwa, mwanzo kabisa simulizi ilichukuliwa kuwa hadithi fupi yenye mafundisho ya kimaadili kama ilivyo simulizi ya Wajenzi Wawili katika Mathayo 7:24-27. Kadri muda ulivyosonga, maana hii ikaongezewa ufafanuzi na simulizi ikawa mafundisho ya kiajabu yaliyo na maana nyingi au sitiari yenye viwango viwili vya maana, maana fiche na maana wazi. Ingawa Gabel ameelezea kuhusu simulizi, hajazingatia matumizi ya simulizi hizi hasa katika kazi za fasihi.

Kutokana na urefu wa historia ya ushairi wa Kiswahili, wataalamu mbalimbali wamehakiki vipengele tofauti tofauti katika utanzu huu. Shitemi (1997)

ameshughulikia uaminifu katika ushairi wa jadi wa Kiswahili katika *Utenzi wa Mwana Kupona, Mashairi ya Muyaka na Utendi wa Inkishafi*. Anachunguza suala la tafsiri na uaminifu katika tendi teule. Kazi ya Shitemi ni muhimu kwa kuwa ilimpa mtafiti maarifa zaidi kuhusiana na tenzi za kijadi. Baadhi ya tenzi za kijadi ni pamoja na *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa* ambazo zimeshughulikiwa katika utafiti huu. Tofauti na utafiti uliofanywa na Shitemi, utafiti huu unashughulikia suala la mwingiliano wa kimatini katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa* na *Simulizi ya Samsoni* kwa kuzingatia sifa za wahusika wakuu kama kipengele kimoja cha uhakiki.

Wamitila (2003) amefafanua suala la uhusika katika matini za kifasihi kwa upana. Anaelezea kwamba uhusika katika fasihi ni mbinu na mikakati inayotumiwa na mwandishi kuwasawiri wahusika katika kazi yake. Waandishi hutofautiana katika kushughulikia suala la wahusika na uhusika. Waandishi wanaolitia uzito suala la uhusika wanaamini kuwa kilicho na uzito na maana katika fasihi ni jinsi matukio yanayopatikana katika kazi yanavyowaathiri wahusika. Waandishi hutumia mbinu tofauti kuwasawiri wahusika wake. Kwa mfano, mbinu ya maelezo kuhusiana na matendo yao, mbinu ya kimazungumzo (kidrama), mbinu ya uzungumzi-nafsi na matumizi ya majazi. Mbinu hizi ni muhimu katika ujenzi wa hadithi, dhamira na maudhui ya kazi ya fasihi. Tofauti na maandishi ya Wamitila, utafiti huu umechanganua sifa za wahusika katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa* na *Simulizi ya Samsoni*.

Kipengele cha uhusika ni muhimu katika uchambuzi wa tungo za kifasihi. Wamitila (2008) amechanganua nafasi ya wahusika na uhusika katika uigizaji au drama. Anaelezea kuwa wahusika wana nafasi kubwa katika kazi ya kidrama. Anazungumzia msingi wa uchanganuzi wa wahusika wa kidrama kwa kuzingatia nafasi, utanzu,

umakundi, usemi na ulinganuzi. Kati ya mambo yanayoweza kulinganishwa ni wahusika na uhusika kwa jumla. Maandishi ya Wamitila yalitufaa katika uchambuzi wa wahusika wakuu katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa* na *Simulizi ya Samsoni*. Dhima ya fasihi katika jamii kote ulimwenguni ni ileile; kuburudisha, kuelimisha, kuonya na kadhalika. *Utenzi wa Gilgamesh na Simulizi ya Samsoni* ni zao la fasihi za Kimagharibi zikilinganishwa na *Tenzi za Fumo Liyongo na Mikidadi na Mayasa* ambazo ni zao la fasihi ya Kiafrika. Kwa hiyo, fasihi ya jamii mbalimbali duniani huingiliana, huathiriana na kusababisha mwingiliano wa aina mbalimbali.

Athari ya dini ya Kiislamu pia ilichangia pakubwa katika uandishi wa fasihi ya Kiafrika. Kihistoria, dini ya Kiislamu ilikuwa imeingia katika Bara la Afrika kufikia Karne ya Kumi na Mbili (K12). Ushairi wa Kiswahili ulikuwa umekita mizizi katika eneo la Afrika Mashariki kufikia K19. Mshairi Muyaka bin Haji (1776-1840) anasemekana kuwa aliutoa ushairi msikitini na kuupeleka sokoni. Muyaka alijitenga na maudhui ya kidini na kuzungumzia masuala yaliyohusiana na shughuli za maisha ya kila siku ya binadamu. Mbali na kuwa na athari ya dini ya Kiislamu, mashairi ya Muyaka yaliangazia maudhui mbalimbali kama vile Maisha ya Jamii, Uzalendo, Mapenzi, n.k. (Shitemi, 2010). Tenzi nyingi za Kiswahili zina athari ya dini ya Kiislamu na baadhi zina athari ya dini ya Kikristo. Maelezo haya yanaonyesha kuwa, sawa na Kurani, *Biblia* ni matini ambayo inastahili kufanyiwa utafiti zaidi ili kurutubisha fasihi ya Kiswahili.

Kwame (2013) amejadili dhamira zinazoibuliwa katika *Utendi wa Gilgamesh*. Katika kuzungumzia dhamira, amegusia vilevile maudhui katika kazi za fasihi. Ametumia nadharia ya Ruwaza ya Shujaa kuonyesha namna inavyoibua dhamira katika utendi. Kazi hii ni muhimu kwa sababu ilitumika kupanua maarifa kuhusu wahusika katika

utendi. Vilevile, kazi ya Kwame ni muhimu katika uelewaji zaidi wa sifa za wahusika wakuu katika tendi teule zilizorejelewa katika utafiti huu. Hata hivyo, kazi yake inatofautiana na utafiti wetu kwa sababu yeye amechambua dhamira zilizoibuliwa katika utendi ilhali utafiti wetu umezingatia vipengele vya kisimulizi, uhusika na vikale katika matini teule.

Miaka mingi imepita tangu kutungwa kwa *Utendi wa Fumo Liyongo*. Muda huo umeona tahakiki na tungo mbalimbali zinazohusiana na utendi huu, zikiwemo *Hadithi za Mashairi: Kisa cha Fumo Liyongo* (2007) na *Tamthilia ya Liyongo* (2009). Hii inatokana na umaarufu wa utendi wenyewe na ustadi wa uandishi wa kisa cha Fumo Liyongo. Mningo (2015) amejadili kuhusu mwingilianomatini katika tamthilia za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988) na *Fumo Liyongo* (2009). Kazi yake imeonyesha mwingilianomatini baina ya kazi za mwandishi mmoja, Emmanuel Mbogo. Aidha, tamthilia hizi ziliandikwa katika vipindi tofauti iwapokuwa mwandishi ni mmoja. Mningo anachunguza endapo kuna mabadiliko yoyote ya kiubunifu katika tamthilia teule. Utafiti wa Mningo ni tofauti na utafiti huu kwa sababu yeye amechambua tamthilia ya *Fumo Liyongo* ilhali utafiti huu unazingatia mwingilianomatini katika UFL, UMM, UG na SS kwa kurejelea vipengele vya usimulizi, wahusika na tanzia.

Utafiti uliofanywa na Nabea, Mwangi na Mayaka (2017) unahakiki matendo ya wahusika wakuu katika tendi teule za Kiswahili. Wanajadili iwapo wahusika hao wanadhihirisha ushujaa ama uhayawani. Mjadala huu wameuendeleza kwa kurejelea *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* na *Utendi wa Fumo Liyongo*. Kauli ya Nabea na wengine (Khj) ni kuwa matendo yanayodhihirishwa na Mikidadi na Mayasa yanahitaji kujadiliwa upya, iwapo ni ushujaa au uhayawani. Vilevile, wanaendeleza mjadala huo huo katika *Utendi wa Fumo Liyongo* kwa kurejelea mhusika mkuu, Fumo Liyongo. Wanadai kuwa ushujaa wa Fumo Liyongo unatiliwa shaka kwa kuwa

akimtokea mtu ghafla, mkojo humpotea na kuanza kulia. Pamoja na sifa zake zingine, inadaiwa kuwa Fumo Liyongo alikuwa na umbo la kushtua lililowafanya watu kuzirai alipowakodolea macho. Wahakiki hao wanaeleza kuwa sifa zinazodaiwa kuwa za kishujaa katika wahusika hao zinapotosha kwa sababu matendo yao yanaogofya na yanadhihirisha uhayawani. Wanasema kuwa japo wasomi wameshikilia kuwa tendi za Kiswahili ni kazi za kishujaa, matendo na sifa za wahusika wakuu hazilandani na ushujaa. Wahusika hao wanadhihirisha matendo ya kuogofya na kustaababisha ambayo yanawafanya jamii isiweze kutangamana nao kwa urahisi. Kazi yao ni muhimu kwa kuwa inazungumzia matendo ya wahusika wakuu katika matini teule. Hata hivyo, kazi hii ni tofauti na utafiti wetu kwa sababu utafiti huu ulichunguza mwingilianomatini katika vipengele vya vikale, mbinu ya kisimulizi na sifa za wahusika wakuu kwa kurejelea *Simulizi ya Samsoni* katika *Biblia* (Waamuzi 13- 16), *Utendi wa Fumo Liyongo*, *Utendi wa Gilgamesh* na *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*.

Katika misingi ya wahusika na uhusika kwa jumla, kuna mwingiliano wa matini katika Tenzi za *Fumo Liyongo*, *Gilgamesh* *Mikidadi na Mayasa* na *Simulizi ya Samsoni*. Wahusika wakuu wamesawiriwa kama wale wanaoendeleza dhamira katika matini teule. Wamekuzwa kutegemea matendo na tabia zao. Wahusika hao wamepewa nafasi ya kusukuma mbele hadithi au kisa chao kwa njia inayofanana. Uumbaji wa wahusika katika matini teule unaingiliana na kuathiriana kwa njia moja ama nyingine. Wahusika wana sifa ambazo zinafanana na kuingiliana. Samsoni, Fumo Liyongo na Gilgamesh ni wahusika wanaoonyesha mkondo wa maisha na matukio yanayofanana. Wameonyeshwa kuwa wahusika wanaofanya mambo yao kiajabujabu ijapokuwa kila mmoja wao ana dosari ambayo husababisha maangamizi yake. Kwa jumla, wahusika wanaoonyeshwa katika Tenzi za *Fumo Liyongo*, *Mikidadi na*

Mayasa, Gilgamesh na *Simulizi ya Samsoni* wanaingiliana na hivyo kuzua mwingilianomatini katika misingi ya wahusika.

2.1.2.1 Tanzania kama Sifa Muhimu ya Wahusika Wakuu katika Tenzi

Suala la tanzia linahusishwa hasa na mwanafalsafa wa zamani wa Kigiriki, Aristotle aliyezungumzia uigizaji au drama katika fasihi. Kwa mujibu wa Aristotle, tanzia ilihusisha uigizaji uliozingatia mambo ya kimsingi katika maisha. Alisisitiza kuwa uigizaji wa ki-tanzia ni lazima kuibua hisia za woga miongoni mwa hadhira.

Wazo la tanzia limepanuliwa na Dorsch (1965) anayeeleza kuwa ni aina ya tamthilia yenye huzuni inayogusia hisia za watazamaji kiasi cha kuwaogofya na kumwonea huruma mhusika mkuu ambaye atapata janga. Mhusika mkuu anasawiriwa kuwa shujaa anayeweza kukabiliana na mambo hatari yanayotokea. Hivyo, mhusika huyu huwa na mwenendo bora unaokubalika katika jamii. Anaheshimiwa na kupewa nafasi ya kipekee katika jamii. Mawazo ya Dorsch aidha yanasisitiza hisia za woga miongoni mwa hadhira sawa na Aristotle. Hii ina maana kuwa hadhira ilibidi kuchochewa kihisia hasa kuhusiana na matendo ya mhusika mkuu aliyefikiriwa kuwa shujaa katika tamthilia.

2.1.2.2 Maandishi kuhusu Tanzania

Tanzia inahusisha maigizo yanayogubikwa na huzuni hasa kutokana na uchaguzi au uamuzi mbaya unaofanywa na mhusika mkuu. Ni maigizo yanayoonyesha anguko la shujaa anayekosa kutimiza malengo yake kama kiongozi. Aghalabu, kutofanikiwa kwake kunatokana na hatia au kosa analolitenda. Jamii inahesabu kuwa tanzia inatokea katika maisha ya kila siku kwa mfano, wakati mtu anakufa akiwa na umri mchanga, akiwa katika upeo wa maisha yake na katika umri wa makamu. Vilevile,

vifo vya watu wengi vinapotokea kutokana na ajali barabarani, ajali ya ndege au mkasa wa moto, huzua huzuni katika jamii husika.

Katika kazi za kitanzia, mhusika mkuu aghalabu huonekana kuwa na sifa zinazoakisi ushujaa. Dhana ya ushujaa imejadiliwa na wataalamu tofautitofauti katika fasihi, miongoni mwao Wamitilia (2003). Anaeleza shujaa kama mhusika mkuu katika kazi ya kifasihi ambaye anaweza kuwa wa kike au wa kiume. Anafafanua kuwa kuna aina tofauti ya shujaa; kwa mfano shujaa chanya, shujaa hasi na shujaa kinzani katika kazi za kifasihi. Maelezo yake yanaonyesha kwamba dhana ya ushujaa katika fasihi inadhihirika na suala hili linaweza kuchambuliwa kwa kuzingatia kazi teule za kifasihi. Ingawa suala la ushujaa limetafitiwa katika baadhi ya tenzi, linazua mjadala iwapo matendo yanayofikiriwa kuwa ya kishujaa ni ya kweli, ni uchawi, ni uganga ama uhayawani katika jamii?

Kulingana na Wafula na Njogu (2007) tanzia ni maigizo ya matukio yenye ujumbe mzito yanayowasilishwa kwa lugha inayonawiri, yazindue hofu na huruma ili hatimaye maigizo hayo yaripue hisia za ndani kutoka katika nafsi za hadhira. Hivyo basi tanzia ni lazima kuibua hisia, tena hisia za hofu na huruma miongoni mwa hadhira. Wafula na Njogu (khj) wanasema kuwa tanzia ina sehemu tatu muhimu: mwanzo, katikati na mwisho. Mwanzo huwa na kichocheo, katikati kilele na mwisho unashirikisha mafunzo ambayo hadhira hupata kutokana na tajriba ngumu ambazo wahusika wamepitia. Matini zilizoteuliwa kwa ajili ya utafiti huu zinaakisi maelezo ya tanzia, suala linalochunguzwa katika lengo la tatu la utafiti huu.

Achieng (2012) amechunguza sifa za mashujaa na umuhimu wao katika jamii zao kwa kulinganisha Fumo Liyongo na Lwanda Magere. Anajadili suala hilo kwa msingi wa sifa bia za mashujaa. Katika utafiti wake amechanganua wahusika kutoka katika jamii

za Kiafrika ambazo ni jamii za Kibantu (Fumo Liyongo) na Kinailoti (Lwanda Magere). Anaendeleza mada yake kwa kuzingatia misingi ya kihistoria ya jamii za Kiafrika. Achieng' anashadidia madai kuwa sifa za mashujaa kote duniani ni karibu sawa. Swali linalojitokeza hapa ni je, kigezo cha tanzia au anguko la mashujaa hao ni ishara moja ya udhaifu wa binadamu kote ulimwenguni?

Gathara (2015) ameshughulikia taswira ya jagina katika tendi kwa kulinganisha Fumo Liyongo na Nabii Isa. Ameonyesha sifa za majagina hawa na kubainisha kuwa Fumo Liyongo na Nabii Isa wana sifa zinazolingana kwa kiasi kikubwa. Ameendeleza mawazo yake kwa kuzingatia tendi ambazo ni *Utendi wa Nabii Isa* na *Utendi wa Fumo Liyongo*. Kazi yake inamrejelea Nabii Isa katika msingi wa dini ya Kiislamu na Fumo Liyongo katika msingi wa Kihistoria. Mtazamo wake ni kuwa Nabii Isa na Fumo Liyongo wana taswira inayolandana. Kazi ya Gathara ilitofautiana na kazi yetu kwa sababu Gathara analinganisha sifa za majagina wawili, Fumo Liyongo na Nabii Isa ilhali utafiti wetu umeshughulikia mwingilianomatini katika tenzi teule na *Simulizi ya Samsoni*.

Wahusika wakuu katika tendi mara nyingi husawiri sifa za kishujaa. Hata hivyo, anayedhaniwa kuwa shujaa hatimaye huonekana kuanguka kutokana na kosa fulani analolitenda. Clemence (2015) amechunguza mbinu za kitanzia za Ki-Aristotle katika *Tamthilia za Fumo Liyongo na Sundiata*. Anachambua dhamira katika tamthilia za *Fumo Liyongo na Sundiata* kwa kuongozwa na vigezo vya Aristotle vya tanzia. Kazi hii ilikuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu ilimpa mtafiti mawazo zaidi kuhusiana na tanzia katika tenzi. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kwa kiasi kikubwa kwa sababu umechunguza mbinu ya kisimulizi, sifa za wahusika na suala la kikale cha safari kwa kuzingatia nadharia za Mwingilianomatini na nadharia ya Vikale.

2.1.2.3 Maandishi kuhusu Tanzania-ramsa

Kinyume na tanzia, tanzia-ramsa ni aina ya tanzia inayoishia kwa furaha. Wamitila (2003) anaeleza tanzia- ramsa kama aina ya tanzia inayohusisha mbinu za futuhi aghalabu kwa kuisha kwa furaha. Katika hali hiyo inaweza kupatikana hasidi au mui anayejutia makosa yake na kutubu. Aidha, kunaonekana kuwepo kwa mandhari ya kilimbwende. Wamitila anaeleza zaidi kuwa tanzia-ramsa huweza pia kutumiwa kwa tanzia ambayo ina kisuko cha kuchekesha ambacho kinakuwa kama kijalizo cha msuko mkuu wa kitanzia.

Katika misingi ya ki-Aristotle, tanzia ni igizo linalosawiri mhusika mkuu, ambaye mara nyingi huwa shujaa, kama mhusika anayetenda kosa ambalo lingeweza kuepukika. Kosa hili analolitenda ndilo linalosababisha kuanguka kwake. Ingawa mhusika anapitia changamoto nyingi katika maisha yake, anaonekana kujitahidi kadri ya uwezo wake na kuibuka mshindi. Hata hivyo, ushindi huo huegemezwa kwenye uwezo wa kimiujiza unaohusishwa na miungu fulani. Kujuta kwa shujaa katika maisha kunasababisha kiini cha kimaudhui katika tanzia.

Tanzia-ramsa ni aina ya tamthilia iliyochanganya tanzia na furaha. Hili hutokea wakati mhusika mkuu anaonekana kwamba hatima yake ni kifo ila mabadiliko ya ghafla yanatokea na mwisho wake inakuwa furaha. Tofauti na tanzia, mhusika mkuu anakabiliwa na changamoto nyingi ila anajitahidi na mwishowe kuibuka mshindi. Kimsingi tanzia-ramsa ni aina ya tanzia inayoisha kwa furaha. Matukio ya kishujaa yanayohusishwa na nguli hutokea kwa njia tofauti na hali ya kawaida ya tanzia ilivyozoeleka.

Mtiririko wa matukio katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* unaakisi sifa za tanzia-ramsa. Hila za kumhadaa na kumwua Mikidadi kupitia kwa wahusika wawili, Malik

na Jabir, mwishowe hazikufaulu. Badala yake Mikidadi anakombolewa huku Malik na Jabir wakiuawa. Jambo hili linaonyesha kuwa uhalifu haulipi. Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, jitihada na bidii zinazoonekana kupitia kwa mhusika Mikidadi zina malipo mazuri.

Kutokana na maelezo yaliyotolewa, tanzia-ramsa inaweza kufafanuliwa kuwa ni mchezo wa kuigiza ulio na matukio ya kitanzia lakini matukio hayo yanageuka ghafla na kuwa ya furaha. Mageuko yanayotokea yanatokea wakati mhusika mkuu anaonekana kukata tamaa. Wakati mwingine anakuwa amewekwa tayari kwa kifo na mahasidi wake ila mambo yanageuka kuwa mazuri na kipindi hicho kinakuwa mwisho wa mchezo. Hali kadhalika, (ma)hasidi anaishia kuchekwa au kukejeliwa na hadhira kwa sababu ya hila zake ambazo zinakuja kumrudia. Wakati mwingine hasidi hufa ila haonewi huruma. Kufa kwake kunakuwa kama malipo ya matendo yake maovu.

Katika dini ya Kikristo, kisa cha kuteswa, kusulubiwa, kufa na hatimaye kufufuka kwa Yesu Kristo, kinasawiri maelezo ya tanzia-ramsa. Hisia za huruma zinampata yeyote anayesoma kisa cha kukamatwa na kusulubiwa kwake Yesu Kristo. Kitendo cha kumdhihaki na kumkejeli akiwa msalabani ni cha kusikitisha, jinsi ilivyoandikwa katika *Biblia*, vitabu vya Mariko 15:21-32 na Mathayo 27:32-40. Kufufuka kwake Yesu Kristo kulileta furaha na hivyo ushindi mkuu kwa waliomwamini ilhali mahasidi waliodhani kuwa wamemwua walifedheheshwa walipopata habari kuhusu kufufuka kwake. Tanzia-ramsa basi ni aina ya uigizaji unaosawiri matatizo na changamoto za kimaisha kiasi cha kumtamausha mhusika mkuu lakini mwisho wake unakuwa wa kufurahisha.

2.1.3 Maandishi Kuhusu Vikale

Wafula (1999) anaeleza kikale kuwa ni taswira kongwe inayojitokeza mara kwa mara katika kazi za fasihi. Anasema kuwa kikale kinapoonekana, huwasilisha dhana fulani kongwe inayopatikana katika jamii inayozungumziwa. Maelezo yake Wafula yanaashiria kwamba kuna vikale vinavyofanana na kuchukua maana sawa katika jamii mbalimbali ulimwenguni. Ingawa taswira za vikale hudhihirika kwa namna nyingi kama vile watu, majitu, maumbo na nambari, Jung (2008) aliamini kuwa vikale vyenyewe vina kikomo.

Wamitilia (2008), kwa kumnukuu Freud anasema kuwa kazi za kifasihi au tokeo la ubunifu huwa kama fantasia au njozi ya kibinafsi ya mwandishi au msanii anayehusika. Freud anataja kuwa tajriba fulani inayotokea wakati uliopo huamsha kumbukumbu fulani ya siku za utotoni katika akili ya mwandishi au msanii. Kwa njia hiyo msanii hujiwa na msukumo wa kutimiza au kutosheleza hamu au tamaa hiyo aliyokuwa nayo kwa njia ya kazi ya kifasihi. Kazi ya kifasihi kwa hiyo ni ridhio la kifantasia la ndoto fulani ya utotoni.

Wamitila anasema kuwa mkabala wa kisaikolojia unatuwezesha kufahamu mambo kadha hasa kuhusiana na sifa mbalimbali (na hasa zinazofanana) katika fasihi tofauti. Kwa mujibu wa Wamitila (2002), fasihi ina sifa bia ambazo zinaweza kulinganishwa. Anasema kuwa fasihi za jamii mbalimbali huingiliana kwa kuwa msingi wa fasihi hizo ni binadamu mwenyewe. Kwa hivyo, fasihi ya jamii mbalimbali duniani huingiliana, na kwa sababu jamii hizi zimeundwa na binadamu, mwingiliano wa aina mbalimbali hutokea.

Vikale muhimu hasa ni kama vile kuzaliwa, kufa, kuzaliwa upya, uongozi, miujiza, umoja, shujaa, mtoto, mungu, shetani, mkongwe, mama na mnyama. Kikale cha shujaa kwa mfano, hufunganishwa na safari ya jua kuanzia asubuhi, mchana hadi usiku na hili ni jambo lililo katika akili za binadamu tangu jadi. Ruwaza hii hupatikana ulimwenguni katika visakale vya shujaa anayezaliwa baharini, kuchukuliwa na miale ya jua na jioni anangojewa na mama tajika anayemwangamiza lakini anasafiri akiwa tumboni mwa jimama lile. Usiku wa manane anamwangamiza jimama lile baharini na hatimaye huzaliwa tena. Matini teule za utafiti huu zimeonyesha kuwa na mwingilianomatini kwa kuzingatia misingi ya kikale cha safari. Lengo la tatu la utafiti huu limehakiki maingiliano ya kikale cha safari katika UFL, UG, UMM na SS.

2.2 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu umetumia nadharia mseto ili kufanikisha malengo yake ya utafiti. Nadharia zilizotumika ni nadharia ya Mwingilianomatini na nadharia ya Vikale. Nadharia ya Mwingilianomatini imetumika kuhakiki malengo ya kwanza na pili huku nadharia ya Vikale ikitumika kuhakiki lengo la tatu la utafiti huu.

2.2.1 Nadharia ya Mwingilianomatini

Utafiti huu unahusu Mwingilianomatini katika *Simulizi ya Samsoni*, *Utendi wa Fumo Liyongo*, *Utendi wa Gilgamesh* na *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Matini hizi zimechanganuliwa kwa kutumia nadharia za Mwingilianomatini na Vikale. Nadharia ya Mwingilianomatini ilitumika katika uchambuzi wa vipengele vinavyozua mwingiliano wa kimatini vya kisimulizi na wahusika wakuu katika matini teule.

Nadharia ya Mwingilianomatini iliasisiwa na Julia Kristeva mwaka 1966. (Allen, 2000). Mwingilianomatini inasisitiza kuwa matini zote za kisanaa hujibizana na

kusemezana. Kwa njia hiyo, matini zenyewe hutegemeana ili kuzalisha maana. Nadharia hii ina misingi yake kwenye nadharia ya Usemezano ya Bakhtin. Katika uundaji wa nadharia ya Mwingilianomatini, Julia Kristeva aliathiriwa na mawazo ya mwanaisimu wa Uswizi Ferdinand de Saussure na mwananadharia wa Kirusi Mikhail Bakhtin. De Saussure alipendekeza kwamba lugha ichanganuliwe kimuundo kwa kuangalia uhusiano baina ya viambajengo mbalimbali vya kiisimu.

Allen (2000) anayeeleza kuwa nadharia ya Mwingilianomatini iliasisiwa na Mfaransa, Julia Kristeva, mwaka 1966 kutokana na nadharia ya Usemezano ya Mikhail Bakhtin. Katika miaka ya 1960, wataalamu wa Kifaransa waliojijhusisha na saikolojiana, walibadilishwa na wanamuundo waliokuwa wafuasi wa Ferdinand de Saussure. Baadaye kukatokea wahakiki waliopinga nadharia za Umuundo-leo (Post-structuralism). Wanamuundoleo walizingatia hasa nafasi ya lugha na isimu katika fasihi, mmoja wao akiwa ni Julia Kristeva. Kristeva anajadili kazi za Bakhtin katika makala yake "The Bounded Text" (uk.64-91). Katika kazi hii, Kristeva anajadili kazi za Bakhtin wakati ambapo kulikuwa na majadiliano makali yaliyohusiana na Umuundo na Umuundo-leo nchini Ufaransa.

Katika mjadala wake, Allen anaelezea kuwa mwingilianomatini ulitumika kwa mara ya kwanza katika kazi za Julia Kristeva za *Word, Dialogue and Novel* (1966). Kulingana na Kristeva kila matini ni matokeo ya mwingiliano wa matini nyingine. Anasema kuwa matini mpya huundwa kwa mkusanyiko wa matini nyingine tofautitofauti. Hivyo basi, mwingilianomatini ni mazungumzo au usemezano baina ya matini kadhaa.

Ingawa de Saussure na Bakhtin walizungumzia mahusiano kati ya vipengele tofautitofauti vya lugha, hakuna mmoja wao aliyetumia dhana mwingilianomatini.

Hivyo basi, wataalamu wengi wamesema kuwa Julia Kristeva ndiye mwasisi wa dhana mwingilianomatini. Davidson (1993), Allen (2000), Kehinde (2003), Wamitila (2008), Njogu na Wafula (2007), Raj (2015) na Jilala (2016) ni miongoni mwa wataalamu waliojadili masuala ya mwingilianomatini katika fasihi. Wametoa kauli jumla kwamba hakuna kazi ya kifasihi inayojitegemea bila kuwa na athari ya kazi nyingine.

Mwanzoni mwa maandishi yake katika “Discourse in the Novel”, Bakhtin anajadili kuwa wahakiki wamejikita zaidi kwenye maandishi ya kimuundo pekee na kutotilia maanani vipengele vingine vya uandishi na uhakiki. Davidson (1993) anaeleza kwamba Bakhtin alitoa ufafanuzi mpya wa maana ya riwaya na sehemu zake kuwa ni matini iliyo na uanuwai wa kimtindo na sauti mbalimbali zinazolingiliana. Bakhtin aliamini kuwa matini ya kifasihi inaweza kulinganishwa na uwanja mkubwa unaobeba sifa mbalimbali za kijamii, kiisimu, kihistoria na kiuchumi, ambazo huathiri uhakiki. Kwa misingi hiyo, mhakiki anapaswa kuzingatia sauti hizo mbalimbali na kuelewa kuwa matini zina athari za kijamii, kihistoria na kitabaka. Kutokana na mawazo ya Bakhtin, Kristeva aliunda na kuendeleza nadharia ya Mwingilianomatini.

Kristeva anapinga mtazamo wa kifasihi na matini zozote zile zinazoamini katika umoja wa maana na badala yake kusisitiza mabadiliko na ukuaji wa maana. Anaunga mkono dhana ya usemezano ya Bakhtin ingawa kwake yeye anazua dhana ya mwingilianomatini. Hata hivyo, Kristeva anaona matini kama mkusanyiko wa matini nyingi. Kwa upande wake, Bakhtin aliamini kuwa mahusiano ya lugha hutokea katika sajili maalum ya kijamii na athari baina yazo. Kwa mujibu wa Tuglu (2011), Bakhtin anaeleza kuwa matini hubadilika kila wakati kwa sababu ya hali yake ya ukuaji. Katika makala yake ‘Epic and Novel’, anaeleza kuwa riwaya ni utanzu wa kipekee unaoendelea kukua, hivyo kusemwa kwamba haujakamilika.

Nadharia ya Mwingilianomatini hurejelea dhana kuwa kazi zozote za kifasihi huhusiana kwa njia moja ama nyingine. Uhusiano huu huweza kuwa wa kimuundo, kimaudhui, usawiri wa wahusika, matumizi ya lugha na mandhari. Finnegan (1970) anapofafanua kuhusu fasihi ya Kiafrika, anasema kwamba fasihi simulizi ilichukuliwa kuwa mali ya jamii na kwamba ilipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa njia hiyo, simulizi za Kiafrika ziliathiriana na kuingiliana. Matini zilizoteuliwa kwa ajili ya utafiti huu zinaonyesha sifa ya urudiaji hivyo kuleta mwingiliano kwa namna fulani. Eagleton (1983) anashadidia mwingilianomatini katika fasihi kuwa ni matini “iliyoandikwa tena” japo kwa kutofahamu. Anasema kuwa hakuna usomaji wa matini ambayo si urudiaji wa maandishi ya matini nyingine. Mwingilianomatini huonekana kuwa ni ufafanuzi wa jambo au wazo ulioathiriwa nao.

Wataalamu waliozungumzia mwingilianomatini wanakubaliana kuwa nadharia hii inatumika kuhakiki kazi za kifasihi. Aidha, ni nadharia iliyoanzishwa na Julia Kristeva baada ya kuathiriwa na mawazo ya Mikhail Bakhtin ya Usemazano. Kule kuathiriwa kwa Kristeva na maandishi ya Bakhtin kunaonyesha kuwa binadamu wana ubia fulani ingawa mabadiliko hutokea kutegemea muktadha. Hii ndiyo sababu moja ya kusema kuwa kazi za fasihi huathiriana kwa sababu fasihi ni zao la jamii. Hivyo, nadharia ya Mwingilianomatini ni faafu katika uhakiki wa kazi za kifasihi zinazoonyesha kuwa na mfanano fulani. Anavyosema Kristeva, tunakubaliana naye kuwa kila matini ni matokeo ya mwingiliano na matini nyingine.

Tanzu za fasihi simulizi za Kiafrika zinajulikana kwa sababu ya ‘ujamaa’ wake hivi kwamba hakuna mtu anayeweza kusema kuwa ndiye mmiliki wa kazi hii tofauti na fasihi andishi. Madai haya yanachukuana na mawazo ya Finnegan (khj) kwamba fasihi simulizi za kiafrika zilichukuliwa kuwa mali ya jamii. Kehinde (2003) anaeleza kuwa ijapokuwa nadharia ya Mwingilianomatini ina misingi yake huko magharibi, ina

nafasi katika fasihi simulizi za Kiafrika. Katika uchambuzi wake, Kehinde anaonyesha kuwa mwingilianomatini katika riwaya za Kiafrika unaingiliana na fasihi simulizi. Anaonyesha umuhimu wa nadharia hii katika uchambuzi wa riwaya ya Kiafrika ya kisasa.

Miaka mingi baada ya kuasisiwa kwa nadharia ya Mwingilianomatini, wataalamu mbalimbali wameendelea kutoa maoni yao. Hii inaonyesha uamilifu wa nadharia hii katika kazi za fasihi. Njogu na Wafula (2007) wanasema kuwa nadharia hii ilizuliwa kutokana na nadharia ya Usemezano ya Mikhail Bakhtin (1895-1975). Nadharia ya Usemezano inadai kwamba matini za kifasihi ni kama sauti zinazosemezana. Hivyo, kusemezana huku kunaleta kuathiriana kwa matini moja na nyingine. Bakhtin aliamini kuwa kazi za kifasihi zina sauti mbalimbali zinazoingiliana na kupiga mwangwi katika kazi zingine zilizotangulia, zilizopo au zitakazokuja baadaye. Huu ndio msingi wa nadharia ya Mwingilianomatini.

Binadamu kote ulimwenguni hutagusana na kuathiriana kwa sababu ya mahitaji ya kijamii. Vivyo hivyo, tamaduni za jamii huingiliana na kulingana. Raj (2015) anaeleza kuwa ufasiri wa maana katika misingi ya mwingilianomatini ni lazima uzingatie uhusiano wa matini, jamii na tamaduni za kukusanya matini. Anasisitiza hoja ya Usemezano ya Bakhtin kuwa inazingatia jinsi binadamu wanavyotumia lugha katika miktadha tofauti ya kijamii ilhali Kristeva anaegemea zaidi matini na umatini. Hata hivyo, Bakhtin na Kristeva wanakubaliana kuwa matini haziwezi kutenganishwa na jamii ambayo ni msingi wa uandishi na matini. Matini kijamii (social text) na matini kifasihi (literary text) hazitenganishwi kwa kuwa zinaonekana kama nyuzi zilizofumwa pamoja. Kwa msingi huo, utamaduni wa jamii huchukua nafasi kubwa katika utunzi na ukamilifu wa kazi za kifasihi.

Nadharia ya Mwingilianomatini ni mojawapo ya nadharia inayotumika katika fasihi linganishi. Hii ni kwa sababu ya wazo kuwa kazi za kifasihi hurejelea matini nyingine zilizotangulia kwa kuibadili, kuieleza upya na kuihusisha na muktadha wa kijamii uliopo. Kutokana na mawazo ya wataalamu waliotajwa, tunakubaliana nao kwamba Mwingilianomatini ni nadharia inayotumika katika uhakiki wa kazi za fasihi simulizi na andishi. Kulingana na Jilala (2016), Mwingilianomatini kwa ujumla wake ni dhana inayorejelea uhusiano wowote unaoweza kuonekana katika matini moja na nyingine au matini zaidi ya moja. Uhusiano huu unaweza kujitokeza katika kipengele kimoja au vipengele mbalimbali kama vile fani, maudhui au hata vyote kwa pamoja. Kwa hivyo, katika uchunguzi wa kimwingilianomatini, mhakiki anapaswa kufafanua vipengele vinavyohusiana na kwa njia gani. Hivyo, nadharia hii ni bora katika uhakiki wa fasihi linganishi.

2.2.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Mwingilianomatini

Nadharia ya Mwingilianomatini inabainisha kwamba matini za kifasihi zina uhusiano wa namna fulani. Ifuatayo ni baadhi ya mihimili iliyotumika katika uchambuzi wa kazi hii.

Nadharia ya Mwingilianomatini inadai kuwa matini yoyote ya kifasihi ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingine tangulizi. Hii ina maana kuwa matini huweza kubadilishwa kutoka, kwa mfano, utanzu wa ushairi hadi utanzu wa tamthilia. Mfano mzuri ni *Utenzi wa Fumo Liyongo* (Mulokozi, 1999) unaorejelewa katika tamthilia ya *Fumo Liyongo* (Mbogo, 2009). Mbogo, amebadilisha usimulizi wa Fumo Liyongo kutoka utanzu wa ushairi hadi tamthilia, hivyo ameathiriwa na matini tangulizi katika utunzi wake. Katika utafiti huu, nadharia ya Mwingilianomatini ilitumika kuchambua namna *Simulizi ya Samsoni* na *Tenzi za Fumo Liyongo*, *Gilgamesh*, *Mikidadi* na *Mayasa* zinavyoingiliana na kufanana ama kutofautiana.

Kazi zilizochunguzwa zilitungwa katika vipindi tofauti ilhali kuna mfanano fulani. Hali hii ilimchochea mtafiti kujaribu kuchunguza na kubainisha mfanano ama ulinganifu huu kwa kuzingatia vipengele vya miktadha ya kisimulizi, sifa za wahusika na tanzia katika matini za fasihi na kidini.

Nadharia ya Mwingilianomatini huchukulia kwamba kila kazi ya kifasihi inahusiana na kazi iliyoandikwa kabla kwa namna moja au nyingine. Wamitila (2008) anaeleza kuwa njia bainifu za mwingilianomatini ni unukuzi au kudondoa, wizi wa kiuandishi na Wigobezi. Kwa njia hii, tungo za kifasihi huingiliana, huhusiana na kutegemeana ili kuzalisha maana. Mwingiliano huu wa kimatini huweza kuwa katika kiwango cha muundo, maudhui, uhusika, msuko na matumizi ya lugha. Mtafiti alichunguza mahusiano katika usawiri wa wahusika na kubainisha kwamba wahusika wakuu wanaonyesha sifa zinazofanana kwa namna fulani katika matini teule.

Mwingilianomatini inadai kuwa maana ya matini moja hutokana na matini nyingine. Ni urejelezi wa maana kwenye matini nyingine. Hivyo basi nadharia ya Mwingilianomatini ni nadharia inayofafanua hali ya matini moja au zaidi kujitokeza katika matini nyingine. Mtunzi huiumba kazi ya fasihi upya kwa kutumia malighafi iliyopo na kuongeza mabadiliko kidogo ya kimtindo au kimuundo.

Matini za fasihi huwa zinanukuu, zinageuza, zinaiga na kutafsiri kwa namna ya kurejelea matini nyingine tangulizi. Baada ya kuzisoma *Simulizi ya Samsoni* na *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa*, ilibainika kwamba kazi hizi zinafanana kwa kiwango fulani. *Simulizi ya Samsoni*, ambayo ina misingi ya kidini ya Kikristo, na *Utendi wa Fumo Liyongo*, kwa mfano, ni matini mbili tofauti ilhali kuna mwangwi unaohisika kisimulizi.

Mwingilianomatini huhusisha pia mwingiliano wa mitindo fulani ya kiusemi na misimbo fulani ambayo imesaidia katika uashiraji wa kazi za baadaye. Jilala (khj) anaeleza kuwa hakuna matini yoyote katika fasihi inayoweza kuangaliwa peke yake na kwa kujitegemea. Matini teule zilizohakikiwa katika utafiti huu zilionyesha kwamba kuna ‘Kani kitovu’ na ‘Kani pewa’ miongoni mwao. Hivyo, utafiti huu ulichunguza uingiliano wa kimtindo wa kisimulizi na uhusika ili kubainisha mwingilianomatini katika *Simulizi ya Samsoni na Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa* pamoja na *Gilgamesh*.

Mtagusano wa kijamii husababisha mtagusano wa kifasihi. Hii ni kwa sababu moja kuwa fasihi ni zao la jamii. Jamii zinapotagusana, matokeo ni kuazimana baadhi ya mila, desturi na tamaduni zao. Katika utafiti huu, mtafiti anaafikiana na wataalamu waliotangulia kuwa mwingilianomatini ni uumbaji upya wa matini nyingine. Matini zote huhusiana kwa njia moja au nyingine hivyo kutegemeana ili kuzalisha maana. Baada ya kuzihakiki matini zilizoteuliwa kwa ajili ya utafiti huu, ilibainika kwamba kuna mwanngwi fulani unaohisika katika kazi hizi. Nadharia ya mwingilianomatini ilifaa katika utambuzi wa mwanngwi huu. Ilitumika kuchambua namna *Simulizi ya Samsoni na Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa* zinavyoingiliana na kufanana ama kutofautiana. Kwa muhtasari, ifuatayo ni baadhi ya mihimili iliyotumika:

- a) Matini yoyote ya kifasihi ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingine tangulizi.
- b) Maana ya matini moja hutokana na matini nyingine.
- c) Kila kazi ya kifasihi inahusiana na kazi iliyoandikwa kabla kwa namna moja au nyingine.

- d) Mwingilianomatini huhusisha mwingiliano wa mitindo fulani ya kusemi na misimbo ambayo husaidia katika uashiraji wa kazi za baadaye.

Nadharia ya mwingilianomatini imetufaa katika kutimiza malengo ya utafiti huu. Imetumika katika uhakiki wa malengo mawili ambayo ni kufafanua mwingiliano wa kisimulizi na wahusika wakuu katika UFL, UMM, UG na SS. Nadharia hii imetuwezesha kufafanua vipengele vilivyozua mwingiliano wa kisimulizi katika matini teule. Ilibainika kwamba visa vya Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa pamoja na Samsoni vinaonyesha mwingiliano wa matini kwa kuzingatia mtiririko wa matukio yanayojitokeza katika matini teule. Aidha, nadharia hii ilituwezesha kuonyesha mwingiliano wa kimuundo katika matini teule. Imetusaidia kutambua uwiano wa vipashio vya matumizi ya lugha kama vile tashbihi, balagha, taswira na matumizi ya barua katika matini teule.

Kadhalika nadharia hii imetumika kuhakiki mwingiliano wa sifa za wahusika katika matini teule. Nadharia ya mwingilianomatini imetuwezesha kuonyesha sifa za wahusika wakuu katika UFL, UG, UMM na SS na kubainisha kuwa matini za fasihi huwa zinarejelea kwa kunukuu, kuigeuza, kuiga na kutafsiri matini nyingine tangulizi. Wahusika wakuu, ambao ni Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Samsoni wamesawiri sifa za ukatili, uongozi, ushujaa, majigambo na sifa ya kitanzia. Miktadha iliyosababisha sifa hizo kutokea ilifanana kwa kiasi fulani. Kutokana na maelezo hayo, ni dhahiri kuwa uhakiki wa matini teule unaakisi mwingilianomatini baina yazo hivyo kuonyesha ufaafu wa nadharia hii katika utafiti huu.

2.2.2 Nadharia ya Vikale

Nadharia ya vikale inahusu ubia wa ishara na visasili mbalimbali kote ulimwenguni. Nadharia hii ina misingi yake katika kazi za mwanasaikolojia Sigmund Freud (1856-

1939). Sigmund Freud alijaribu kuelewa tabia fulani za binadamu. Katika kufanya hivyo, aliibuka na nadharia ya kisaikolojia ili kudadisi zaidi kuhusu tabia za kiajabu zilizojitokeza baina ya wagonjwa wa kiakili aliokuwa nao. Baada ya uchunguzi wa kina, Freud aliona kwamba tabia zingine zilizojitokeza ilikuwa kwa sababu ya athari ya tajriba za utotoni. Alizindua mbinu za kumsaidia mgonjwa (wa kiakili) kusema wazi aliyoyapitia. Sigmund Freud alifanya kazi na wanaisimu-nafsia ili kusaidia wagonjwa kusema kwa uwazi tajriba zao za utotoni, ndoto zao na matendo ya kustaajibisha yaliyokuwa yamewekwa katika akili-laza zao. Dobie (2002), anasema kuwa mawazo yao yanapotumikizwa katika fasihi, uhakiki hufanyika kwa kuzingatia mada na mbinu ili kulinda msingi wa kuhakiki matini za kifasihi.

Pamoja na wafuasi wengine wa Freud ni Carl Jung (1875-1961). Gijo na George (2021) wanataja kuwa Jung alianzisha dhana ya vikale katika kitabu chake “The Spirit in Man, Art and Literature” mwaka 1922. Wanaeleza kuwa Jung alikuwa mwanafunzi wa Freud na mwanafalsafa wa kwanza kuipa uzito dhana ya vikale. Kwa mujibu wa Dobie (khj), Jung aliamini kuwa akili-laza ya binadamu inaathiri na kuongoza pakubwa hulka yake. Jung anasema kwamba kuna mawazo ya kikale ya binadamu wa sasa ambayo yanafanana na mawazo ya kale ya binadamu wa awali. Jumla ya mawazo haya ya kikale yaliyomo kwenye akili-laza za binadamu, ndiyo anayorejelea Jung kama vikale. Ruwaza hizi za kivikale hujitokeza kupitia ndoto, matambiko ya kidini, sanaa na fasihi. Ni njia ya kusema kuhusu vikale vya kibinadamu. Kulingana na Jung, vikale hivi ni daraja kati ya akili-laza na akili-tambuzi. Kwa njia hii, anavyosema Jung, binadamu anaweza kuishi maisha makamilifu kwa kuunganisha yaliyomo kwenye akili-laza na akili-tambuzi. Anajadili kuhusu ruwaza za kivikale kwamba zinawekwa katika makundi matatu ambayo ni;

- i) Kivuli (The shadow)

ii) Anima (The anima/ animus)

iii) Pasona (The persona)

Dhana hizi vilevile zinajitokeza katika fasihi. Kivuli ni sehemu ya maisha ya binadamu iliyo na matendo hasi ambayo kwayo mhusika hapendi kuhusishwa nayo, kwa mfano matendo yanayohusishwa na shetani. Anima ni sehemu ya ‘ndani’ inayoonyesha hulka ya mtu binafsi. Ni taswira ya kiume (anima) au uke (animus) ambayo pia inaweza kuonekana kupitia kwa hulka ya mtu yeyote. Pasona ni taswira yetu binadamu jinsi inavyoonekana na watu wengine. Jung hivyo basi anasema kwamba ni lazima binadamu kuwa na mizani ya kiasi, hivi kwamba tujikubali jinsi tulivyo hata kama kuna sifa hasi ambazo tusingependa kuhusishwa nazo. Kwa njia hiyo, ndoto huwa kifaa muhimu katika kusuluhisha migogoro inayojitokeza katika maisha ya kila siku ya binadamu.

Njogu na Wafula (2007) wakimnukuu Jung (1972), Cuddon (1997) na Wamitila (2001) wanadai kuwa Jung alichukulia kikale kama aina ya mtiririko au picha kongwe iliyojitokeza mara kwa mara katika tajriba anayopitia mwanadamu. Maoni ya Jung ni kwamba ijapokuwa utu wa mtu ni wa kibinafsi, mtu huyo huathiriwa na jamii inayomzunguka, na kwamba mtu na utamaduni wake ni nakala ya wanadamu wengine waliokuwepo miaka mingi iliyopita. Katika fasihi, mtunzi huonyesha utu wake, mambo anayoyapenda na mambo anayoyachukia kupitia vikale.

Joseph Campbell (1904-1987) anaendeleza mawazo ya Jung ya vikale kwa kurejelea motifu ya safari. Campbell anaonyesha ulinganifu baina ya mashujaa ulimwenguni. Anaendeleza uhakiki wa kivikale katika kitabu chake “Hero with a Thousand Faces.” Anaendeleza kuwa kihistoria kuna mawazo fulani ya vitendo vya mashujaa ambavyo vinajitokeza katika hadithi za vikale kote duniani. Anadai kuwa kuna mshikamano na mfanano wa visasili na ngano katika sehemu mbalimbali za kijiografia, nyakati

mbalimbali za kihistoria na tamaduni mbalimbali kote ulimwenguni. Campbell aliamini kuwa vikale vina ubia kwa sababu vinatokana na jumla ya mawazo yaliyomo kwenye akili za binadamu. Kikale cha safari kinaonyesha kuwa kuna maudhui yanayolingana na kufanana katika jamii mbalimbali duniani. Kwa sababu hiyo, inaweza kusemwa kuwa huenda kuna shujaa mmoja wa kikale ila simulizi yake imerudiwarudiwa katika nchi mbalimbali na watu wengi.

Kikale cha safari kinaashiria maisha ya shujaa kuanzia utotoni hadi kufa kwake. Kwa kawaida, maisha ya binadamu huwa na hatua tano kuu: kuzaliwa, utotoni, ujana, utuzima na kifo. Hata hivyo, shujaa huwa na changamoto nyingi maishani, jambo linalofanya dhana ya maisha kuwa pana. Matendo ya mhusika yanavyojitokeza katika safari, yanasawiri maisha yake kuanzia utotoni hadi kifo. Hadithi nyingi zina elementi za kimuundo zinazopatikana katika ndoto, visasili na ngano. Mwanasaikolojia na mtafiti wa vikale, Campbell (khj), katika utafiti wake aligundua motifu zinazopatikana katika hadithi za kishujaa na hadithi zingine kote ulimwenguni. Aligundua hatua tofautitofauti za kimsingi zinazopitiwa na shujaa katika tamaduni mbalimbali. Muundo huu ndio anaouita Kikale (The Monomyth).

Mhakiki mwingine aliyeathiriwa na Campbell ni Vogler (2007). Vogler anatumia mawazo ya Campbell kuandika na kutayarisha filamu zake hadi sasa. Vogler ndiye mshauri mkuu wa kikundi cha usanii cha *Hollywood*. Hii inaonyesha kwamba nadharia ya Campbell ni amilifu hivi kwamba athari yake ingali inahusika katika kazi za kisanii za Karne hii ya Ishirini na Moja. Campbell aliathiriwa pakubwa na Jung (1959) ambaye nadharia yake *The Collective Unconscious* ilihusika. Wafuasi mbalimbali wameeleza hatua za Kikale cha Safari kwa njia tofauti ila kuna hatua za kimsingi zilizozeleka. Vogler, ameorodhesha hatua kumi na mbili zinazofuatwa na

shujaa kutoka kwa hatua kumi na saba za mwanzo zilizotumikizwa na Campbell. Hatua hizi zinaonekana kurudiwarudiwa katika visasili mbalimbali ulimwenguni.

Miyamoto (2020) anaeleza kuwa safari ya shujaa ni muundo unaohitaji kuongezewa matukio mengine ya kipekee kulingana na kila hadithi. Hatua hizi vilevile huenda zikaondolewa ama kuongezwa pasipo kuathiri kisa cha kikale chenyewe.

1) Ulimwengu wa Kawaida (The Ordinary World)

Shujaa anaonekana akiwa na sifa tofauti na wale wanaoishi katika dunia halisi. Wanaodhamiriwa kuwa shujaa wanaonekana kuwa na sifa zinazowafanya kujiona tofauti na watu wengine.

2) Mwito wa Ziara (The Call to Adventure)

Ili shujaa aweze kuanza safari yake, ni lazima ajitenge na dunia halisi. Anaondolewa katika mazingira yake ya kawaida. Ulimwengu unaoingwa na shujaa ni tofauti. Campbell anataja ulimwengu huu kwamba huweza kuwa hatari au wa kufanikisha. Shujaa anahitajika kuenda katika nchi ya mbali, msitu, ufalme chini ya ardhi, ziwani, mlimani au kuwa katika hali ya ndoto. Ulimwengu huu huwa na watu wasio wa kawaida, matendo ya kiajabu na ya kutoaminika. Hata hivyo, shujaa anakabiliwa na tukio, mgogoro au changamoto inayoanzisha msako wa safari yake.

3) Kukataa Mwito wa Ziara (Refusal of the Call)

Shujaa anakataa kuitikia mwito wa safari kutokana na uoga, ukosefu wa usalama na changamoto zozote zinazomkabili. Mhusika anaona afadhali kubaki katika ulimwengu wake wa kawaida kuliko kuanza safari ya kuelekea kusikojulikana. Hatua hii ni muhimu katika uwasilishaji wa hatari zinazomngoja shujaa katika ziara inayotarajiwa.

4) Kukutana na Mshauri (Meeting the Mentor)

Shujaa anakutana na mshauri ambaye anampa wosia, maneno ya hekima, ujumbe maalum au zana zozote muhimu kwa ajili ya safari inayomsubiri. Mshauri huyu anaanzisha uhusiano wa kipekee na mhusika mkuu (shujaa) na wahusika wengine.

5) Kivuko cha Kizingiti (Crossing the Threshold)

Hatua hii inaashiria kwamba shujaa ameanza safari yake na yuko tayari kuvuka mlango unaotenganisha ulimwengu wa kawaida na ulimwengu mpya. Inabidi shujaa akabiliane na tukio lenye nguvu za kiajabu kusudi aingie katika ulimwengu mpya maalum ambapo hakuna nafasi ya kurudi nyuma.

6) Majaribu, Marafiki na Maadui (Tests, Allies and Enemies)

Baada ya kuvuka kizingiti na kuingia katika ulimwengu mpya, shujaa anapata majaribu, anakutana na marafiki na maadui vilevile. Katika hatua hii, shujaa anahitaji kutambua ni nani kati ya marafiki wake anaweza kuaminika. Shujaa aidha anajifunza kanuni na sheria za ulimwengu mpya.

7) Kuelekea Pangoni (Approach to the Inmost Cave)

Katika hatua hii, shujaa anapaswa kujitayarisha kwa makabiliano ya hofu na migongano inayomwandama. Pango hapa huenda ikawa ni mahali halisi ambapo hofu, hatari na changamoto nyingi zinatokea au hali ya mvutano wa kihisia inayotatanisha ilhali ni hali iliyotarajiwa kutokea ili shujaa akabiliane nayo. Ni hatua inayosababisha wasiwasi na taharuki miongoni mwa hadhira iwapo shujaa ataweza kuikabili changamoto inayomkumba au la.

8) Tatizo (The Ordeal)

Hatua hii inamwonyesha shujaa akikabiliana na tatizo lake kuu katika safari. Hadithi ya shujaa imefikia nusu na tatizo analokabiliana nalo linaonekana kuwa kilele japo

sivyo. Katika hali hiyo, shujaa anashushwa moyo. Katika hatua hii, washauri wa karibu wa shujaa huuliwa na kumweka shujaa katika hali ya kusononeka. Hata hivyo, anang'ang'ana na tatizo au maadui wake na mwishowe kuibuka mshindi.

9) Kutuzwa (The Reward)

Baada ya kukabiliana na hatari ya kifo na kushinda, shujaa anahitaji kupokea tuzo. Tuzo hii ni muhimu kwake ili kumpa nguvu zaidi anapokabiliana na changamoto za mwisho katika safari yake. Shujaa anaweza kutuzwa kwa njia mbalimbali kama vile kupata zana ya kiajabu, tajriba ya kiajabu, dawa ya kiajabu (elixir), hekima na maarifa zaidi au kuwa na upatanisho, kwa mfano na mpenzi. Hatua hii ni muhimu kwa sababu humpa moyo shujaa baada ya kukabiliana na hatari nyingi katika safari yake.

10) Kurudi Nyuma (The Road Back)

Shujaa anarudi katika ulimwengu wa kawaida. Hatua hii inajengwa kwa kumwonyesha shujaa akiwa katika mapambano makali yanayomsukuma kuamua kurudi katika ulimwengu wake wa kwanza (wa kawaida). Ingawa anaona matumaini ya kukamilisha azma yake, kwa mara ya kwanza anakabiliwa na changamoto hatari zaidi. Hii ni hatua inayofafanua (mambo) yote yaliyo hatarini huku safari ya shujaa ikielekea kufikia kileleni. Ni hatua inayomfanya shujaa, msomaji na hadhira kutafakari kuwa safari/igizo linafikia mwisho hivyo kujitayarisha kwa mapigano makali zaidi.

11) Ufufuo (The Resurrection)

Hatu hii ni kilele cha safari ya shujaa. Shujaa anapokamilisha mapambano yake makali, anaibuka akiwa mwenye sifa tofauti, baada ya kutoka katika ulimwengu wa kifo. Shujaa anazaliwa upya kwa sababu ya mabadiliko yaliyomfanyikia. Anapata sifa nyingine zinazomfanya kuwa tofauti. Katika hatua hii, shujaa anaonyesha tofauti kwa

kukubali kujitoka kama kafara ili kuokoa watu wake walio katika ulimwengu wa kawaida. Hapa ndipo shujaa anaonyesha ushujaa wake kwa kuwaokoa watu walio hatarini pasipo kujali hatari ya kifo inayomkabili.

12) Kurudi na Zawadi (Return with the Elixir)

Hii ni hatua ya mwisho iliyo na tuzo kwa shujaa. Shujaa amepata ufufuo, amezaliwa upya hivyo kupata kibali cha kurudi katika ulimwengu wa kawaida na kuigawa zawadi aliyopata safarini mwake. Zawadi hii huenda ikawa ni kitu cha thamani kubwa au uchawi (magical potion). Aidha, huenda ikawa ni mapenzi, hekima au tajriba ya maisha katika ulimwengu wa kipekee alioupitia. Hatua hii ya kurudi katika ulimwengu wa kawaida inamwezesha msomaji kuona mwisho wa safari au maisha ya shujaa. Hatua hii basi inakamilisha duara ya safari ya shujaa. Kikale cha safari ya shujaa huchukua muundo huu wa kimsingi japo si lazima kila shujaa kupitia hatua kumi na mbili zilizoordheshwa. Vogler (2007) anaeleza kuwa muundo huu ni wa kimsingi tu na huhitaji kujengwa kutegemea kila hadithi. Aidha, hatua za safari si lazima kufuatana moja kwa moja bali huenda kukatokea tofauti chache pasipo kuboronga na kupoteza uzito au nguvu ya kikale chenyewe.

2.2.2.1 Mihimili ya Nadharia ya Vikale

Kutokana na mawazo ya wafuasi wa nadharia kama vile Jung, Frye, Rank na Campbell, mihimili ya nadharia ya vikale ifuatayo inadhihirika:

- a) Vikale ni ishara bia zilizoenea hivyo kutambulika katika kazi zote za kisani.
- b) Kazi ya sanaa hutokana na maudhui, wahusika na taswira zinazorudiwarudiwa katika matini.
- c) Binadamu kote ulimwenguni wana ruwaza za kivilikale zinazofanana.
- d) Ishara za kijazanda zinazotumiwa na binadamu zina maana sawa.

- e) Kuna ubia katika fasihi, dini, anthropolojia na saikolojia ya binadamu kote ulimwenguni.

Utafiti huu umetumia nadharia ya vikale kuhakiki ulinganifu na mfanano wa kikale cha safari katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh na Simulizi ya Samsoni*.

Ingawa kikale cha safari ya shujaa huonekana kuwa ya kijadi, ni muhimu katika uelewa wa fasihi na tajriba za maisha ya kila siku ya binadamu. Aidha, husaidia kunoa ubongo wa binadamu, kutatua changamoto za kimaisha na kuthamini hatua mbalimbali katika maisha ya binadamu. Nadharia hii imetumika katika uhakiki wa lengo la tatu la utafiti huu. Imetumika hasa kujibu vipi ubia wa kikale cha safari ulivyobainishwa katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh na Simulizi ya Samsoni*?

2.3 Hitimisho

Sura hii imehakiki mapitio ya maandishi ya wataalamu mbalimbali na misingi ya nadharia zilizoongoza utafiti huu. Nadharia zilizotumiwa ni Mwingilianomatini na nadharia ya Vikale. Tumefafanua nadharia hizi kwa kuangazia mawazo ya wataalamu mbalimbali. Nadharia ya Mwingilianomatini imetumika kujibu maswali ya kwanza na pili ya utafiti na kubainisha kwamba kuna mwingilianomatini katika matini zilizoteuliwa kwa ajili ya utafiti huu. Nadharia ya Vikale ilitumika katika uhakiki wa lengo la tatu na kuonyesha ubia wa kikale cha safari katika fasihi. Sura inayofuata inashughulikia mbinu za utafiti.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Katika sura ya pili tulihakiki maandishi yaliyoandikwa kuhusu mada na kufafanua nadharia iliyotumika katika utafiti huu. Sehemu hii inaelezea mbinu za utafiti zilizotumika katika kukusanya na kuchanganua data. Aidha, inaelezea kuhusu eneo la utafiti, sampuli na hatimaye kuelezea njia za uwasilishaji wa matokeo ya utafiti huu.

3.1 Mbinu za Utafiti

Katika tafiti zozote na hasa za kitaaluma, mbinu zilizotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data ni muhimu. Mbinu za utafiti ni njia zinazotumiwa na mtafiti kukusanya na kuchanganua data kwa lengo la kufanikisha malengo yake ya utafiti. Utafiti huu ulitumia mbinu ya maktabani iliyohusisha usomaji wa majarida, magazeti na vitabu mbalimbali vilivyokuwa na data muhimu ya utafiti. Mbali na kuhakiki maandishi teule ya utafiti, mtafiti vilevile alitumia rejeo za mtandaoni kwa kutumia 'google' na kuyasoma maandishi mengine ya fasihi yaliyohusiana na mada ya utafiti.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu unahusu *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni* katika *Biblia*. Mtafiti amesoma kazi mbalimbali zinazohusu tenzi teule na matini za kidini na kuchunguza kwa makini matini teule ili kudadisi suala la mwingilianomatini katika vipengele vya kisimulizi, sifa za wahusika na kikale cha safari. Kombo na Tromp (2006) wanasema kuwa kimsingi, utafiti unaweza kufanywa maktabani au nyanjani.

Utafiti huu ni wa maktabani. Utafiti wa maktabani unahusika zaidi na ukaguzi wa matini mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti. Data za msingi zimepatikana

katika kazi teule ilhali data za upili zimepatikana katika vitabu, tasnifu, maandishi na majarida mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti huu.

3.3 Sampuli

Sampuli ya utafiti huu ni simulizi nne; tatu zikiwa tenzi na moja ikiwa ni matini ya kidini kutoka kwa *Biblia*. Uteuzi huu umetumia mbinu ya sampuli ya kimaksudi. Tumetumia uteuzi wa aina hii kwa kurejelea malengo na mada ya utafiti huu inayohusu mwingilianomatini katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa* na *Simulizi ya Samsoni*. Matini hizi ziliteuliwa kimaksudi kulingana na malengo ya utafiti huu.

Matini ya kidini, *Simulizi ya Samsoni* kutoka *Biblia* vilevile iliteuliwa kimaksudi kwa sababu ya uwiano wake na tenzi teule. Hii ilitokana na usomaji tangulizi uliofanywa na mtafiti kabla ya kuanza utafiti huu. Mtafiti amesoma kwa makini *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa* na *Simulizi ya Samsoni* ili kuimarisha hoja na kauli zake na kubainisha mwingilianomatini unaodhihirika.

3.4 Ukusanyaji wa Data

Mbinu ya uchambuzi wa yaliyomo ilitumika kukusanya data. Kwa kuzingatia malengo ya utafiti ya kufafanua mbinu ya kisimulizi, kuonyesha mwingiliano wa sifa za wahusika wakuu na kuhakiki maingiliano ya motifu ya safari, mtafiti alikusanya data ili kubainisha udhihirikaji wa mwingilianomatini katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni*. Mtafiti alisoma maandishi teule, majarida, vitabu malimbali vya fasihi na rejea muhimu za mtandaoni ili kupata data iliyolingana na malengo ya utafiti. Kwa kurejelea matini teule, mtafiti amenakili vipengele muhimu vinavyohusiana na mbinu ya kisimulizi, sifa za wahusika wakuu na kikale cha safari. Ili kupata maelezo zaidi kuhusu tendi, mtafiti amezingatia

maandishi mbalimbali kwenye maktaba. Vilevile, mtafiti amesoma kazi zinazohusiana na mada ya utafiti huu mtandaoni.

Maelezo kuhusu *Simulizi ya Samsoni* ilipatikana katika *Biblia Takatifu*, kitabu cha Waamuzi sura za kumi na tatu hadi kumi na sita. Vifungu vya maneno vinavyohusiana na usmulizi, sifa za wahusika wakuu na kikale cha safari vilidondolewa. Data inayohusiana na Fumo Liyongo ilipatikana katika *Utendi wa Fumo Liyongo* kama ulivyotungwa na Muhammad Kijumwa katika *Tenzi Tatu za Kale* (Mulokozi, 1999). Aidha, beti zilizokuwa na habari kuhusu mwingiliano wa kisimulizi, uhusika na kikale cha safari zilinakiliwa.

Usimulizi wa Mikidadi na Mayasa ulirejelewa kutoka *Utendi wa Mikidadi na Mayasa. Utendi wa Gilgamesh* tafsiri ya Kiingereza ya Kovacs (1998) ambayo ni nakala ya mtandaoni ulitumika kudondoa hoja zote zilizohusiana na mhusika mkuu Gilgamesh na simulizi yenyewe. Mtafiti alinakili hoja zinazohusiana na mbinu ya kisimulizi, sifa za wahusika wakuu na kikale cha safari kutoka katika matini teule na hatimaye kuchambua kwa kuoanisha na malengo ya utafiti huu.

3.4.1 Mwingiliano wa Mbinu ya Kisimulizi katika UFL, UMM, UG na SS

Lengo la kwanza katika utafiti huu lilikuwa kuchanganua mwingiliano wa kisimulizi katika *tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni*. Mbinu ya kisimulizi ilionyesha uwiano wa kimatini katika matini teule. Ili kutimiza mahitaji ya lengo la kwanza la utafiti huu, mtafiti ametumia baadhi ya maneno, vifungu vya aya na beti kuonyesha mwingiliano wa kisimulizi kama ilivyobainishwa katika matini teule. *Utenzi wa Fumo Liyongo* una jumla ya beti mia mbili thelathini na mbili (232). Kati ya beti hizi, mtafiti ameteua beti ishirini (20)

ambazo zinaonyesha usimulizi katika kisa cha Fumo Liyongo. Beti hizo zimeonyeshwa katika sehemu ya viambatisho katika utafiti huu.

Utenzi wa Mikidadi na Mayasa una jumla ya beti mia saba sabini na nane (778). Kati ya hizi beti, mtafiti ameteua beti thelathini na saba (37) ambazo ziliakisi lengo la kwanza la kufafanua mwingiliano wa kisimulizi katika matini husika. *Utenzi wa Gilgamesh* umenakiliwa katika Vibao (Tablets) kumi na moja (11) badala ya beti kama zilivyo *Tenzi za Fumo Liyongo na Mikidadi na Mayasa*. Hivyo, uteuzi wa data iliyohusika na mbinu ya kisimulizi ulifanywa kimaksudi kwa kuteua vifungu kumi na tano (15) viliyokuwa na mistari kadha iliyoendana na lengo la kwanza katika kila Kibao. Mistari hii imeonyeshwa katika kurasa za viambatisho vilivyomo sehemu ya mwisho ya utafiti huu.

Data iliyohusiana na *Simulizi ya Samsoni* vilevile iliteuliwa kimaksudi. SS ilipatikana katika *Biblia*, kitabu cha Waamuzi sura za kumi na tatu hadi kumi na sita (13-16). Katika sura hizi, vifungu ishirini na moja (21) vya mistari iliyowiana na mbinu ya kisimulizi viliteuliwa.

3.4.2 Sifa za Wahusika Wakuu katika UFL, UMM, UG na SS

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa kuonyesha mwingiliano wa sifa za wahusika wakuu katika matini teule. Mtafiti alifanikisha lengo hili kwa kuteua data mahususi kutoka beti ishirini na saba (27) katika UFL. Beti hizi zilikuwa muhimu katika kuonyesha taswira ya mhusika mkuu, Fumo Liyongo na kumlinganisha na wahusika Mikidadi katika UMM, Gilgamesh katika UG na Samsoni katika SS. Beti zilizochambuliwa zimeonyeshwa katika kurasa za viambatisho.

Katika UMM, mhusika mkuu aliyechunguzwa ni Mikidadi, kwa lengo la pili la kuonyesha mwingiliano wa sifa za wahusika wakuu katika matini teule. Mtafiti

aliteua beti thelathini na mbili (32) ambazo zimeambatishwa katika sehemu ya viambatisho. Beti hizi zilibainisha mwingiliano wa sifa za mhusika Mikidadi na wahusika Fumo Liyongo, Gilgamesh na Samsoni katika matini teule. Baadhi ya sifa za Mikidadi zilizobainishwa ni ukatili, ushujaa, majigambo na tanzia.

Utenzi wa Gilgamesh una mhusika mkuu Gilgamesh, akiwa na rafiki yake wa karibu, Enkidu. Katika kuhakiki mwingiliano wa wahusika, mtafiti aliteua vifungu kumi na nane (18) vyenye mistari mbalimbali kutoka Vibao I, II, III, V, na VI katika kurasa zilizoonyeshwa kwenye ukurasa wa viambatisho. Vifungu hivi vilionyesha mhusika mkuu Gilgamesh akiwa kiongozi dhalimu, muuaji, katili na hali kadhalika, shujaa.

Vifungu vilivyoteuliwa katika SS vya kubainisha mwingiliano wa sifa za wahusika wakuu katika matini teule ni vifungu vya mistari kumi na mitatu (13). Vifungu hivi viliteuliwa kutoka *Biblia*, kitabu cha Waamuzi sura za kumi na tatu hadi kumi na sita na kuambatishwa katika kurasa za viambatisho. Vifungu vya mistari iliyohakikiwa vilionyesha Samsoni akiwa mhusika aliye na hasira, anayejigamba, muuaji na shujaa.

3.4.3 Maingiliano ya Motifu ya Safari katika UFL, UMM, UG na SS

Katika UFL, UMM, UG na SS mtafiti alizingatia lengo la tatu la kuhakiki maingiliano ya motifu ya safari katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni*.

Beti kumi na sita (16) zinazodhihirisha kikale cha safari katika UFL ziliteuliwa na kuambatishwa katika sehemu ya viambatisho. Beti hizi zinaelezea safari inayohusishwa na mhusika mkuu, Fumo Liyongo, na jinsi anavyokabiliana na changamoto anazokutana nazo safarini.

Mtafiti aliteua beti kumi na tisa (19) katika UMM zilizohakikiwa ili kubainisha lengo la tatu katika utafiti huu. Kupitia beti hizi, motifu ya safari ilibainika kuwa moja ya vikale vinavyotumika katika jamii za binadamu ulimwenguni. Mistari iliyoteuliwa katika UG kwa kusudi la kufanikisha lengo la tatu la utafiti huu ilitoka katika vibao kumi (10) ambavyo ni I:1, I:6, III:13, IV:14, VI:22, VI:23, VI:24, XI:50, XI:52, XI:50(b). Mistari kutoka kila kibao imeambatishwa katika kurasa za viambatisho. Uchunguzi wa data hii ilionyesha kuwa kikale cha safari kinabainika katika UG sawa na UFL, UMM na SS.

Katika SS, vifungu vitano (5) vya mistari viliteuliwa kimaksudi kwa kuzingatia lengo la tatu la kuhakiki maingiliano ya motifu ya safari katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni*. Vifungu hivi vimeorodheshwa katika kurasa za viambatisho katika sehemu ya mwisho ya utafiti huu. Uchunguzi wa vifungu vilivyoteuliwa ulionyesha kuwa mashujaa Fumo Liyongo, Mikidadi, Gilgamesh na Samsoni wanasawiri mfanano wa hatua mbalimbali zinazobainishwa katika motifu ya safari ya shujaa kote ulimwenguni.

3.5 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data ulifanywa kulingana na malengo ya utafiti ambayo ni kuchanganua mwingiliano wa kisimulizi, kuhakiki mwingiliano wa sifa za wahusika wakuu na kuhakiki maingiliano ya motifu ya safari katika matini teule. Katika sura za uchambuzi wa data, mtafiti ameonyesha madondoo kadhaa ambayo yalitumika kuhakiki hoja fulani kwa lengo la kuyatimiza malengo na kuyajibu maswali ya utafiti huu. Data iliyokusanywa ni beti na vifungu vya mistari mbalimbali vilivyohusiana na mbinu za kisimulizi, sifa za wahusika wakuu na hali kadhalika kikale cha safari katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa* na *Simulizi ya Samsoni*.

Mtafiti alichunguza kitabu cha Waamuzi sura za kumi na tatu hadi kumi na sita katika *Biblia Takatifu* ili kupata data iliyohusiana na usimulizi, wahusika na kikale cha safari katika *Simulizi ya Samsoni*. Vifungu mahususi vya mistari vilichunguzwa na kulinganishwa na beti mahususi katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa* pamoja na *Gilgamesh* ili kutathmini mwingiliano wa kimatini katika matini zilizotajwa.

3.5.1 Mihimili ya Nadharia ya Mwingilianomatini

Data iliyokusanywa ilihakikiwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia za Mwingilianomatini. Baaadhi ya mihimili iliyotumika katika nadharia ya Mwingilianomatini ni:

- a) Matini yoyote ya kifasihi ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingine tangulizi.
- b) Maana ya matini moja hutokana na matini nyingine.
- c) Kila kazi ya kifasihi inahusiana na kazi iliyoandikwa kabla kwa namna moja au nyingine.
- d) Mwingilianomatini huhusisha mwingiliano wa mitindo fulani ya kiusemi na misimbo ambayo husaidia katika uashiraji wa kazi za baadaye.

Nadharia ya Mwingilianomatini inadai kuwa matini yoyote ya kifasihi ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingine tangulizi. Matini teule zilichunguzwa ili kubainisha dai hili. Mtafiti alichunguza iwapo kuna mabadiliko ya aina yoyote katika mpangilio ama msuko wa kazi teule. Mhimili huu ulitufaa katika uchanganuzi wa kisimulizi kwa kuzingatia mtiririko wa matukio yanayotokea katika matini teule.

Mhimili kuwa kila kazi ya kifasihi inahusiana na kazi iliyoandikwa kabla kwa namna moja au nyingine ulitumika kuhakiki na kubainisha mwingiliano wa sifa za wahusika

wakuu katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa* na *Simulizi ya Samsoni*. Matini zilionyesha mfanano wa sifa za wahusika wakuu katika matini teule za utafiti huu. Kwa misingi hiyo, matini za kifasihi huingiliana na kutegemeana hivyo kubadilika sawa na binadamu anayebadilika kila wakati. Kwa sababu hiyo, maana ya matini moja hutokana na matini nyingine.

3.5.2 Mihimili ya Nadharia ya Vikale

Mihimili ya nadharia ya Vikale ifuatayo ilitumika ili kufanikisha lengo la tatu la utafiti huu:

- a) Vikale ni ishara bia zilizoenea hivyo kutambulika katika kazi zote za kisanii.
- b) Kazi ya sanaa hutokana na maudhui, wahusika na taswira zinazorudiwarudiwa katika matini.
- c) Binadamu kote ulimwenguni wana ruwaza za kivikale zinazofanana.

Utafiti huu umetumia nadharia ya vikale kuhakiki ulinganifu na mfanano wa kikale cha safari katika UFL, UMM, UG na SS. Kikale cha safari kilibainika katika matini teule za utafiti huu. Visa vya wahusika wakuu katika UFL, UMM, UG na SS vilithibitisha madai ya mhimili kuwa vikale ni ishara bia zilizoenea hivyo kutambulika katika kazi zote za kisanii. Aidha, binadamu kote ulimwenguni wana ruwaza za kivikale zinazofanana. Kwa sababu hiyo, mihimili hii ilitufaa katika uhakiki wa hatua mbalimbali za safari zilizoshuhudiwa na wahusika wakuu katika matini teule za utafiti huu. Utafiti huu umeonyesha mwangwi wa kifasihi ambao unahisika kupitia vipengele vya kisimulizi, uhusika na kikale cha safari. Utafiti ulichunguza madai hayo ili kubainisha ukweli uliopo. Mtafiti ameonyesha kuwa mwingiliano katika vipengele vya kisimulizi, sifa za wahusika na kikale cha safari

vinadhihirika. Baada ya kusoma, kuhakiki na kuelewa yaliyomo katika matini zilizoteuliwa kwa ajili ya utafiti huu, mtafiti alitumia njia ya maelezo kuzichambua data husika.

3.6 Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti

Data zilizokusanywa ziliratibiwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Uwasilishaji wa matokeo ulifanywa kwa kuongozwa na malengo ya utafiti. Maelezo haya yalizingatia uchanganuzi wa mbinu ya kisimulizi na ulinganishi wa sifa za wahusika wakuu kama inavyosawiriwa katika matini teule. Aidha, utafiti ulionyesha kikale cha safari kama ishara bia katika jamii za binadamu kote ulimwenguni. Ripoti ya utafiti imewasilishwa kwa kutumia maandishi yaliyoambatana na maelezo ya kiufafanuzi katika sura mbalimbali za utafiti huu.

3.7 Hitimisho

Katika sura ya tatu tumefafanua mbinu za utafiti zikiwemo eneo la utafiti, ukusanyaji wa data, sampuli, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Kazi mahususi zilizochunguzwa katika utafiti huu ni *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa* na *Simulizi ya Samsoni*. Sura inayofuata inahakiki mwingiliano wa kisimulizi kwa kujadili mbinu za kisimulizi na vipengele vya lugha vilivyotumika katika matini teule.

SURA YA NNE

MWINGILIANO WA KISIMULIZI KATIKA *TENZI ZA FUMO LIYONGO*,

GILGAMESH, MIKIDADI NA MAYASA PAMOJA NA SIMULIZI YA

SAMSONI

4.0 Utangulizi

Katika sura ya tatu, tulifafanua mbinu za utafiti zilivyotumika katika utafiti huu. Sura hii inalenga kutoa ufafanuzi wa mwingiliano wa kisimulizi katika *Tenzi za Fumo Liyongo* (UFL), *Gilgamesh* (UG), *Mikidadi na Mayasa* (UMM) pamoja na *Simulizi ya Samsoni* (SS). Inajadili mbinu za kisimulizi za nafsi ya kwanza, pili na tatu, usimulizi wa ki-utendi na usimulizi maizi katika UFL, UMM, UG na SS. Kwa kufanya hivyo, tumeangazia lengo la kwanza la utafiti huu ambalo ni kupambanua mwingiliano wa kisimulizi katika UFL, UMM, UG na SS. Aidha, tumechunguza mwingiliano uliopo kimuundo katika matini zilizohakikiwa kwa kuzingatia vipengele vya utangulizi, dhamira na muundo wa kuhitimisha kila matini. Ili kubainisha mwingiliano wa kisimulizi vilevile, tumechambua matumizi ya lugha katika matini teule. Baadhi ya vipengele vilivyojadiliwa katika matumizi ya lugha ni pamoja na matumizi ya tashbihi, sitiari, maswali ya balagha na taswira. Pia, tumetoa maelezo mafupi kuhusu dhana ya usimulizi na matini za UFL, UMM, UG na SS.

4.1 Dhana ya Usimulizi

Kimsingi, usimulizi unahusishwa na hadithi. Hadithi huwa na matukio yanayohitaji kuelezwa kwa njia ya kisimulizi. Aghalabu, usimulizi huhusishwa na tanzu za fasihi simulizi. Katika fasihi andishi, usimulizi hudhihirika hasa katika tanzu za riwaya na hadithi fupi. Katika usimulizi, lazima kuweko na kisa kinachosababisha usimuliaji. Ushairi huwa na mtindo maalum wa uwasilishaji ujumbe kwa hadhira lengwa.

Inabainika kwamba ushairi una mapigo maalum ya kisauti ambayo yanajenga urari wa vina na mizani. Katika ushairi, uwasilishaji wa ujumbe maalum husisitizwa kupitia urudiaji wa mshororo, neno au sauti katika shairi lenyewe.

Fasihi simulizi za Kiafrika zina vipera mbalimbali vilivyowekwa chini ya utanzu wa fasihi simulizi. Vipera hivi ni pamoja na nyimbo na ngano. Jambo kuu linalobainika ni maelezo yanayotolewa kisimulizi wakati wa kuwasilisha ujumbe mahususi. Usimuliaji huu hutolewa kwa ustadi ili kushika makini ya hadhira lengwa. Genette (1980) anasisitiza kwamba usimulizi hutokea wakati ambapo kuna kisa kilicho na mpangilio wa matukio hatua kwa hatua. Aidha, anasema kuwa ni muhimu kubainisha wakati wa usimulizi na wahusika katika simulizi yenyewe. Hayo yote huchangia utokeaji wa kitendo cha usimuliaji. Matini teule za UFL, UG, UMM na SS zinadhihirisha matumizi ya mbinu ya kisimulizi katika uwasilishaji wa ujumbe.

Usimulizi hubainika katika fasihi simulizi na vilevile fasihi andishi. Hata hivyo, usimulizi katika fasihi simulizi huhusisha hadhira hai, jambo linalosababisha tofauti kuu katika tanzu hizi mbili za fasihi. Asili ya 'tendi andishi' ni 'tendi simulizi', hivyo kuchukua sifa za usimulizi. Mulokozi (2002) anaeleza kuwa sauti ya usimulizi katika tendi ni tofauti inapolinganishwa na sauti ya usimulizi katika fasihi andishi. Anafafanua kuwa mwandishi katika fasihi andishi analenga hadhira tuli huku mwandishi (msimulizi) katika fasihi simulizi hulenga hadhira hai na hivyo kusababisha tofauti za kiutendaji. Msimulizi katika kazi za fasihi simulizi ana uwezo wa kuwa mtendaji na vilevile mhusika. Kwa sababu hii, malenga katika utendi huibuka kuwa na aina tatu za sauti za kipekee katika simulizi ambazo ni; taarifa, uigaji na ushiriki.

Maelezo yanayotolewa na Mulokozi yanaonyesha kuwa malenga ana nafasi bora ya kuwasilisha utendi wake kwa njia anayoiona mwafaka zaidi. Aina hizi za kisimulizi huzua athari tofautitofauti kwa msomaji /msikilizaji. Kwa mfano, sauti ya usimulizi wa kitaarifa inapotumika katika tendi, msimulizi ana nia ya kusimulia mambo yanayoonekana wazi huku akizibana hisia za kindani za mhusika. Vilevile, sauti ya usimulizi shirikishi mbali na kuonyesha uhusika wake katika hadithi, hudhihirisha uelewa wa matukio na hivyo kuleta uaminifu katika simulizi yenyewe. Hadhira hushawishika kuamini mambo yanayoelezwa katika hadithi.

Katika usimulizi, msimulizi anapaswa kuwa na maelezo ya kifasaha ili kuelezea visa mbalimbali katika hadithi. Wamitila (2003) anafafanua kuwa usimulizi ni uelezeaji wa matukio katika hadithi. Ni utambaji wa hadithi. Ni njia ya kimsingi inayotumika katika kupokeza kazi za fasihi simulizi. Hii ina maana kwamba ni vigumu kuwa na usimulizi pasipo na matukio. Matukio mbalimbali katika kazi husika huwezesha msimulizi kuwasilisha ujumbe kwa njia ya usimulizi. Ijapokuwa dhana ya usimulizi inahusishwa na utanzu wa riwaya katika fasihi, hudhihirika vilevile katika tendi.

Utafiti huu umechunguza mbinu ya usimulizi inavyotumika katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa* na vilevile *Simulizi ya Samsoni*. Dhana ya usimulizi kwa kawaida huhusishwa na utanzu wa fasihi simulizi, ilhali katika fasihi andishi tanzu zinazotambulika kwa usimulizi ni tanzu za riwaya, ushairi, novela na hadithi fupi. Kwa ujumla ni kwamba usimulizi unahusishwa na kazi za kinathari. Wamitila (2008) anaeleza kwamba sifa ya usimulizi inahusishwa kwa kiasi kikubwa na kazi za kinathari ijapokuwa huweza kujitokeza katika ushairi na hasa katika tungo ndefu kama vile tendi. Hata hivyo, si tenzi zote ambazo zinasimulia hadithi. Matini zilizotajwa zina sifa zinazotosheleza usimulizi kama ilivyo katika kazi zozote za

kinathari, kwa mfano, kuwa na matumizi ya mbinu ya usimulizi wa nafsi ya kwanza na tatu, uwepo wa kisa na uwepo wa wahusika.

Wamitila anataja baadhi ya tungo za kishairi (tenzi) zilizo na muundo wa hadithi kama hadithi zinazopatikana katika kazi za kinathari. Anaorodhesha baadhi ya tenzi hizo ambazo ni; *Utenzi wa Rasi'l Ghuli*, *Utenzi wa Tambuka*, *Utenzi wa Fumo Liyongo*, *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*, *Utenzi wa Paa na Ngamia*. Utafiti huu umechunguza suala la mwingilianomatini katika mbinu ya kisimulizi katika *Tenzi za Fumo Liyongo*, *Gilgamesh*, *Mikidadi na Mayasa* na vilevile *Simulizi ya Samsoni*.

4.1.1 Utenzi wa Fumo Liyongo

Utenzi wa Fumo Liyongo ni moja kati ya tungo maarufu za jadi. Shitemi (2010) anaeleza kuwa ni utenzi uliotungwa na Muhamadi Kijumwa (1913) na kuhaririwa na Abdilatif Abdalla (1973). Ni simulizi ndefu inayosifia maisha ya mhusika mkuu, Fumo Liyongo. Mulokozi (1999) anaeleza kwamba *Utendi wa Fumo Liyongo* ulitungwa na Bwana Muhamadi bin Abubakar, bin Omari al-Bakry, anayejulikana zaidi kwa jina la Muhamadi Kijumwa, mwaka 1913. Mulokozi anasema kuwa Kijumwa hakuibuni hadithi ya Liyongo bali aliipata kutokana na mapokezi simulizi ya Waswahili wa Kenya. Kijumwa alianza kujitokeza katika utunzi kwenye miaka ya 1890, alipoanza kuwasaidia watafiti wa Kizungu kama vile Alice Werner (miaka ya 1900-1935) na William Hichens (miaka ya 1930) miongoni mwa wengine (Mulokozi, 1999). Maelezo ya wataalamu hawa hayapingani angalau kuhusu tarehe za uandishi wa utendi huu.

Utenzi wa Fumo Liyongo ni kisa kinachohusu mgogoro kati ya Liyongo na Mfalme wa Pate. Kihistoria, Liyongo alijulikana kwa ushujaa wake katika karne ya kumi na saba na kumi na nane. Jahadhmy (1975) anaeleza kuwa Sultani wa Pate, alimwonea

wivu shujaa Liyongo na kumwona kama tisho kwa uongozi wa ufalme wake. Kwa sababu hiyo, alipanga njama za kumwua kwa kuzungumza na viongozi wa kabila la Wagalla. Wanaume kwa wakati huo walienda kuishi katika ukoo wa mke aliyemwoa. Hii ndiyo sababu kuu iliyomfanya Sultani wa Pate kumpangia Liyongo msichana Mgalla ambaye angemwoa ili aende kuishi na Wagalla. Viongozi wachache wa Wagalla walihongwa ili wamwue Liyongo. Hata hivyo, mipango mingi ya kumwua Liyongo haikufaulu. Mwishowe Sultani anamshawishwi mwanawe Liyongo aende kwa baba yake na amwulize kitu gani kiwezacho kumwua. Iwapo angefaulu kujua siri ya baba yake, Sultani aliahidi kumwoza bintiye na kumpa uwaziri.

Baada ya kushawishika, mwanawe Liyongo akaamua kwenda kumwuuliza baba siri ya kinga ya kifo chake. Liyongo alishikwa na shauku na kujua kwamba mtoto huyo huenda alikuwa ametumwa na adui wake. Hata hivyo, alimweleza siri yake, kuwa kimwuacho ni sindano ya shaba kitovuni mwake. Basi kijana akamngoja hadi baba yake alipolala usingizi ndipo alipomchoma sindano ya shaba kitovuni. Liyongo aligutuka usingizini na kwa hasira na ghadhabu akachukua upinde na mshale wake huku akielekea kisimani. Hapo alitia mshale upinde huku amepiga goti na kuelekeza mshale ule mjini kisha akakata roho. Katika hali hiyo, watu walioenda kisimani kuchota maji walishikwa na woga kwa sababu walidhani Liyongo alikuwa hai. Baada ya siku kadhaa, mama yake aliitwa ili aende kumbembeleza aondoke kisimani kusudi watu waweze kuchota maji. Ingawa mama yake alikwenda hapo kila siku na kumbembeleza kwa mashairi, alikosa kufanikiwa. Baada ya siku kadhaa mwili wa Liyongo ulioza na kuanguka. Hapo ndipo watu walipoweza kubaini kwamba Fumo Liyongo alikuwa amekufa.

Sultani alipopata habari kuhusu kifo cha Fumo Liyongo, alifurahi sana na kuagiza mwana wa Liyongo aende kwake ili amweleze kuhusu kifo cha baba yake. Kwa

kawaida, mtu hulia kifo kinapotokea, lakini badala ya kijana kulia, yeye akacheka. Kwa sababu hiyo, mfalme akakasirika na kumnyang'anya kijana huyo nguo na mali yote aliyompa na kisha kumfukuza mjini. Kijana anakimbilia porini kwa Wagalla na hapo ndipo alipopata kifo chake.

Kisa cha Fumo Liyongo ni masimulizi ya kihadithi yaliyo na historia ya jamii ya Waswahili. Mtiririko wa matukio katika simulizi yenyewe unaonyesha usanii unaotumika hasa katika ushairi. Hivyo Jahadmmmy (khj) anataja kwamba simulizi ya *Utenzi wa Fumo Liyongo* inaimbwa na kukumbukwa na watu wa Mwambao hadi leo. Anamnukuu Askofu Steere kwamba utenzi huu uliimbwa katika hafla mbalimbali ya jamii ya Waswahili. Anataja kwamba kifo cha Liyongo kilipotajwa, watu walipandwa na jazba na kulia kama watoto hasa walipofikia sehemu iliyomtaja mama akigundua kuwa mwanawe (Liyongo) amekufa.

4.1.2 Utendi wa Mikidadi na Mayasa (UMM)

Utendi wa Mikidadi na Mayasa ni utendi mmoja ambao haujasambaa wala kujulikana kama tendi nyinginezo za mwanzo kama vile *Utendi wa Fumo Liyongo*, *Utendi wa Mwana Kupona* na *Inkishafi* miongoni mwa nyingine. Allen (1971) anaeleza kuwa mwandishi wa UMM ni Said Abdalla Masud el Buhry, aliyeishi Pemba na baadaye kuhamia Mtang'ata na kuwa Gavana wa Mazrui. Ni Mtunzi aliyejulikana wakati huo ijapokuwa kazi zake hazijaangaziwa kwa kina. Allen anafafanua kuwa UMM ni hifadhi ya historia na tamaduni ya kisa kizuri cha mashujaa wa wakati huo.

UMM ni usimuliaji wa kisa cha mashujaa wawili Mikidadi (rijali) na Mayasa (binti). Mayasa anaweka masharti magumu kwa mwanamume atakaye kumwoa. Anasema kwamba ni sharti kupigana naye ili aweze kuona ujasiri wake. Mikidadi anashinda vita hivi kwa kupigana na Mayasa vikali na hivyo kumvua taji lake. Hata hivyo, baba

yake Mayasa, Jabiri, anaweka pingamizi kwa kuwa hataki mtoto wake aolewe na maskini. Kwa sababu hiyo, Mikidadi akawekewa mahari ya thamani kubwa yaliyohitajika kulipwa ndani ya miezi mitatu. Kutokana na hali yake ya umaskini, Jabiri alijua kwamba ingekuwa vigumu kwake Mikidadi kutimiza masharti haya.

Ingawa Mikidadi alikuwa maskini, anajitahidi hata akaweza kulipa mahari iliyohitajika. Wakati mmoja alipigana na jini na akamshinda. Katika vita vingine, Mikidadi anawaokoa vijana wawili kutokana na mateso ya Luhani, ambaye anauawa katika vita vikali ambapo Mikidadi ananyang'anya mali kwa urahisi ili apate mahari. Baada ya kupata mahari yaliyotosha, Mikidadi anayapeleka kwa babake Mayasa. Anakabiliana naye pamoja na mjombake Mayasa. Wao walimtaka Mayasa kuolewa na Maliki ambaye alikuwa tajiri akilinganishwa na Mikidadi, lakini Mayasa anamchagua Mikidadi. Jeshi la askari lililokuwa limetengwa ili kumchungua Mayasa lilikataa uamuzi wa Mayasa. Hivyo basi vita vikaanza baina yao na Mikidadi. Hatimaye Mikidadi akawashinda na kuungana na Mayasa. Baada ya kuhadaiwa, Jabiri, anampa Mikidadi vileo kwa kusudi la kumlevya ili aweze kumtia nguvuni. Mikidadi amwomba mama yake (Tamima) amwombee radhi ili ajinasue.

Kasiri anapopata habari za Mikidadi, anapeleka vikosi vya askari kwenda kumkamata. Hata hivyo, vikosi hivyo vinashindwa na hatimaye Mikidadi anamteka nyara kiongozi wao. Mikidadi anafaulu kutwaa silaha na mali yao. Sultani anapopata habari hiyo, anachukizwa na tukio hilo. Kwa kutaka kuona ujasiri wa Mikidadi, Sultani anamwamuru apambane na Simba. Mikidadi kwa ujasiri anamshambulia simba na kumwua. Kwa njia hiyo anapata mali zaidi na vilevile kupewa taji na Sultani.

Baada ya kupata mahari yaliyohitajika, Mikidadi anarudi kwa babake Mayasa. Anapokaribia mjini kwao, anapata habari kuwa kuna harusi ya Mayasa kuozwa

Maliki Bin Riyahi (tajiri aliyependekezwa na baba). Mikidadi anakabiliana na jeshi kubwa lililokuwa limeandamana na Mayasa ili kumchungu dhidi yake. Mikidadi anapigana vita vikali na mwishowe anamfikia Mayasa. Baadaye jeshi linaona ni heri kutafuta suluhu kwa kumwuliza Mayasa ni nani angemtaka baina ya Mikidadi na Maliki. Mayasa amchagua Mikidadi lakini askari wanakataa uamuzi huo. Mapigano makali yanaanza kwa mara nyingine hata anampokonya Imam taji lake ili ampe Mayasa. Mikidadi anawashinda na kuungana tena na Mayasa.

Jabiri alipoona kuwa Mikidadi ameshinda vita vile, alimhadaa aende kwake na kumpa kileo ili apate kumtia nguvuni. Mikidadi analewa na kufungwa kwa kamba. Anapogutuka na kurudiwa na fahamu zake, anajipata kwamba amefungwa na analia machozi. Katika hali hiyo, anamlilia mama yake mzazi, Tamima, ambaye anamwomba dua ili ajinasue kutokana na janga hilo lililomkabili. Tamima anafanya hima kwenda Madina ili apate msaada kutoka kwa Mtume. Hivyo anapewa Ali na Haidari, (walinzi wa Mtume) kwenda kumtetea Mikidadi kusudi asiawe na Maliki. Wanapofika pale, wanamfungua Mikidadi na katika vita vilivyofuatia, Maliki na Jabiri wanauawa. Mikidadi basi anamchukua Mayasa mke wake na kufanya karamu kubwa sana ya kusherehekea ushindi wao.

4.1.3 Utendi wa *Gilgamesh* (UG)

Utendi wa Gilgamesh ni muunganiko wa Vibao kumi na viwili vinavyokamilishana. Utafiti huu unatumia nakala ya Kovacs (1998) iliyo na Vibao kumi na moja (XI). Kibao cha mwisho cha XII, hata hivyo kimechukuliwa kuwa kiambatisho. Heidel (1949) anasema kwamba utungo wa kwanza wa UG uliokamilika; wenye anwani *Das Babylonische Nimrodepos* uliandikwa na Paul Haupt (1858-1926).

Utenzi huu ulitafsiriwa na kuandikwa katika lugha nyingi zikiwemo Kisumeri, Kikabari na hatimaye Kiingereza. Chapisho la kwanza katika lugha ya Kiingereza, *The Epic of Gilgamesh*, lilichapishwa na Campbell Thomson (Oxford, 1930). Utafiti huu unashughulikia *Utendi wa Gilgamesh*, nakala ya mtandaoni kwa hisani ya Wolf Carnahan (1998) iliyotafsiriwa katika lugha ya Kiingereza na Maureen Kovacs (1998). Inaaminika kwamba UG ni moja kati ya simulizi za kale za Wababeli. Utendi huu unafahamika zaidi kwa sababu ya ulinganifu wake na hadithi ya gharika ya dunia kwenye habari za Nuhu katika Biblia.

UG unahusu matukio ya Gilgamesh aliyekuwa Mfalme wa mji wa Uruk (kwa sasa Iraq). Gilgamesh alikuwa kiongozi dhalimu aliyekuwa na sifa za kiungu. Anaonyeshwa kuwa na nguvu za ajabu kiasi cha kulinganishwa na nyati. Maelezo kuhusu kuzaliwa kwake si dhahiri ijapokuwa Heidel (khj) anaeleza kuwa alikuwa mtoto wa mungu wa kike, Ninsun. Habari kuhusu baba yake si dhahiri ingawa Heidel (khj) pia anasema kuwa baba yake Gilgamesh alikuwa kasisi mkuu wa Kullab, Wilayani Uruk. Maelezo hayo yanasadiki sababu ya Gilgamesh kusemekana kwamba ni nusu-mungu na nusu-binadamu.

Kwa sababu ya pepo mbaya ndani yake na tamaa ya mwili, Gilgamesh ana mazoea ya kumchukua bikira kila wakati kunapotokea harusi. Wakati huo, anamfukuza bwana harusi na kumfanyisha kazi ya sulubu katika hekalu la Eanna. Jambo hili linawakera kina mama na raia wa Uruk na hivyo kupeleka malilio yao kwa miungu (Aruru, aliyemuumba binadamu). Aruru basi anamwomba Enkidu, aliyekuwa na nguvu sawa na Gilgamesh ili awe mpinzani wake na kuwawezesha watu wa Uruk kuwa na amani. Kupitia ndoto, Gilgamesh anajua kuhusu Enkidu na wanapokutana naye wanapigana vita vikali. Nguvu zao zinalingana na hakuna mshindi. Baadaye, Enkidu anakubali

kuwa Gilgamesh ni jasiri na kila mmoja akipendezwa na mwenzake, wakawa marafiki wa dhati.

Gilgamesh na Enkidu wanaenda kwenye Msitu wa Mikangazi, msitu ulioaminika kuwa makao ya miungu. Pamoja wanajihami na kumvamia Humbaba, mlinda lango wa msitu ule. Wanamwua Humbaba ili wapate kuingia msituni na kukata miti ya seda kinyume cha mapenzi ya miungu. Matokeo ni kwamba mkono wa Enkidu unakufa ganzi na anadhoofika kiafya. Gilgamesh anaingiwa na hofu nyingi kwa sababu ya afya ya rafiki yake. Baada ya Enkidu kuugua kwa muda mrefu, anaaga dunia. Kifo chake kinamfanya Gilgamesh kuhuzunika mno. Anamwomboleza rafiki yake siku saba kabla ya kumzika. Hatimaye Gilgamesh anaamua kutafuta siri ya kuepuka kifo. Anakutana na Utnapishtim aliyeepuka kifo kutokana na mafuriko yaliyotokea. Utnapishtim anampa Gilgamesh dawa ya mmea fulani na kumshauri asilale siku saba ili apate kushinda kifo. Vilevile anamshauri arudi kwa watu wake Uruk.

Safari ya kwenda Uruk ilikuwa ndefu na ya kuchosha, hivyo Gilgamesh anapopata bwawa la maji anaingia pale kuoga. Katika harakati ya kuoga, harufu ya dawa ile inamvutia nyoka ambaye ananyemelea na kuenda na dawa hiyo inayomfanya kubambuka ngozi (ndiyo sababu ya nyoka kubambuka ngozi hadi leo). Gilgamesh anapogundua hivyo, anajuta sana. Hapo anamlilia Urshanabi (mvushaji feri) ambaye anaambatana naye hadi Uruk. Anamwonyesha ukuu wa mji wa Uruk, kazi ya uashi, ukumbi wa hekalu ya Ishtar na usanii wa hali ya juu wa kazi ya mikono yake. Utendi unaisha Gilgamesh akimweleza Urshanabi kwa majuto akague kazi kubwa ya ujenzi aliyoifanya. Anajuta kwa kutokamilisha azma yake ya kutafuta siri ya kifo kwani alikuwa amemfanikisha ‘simba wa ardhi’ (nyoka) kuishi maisha ya milele badala yake. Kibao cha XII kimechukuliwa kama kiambatisho hivyo hakijatumika katika utafiti huu.

4.1.4 Simulizi ya Samsoni (SS)

Simulizi ya Samsoni, katika utafiti huu inarejelewa katika *Biblia*, kitabu cha Waamuzi sura za kumi na tatu hadi kumi na sita. Kitabu cha Waamuzi katika *Biblia* kinaonyesha uongozi wa Israeli kwa wakati huo ambapo walikuwa chini ya utawala wa Wafilisti, kwa miaka arobaini (Unger, 1967:176). Waisraeli walihitaji kiongozi ambaye angewaokoa kutoka katika mikono ya Wafilisti. Waisraeli walikuwa wamemuasi Mwenyezi Mungu na hivyo Mungu alikuwa amewaacha wateseke chini ya utawala wa Wafilisti. Mmoja kati ya viongozi wa Israeli, Samsoni ndiye aliyewakomboa Waisraeli dhidi ya Wafilisti. Samsoni ni kiongozi aliyekuwa na “upako” wa Mungu kuanzia akiwa tumboni mwa mama yake hadi kufa kwake. Hii ina maana kwamba alikuwa ameteuliwa na Mungu ili kuwaokoa Waisraeli kutoka katika utesi wa Wafilisti (Unger, khj).

Simulizi ya Samsoni inahusu mhusika mkuu, Samsoni ambaye ana sifa za kiungu. Baba yake ni Manoa, aliyetoka katika ukoo wa Wadani (Dannites). Mama yake Samsoni alipewa masharti ya kufuata katika kumlea mwana wake (Waamuzi 13:4-5). Hivyo basi, Samsoni alipokuwa mkubwa alikuwa na umbo la jitu, hasa kwa nguvu alizokuwa nazo na nywele ndefu, ambazo mama yake alipewa masharti kwamba asimnyoe kamwe.

Samsoni alipobaleghe, alipendezwa na mwanamke Mfilisti kutoka Timna. Hata hivyo, wazazi wake walisita kumwoza huyo mwanamke kwa sababu ilikuwa nadra kwa Myahudi na Mfilisti kuoana. Baadaye, walikubaliana na mwanao na wote wakaenda hadi Timna ili kumchukua yule mwanamke kuwa mke wa Samsoni. Njiani, walikutana na simba na ajabu ni kwamba Samsoni alimkabili simba huyo kwa kumrarua kwa mikono yake ingawa hakuwaelezea wazazi wake.

Wakiwa njiani kuelekea nyumbani baada ya kukubaliwa kumchukua mwanamke Mtimna kuwa mkewe, Samsoni alipata mzoga wa yule Simba aliyemwua. Ajabu ni kwamba kulikuwa na asali na nyuki pale. Samsoni alitwaa asali akaila na hata kuwapatia wazazi wake. Walipofika nyumbani, karamu iliandaliwa kwa ajili ya mkewe Samsoni. Katika harakati za hafla hiyo, Samsoni aliwategea kitendawili ambacho kilihitajika kuteguliwa kabla ya siku saba kuisha. Watu waliokuwa karamuni walishindwa kukitegua kitendawili kile:

Katika huyo mwenye kula
Kikatoka chakula
Katika huyo mwenye nguvu.
Ukatoka utamu (Waamuzi 14:14)

Watu waliokuwa karamuni walijaribu kutegua kitendawili hiki lakini hawakufanikiwa. Hivyo basi wakamwagiza Mtimna kumbembeleza Samsoni ili amtegulie kitendawili. Mkewe alifaulu na hivyo baada ya kupata jibu, alienda na kuwaeleza watu wake. Wafilisti wakaweza kumtegulia Samsoni kitendawili kile asubuhi na mapema ya siku ya saba kabla jua kuchomoza. Hii ilimaanisha kwamba wangepewa zawadi kwa sababu ya kutegua kitendawili. Samsoni alipoona kwamba Wafilisti wamefaulu kutegua kitendawili, aliteremkia Ashkeloni*¹ na kuwapiga wanaume thelathini, akawanyang'anya mavazi yao ili kwenda kuwapatia Wafilisti wale waliotegua kitendawili. Wakati huo, Samsoni alikuwa amepandwa na hasira na hivyo akaenda kwa baba yake pasipo kurudi kwa mkewe usiku wa saba wa harusi, kama ilivyokuwa desturi yao. Usiku huo, mkewe (Mtimna) akaozwa rafiki yake aliyekuwa kwenye karamu ya ndoa.

¹ Ashkeloni* Ni moja kati ya miji mikuu mitano ya Palestina iliyonawiri katika biashara. *NIV Study Bible*, (Michigan: USA, Zondervan Publishers, 2002) 331.

Baada ya muda mrefu, Samsoni akarudi kwa mkewe (Mtimna) akiwa amemchukulia mwanambuzi kama zawadi yake. Baba mkwe wake akamkataza Samsoni kuingia katika chumba cha mke wake. Baada ya muda mfupi tena, Samsoni akagundua kwamba mkewe alikuwa ameoza rafiki yake. Jambo hili lilimkasirisha mno kiasi cha kulipiza kisasi kwa Wafilisti. Akaenda hadi shamba la ngano akiwa amewakamata mbweha mia tatu waliofungiwa vienge vya moto kwenye mikia yao. Akiwa na hasira, Samsoni aliwaachilia mbweha hao kuyateketeza mashamba ya mizeituni. Wafilisti walipokuja kujua kwamba kitendo hiki kilitekelezwa na Samsoni (kwa sababu ya hasira juu ya mkewe), walienda kumshika mkewe pamoja na baba yake na kuwateketeza kwa moto (Waamuzi 15:6-8). Katika hali hiyo vilevile, Samsoni aliona alipize kisasi tena kwa kuwaua Wafilisti wengi na kuenda kukaa katika ufa wa jabali la Etamu.

Wafilisti waliomba Samsoni aadhibiwe kwa kitendo alichokifanya naye akakubali. Hivyo, watu wake wa Yuda wakamfunga na kumkabidhi Wafilisti ili naye aadhibiwe. Maajabu ni kwamba alikata minyororo aliyofungiwa na kuwaua Wafilisti elfu moja kwa kutumia mfupa wa utaya wa punda. Alipomaliza kutekeleza mauaji hayo, alihisi kiu ambapo alimwita Mungu wake na Mungu akamsikia na kumpa maji kutoka mahali pale palipoitwa Lehi. Baada ya kunywa maji, Samsoni akarudiwa na nguvu tena.

Kwa mara nyingine, Samsoni alimwoa mwanamke kahaba huko Gaza aliyempenda na kuingia kwake. Watu wa Gaza walipojua kuwa Samsoni ameingia kwa nyumba yake walipazingira mahali pale kusudi wamwue. Kulikuwa na njama za kumwua Samson wakati wa mapambazuko lakini hila hiyo ilitibuka. Samsoni alilala hadi usiku wa manane ambapo aliamka na kung'oa vizingiti vya milango kwa mabega yake na kuvipeleka umbali wa yadi arobaini.

Sehemu ya mwisho wa maisha ya Samsoni ni wakati alipokutana na Delilah aliyemchukua kuwa mke wake. Delilah alipoishi na Samsoni, alijaribu kadiri alivyoweza ili ajue siri za nguvu zake. Mwishowe, alifaulu kujua kwamba nguvu za Samsoni zilikuwa kwenye nywele zake. Hapo ndipo alipowaeleza Wafilisti waliokwenda kumnyoa na nguvu zake zikamtoka. Samsoni basi alifungwa kwa pingu za shaba baada ya kunyolewa. Aidha, aling'olewa macho yake na kupelekwa gerezani. Alipokuwa pale gerezani, Samsoni aliteswa sana. Kazi yake ilikuwa ni kusaga ngano na kuwaburudisha maadui zake kwa kucheza. Baada ya muda mfupi, nywele zake zikamea tena. Safari hii Samsoni alimwomba Mungu amrejeshee nguvu zake ili alipize kisasi dhidi ya Wafilisti waliomng'oa macho. Mungu alisikia ombi lake na kumtia nguvu tena. Kwa kusimama katikati ya nguzo mbili zilizosimamisha nyumba ile Samsoni aliinama, na kwa nguvu zake zote akaliangusha jengo hilo. Lile jengo lilianguka juu ya viongozi na watu wote waliokuwamo mle ndani wakaangamia. Hivyo basi, Samsoni aliwaua watu wengi wakati wa kufa kwake kuliko siku za uhai wake. Samsoni alikuwa Mwamuzi wa Israeli kwa miaka ishirini.

4.2 Mbinu za Kisimulizi katika UFL, UG, UMM na SS

Utafiti huu umechunguza mbinu za kisimulizi zilizotumika katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa* na *Simulizi ya Samsoni*. Mbinu hizi ni pamoja na usimulizi wa ki-utendi, usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya tatu na usimulizi maizi. Usimulizi ni njia kuu ya kuwasilisha ujumbe katika tungo za kinathari. Katika utafiti huu, tumetambulisha usimulizi kama mbinu kuu iliyotumika katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa* na *Simulizi ya Samsoni*.

4.2.1 Usimulizi wa ki-Utendi katika UFL

UFL umetumia mbinu changamano za usimulizi ili kuendeleza hadithi yake. Katika fasihi simulizi za Kiafrika, mtambaji alipaswa kuwa na mbinu maalum ya kuchangamsha hadhira yake kwa kusudi la kuwateka makini yao. Vivyo hivyo, katika ushairi (simulizi au andishi), msimulizi anafaa kutumia ubunifu wake ili kutimiza lengo lake kikamilifu. Mbali na matumizi ya lugha bunifu, mbinu za kisimulizi zinazotumika na msimulizi zinachangia katika kufanikisha malengo ya kazi husika. Jinsi anavyoeleza Wamitila (khj), moja kati ya mbinu za kisimulizi ni usimulizi wa ki-utendi. Anafafanua kuwa mbinu hii ni usimulizi wa nafsi ya kwanza ambapo msimulizi anasimulia hadithi ambayo hashiriki katika matendo yake. UFL unatumia mbinu hii kuelezea matukio yanayotokea katika kisa cha Fumo Liyongo. Katika beti za nne na tano, mwandishi anabainisha kwamba hajashiriki katika matendo yaliyotokea bali anaripoti tu mambo yaliyomzingira mhusika ambaye ni Fumo Liyongo:

Mf 1

UFL
Hadithi niwandikiye
Ya ajabu musikiye
Yalojiri amriye
Mupate kufahamiya (ub. 4)

Niweleze kwa utungo
Hadithi yake Liyongo
Niweleze na mazinga
Mambo yalomzingiya (ub. 5)

Beti hizi zinaonyesha kwamba kuna kisa fulani ambacho msimulizi anataka wasomaji wake wajue. Kwa kutaja *hadithi*, ina maana kwamba kuna mfululizo wa matukio ambayo yanatosha kuelezwa ki-simulizi. Tulivyotangulia kutaja, usimulizi mara nyingi huhusishwa na tanzu za riwaya na hadithi fupi katika fasihi andishi. Hata hivyo, inabainika kuwa usimulizi hutokea kama mbinu mojawapo ya kupasha ujumbe

katika tendi. Mtunzi wa UFL anasimulia mambo mengi yanayohusu mhusika Liyongo. Beti zifuatazo zinadhihirisha kwamba mtunzi si mshiriki katika usimulizi wenyewe, hivyo kubainisha usimulizi wa ki-utendi:

Mf 2

UFL
Wagala wakabaini “Huyu
Liyongo ni nyani Kwetu
hayusilikani
Wala hatuyasikiya” (ub. 11)

“Ni mwanamume Swahihi
Kama simba una zihi
Usiku na asubuhi
Kutembea ni mamoya (ub. 12)

Katika dondoo hili, msimulizi anabainisha kutoshiriki katika matendo yanayojiri. Mtunzi anasema *huyu Liyongo ni nyani kwetu hayusilikani wala hatuyasikiya*. Hapa ni wazi kwamba mhusika Liyongo amesikika tu kwa hao Wagalla, bali hajulikani hasa ni nani (nyani). Mtunzi anasimulia mambo yanayosemwa kuhusu Fumo Liyongo. Anataja sifa za mhusika na kumsifu kwa sababu ya ujasiri wake kwa kusema kuwa yeye ni mwanamume swahihi. Usimulizi wa ki-utendi umetumika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* kusimulia kisa kirefu cha mhusika mkuu. Ni mbinu inayotumika katika uwasilishaji wa tenzi ambapo msimulizi anaonyesha kutoshiriki katika visa mbalimbali anavyovisimulia. Usimulizi wa ki-utendi umetumika kama mbinu moja iliyotumika kikamilifu kuwasilisha ujumbe kisimulizi katika UFL.

4.2.2 Usimulizi wa ki-utendi katika UMM

Mbinu ya usimulizi ya ki-utendi imetumika vilevile katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Hii inadhihirisha uwepo wa kisa au hadithi inayoendelezwa ambayo msimulizi anakusudia hadhira yake ifuate. Kisa kinasimuliwa cha kuonyesha matukio ya mhusika mkuu ambaye ni Mikidadi. Baada ya kutwaa mali ya kutosha, alijihisi

shujaa na kuanza kujigamba hasa wakati aliposhurutishwa kumwua simba, tendo alilolifanya kwa urahisi sana. Mbali na beti zingine, msimulizi anawasilisha majigambo hayo katika beti zifuatazo:

Mf 3

UMM
 Simba awele kuruka
 Ili kutaka mshika
 Upanga ukamtoka
 Mikidadi katwaa (ub.455)

Alipokwisha mkataa
 Simba akamkukuta
 Na shairi akaleta
 Kujisifu ushujaa (ub.456)

Matendo ya Mikadadi yalishangaza watu wengi, miongoni mwao Sultani aliyeona heri kumvisha Mikidadi taji lake kwa sababu ya ushujaa aliouonyesha. Hata hivyo, waziri wa Sultani hakufurahishwa na kitendo hiki kilichofanywa na Sultani. Alimkosoa Sultani kwa kusema kuwa ilikuwa ni radhi kumpatia mali lakini sio kumvulia taji kwa sababu Mikidadi alikuwa mgeni. Aidha, ni tendo la aibu na kufedhehesha kwa Sultani kumvulia mtu taji lake. Maneno katika Beti 455 na 456 yanadhihirisha kwamba msimulizi anaripoti tu, bali si mshiriki katika kisa chenyewe.

Usimulizi wa ki-utendi aidha unabainika katika beti zinazofuata:

Mf 4

UMM
 Huwaje mgeni wako
 ukampa taji lako
 lililo kitwani mwako
 ukamvika kavaa (ub.467)

Mimi naona aibu
 Ndipo hufanya ghadhabu
 Mgeni mja gharibu
 Uyasidi kumwatia (ub.470)

Usimulizi wa ki-utendi aidha unadhihirika katika mipango ya mikidadi ya kumwoa Mayasa. Wakati huo pia, baba yake Mayasa anapanga njama za kumwoza Mayasa kwa rafiki yake Malik. Jabiri alionywa na jeshi lake kwamba mipango yake ingetibuka kwa sababu wao walijua kwamba Mikidadi alikuwa shujaa ambaye angeleta balaa kwa yeyote aliyethubutu kumchukua Mayasa. Ukweli ni kwamba Mikidadi alikutana na askari waliokuwa mbioni kumchukua Mayasa kwa mume wake wa kupangiwa, Malik. Vita vikali vilianza baina ya Mikidadi na askari. Mwishowe, Mikidadi aliwashinda na kumwendea Mayasa ambaye alikuwa na heri kusema:

Mf 5

UMM
Wakanioza Maliki
Wala mimi simtaki
Illa nafuata haki
ya idhini ya abia (ub. 551)

Sasa upigane nao
uwashinde wende zao
utwae mali zao
nami upate nitwae (ub. 552)

Matokeo ya vita hivyo ni kuwa Mikidadi aliwaua wote na hatimaye akapata nafasi ya kumchukua mke wake Mayasa. Wawili hao walihimizana na kufarijiana kwa huba. Katika maelezo ya hapo juu (551,552), tunaona kuwa matukio katika kisa cha Mikidadi na Mayasa yanaunda hadithi ambayo ina sehemu za mwanzo, kati na mwisho. Beti hizi, zinazodhihirisha usimulizi wa ki-utendi ni baadhi ya beti zinazounda sehemu ya kati ya kisa chenye.

Mazungumzo ya ki-utendi aidha yanaendelea baina ya Mikidadi, Mayasa na Ali (Imam) kutokea beti 590-628. Ali ni mume wa Fatuma ambaye alikuwa na taji lililomtamanisha Mayasa hivyo kumfanya Mikidadi kupigana na Ali kusudi apate taji hilo ili ampelekee mkewe Mayasa. Vita baina ya Mikidadi na Ali vilianza na kwa

mara ya kwanza, umahiri wa Ali katika vita ulimtisha hasa alipomweleza kwamba yeye (Ali) ni ‘Simba wa Mungu anayeharibu miji na vitongoji na kuwa anawaua wapendanao.’ Mapigano yaliendelea na Mayasa alipomwona mumewe akilegea, alijitolea kwenda mwenyewe kupigana na Ali, jambo lililomfanya Mikidadi kutia bidii zaidi katika vita. Mayasa, kwa upande wake akamsihi Ali kutomwua mumewe, japo kwa kumlimbikizia sifa. Maneno yake yalimghusa Ali na akalegea katika vita.

Beti zifuatazo zinaeleza mazungumzo yanayoripotiwa ki-utendi kati ya Mayasa na Ali:

Mf 6

UMM
 Akatamka Mayasa
 Ewe samba mnafisi
 Simtinde kwa upesi
 Laala akalekea (ub. 620)

Mayasa rejea kwako
 utilize moyo wako
 hana dhara mume wako
 Mayasa akarejea (ub. 623)

Katika majibizano yaliyoendelea, katika ubeti wa 620, Mayasa anamshauri Ali asiwe na haraka kumwua Mikidadi kwa sababu tayari alikuwa amechoka na angejiuzulu katika mapigano hayo. Ushauri huo ulimtuliza Imamu Ali ambaye alimwachilia Mikidadi na kumweleza Mayasa kuwa mume wake alikuwa salama (ubeti 623). Hata hivyo, Imamu Ali alipoona kwamba ni vigumu kumshinda Mikidadi, aliamua kumsilimisha pamoja na mkewe Mayasa. Hivyo, Mikidadi na Mayasa wakashikwa baada ya kufunzwa maombi na masharti ya dini ya Kiislamu wakaachwa kwenda zao nyumbani. Tangu siku hiyo wakawa marafiki wa Imam Ali.

4.2.3 Usimulizi wa Nafsi ya Kwanza katika UG

Utendi huu unabainisha mitindo miwili ya kisimulizi ambayo ni usimulizi wa nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu. Kwanza kabisa, ni muhimu kuelewa kwamba UG una wahusika wengi (hasa wa kiungu) ambao huenda wakakanganya mtiririko wa simulizi. Hata hivyo, simulizi inahusu hasa wahusika wakuu wawili, Gilgamesh na Enkidu. Vilevile, kuna wahusika wa kike, Shamhat na Ishtar ambao wanachangia katika kuendeleza simulizi ya UG. Wahusika wengine wajenzi katika UG ni Humbaba, mlinzi wa msitu wa Seda na Utnapishtim. Utnapishtim ni mhusika aliyekuwa na uwezo wa kutunza maisha ya binadamu baada ya gharika iliyomaliza uhai wa binadamu na wanyama. Hivyo, Utnapishtim alijua ‘siri ya kifo’.

Katika UG, mbinu ya usimulizi wa nafsi ya kwanza imetumika katika sehemu mbalimbali ya utendi; mwanzo, kati na mwisho japo kwa kubadilishana zamu na mbinu nyingine. Ufafanuzi wa Fludernik (2009) kuhusu usimulizi wa nafsi ya kwanza unaeleza kuwa ni aina ya usimulizi unaolenga matukio yanayosisimua. Anataja kwamba msimulizi wa nafsi ya kwanza anajidhihirisha kama msimulizi anayepatikana sasa hivi, wakati wa masimulizi na aliyekuwepo wakati wa matukio yanayoendelezwa katika usimulizi. Kwa sababu hiyo, msimulizi wa nafsi ya kwanza anakuwa kama mhusika kwani yeye hutambulika katika msuko wa hadithi.

Mwanzoni mwa utendi tunapata msimulizi anayefafanua sifa za mhusika Gilgamesh. Mbinu ya usimulizi inayotumika hapa ni ya nafsi ya kwanza. Msimulizi anamsifu Gilgamesh kwa kumlimbikizia sifa za kishujaa na za kiungu katika mistari ifuatayo:

Mf 7

UG

M.A	M.T (Tafsiri yangu)
<i>(He who has seen everything I will make known to the lands</i>	“Nitaifahamisha nchi yote, kumhusu yeye aliyeyaona yote
<i>I will teach about him who experienced all things alike</i>	Nitatoa mafundisho kumhusu yeye aliyeyapatia mambo yote
<i>Anu granted him the totality of knowledge of all</i>	Anu alimtunuku ukamilifu wa ufahamu wa yote
<i>No later king or man ever equaled)</i> <i>(Tablet 1:1)</i>	Hakuna mtu au mfalme wa baadaye aliyefikia utukufu wake (Kibao cha 1:1)

Katika UG, mbinu ya usimulizi wa nafsi ya kwanza imetumika katika sehemu za mwanzo, kati na mwisho wa utendi. Usimulizi wa nafsi ya kwanza unaendelezwa na msimulizi wakati anaonekana kushuhudia matendo ya Gilgamesh na Enkidu walipokuwa wakikabiliana na Humbaba, mlinzi wa msitu wa seda. Katika Kibao IV, ukurasa 17, msimulizi anaeleza:

Mf 8

UG

M.A	M.T(tafsiri yangu)
<i>(They (Gilgamesh and Enkidu)...</i>	Wao (Gilgamesh na Enkidu) wanarukiana
<i>They lunge at each other like raging wild bulls....</i>	kama fahali mwitu walioghadhabika
<i>One name he bellowed full of.....</i>	Jina moja alinguruma akijawa na...
<i>The guardian of the forest bellowed...Humbaba like.....</i>	mlinzi wa msitu alinguruma.... Humbaba kama...
<i>“one alone cannot” Strangers.....</i>	...“Mmoja pekee hawezi” wageni...
<i>A slippery path is not feared by two people who help each other”</i>	Njia yenye utelezi haiogopwi na watu wawili wanaosaidiana’
<i>Twice, three times...</i>	Mara mbili, mara tatu...
<i>Why, my friend, we ...so wretchedly? We have crossed all the mountains together... (Tablet IV: 17a)</i>	Kwa nini rafiki yangu, tuta...ovyoy hivyo? Tumeivuka milima yote kwa pamoja... (Kibao cha IV: 17a)

Katika Kibao cha IV: 17a, msimulizi anatupatia mazungumzo yaliyoendelezwa na wahusika walewale, Enkidu na Gilgamesh. Kwa mfano, Gilgamesh anaposema (*“Why, my friend, we.... So wretchedly? We have crossed all the mountains together...”*) (Kwa nini rafiki yangu tuta...ovyo hivyo. Tumeivuka milima yote kwa pamoja). Dondoo hili linaonyesha kuwa msimulizi amechukua nafasi ya mhusika. Hivi ndivyo anavyosema Mohochi (khj) kwamba mbinu hii inawasilisha hadithi kama ambayo imesimuliwa na mmoja wa wahusika wake. Katika UG, mbinu hii inatumika hapa na pale hasa inapozingatiwa kuwa utenzi wenyewe ni mrefu. Katika mahali pengine, katika kibao cha kumi na moja, msimulizi anaeleza kuhusu hadithi ya mafuriko. Masimulizi hayo yanafanywa kwa kutumia mbinu ya nafsi ya kwanza. Anasema:

Mf 9

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(I fell to my knees and sat weeping, Tears streaming down the side of my nose...</i>	<i>Nilipiga magoti na kukaa nikiomboleza Machozi yalinibubujika na kuteremka kando ya pua yangu</i>
<i>When a seventh day arrived, I set forth a dove and released it..... I sent forth a swallow and released it... I sent Enkiduforth a raven and released it.....(Tablet XI: 46)</i>	<i>...siku ya saba ilipofika, nilimtuma njiwa na kumwachilia... nilimtuma mbayuwayu na nikamwachilia... nilimtuma kunguru na nikamwachilia... Kibao cha XI: 46)</i>

Mistari iliyotangulia inaonyesha kwamba msimulizi hapa ni mhusika kama wahusika wengine katika hadithi. Inakuwa vigumu kuyatenganisha mawazo ya mwandishi au mtunzi wa kazi husika na yale ya msimulizi ambaye ni mshiriki katika msuko wa hadithi. Kwa mfano, maneno katika mstari wa kwanza ‘*Nilipiga magoti na kukaa nikiomboleza*’ ni maneno yaliyosemwa na mhusika Gilgamesh alipomwomboleza rafiki yake Enkidu. Madai ya Fludernik (2009) kuwa usimulizi wa nafsi ya kwanza ni

aina ya usimulizi unaolenga matukio yanayosisimua yanadhihirishwa katika *Utendi wa Gilgamesh*.

4.2.4 Usimulizi wa Nafsi ya Kwanza katika SS

Usimulizi unachukua mkabala wa nafsi ya kwanza katika Waamuzi 14 vifungu 12-13. Mhusika mkuu, Samsoni, anakuwa mshiriki katika matukio yanayoendelezwa katika hadithi. Baada ya Samsoni kupewa Mtimna kuwa mkewe, alifanya karamu kama ilivyokuwa desturi. Vijana walikusanyika kwa ajili ya karamu hiyo na Samsoni akawategea kitendawili.

Mf 10

SS

Samsoni akawaambia,

Mimi nitawategea ninyi kitendawili, Kama mnaweza kunionyesha katika hizo siku saba za karamu, na kukitambua, ndipo hapo nitawapa mavazi thelathini ya kitani na mavao mengine thelathini (Waamuzi 14: 12).

Mofimu (ni) na (mimi) zimetumika kama viwakilishi vya nafsi ya kwanza. Msimulizi hapa amegeuka na kuwa mhusika katika hadithi yake. Kwa mfano Samsoni anaposema, ***Mimi nitawategea ninyi kitendawili...*** Mkewe Samsoni vilevile amekuwa msimulizi mhusika pale ambapo anamsihi mumewe kumteguulia kile kitendawili kusudi asiangamizwe kwa kuteketezwa moto na watu wake. Katika Waamuzi 14:16, tunapata maneno yafuatayo:

Mf 11

SS

Wewe wanichukia tu, wala hunipendi, wewe umewategea kitendawili hao wana wa watu wangu, nawe hukuniambia mimi....

Mazungumzo baina ya Samsoni na mkewe yanaendelezwa kwa njia ya kimapokezano. Katika hali hii kila mmoja wao anachukua nafasi ya kuwa msimulizi na mhusika wakati mmoja. Mkewe Samsoni alilia siku saba mbele ya mumewe na

hatimaye Samsoni alikubali kumteguulia kile kitendawili, na akaenda kuwaeleza watu wake. Hata hivyo, Samsoni alijua kwamba mkewe ndiye aliyewapatia jawabu na hivyo akapandwa na Roho, hasira zikamwaka na akawapiga wanaume thelathini waliokuwa pale Ashkeloni. Baada ya kufanya hivyo, Samsoni alienda nyumbani kwa wazazi wake na mkewe akaozwa rafiki yake aliyekuwa kwenye karamu ya ndoa.

Kisa cha mkewe Samsoni kinaendelezwa katika Waamuzi sura ya (15). Msimulizi anaeleza kwamba Samsoni aliona heri kwenda kwa mkewe na kumpelekea zawadi. Samsoni anazungumza peke yake. Hii ni mbinu ya uzungumzi nafsi iliyotumika ili kukuza zaidi kisa chake Samsoni na hali kadhalika kuonyesha hali ya upweke aliokuwamo Samsoni.

Alipokata kauli kwenda kwa mkewe, alisema “nitaingia chumbani kwa mke wangu”. Kishazi hiki kinaonyesha kusononeka kwake Samsoni, baada ya kukosa kwenda na mke wake hadi nyumbani kwao. Alipofika kwa mkewe, baba mkwe wake alimkataza kuingia chumbani kwa sababu tayari alikuwa amemwoza mwanamke yule mtu mwingine.

4.2.5 Usimulizi wa Nafsi ya Tatu katika UFL

Sawa na usimulizi wa ki-utendi, matumizi ya usimulizi wa nafsi ya tatu ni dhahiri. Katika mbinu hii vilevile, msimulizi anasimulia matukio ambayo hakushiriki (Wamitila, 2003; Mazrui na Syambo, 1992). Aina hii ya usimulizi hubainishwa kwa matumizi ya viambishi vya nafsi ya tatu (a), (wa) na (yeye). Viambishi hivi huashiria kwamba msimulizi hakushiriki katika hadithi. Usimulizi wa aina hii vilevile hutambulishwa na matumizi ya (ali-) kuashiria wakati uliopita. Hili linaonyesha kuwa yale yanayosemwa katika hadithi yanahusu mtu tofauti na msimulizi. Mbinu hii ya usimulizi ndiyo inayochukua sehemu kubwa katika simulizi ya UFL. Kwa mfano,

katika beti chache zifuatazo, msimulizi anaonyesha sifa za Fumo Liyongo na maamuzi ya Wagalla kumhusu. Msimulizi anaeleza:

Mf 12

UFL
 Liyongo akikabili
 Ndiye kenenda rijali
 Alikwenda siku mbili
 Na ya pili ni kungiya (ub. 26)

“Twaitaka mbeu yake
 Nasi kwetu tuipeke
 Kwa furaha tumuweke
 Apate kutuzaliya” (ub. 41)

Katika beti hizi, msimulizi anaonyesha kwamba Fumo Liyongo alikuwa kijana wa ajabu aliyetenda mambo ya kiajabu. Msimulizi anaeleza kuwa alichukua muda wa siku mbili tu kwenda mwendo ambao ungechukua siku nne kwa mtu wa kawaida. Sifa hii ya kipekee ndiyo iliyowafanya Wagalla kutamani mbegu za Fumo Liyongo. Walitamani kuwa na mtu kama Fumo Liyongo na hivyo wakataka awazalie. Simulizi yenyewe inaendelezwa kwa njia inayomtamanisha msomaji kutaka kujua yale yaliyojiri kitendo baada ya kitendo.

Mohochi (2000) anaelezea kuwa katika mbinu ya usimulizi wa nafsi ya tatu mwandishi anajikita zaidi katika mhusika mmoja tu. Anajibana na kujipunguzia anayoyafahamu kwa kudhihirisha ufahamu wa mhusika mmoja peke yake. Anaendelea kutaja kwamba mwandishi haonyeshi kuwafahamu wahusika wake wengine. Mbinu hii aidha imetumika katika UFL. Mwandishi anatumia mbinu hii kwa “upendeleo” ili kuonyesha msisitizo alio nao kwa mhusika wake mkuu ambaye ni Fumo Liyongo. Anaendeleza simulizi kwa kuonyesha mfuatano wa matukio katika UFL. Beti zifuatazo zinaonyesha kuwa masharti yaliyotolewa na Sultani ya kutaka mbegu za Fumo Liyongo yalitimia. Beti 45 na 46 zinafafanua:

Mf 13

UFL
 Sharuti wakatimiza
 Liyongo wakamuoza
 Kwa furaha na kuteza
 Nyumbani akaingiya (ub. 45)

Mke katukuwa mimba
 Akazaa mwane simba
 Mwanamume wa kutamba
 Mwane Liyongo sikiya (ub. 46)

Beti 45 na 46 zinakamilisha matamaniao ya Wagalla kupata mbegu ya Fumo Liyongo jinsi ilivyoonyeshwa katika ubeti 41. Msimulizi anaeleza kwamba Wagalla walitimiza masharti yao ya kumwoza Liyongo mke (*Sharuti wakatimiza, Liyongo wakamuoza*) na baadaye mke huyo akachukua mimba na kumzaa mwana ambaye alikuwa na sifa za simba, kuonyesha umahiri wake (*Mke katukuwa mimba, akazaa mwane simba, mwanamume wa kutamba*). Hii ni moja kati ya sifa za kuonyesha mfuatano wa matukio katika hadithi, hivyo kuzua usimulizi katika tendi.

4.2.6 Usimulizi wa Nafsi ya Tatu katika UMM

Katika beti za mwanzo (1-10), mtunzi (msimulizi) anaanza kwa kutambua uwezo na uwezo wa Mola katika maisha yake. Mtunzi, ambaye ni msimulizi katika UMM, anaeleza hivi katika beti tatu (1, 7 na 8). Anaomba kibali kutoka kwa Mungu aweze ‘kusoma’ hadithi. Mtunzi anasadiki ukuu wa Mola kwa kutaja kuwa ni lazima afanye hivyo ili asije akahesabiwa makosa kwa kutotambua Mola. Hili analifanya kwa sababu ni jambo la kawaida kwa kila atungaye utenzi kumtambua Mungu kwani yeye ndiye apeanaye uwezo wa kutunga (Allen, 1971). Usimulizi wa nafsi ya kwanza, kama tulivyotangulia kutaja unahusisha msimulizi katika matukio yanayoendelezwa katika hadithi. Matumizi ya vivumishi vya sifa “ni” ni dhihirisho kwamba msimulizi anahusishwa na matukio katika simulizi kwa njia moja ama nyingine.

Mbinu iliyotumika kwa upana katika UMM ni mbinu ya usimulizi wa nafsi ya tatu. Katika mbinu hii, msimulizi anaripoti yale yaliyotukia katika hadithi. Genette (1980) anaita mbinu hii *heterodaigesia (heterodiegetic)*. Anafafanua mbinu hii kama inayotumiwa kutambulisha sauti ya msimulizi. Fludernik (2009) akielezea nadharia ya Naratolojia inayohusishwa na Genette (khj), anatambua kuwa usimulizi wa ki-heterodaigesia hutumika kuonyesha utengano wa msimulizi na ulimwengu wa kibunilizi. Anaeleza kwamba usimulizi wa aina hii hubainika kwa kutumia vivumishi vya sifa ‘a’, ‘yeye’ au ‘wao’.

Katika beti za 11- 16, msimulizi anaeleza kuhusu mhusika Mikidadi. Anataja kwamba Mikidadi alipofiwa na baba yake, hakurithi chochote na ilimbidi aende kuishi na mjomba wake (Turadi), kusudi amchungie mbuzi. Hili linaonyesha umaskini aliokuwa nao Mikidadi, kiasi cha kukosa kupata hata mke. Msimulizi anaeleza hivyo katika mistari ifuatayo:

Mf 14

UMM
 Urathi wa baba yake
 Mikidadi asishike
 Hakuwa hata na mke
 Kwa unyonge kumngia (ub.15)

Mf 14 unaeleza zaidi kuhusu umaskini wa Mikidadi, usimulizi unaotolewa katika nafsi ya tatu. Msimulizi anatoa taarifa ya maisha ya Mikidadi. Msimulizi anapotaja, kwa mfano kwamba *Mikidadi hakuwa hata na mke*, inaonyesha utengano wake na ulimwengu wa kibunilizi.

Mikidadi vilevile alikuwa na mjomba wa pili, Jabir, aliyekuwa na msichana mrembo kwa jina Mayasa. Urembo wa Mayasa ulisikika kwa mbali na karibu, hivyo kila mtu alitamani kumwoa. Waarabu walikusanya mali nyingi na kufunga safari kwenda kwao kumposa. Hata hivyo, walikutana na masharti kwamba kila aliyetaka kumwoa Mayasa

ilikuwa ni sharti apigane naye, mapigano ya kifo. Yule ambaye angemshinda (Mayasa) angekuwa mume wake. Msimulizi anaeleza:

Mf 15

UMM
Aliambia shuruti
Mume mtaka binti
Akhitarie mauti
Ndiyo aliyonambia (ub.31)

Shoti apigane naye
Hiyo ndiyo shartiye
Na mtu amshindaye
Ndiye mume wa kuoia (ub.32)

Mbali na kufafanua masharti yaliyotolewa na Mayasa katika beti 31 na 32, msimulizi anaonyesha kwamba kuna mazungumzo yanayoendelea kati ya Mayasa, baba yake Jabir na wale waliotaka kumposa. Hivyo, usimulizi unabainisha mazungumzo baina ya wahusika. Msimulizi anaripoti maneno yaliyosemwa na mhusika (Jabir); *Aliambia shuruti Ndiyo aliyonambia... Shoti apigane naye*. Jabir anaeleza wageni wake kuhusu masharti yaliyotolewa na binti yake, Mayasa. Mazungumzo yanayoendelea baina yao yanaendeleza kisa katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Wamitila (2008) anaeleza aina hii ya mazungumzo ya kishairi "...kuna mazungumzo ambayo hutokea baina ya wahusika lakini ambayo yanafungamanishwa na hadithi ya shairi kama inavyotokea katika tenzi na tendi nyingi". Mazungumzo yenyewe huwa yamesimuliwa.

Kisa hiki kinaendelea kuonyesha juhudi za Mikidadi za kumposa Mayasa na vilevile masharti ya Mayasa kwa mume atakaye kumwoa. Wawili hao walipigana na hatimaye kila mmoja akapendezwa na mwenzake jinsi inavyosimuliwa katika beti zifuatazo:

Mf 16

UMM
 Mayasa kuona hivyo
 Mikidadi aanavyo
 Na upanga apigavyo
 Kamjua ni shujaa (ub. 116)

Kawambie Warabuo
 Warudi na mali yao
 Mume wangu nitakao
 Ni huyu nimekwambia (ub. 126)

Baada ya kuridhika kuwa Mikidadi ndiye mume aliyemtaka, Mayasa akamweleza baba yake ambaye alikuwa bado hajaridhika, kwani alitaka bintiye aolewe na angalau mtu tajiri. Mayasa anakataa mtu mwingine isipokuwa Mikidadi. Jambo hili linamfanya baba yake kumwekea Mikidadi mahari ya mali nyingi sana huku akitakikana kutimiza katika muda wa miezi mitatu. Mikidadi anafanya bidii kutafuta mali kwa udi na uvumba. Anakutana na askari jeshi wa Sultan na anawanyang'anya mali yote waliyokuwa nayo. Habari za mikadadi zilienea na waliporudi kwa Sultan na ripoti hiyo, Sultani anashangaa jinsi jeshi lake lilivyoshindwa na mtu mmoja. Msimulizi anaeleza:

Mf 17

UMM
 Mtu huyo awanaje
 Upanga aushikaje
 Aula autupaje
 Naye ni mtu mmoja (ub.352)

Awanaje mtu huyo
 Hata mkatoka mbiyo
 Silaha mlio nayo
 Jamii kawatwalia (ub.353)

Mikidadi anaendelea kutafuta mahari kwa kupigana vita na kila mpitanjia. Mahali pengine alipigana na askari elfu moja walioteuliwa na Sultan kusudi aone ujasiri na ushujaa wa Mikidadi. Wawili hao (Sultan na Mikidadi) wanawekeana miadi hivi

kwamba yule ambaye angeshindwa, angenyang'anywa mali yake yote pamoja na farasi pia. Vita vilipoanza Mikidadi anawashinda wote. Sultan anashangaa huku akifurahishwa na Mikidadi, jambo lililomfanya kumpatia chochote alichohitaji. Hivyo basi, Mikidadi alipata mali ya kutosha kumpelekea Jabiri kama mahari.

Katika sehemu ya mwisho wa utendi, usimulizi unaendelea katika nafsi ya tatu kwa kuelezea habari za Mikidadi na Jabiri. Jabiri aliposikia kuwa Mikidadi amerudi na kwamba amemtwa Mayasa kuwa mkewe, aliingiwa na hofu sana ingawa alimpokea Mikidadi kwa kumfanyia karamu. Katika beti 667- 675, msimulizi anaonyesha hila za Jabir za kumwua Mikidadi. Jabir anamwandikia Sheikh barua huku akimwelezea habari zote Mikidadi na kumwagiza amwue. Hivyo, katika sehemu hii kuna matumizi ya barua japo katika usimulizi wa nafsi ya tatu. Ili kutimiza mpango wao wa hila, Jabir alitengeneza karamu kwa Mikidadi na watu wake. Katika hali hiyo, Mikidadi alipewa pombe aliyokunywa hata akapotewa na fahamu. Hapo ndipo alipofungwa kwa kamba tayari kwa mateso na mauaji. Msimulizi anaeleza katika beti zifuatazo:

Mf 18

UMM
Hata zikija akili'
amefungwa silisili
na mapingu ya rujuli
Mikidadi akalia (ub.690)

Akalia kwa mayowe
hino dunia ya lewe
ee msiba wa kuwe
mamaye kamlilia (ub.691)

Wakati huu mgumu kwa Mikidadi ulimfanya kumkumbuka mama yake (Tamima). Ikawa kwamba mama alipoona hatari iliyomkabili mwanawe, alifanya haraka kwenda kutafuta usaidizi. Malaika Gabrieli alitumwa na Mungu huko Medina ili kumpeleka mamaye Mikidadi kwa nabii. Beti 695-700 zinaeleza maelekezo ya Mungu kwa Malaika Gabriel na Malaika Mikail kuhusu usaidizi waliofaa kumpatia mamaye

Mikidadi. Tamima alipofika Medina alimpata Mtume Mohammed ambaye tayari alikwisha kupata habari ya Mikidadi. Hivyo basi, Mtume aliagiza Ali na Haidari kwenda upesi ili waweze kumtetea Mikidadi kabla Jabir hajamwua. Msimulizi anaeleza kuwa Mikidadi alikuwa amefungwa na alikuwa anangoja kuuawa ifikapo asubuhi (beti 717-719). Masimulizi hayo yanatolewa kama ripoti, hivyo usimulizi wa nafsi ya tatu unatumika katika sehemu hii ya mwisho wa utenzi. Ali na Haidari walifika maskani mwa Jabir upesi na kupata fursa ya kuokoa maisha ya Mikidadi. Msimulizi anasema:

Mf 19

UMM
 Ali akisafika
 Mikidadi kamshika
 mikufu aliyovikwa
 jamii akaivua
 (ub.743).

Baada ya Mikidadi kufunguliwa, vita vilianza ambapo Jabir na Malik waliuawa. Hapo Mikidadi anaulizwa iwapo angetaka kuwa gavana wa nchi hiyo au angependa kurudi kwa Mtume Muhammed ili apigane vita vya jihadi kwa niaba yake. Mikidadi, Ali na Haidari walikusanya mali yote kisha wakagawia wale waliojiunga na dini ya Kiislamu. Walifunga safari kwenda kwa Mtume aliyewakaribisha kwa kufanya karamu kubwa kwa watu wote, miongoni mwao vipofu na hata viwete. Katika kumaliza usimulizi, msimulizi anataja kwamba amehitimisha hadithi ya Mikidadi na Mayasa na akawataka waliosikiliza (au kusoma) waiendeleze kwa kizazi kingine. Tunapata hayo katika beti za mwisho.

Mf 20

UMM
 Kisa utendi wa vita
 simulia yalopita
 Hijazi yenye matata
 jamaa nimewambia (ub. 777)

Nami mwenye kuradidi
 Ismu yangu Saidi
 wa Abdalla Masudi
 Jina langu nawambia (ub. 778)

Beti za mwisho zinaashiria mwisho wa simulizi na msimulizi anajitambulisha. Maneno katika beti 777 na 778 ni ishara kuwa msimulizi amehitimisha kisa chake. Inabainika kwamba mbinu ya usimulizi wa nafsi ya tatu inatumika hasa katika usimulizi wa ngano katika fasihi simulizi. Hivyo, UMM ni usimulizi (utenzi) ambao umetumia kwa upana mbinu ya usimulizi wa nafsi ya tatu.

4.2.7 Usimulizi wa Nafsi ya Tatu katika UG

Mbinu ya usimulizi wa nafsi ya tatu katika UG imetumika kuonyesha kuwa msimulizi hakuwa mshiriki katika matukio yaliyotokea. Msimulizi anaripoti yaliyojiri hivyo kuashiria kwamba yeye hajashiriki katika matukio husika. Msimulizi anaonyesha kuwa huenda ameona au kusikia yaliyotendeka katika kisa chenyewe. Mbinu hii imetumika katika sehemu chache katika UG. Kwa mfano, katika kibao cha V, ukurasa wa 18, tunasikia sauti ya msimulizi katika mistari ifuatayo:

MF 21

UG	
M.A	M.T(tafsiri yangu)
...They stood at the forest's edge, gazing at the top of the Cedar Tree, gazing at the entrance to the forest, where Humbaba would walk there was a trail... (Tablet v:18)	...Walisimama pembeni mwa msitu, wakitazama kilele cha mti wa mkangazi, wakitumbulia macho kiingilio cha msitu. Palikuwa na alama kila ambapo Humbaba alitembea... (Kibao V:18)

Msimulizi anaonyeshwa kama aliyeshuhudia matendo yaliyotendeka katika hadithi.

Ni kana kwamba walikuwa wameandamana na wahusika waliotajwa (Gilgamesh na Enkidu). Anaonyesha kutoshiriki katika matukio kwa kutaja kwamba '*walisimama pembeni*'. Aidha, msimulizi anasimulia kile alichoonwa kwa kueleza kuwa '*Palikuwa*

na alama kila ambapo Humbaba alitembea...'. Msimulizi anaripoti kuwa aliona nyayo za Humbaba kwani kila Humbaba alipokanyaga, kulikuwa na alama. Katika sehemu nyingine, mbinu hii inabainika katika mistari ifuatayo:

MF 22

UG

M.A	M.T(tafsiri yangu)
<i>(Enkidu lies down a first day, a second day, That Enkidu....in his bed;</i>	(Enkidu analala chini siku ya kwanza, ya pili,
<i>A third day and fourth day, that Enkidu...in his bed;</i>	Siku ya tatu na ya nne, Yule Enkidu...kitandani mwake;
<i>A fifth, a sixth, and seventh, that Enkidu...in his bed;</i>	Siku ya tano na sita na ya saba, Yule Enkidu...kitandani mwake;
<i>An eighth, a ninth, a tenth, that Enkidu...in his bed</i>	Siku ya nane, ya tisa, ya kumi, Yule Enkidu...kitandani mwake
<i>Enkidu's illness grew ever worse...).</i>	Maradhi ya Enkidu yalizidi kuwa mabaya...) (Kibao VII:29)

Maneno katika dondoo hili yanamtambulisha msimulizi aliyeshuhudia masaibu ya mhusika, Enkidu, hivyo kuelezea yaliyotokea. Katika usimulizi wa nafsi ya tatu vilevile, usimulizi huhusisha hadithi. Maneno yaliyokolezwa, kwa mfano **yule Enkidu...kitandani mwake;** yanaonyesha kwamba kuna kisa fulani kinachozungumziwa ambacho kinahusisha mhusika Enkidu.

Katika muktadha huu, msimulizi anafafanua kwamba afya ya Enkidu ilizidi kudhoofika baada ya kukabiliana na Humbaba akiwa na rafiki yake Gilgamesh msituni, hivyo kulala tu kitandani mwake. Usimulizi wa nafsi ya tatu umetumika pakubwa katika UG kuelezea kisa cha Gilgamesh, mhusika mkuu katika *Utendi wa Gilgamesh*.

4.2.8 Usimulizi wa Nafsi ya Tatu katika SS

Simulizi ya Samsoni inatokea wakati ambapo Waisraeli walikuwa wamemuasi Mungu. Waisraeli walikuwa wametenda mabaya na hivyo Mungu akawaadhibu kwa kuwaweka katika mikono ya Wafilisti kwa muda wa miaka arobaini (Waamuzi 13:1).

Hivyo basi, Samsoni ndiye aliyekuwa mwamuzi wa kumi na tatu na wa mwisho katika historia ya Waamuzi wa wana wa Israeli. Ingawa mbinu ya usimulizi wa nafsi ya tatu ilitumika pakubwa katika SS, kisa cha Samsoni kinaanza kwa mtindo wa usimulizi wa kinathari. Katika mfano ufuatao, msimulizi anasema:

Mf 23

SS

Palikuwa na mtu mmoja wa Sora, wa jamaa
ya Wadani, jina lake akiitwa Manoa, na
mkewe alikuwa tasa, hakuzaa watoto
(Waamuzi 13:2)

Msimulizi anatoa maelezo ya wazazi wa Samsoni kwa njia ya kihadithi. Matumizi ya maneno *Palikuwa na...* yanaonyesha kwamba kuna jambo fulani ambalo msimulizi anatarajia kuliieleza. Hii ni mbinu ambayo imezoeleka katika uandishi wa riwaya katika fasihi. Aidha, ni mbinu inayotumika katika fasihi simulizi hasa katika utambaji wa hadithi. Msimulizi anatoa mtiririko wa kisa chote kwa kutoa taarifa ya yale yaliyotokea kwa kutumia mbinu ya usimulizi wa nafsi ya tatu. Katika Waamuzi 13:3 msimulizi anasema:

Mf 24

SS

Malaika wa BWANA akamtokea yule mwanamke,
akamwambia, Tazama, wewe sasa u tasa, huzai, lakini
utachukua mimba,
nawe utamzaa mtoto mwanamume (Waamuzi 13:3)

Sehemu zilizopigwa mstari zinaonyesha kwamba msimulizi anaelezea mambo yatakayomfanyikia mwanamke yule. Aidha, kiumbe anayeripotiwa kumzungumzia mwanamke yule si wa kawaida kwani ni malaika. Katika mbinu ya usimulizi wa nafsi ya tatu, msimulizi anasimulia matukio ambayo hakuyashiriki. Mkabala huu unazidi kubainika katika vifungu vifuatavyo:

Mf 25

SS

Ndipo huyo Manoa akamwomba BWANA akisema,
Ee Bwana, nakuomba, Yule mtu wa Mungu
uliyemtuma na aje kwetu mara ya pili, atufundishe
hayo yatupasayo kumfanyia huyo mtoto atakayezaliwa
(Waamuzi 13:8).

Katika muktadha huu, Manoa, baba wa mtoto atakayezaliwa (Samsoni) anamwomba Mungu amtume Malaika wake kwa mara ya pili ili awafundishe jinsi watakavyomtunza mtoto atakayezaliwa. Hii ni kwa sababu mkewe alipewa masharti ya kufuata kabla ya mtoto kuzaliwa na hata baada ya kuzaliwa. Ilikuwa kwamba mtoto huyo angekuwa mnadhiri wa Mungu tangu tumboni hadi kufa kwake. Kwa sababu hiyo, mama alipaswa ‘kujiweka safi’ kwa kutokunywa divai wala kileo chochote hadi wakati wa kujifungua. Aidha, mtoto atakayezaliwa asinyolewe nywele zake hadi kufa kwake.

Maelezo ya matukio yaliyofuatia hapo yanaendelezwa kwa kutumia mbinu ya usimulizi wa nafsi ya tatu. Msimulizi anaeleza tendo la ajabu lililofanywa na Samsoni kama njia ya kulipiza kisasi. Anaeleza kwamba Samsoni alienda kuwakamata mbweha mia tatu (300) na kuchukua vienge vya moto na kuwafunga mbweha hao mkia kwa mkia. Msimulizi anasema:

Mf 26

SS

Alipokwisha kuviwasha moto vile vienge akawaachia mbweha kati ya ngano ya Wafilisti, akayatekeleza matita na ngano, hata na mashamba ya mizeituni (Waamuzi 15:5).

Matumizi ya mofimu *a-* na *li-* ya wakati uliopita ni dhahirisho kwamba msimulizi anaelezea matukio yanayohusu mtu mwingine. Mbinu hii imetumika kwa upana katika sura za 15 na 16.

Katika tukio jingine lililofuata, Wafilisti walimteketeza yule mke wa Samsoni pamoja na baba yake baada ya kugundua kwamba yeye ndiye aliyesababisha hasira za Samsoni za kuwachomea ngano. Mara hiyo, Samsoni tena alikasirika kwa sababu ya mauaji ya mkewe, na kuwaahidi Wafilisti kwamba wangejuta. Katika hali ya kulipiza kisasi, Samsoni aliwaua Wafilisti elfu moja kwa kutumia mfupa wa taya ya punda jinsi inavyoelezwa katika (Waamuzi 15:15-16).

Katika sura 16, mbinu ya usimulizi wa nafsi ya tatu inazidi kutumika. Katika mwanzo wa sehemu hii, msimulizi anaonyesha wanawake wawili walioteka makini ya Samsoni, mmoja ni kahaba asiyetajwa jina na wa pili ni Delila.

Mf 27

SS

1) Samsoni akaenda Gaza, akaona huko mwanamke kahaba, akaingia kwake. 2) Watu wa Gaza wakaambiwa, ya kwamba, huyo Samsoni amekuja huku. Wakamzingira, wakamvizia usiku kucha, penye lango la mji, wakanyamaza kimya usiku kucha, wakisema, Na tungoje mpaka mapambazuko ndipo tutamwua. 3) Basi Samsoni akalala hata usiku wa manane, akaondoka katikati ya usiku, akaishika milango ya lango la mji, na miimo yake miwili, akaing'oa pamoja na komeo lake, akajitwika mabegani, akavichukua hata kilele cha mlima ule unaokabili Hebroni (Waamuzi 16:1-3).

Vifungu hivi, vinasimulia hadithi ya mwanamke kahaba aliyependwa na Samsoni. Msimulizi anaeleza kwamba Samsoni alipoenda Gaza, aliona mwanamke kahaba na akaingia kwake. Watu wa Gaza walipojua kwamba Samsoni alikuwa pale, walimzingira wakiwa na nia ya kumwua asubuhi. Hata hivyo, Samsoni aliamka usiku wa manane akaishika milango ya lango kuu la mji, akaingia na vizingiti vyake akavitwika mabegani hadi mlimani.

Baada ya matukio hayo, Samsoni alimpenda tena mwanamke kwa jina Delila. Wakishajua kwamba Delila amekuwa mke wa Samsoni, wakuu wa Wafilisti walimshauri Delila kumbembeleza mumewe ili apate kujua siri za nguvu zake. Delila

hivyo basi alianza kazi yake ya kumrairai Samsoni kusudi ajue kiini cha nguvu zake. Mazungumzo baina yake na Samsoni yanasimuliwa katika vifungu 6-15. Msimulizi anaonyesha matukio mawili ambayo Samsoni alifungwa kwa kamba lakini alizikata zile kamba kama akatavyo uzi (Waamuzi 16:7-11).

Mbinu ya usimulizi wa nafsi ya tatu inatumika vilevile katika matukio yaliyofuata. Hata hivyo, mbinu hii inahusisha mazungumzo hasa baina ya Samsoni, Delila na Wafilisti. Delila aligundua kwamba Samsoni hakumweleza ukweli na aliendelea kumsumbua kwa maneno yake kila siku hata roho ya Samsoni ikadhikika. Kwa sababu hiyo, Samsoni aliona heri kumweleza mkewe ukweli kuhusiana na nguvu zake. Katika Waamuzi 16:17, msimulizi anasema:

Mf 28

SS

Ndipo alipomwambia yote yaliyokuwa moyoni mwake, akamwambia, wembe haukupita juu ya kichwa changu kamwe; maana mimi nimekuwa mnadhiri wa Mungu, tangu tumboni mwa mama yangu, nikinyolewa, ndipo nguvu zangu zitanitoka, nami nitakuwa dhaifu, nitakuwa kama wanadamu wenzangu (Waamuzi 16:17).

Katika kifungu hiki, usimulizi wa nafsi ya tatu umetumika. Katika aina hii ya usimulizi, wahusika wanazungumza wenyewe pasipo kuingiliwa na mtunzi/msimulizi. Burundi (2014), anasema kuwa ni usimulizi unaobainika katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* ambapo mtunzi anawaacha wahusika kuzungumza na kusemezana baina yao bila kuwaingilia. Katika *Simulizi ya Samsoni*, mbinu hii imetumika katika sehemu ya mwisho ambapo Samsoni, Delila na Wafilisti wanazungumza. Katika Waamuzi 16:18, Delila anawaambia Wafilisti, “Njooi huku mara hii tu, maana ameniambia yote aliyo nayo moyoni mwake”. Katika tukio hilo basi, wakuu wa Wafilisti walimwendea Samsoni baada ya kunyolewa vile vishungi saba vya nywele za kichwa chake na mkewe Delila, ambapo nguvu zake zilimtoka.

Sehemu ya mwisho ya *Simulizi ya Samsoni* inaeleza jinsi Samsoni alivyowaua watu wengi, yeye akiwemo. Mbinu ya usimulizi wa nafsi ya tatu inaendelea kutumika. Msimulizi anaeleza mauaji yaliyotokea wakati Samsoni alipomlilia Mungu wake kumrejeshea nguvu zake ili aweze kulipiza kisasi juu ya Wafilisti kwa ajili ya kung'olewa macho yake mawili. Katika Waamuzi 16:29, msimulizi anasema:

Mf 29

SS

Kisha Samsoni akazishika nguzo mbili za katikati ambazo nyumba ile ilikaa juu yake, akazitegemea, moja kwa mkono wake wa kiume na moja kwa mkono wake wa kushoto...Akainama kwa nguvu zake zote, ile nyumba ikawaangukia hao wakuu, na watu wote waliokuwa ndani yake (Waamuzi 16:29).

Matumizi ya mofu *ali-* na *aka-* katika kifungu hiki inaonyesha kwamba msimulizi hajahusika bali ni masimulizi yanayohusu mtu mwingine. Mhusika anayezungumziwa ni Samsoni, ambaye ni mhusika mkuu katika simulizi. La kustaajibisha ni kwamba Samsoni aliwaua watu wengi wakati wa kufa kwake kuliko wale aliowaua wakati wa uhai wake. Simulizi inafikia tamati kwa kutaja maziko ya Samsoni, katika kiwanja cha kuzikia cha Manoa, baba yake. Msimulizi anatamatisha kwa kueleza kuwa Samsoni alikuwa mwamuzi wa Israeli kwa muda wa miaka ishirini (Waamuzi 16:31).

4.3 Usimulizi Maizi katika SS

Katika sura ya kumi na nne, mbinu inayotumika ni usimulizi maizi. Kisa kinachozungumziwa kinahusu ndoa ya Samsoni. Hapa, msimulizi anaonyesha kujua yote yanayotendeka katika maisha ya Samsoni. Hata hivyo, usimulizi maizi umetokana na usimulizi wa nafsi ya tatu. Maelezo hayo yametolewa na Madumulla (2009):

Usimuliaji maizi, kwa kiasi kikubwa, ni matokeo ya usimuliaji wa nafsi ya tatu. Kwani katika usimuliaji maizi, mtunzi huenda kutoka kwa mhusika mmoja hadi mwingine, mahali pamoja hadi pengine, tukio moja hadi jingine, huku akijipa uhuru mkubwa kabisa wa

kuingia katika fikra na hisia za hao wahusika wake kadri atakavyo na kuwapatia habari na mielekeo jinsi anavyotaka.

Maelezo ya Madumulla yanaonyesha kwamba usimulizi maizi unaenda hatua moja mbele ya usimulizi wa nafsi ya tatu. Msimulizi anaonekana kuelewa yale yanayopitiwa na mhusika katika mawazo yake. Mbinu hii imetumika wakati Samsoni alitaka mwanamke kutoka Timna, mmojawapo wa binti za Wafilisti. Hata hivyo, wazazi wake hawakukubali kwa sababu Wafilisti walikuwa na mila tofauti na wao, ya kutotahiri. Hapo ndipo msimulizi anaonyesha kwamba anajua mambo yote kwa kusema:

Mf 30

SS

Lakini baba yake na mama yake hawakujua ya kuwa jambo hili ni la BWANA; maana alitaka kisa juu ya Wafilisti (Waamuzi 14:4).

Kifungu hiki kinaonyesha kwamba msimulizi anaelewa kuwa jambo hili lilitokea kwa sababu ya mpango wa BWANA (Mungu). Ina maana kwamba msimulizi ana hisia zinazolinganishwa na za Mungu. Katika hali ya kawaida ni vigumu kuelewa hisia na mipango ya Mungu. Msimulizi anaonyesha kujua zaidi kuliko baba na mama ya Samsoni anapotaja kwamba *baba yake na mama yake hawakujua ya kuwa jambo hili ni la BWANA*. Vilevile, usimulizi maizi unatumika katika kifungu cha sita, wakati Roho wa Mungu anapomshukia Samsoni hivi kwamba anaweza kumpararua simba kama mwanambuzi. Msimulizi anaeleza:

Mf 31

SS

Roho ya BWANA ikamjilia kwa nguvu, naye akampasua kana kwamba anampasua mwanambuzi, wala hakuwa na kitu chochote mkononi mwake, lakini hakuwaambia baba yake na mama yake aliyofanya (Waamuzi 14:6).

Msimulizi anaposema kwamba ‘Roho ya Bwana ikamjia kwa nguvu’ inamaanisha alikuwa na sifa zisizo za kawaida kwa sababu ‘Roho’ si kitu kinachoweza kuonekana

kihalisi kwa macho. Ni vigumu kupata taswira ya jinsi *Roho ya Bwana ilipomjia* mhusika Samsoni *kwa nguvu*. Msimulizi anaonyesha kuwa na uhuru mwingi kiasi cha kuelewa mambo ya uungu. Usimulizi maizi unadhihirika vilevile baada ya Samsoni kunyolewa. Msimulizi anasema:

Mf 32

SS

Akaamka katika usingizi wake, akasema, nitakwenda nje kama siku nyingine, na kujinyosha. *Lakini hakujua ya kuwa BWANA amemwacha* (Waamuzi 16:20b).

Kifungu hiki kinaonyesha kuwa msimulizi alikuwa na uwezo wa kutambua kwamba nguvu alizokuwa nazo Samsoni hapo awali zilikuwa zimemtoka. Maneno '*Lakini hakujua ya kuwa BWANA amemwacha*' yanaonyesha kuwa msimulizi alikuwa na uwezo wa kuelewa mambo yaliyokuwa yamemfika Samsoni hata kabla ya Samsoni mwenyewe kutambua. Msimulizi alikuwa na uwezo wa kutambua kuwa 'BWANA' alikuwa amemwacha Samsoni. Mbinu ya usimulizi maizi hapa imetumika kuonyesha mambo yasiyokuwa ya kawaida kwa binadamu. Baada ya Samsoni kukamatwa na Wafilisti, aling'olewa macho, akapelekwa hadi mji wa Gaza, akafungwa kwa vifungo vya shaba na kupewa kazi ya kusaga ngano mle gerezani. Msimulizi anasema kuwa Wafilisti walifurahia sana kuona Samsoni alikipitia dhiki mikononi mwao. Hata hivyo, msimulizi anaeleza kuwa nywele zake Samsoni zilimea tena.

Kutokana na maelezo yaliyotolewa kuhusu SS, UFL, UMM na UG, inabainika kwamba usimulizi ni moja kati ya mbinu zinazotumika kuwasilisha ujumbe katika matini teule. Matukio mbalimbali yanayobainika yanajenga mtiririko wa hadithi katika matini teule. Mbinu za kisimulizi zilizobainika katika matini za utafiti huu ni usimulizi wa nafsi ya kwanza, nafsi ya tatu, usimulizi wa ki-utendi na usimulizi maizi.

4.4 Mwingiliano wa Kimuundo katika UFL, UG, UMM na SS

Dhana ya muundo katika uchambuzi wa ushairi wowote ni muhimu. Kazi zozote za kifasihi huhusiana kwa njia moja ama nyingine. Aidha, uhusiano huu huweza kuwa wa kimuundo, kimaudhui na usawiri wa wahusika. Baadhi ya vipengele vya kimuundo katika ushairi ni mizani, mishororo, beti na vina. Vipengele hivi hukamilishana ili kuunda kazi nzima ya ushairi. Katika uchambuzi wa ushairi, ni muhimu kuzingatia muundo wa ndani na muundo wa nje. Hivyo, mtiririko wa kazi ya kifasihi hutegemea muwala wa vipengele vyote vya kimuundo.

4.4.1 Mwingiliano katika Kitangulizi

UFL, UG, UMM na SS zinaonyesha kuwa kuna uwiano wa kimuundo katika kaida za utunzi wa tenzi. *Utenzi wa Fumo Liyongo* unianza kwa kutanguliza ukuu wa Mwenyezi Mungu sawa na *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*.

Mf 33

UFL

Bismillahi nabutadi
Kwa ina la Muhammadi
Nandikie auladi
Nyuma watakaokuya (ub.1:23)

UMM

Bismillahi Mbuyaza
awali ya kujifunza
sijui taufawaza
au vitanichachia (ub.1:1)

Matumizi ya maneno, '*Bismillahi nabutadi*' na '*Bismillahi Mbuyaza*' katika beti hizi mbili yanadhihirisha kwamba watunzi wanaelewa fika kuwa uwezo wa utunzi hutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hii ndiyo sababu msimulizi katika UMM anataja kwamba hajui kama atafaulu au la (*sijui taufawaza au vitanichachia*). Kwa sababu hiyo, anaona ni heri kufanya yote anayonua kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Watunzi wa tenzi huonekana kutambua ukuu wa Mungu katika kazi zao. Hivyo, hutanguliza

shukrani kwake kwa sababu ya kuwapa uwezo wa utunzi husika. Aidha, ‘Bismillahi’ katika dini ya Kiislamu ni ‘Kwa jina la Mwenyezi Mungu’ na ni desturi ya Waislamu kulitanguliza jina lake Mungu kabla ya kulifanya jambo lolote. Katika UMM, msimulizi vilevile anaomba baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Anasema:

Mf 34

UMM
Sasa nitatawakali
Bismillahi awali
yu pweke Rabi Jalali
ndiye pwekeye mmoya (ub.7:1)

Msimulizi anaomba baraka za Mungu. Anadhukuru ukuu wa Mungu na kukiri kwamba halinganishwi na mtu yeyote kwa kueleza *yu pweke Rabi Jalali, ndiye pwekeye mmoya*. Kuna marudio ya maneno *yu pweke Rabi Jalali* katika beti za saba, nane na tisa kuonyesha kuwa Mungu halinganishwi na yeyote, yeye pekee ana uwezo na kwamba baraka zake hazihesabiki (beti 7-11, UMM).

Katika *Utenzi wa Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni*, kitangulizi kinachukua mkabala tofauti. Wasimulizi wanaanza kwa kutaja sifa za wahusika wakuu, Gilgamesh na Samsoni mtawalia. Wanataja kuwa wahusika hao wana sifa za uungu. Msimulizi katika UG anataja kuwa Gilgamesh alitunukiwa ufahamu wote na kwamba anajua siri zote. Katika mstari wa tatu, Kibao cha kwanza, msimulizi anasema kwamba mhusika alitunukiwa ufahamu wa kila kitu, maelezo yanayolingana na maelezo yaliyotolewa kuhusu Samsoni katika Waamuzi 13:5b

Mf 35

UG

M.A	M.T(tafsiri yangu)
<i>(Anu granted him the totality of knowledge of all... supreme over other Kings, Lordly in appearance, Mighty net, Protector of His people) (Tablet 1:1)</i>	Anu alimtunuku ukamilifu wa ufahamu wote... Mkuu wa Wafalme wengine, mtawala mkuu. Jamvi kuu, mlinzi wa watu wake (Kibao 1:1)

SS

Maana mtoto huyo atakuwa mnadhiri wa Mungu tangu tumboni, naye ataanza kuwaokoa Israeli na mikono ya Wafilisti (Waamuzi 13:5b)

Mfano 35 unatoa maelezo ya wahusika wawili, Gilgamesh na Samsoni mtawalia. Msimulizi katika UG anaeleza kuwa Gilgamesh ana umbo la mungu na kwamba yeye ni mlinzi wa watu wake. Msimulizi katika SS pia anaeleza kuwa Samsoni atakuwa mnadhiri wa Mungu kabla ya kuzaliwa na kwamba ataiokoa Israeli kutoka katika utumwa wa Wafilisti. Maneno yaliyotumika katika sentensi ‘*Anu alimtunuku ukamilifu wa ufahamu wote*’ katika UG na ‘*Mtoto huyo atakuwa mnadhiri wa Mungu tangu tumboni*’, katika SS yanawiana kimatini kwa sababu ya utambuzi wa ukuu wa Mungu. Hata hivyo, tofauti vilevile inatokea kwa sababu ya misingi ya kidini na muktadha. UG ina misingi ya dini ya Kimesopotamia iliyokuwa na uhuru wa kuabudu miungu mingi (polytheism). Kwa sababu hii, ilikuwa vigumu kuwa na muundo maalum wa kutanguliza maandishi mbalimbali.

Simulizi ya Samsoni ina misingi ya dini ya Kikristo ambayo kwayo Mwenyezi Mungu anatambuliwa japo kwa majina tofautitofauti kulingana na uwezo wake. Katika muktadha wa *Simulizi ya Samsoni*, ametajwa kama BWANA Mungu. Kitabu cha Waamuzi kiliandikwa wakati Waisraeli walipokuwa katika ugandamizwaji na dhuluma kutoka kwa mataifa jirani kwa sababu ya kumuasi Mungu wao. Matukio yaliyoambatana na Waamuzi mbalimbali yalifanyika, hivyo kila tukio linaanza kwa kutaja vile Waisraeli walivyomuasi Mungu. Kwa mfano, katika Waamuzi 3:7,12, 6:1, 10:6, na 13:1, kitangulizi ni sentensi maalum, “Waisraeli wakafanya tena yaliyo maovu mbele za BWANA...”. Maelezo katika Waamuzi 13:5 katika mfano 35, yanatokea baada ya kifungu cha kwanza katika Waamuzi 13:1 kinachoeleza kuwa Waisraeli walikuwa wamefanya maovu tena mbele za BWANA, hivyo Mungu

akawatia mikononi mwa Wafilisti kwa muda wa miaka arobaini ndipo akamtuma Samsoni kuwaokoa.

Allen (1971) anaeleza kuwa tenzi za Swahili hasa zina muundo sawa, mtindo wa uandishi na matumizi ya lugha inayofanana. Anasema kwamba mara nyingi, beti za kwanza za tendi zinatanguliza maneno *Bismillahi*, *'rRahmani na 'rRahim*. Beti hizi zinatambua ukuu wa Mungu mwenye upendo na rehema. Aidha, anaeleza kwamba ukosefu wa utangulizi wa aina hii huenda ukaashiria kuwa ukurasa wa kwanza wa utendi umepotea au kubadilishwa kwa njia moja ama nyingine.

Beti za mwanzo za UFL, UG, UMM na SS, ni tangulizi za tendi zikifuatwa na dhamira za watunzi husika. Aghalabu, tangulizi zinatofautiana kwa urefu kutoka utenzi hadi utenzi. Kwa mfano, utangulizi wa UFL unatoka beti 1-3 na UMM beti 112 ilhali katika UG, kuna tofauti hivi kwamba mtunzi anaelezea sifa za mhusika mkuu katika kisa chake, kwa kumsawazisha na Mungu. Haya yanachukua sehemu kubwa katika mwanzo wa kibao cha kwanza. SS vilevile imechukua mkabala sawa na UG katika Waamuzi 13:1-25. Utangulizi unahusu kuzaliwa kwa Samsoni na sheria alizopewa mama yake kabla ya kuzaliwa kwa mtoto. Aidha, mtunzi anasisitiza kuwa mtoto atakayezaliwa ameteuliwa na atakuwa mnadhiri wa Mungu.

4.4.2 Mwingiliano katika Dhamira

Madhumuni ya watunzi katika matini teule yanafuata baada ya kitangulizi. Katika UFL, mtunzi anaeleza kuwa haja yake ni kuviandikia vizazi vijavyo visije vikasahau matendo ya mhusika, Fumo Liyongo. Katika beti za nne na tano, mtunzi anataja kwamba aliona heri aandike hadithi hii ya ajabu ili watu wapate kufahamu mambo yaliyomfika mhusika Liyongo. Katika beti 6-7 na 13-15, mtunzi anafafanua sifa zake

Liyongo, kwamba yeye alikuwa “mwanamume Swahihi” aliyefananishwa na simba (ubeti 13).

UMM unachukua mkondo uleule wa kueleza nia ya kisa husika. Mtunzi anatoa maelezo ya sifa za wahusika wake wakuu ambao ni Mikidadi na Mayasa. Katika beti 13-16 anaeleza umaskini wa Mikidadi kwamba baba yake alipofariki, hakurithi chochote kutoka kwake kwani mali yake “yalitawanyika”. Beti 17-20 zinatoa maelezo ya urembo wa Mayasa. Msimulizi anasema kuwa Mayasa alivutia watu wengi kwa uzuri na sifa za ushujaa wake. Aidha, mtunzi anaonyesha kuwa Mayasa alimtaka mwanamume jasiri aliyekuwa tayari kupigana naye, ili amwone kama alimfaa (ubeti 31). Hivyo, mtunzi anadhamiria kuonyesha kwamba yeyote aliyemtaka Mayasa alikuwa sharti akabiliane na vita mpaka kifo.

Msimulizi katika UG anasifia Gilgamesh kwa ushujaa wake. Madhumuni yake ni kufahamisha hadhira kuhusu matukio ya Gilgamesh na sifa za kiungu alizokuwa nazo. Katika mstari ufuatao, msimulizi anaelezea uzawa wake na kwamba mhusika hana dosari yoyote.

Mf 36

UG

M.A	M.T (Tafsiri yangu)
<i>(Offspring of Lugalbanda, Gilgamesh is strong to perfection, Son of the august cow, Rimat-Ninsun., Gilgamesh is awesome, Gilgamesh is awesome to perfection) (Tablet 1:1)</i>	Mzawa wa Lugalbanda, Gilgamesh, Hodari siye dosari, Mwana wa ng'ombe adhimu, Rimat...Ninsun., Gilgamesh anapendeza hana dosari (Kibao 1:1)

Msimulizi anasisitiza kuhusu uhodari wa Gilgamesh kwamba ni *hodari siye dosari*.

Msimulizi anadhamiria kufafanua ieleweke kwamba Gilgamesh si sawa na mtu yeyote yule ila yeye ni kamilifu, ni hodari na tena anapendeza.

Dhamira katika simulizi ya Samsoni imeelezwa katika sura ya kumi na tatu ya Waamuzi. Kwanza, mtunzi anatoa masharti yatakayofuatwa na wazazi (hasa mama) wa mtoto atakayezaliwa. Mama anaagizwa asinywe divai wala kileo au chochote kisicho safi. Katika Waamuzi 13:4-5, tunapata maelezo yafuatayo:

Mf 37

SS

Basi sasa, jihadhari, nakuomba usinywe divai wala kileo, wala usile kitu kilcho najisi, kwani tazama, utachukua mimba, nawe utamzaa mtoto mwanamume; na wembe usipite juu ya kichwa chake; maana mtoto huyu atakuwa mnadhiri wa Mungu tangu tumboni; naye ataanza kuwaokoa Israeli na mikono ya Wafilisti (Waamuzi 13:4-5)

Kifungu hiki kinaonyesha dhamira ya mtunzi. Anasema kwamba mtoto atakayezaliwa atakuwa mnadhiri wa Mungu. Kwa sababu hiyo, ilikuwa ni lazima mama mzazi ashauriwe jinsi ya kujitunza akiwa na mimba hadi kujifungua. Kupitia mhusika Samsoni, mtunzi anatuonyesha jinsi Waisraeli walivyookolewa kutokana na utumwa wa Wafilisti. Mwandishi anaonyesha kwamba ijapokuwa Waisraeli walikuwa wamemkosea Mungu, bado Mungu aliwarehemu kwa kuwatumia Samsoni kama mwokozi wao. Hata hivyo, mtunzi anasema kuwa Mungu aliwatia katika mikono ya Wafilisti kwa muda wa miaka arobaini (Waamuzi 13:1). Hii ina maana kwamba Waisraeli walikuwa chini ya utawala wa Wafilisti kwa miaka 40 kabla ya kuja kwake Samsoni.

Mwingilianomatini unaonekana katika kipengele hiki cha dhamira kwa namna ambavyo kazi husika imesukwa. Inabainika kwamba kila baada ya kitangulizi, mtunzi anaweka wazi madhumuni ya kuandika/kusimulia kisa chake. Nia ya mwandishi yeyote hubainisha vilevile maudhui yanayotarajiwa. Kutoka matini teule, maudhui yanayotokea yana uwiano wa kimwingiliano matini. Baadhi ya maudhui yanayobainika kimwingiliano matini ni kama vile mauaji, uongozi, mapenzi, usaliti

na majigambo. Maudhui haya yanatokea kupitia kwa wahusika wakuu katika matini teule.

Maudhui ya mauaji ya kikatili kwa mfano, yanawiana katika UG, UMM na SS. Katika UG, mauaji ya kikatili yanatokea pale ambapo Gilgamesh na Enkidu wanamwua Humbaba, mlinzi wa msitu wa Seda. Katika kibao cha tano, aya ya mwisho, mtunzi anasema:

Mf 38

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(They pulled out his insides including his tongue) (Tablet VI:21)</i>	...Walinyofoa viungo vyote vya ndani ya mwili ikiwemo ulimi (KibaoVI:21)

Haya yanaonyesha ukatili aliofanyiwa mhusika Humbaba. Tukio la *kunyofoa viungo vyote vya ndani ya mwili ikiwemo ulimi* ni ukatili wa hali ya juu. Taswira inayojengeka huenda ni ya kutatanisha. Aidha, mauaji mengine ya kikatili yanabainika wakati Gilgamesh na Enkidu wanamwua fahali wa mbinguni kwa kumchinja kisha kutoa moyo wake katika kibao cha sita. Ijapokuwa Fahali wa Mbinguni (Bull of Heaven) hakuwa binadamu lakini kwa kawaida mnyama yeyote hata kama anachinjwa, anachinjwa kwa utaratibu fulani.

Maudhui hayo yanawiana na mauaji ya kikatili katika UMM. Mikidadi alipokutana na jeshi la askari, anamwua kiongozi wao kwa unyama. Katika beti 236-238, maelezo hayo yanatolewa. Katika dondoo hili, msimulizi anasema:

Mf 39

UMM

Akamkamata ndevu
akazivuta kwa nguvu
akashika mashavu
kamtinda akamaa (ub. 237:15)

Akamkamata na rasu,
kwa mkonowe na kisu
akamuekea kesu
mbele ye kamuekea (ub. 238:15)

Kitendo cha kumkamata ndevu na kumkata shingoni, baada ya kumkalia kichwani (ubeti 236) ni unyama usiostahili kufanyiwa binadamu. Unyama uo huo unaelezwa katika mf 39. Msimulizi anataja kwamba Mikidadi anamkamata ndevu, anazivuta kwa nguvu, anamshika mashavu na *kamtinda akamaa*. Hii ina maana kwamba baada ya kumshika vizuri, Mikidadi anamkata shingoni na kummaliza kabisa (*kamtinda akamaa*). SS aidha inawiana katika maudhui yale yale ya kikatili na UG na UMM. Samsoni anawaua Wafilisti 1,000 kwa kutumia mfupa wa taya ya punda;

Mf 40

SS
Naye akaona mfupa mbichi wa taya ya punda, akautwaa, akapiga watu elfu kwa mfupa huo (Waamuzi 15:15)

Hapa ni dhahiri kwamba ukatili upo katika nafsi ya Samsoni. Matumizi ya taya ya punda katika kutekeleza mauaji ya watu elfu moja yanashangaza. Hata hivyo, ni jambo la kutoaminika kwa binadamu wa kawaida kufanya mambo kama hayo.

Maudhui ya usaliti yanayobainika katika utenzi wa Fumo Liyongo yanaonekana vilevile katika UMM na SS. Usaliti unaendelezwa na mwana wa Liyongo. Kijana anaahidiwa mali, cheo cha uongozi na kumwoa binti wa mfalme iwapo atatambua siri ya nguvu za baba yake (UFL, ubeti 127). Uwiano huu pia unaonekana katika UMM, kupitia kwa mhusika Jabir, ambaye ni mjomba wa Mikidadi. Anamsaliti Mikidadi kwa kumkaribisha kwake, kumpa vileo na baadaye kumtia nguvuni ili Maliki (rafiki yake) apate nafasi ya kumwua kwa ajili ya kulipiza kisasi (UMM, beti 667-691). Katika SS usaliti unaonyeshwa wakati Delila, mkewe Samsoni anapofichua siri ya nguvu za mumewe kwa Wafilisti, ambao walikuwa ni maadui wa Samsoni. Katika Waamuzi 16:18, mtunzi anasema:

Mf 41

SS

Delila alipoona ya kuwa amemwambia yote yaliyokuwa moyoni mwake, akatuma mtu akawaita wakuu wa Wafilisti, akisema, njooni huku mara hii tu, maana ameniambia yote aliyo nayo moyoni mwake (Waamuzi 16:18).

Badala ya Delila kumtunza na kumficha mumewe dhidi ya maadui wake, anachukua mkondo tofauti wa kumsaliti. Baada ya Delila kufaulu katika hila zake za kutaka kujua chanzo cha nguvu za mumewe, anafanya hima kuwaita wafilisti ili kuwaeleza yaliyojiri kwa kusema *njooni huku mara hii tu, maana ameniambia yote aliyo nayo moyoni mwake*. Mtiririko wa visa katika matini teule unaonyesha uwiano kutokea mwanzo hadi mwisho. Katika sehemu inayofuata, utafiti umebainisha mwingilianomatini kwa kuonyesha jinsi kila kisa katika matini teule kinavyotamatishwa.

4.4.3 Mwingiliano katika Kimalizio

Dhihirisho la mwingilianomatini wa kimuundo katika UFL, UG, UMM na SS vilevile linaonekana katika sehemu ya mwisho wa kila hadithi. Kuna mfanano kati ya *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Katika tungo zote mbili, hadithi inaisha kwa maombi. Katika UMM, hili linaonekana katika beti 228-232. Tutachukua mfano wa ubeti 228 unaoesema;

Mf 42

UMM

Tumeziya kukhitimu

hapo ndio wasalamu

Illahi tatukirimu

kwa baraka na afiya (ub. 228:15)

Kifungu hiki kinaonyesha kuwa mtunzi wa utendi amefika mwisho. Anaomba baraka na afya njema kutoka kwa Mungu. Katika sehemu ya mwisho ya UMM, Mikidadi

anajiunga na dini ya Kiislamu baada ya kupigana vita na askari wa Sayid Ali. Baadaye, anajifunza sheria za dini ya Kiislamu na hatimaye kupigana vita vya jihad.

Katika karamu ya harusi yao, watu wanakula na kunywa, ikiwa ni pamoja na vipofu na viwete. Mwisho, mtunzi anataja kwamba amehitimisha hadithi ya Mikidadi na Mayasa kwa kutaja jina lake. Aidha, anawasihi waliosikiliza au kusoma wawaeleze kisa hiki kwa vizazi vijavyo. Pamoja na hayo, malaika Gabriel anampa salamu na baraka nyingine. Msimulizi anasema:

Mf 43

UMM
 Kaletewa Jibrili
 akamwambia Rasuli
 akusalimu Jabbari
 na mengine akamwambia (ub. 769:49)

Jambo linalodhihirika ni kuwa katika kumalizia utendi, msimulizi hakosi kutaja mwenyezi Mungu kama mweza yote na mwenye kutoa baraka kwa mtunzi. Si jambo la kawaida kuletewa salamu na malaika (*Kaletewa Jibrili...akusalimu Jabbari*). Kuna ulinganifu katika salamu za malaika ambazo mara nyingi hufuatiwa na jambo kuu. Kwa mfano, salamu za Malaika Gabrieli kwa Maria mamaye Yesu Kristo, salamu za Malaika Gabrieli pia kwa Elizabeth mamaye Yohana Mbatizaji na salamu kwa mamaye Samsoni katika Biblia.

Muundo wa kutamatisha utendi aidha unabainika katika matini teule. Muundo huu hutokea katika beti chache za mwisho katika tendi. Vilevile, kuna uwiano wa watunzi wa matini teule kutaja majina yao. Katika UMM ubeti wa mwisho kabisa, msimulizi anajitambulisha kwa kusema:

Mf 44

UMM
 Nami mwenye kuradidi
 Ismu yangu Saidi

wa Abdalla Masudi
jina langu nawambia (ub. 778:49)

Kabla ya msimulizi kujitambulisha, anataja kwamba amefikia mwisho wa simulizi ya Mikidadi na Mayasa na kuhimiza kwamba kisa hiki kisimuliwe vizazi vijavyo (beti 776, 777). Kitendo cha msimulizi kutaja jina lake ni la maana ili kusitokee mtafaruku wowote kuhusu msimulizi. Inaonyesha uzito wa kisa kinachosimuliwa. Msimulizi anapojitambulisha, ina maana kwamba yuko tayari kushuhudia aliyoyasema. Ni sawa na kitendo cha kutia sahihi barua inapoandikwa ili kuonyesha uwajibikaji.

Katika SS, mtunzi anazungumzia kifo chake Samsoni (Waamuzi 16:23-31). Tukio la mwisho la kufa kwake lilikuja na vifo vya watu wengi (Wafilisti) kushinda wale waliouawa katika uhai wake Samsoni. Katika kifungu cha thelathini na moja, mtunzi anataja kuwa ndugu zake Samsoni walienda kuchukua mwili wake kusudi waende kuuzika katika shamba la baba yake. Jina la baba ya Samsoni, Manoa, linatajwa tena kama ilivyokuwa mwanzoni mwa kisa hiki. Kutajwa kwa majina kuna umuhimu wake hivi kwamba yatatumika kama rekodi kwa vizazi vijavyo. Aidha, kutajwa kwa miaka ya uongozi wa Samsoni kunaonyesha athari aliyoweka katika uongozi wa wakati huo. Mtunzi katika kukamilisha kisa hiki anasema, “Naye alikuwa mwamuzi wa Israeli muda wa miaka ishirini (Waamuzi 16:31).

Utendi wa Gilgamesh aidha unachukua muundo huohuo katika sehemu ya mwisho wa kisa cha Gilgamesh. Mtunzi anayarudia maneno aliyoanza nayo katika kibao cha kwanza. Tumeonyesha muundo huu kwa kulinganisha maneno kwenye mistari ifuatayo:

Mf 45

UG

M.A	M. T(tafsiri yangu)
<i>(Go up on the wall of Uruk and walk around, Examine its foundation, inspect its brickwork thoroughly. Is not even the core of the brick structure made of kiln fired brick</i>	Kwea ukuta wa Uruk na uzunguke, Chunguza msingi wake, kagua uashi wake kwa makini Thibitisha kuwa matofali yake ni ya kukaushwa ndani ya tanuru...
<i>The Ishtar Temple) (Tablet 1:1)</i>	Ukumbi wa hekalu la Ishtar (Kibao cha 1:1)

Maneno yaliyotumika mwanzoni mwa utendi ni yale yaliyotumika mwishoni mwa utendi. Tofauti tu ni kwamba katika aya hii, mhusika Gilgamesh mwenyewe ndiye anayesema maneno haya. Anamweleza Urshanabi (mvushaji katika feri) achunguze ukuta wa Uruk ili ajionee ujenzi huo ulivyokuwa thabiti. Anasema kwamba msingi wake na uashi wake ulifanywa kwa makini. Katika kibao cha kwanza (Mf 45), msimulizi anaeleza kisa cha Gilgamesh kwamba yeye ndiye aliyepena habari za mafuriko ulimwenguni. Anataja kuhusu ushujaa wa mhusika, Gilgamesh. Mtunzi anaeleza ushupavu wa Gilgamesh alipojenga hekalu takatifu na madhabahu takatifu ya Eanna. Anasema kwamba ukuta wake, msingi wake na uashi wake hauwezi kulinganishwa na ujenzi wowote. Aidha, maneno hayo yanarudiwa katika kibao cha kumi na moja, aya ya mwisho.

Mf 46

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(Go up, Urshanabi, onto the wall of Uruk and walk around. Examine its brickwork thoroughly...</i>	Kwea juu Urshanabi kwenye ukuta wa Uruk na utembe pale, Chunguza msingi wake, kagua uashi wake kwa makini...
<i>Is not (even the core of) the brick structure of kiln-fired brick... The open area of the Ishtar Temple (Tablet XI: 51)</i>	Je, si matofali yake si ni ya kukaushwa ndani ya tanuru... Ukumbi wa hekalu ya Ishtar (Kibao cha XI: 51)

Kwa kuzingatia unukuzi wa maneno katika Mf 46, mtunzi anaonyesha kwamba hadithi yake imekamilika. Maneno yaliyosemwa mwanzoni mwa utenzi (Mf 45) yanawiana na yale yanayosemwa mwishoni mwa utenzi; kwa mfano, *Je, si matofali yake si ni ya kukaushwa ndani ya tanuru... Ukumbi wa hekalu ya Ishtar*

Muundo huu wa kumalizia na maneno au mawazo sawa na yale yaliyomo kwenye utangulizi wa utenzi unaonekana kuwa kaida ya tenzi nyingi. Shitemi (2010) anaeleza kuwa tungo za jadi zinadhihirisha vipengele vitatu vya masimulizi kwa njia maalum. Vipengele hivi ni utangulizi, yaliyomo na hitimisho. Anaeleza kuwa sehemu ya mwisho ina sehemu mbili jinsi ilivyo utangulizi na hitimisho kwa maudhui na shukrani kwa Mwenyezi Mungu. Muundo huu umebainika katika tendi teule za utafiti huu. Mbali na kuanza kwa maombi, *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni* zimehitimisha kwa maudhui yanayowiana. Utafiti huu umebainisha kuwa kuna mwingiliano wa kimuundo katika matini teule.

4.5 Mwingiliano katika Matumizi ya Lugha

Lugha ni amali muhimu katika kazi yoyote ya kifasihi. Kupitia lugha, usanii katika fasihi huweza kutambulika. Aidha, lugha anayoitumia msanii hutofautisha baina ya fasihi na sanaa nyingine. Hivyo, matumizi ya lugha ni kipengele muhimu katika uchambuzi wowote wa kifasihi. Katika matini teule za utafiti huu, kuna uwiano wa matumizi ya lugha. Tutachambua baadhi ya vipashio vya lugha vilivyotumika katika UFL, UMM, UG na SS ambavyo ni tashbihi, sitiari, maswali ya balagha, taswira na matumizi ya barua.

4.5.1 Matumizi ya Tashbihi katika UFL

Tashbihi ni aina ya tamathali ya usemi inayojenga sifa ya ulinganifu. Sifa hii husababisha taswira fulani akilini mwa msomaji. Mtunzi anayetumia tashbihi katika

kazi yake hunuia kufafanua jambo fulani kwa ziada au uwazi zaidi kuliko anavyotumia lugha ya kawaida. Matumizi ya tashbihi katika kazi yoyote ya kifasihi husababisha athari kubwa katika misingi ya matumizi ya lugha.

Matini teule za utafiti huu zinawiana katika matumizi ya lugha kitashbihi. UFL, UG, UMM na SS zote zimetumia tashbihi na sitiari kusifia wahusika wao wakuu katika simulizi. Katika UFL, kwa mfano mtunzi amelinganisha Fumo Liyongo na simba. Mtunzi anaeleza kuwa Liyongo ni mwanamume swahihi (sahihi) kama simba. Msimulizi anaeleza ifuatavyo:

Mf 47

UFL
 Ni mwanamume swahihi
 kama simba una zihi
 usiku na asubuhi
 kutembea ni mamoya (ub. 13:24)

Maelezo katika ubeti huu, yanaonyesha kwamba kuna wanaume wengine ambao wana kasoro fulani. Katika jamii za Kiafrika hasa, mwanamume anahitajika kuwa tofauti na mwanamke kwa kuonyesha ujasiri. Jinsia pekee haitoshi kutambulisha mwanamume. Jamii ya Wamaasai, kwa mfano, ina kaida ya mwanamume kumwua simba ili atambulikane na kuitwa 'mwanaume kamili'. Liyongo anasemekana kuwa yeye ni *mwanamume sahihi* au kamili. Kutembea kwake usiku na mchana ni mamoja. Mtunzi ananua kueleza kwamba wanaume wengine hawana ujasiri kiasi cha kutembea usiku bila woga wowote. Mtunzi wa UFL ametumia tamathali hii kuweka mawazo yake wazi kwamba mhusika ana ujasiri unaompa sifa ya kuonekana kuwa tofauti na wanaume wengine. Katika UFL, Liyongo ni mwanamume kamili kwa sababu yeye ni kama simba.

4.5.2 Matumizi ya Tashbihi katika UMM

Katika UMM, matumizi ya tashbihi ni nadra. Hata hivyo kuna baadhi ya tashbihi zilizotumika hivyo kuzua umwingilianomatini katika kipengele cha matumizi ya lugha katika matini teule. Kwa mfano;

Mf. 48

Pale tini ya jabali
 Pana maji afadhali
Tamuye kama asali
 Mikidadi kamwambia (ub. 173)

Mtunzi anasifia maji yaliyopatikana chini ya jabali kwamba yalikuwa *tamu kama asali*. Mtunzi anapolinganisha utamu wa maji na asali, inamaanisha kwamba maji yale yalikuwa na upekee fulani. Ina maana kwamba yalikata kiu kwa kweli na huenda pia maji yale yalikuwa baridi kiasi cha kutuliza joto mwilini. Maneno haya yanatokea wakati Mikidadi alikuwa ameona kiu hasa baada ya kusafiri kwa siku saba njiani (beti 168-170). Siku ya nane Mikidadi akawa amelemewa na njaa na kiu vilevile. Anapouliza maji, anaelezwa kuwa maji yaliyopatikana chini ya jabali yalikuwa tamu mno (*tamuye kama asali*) ila palikuwapo na jini aliyeishi pale (ub.172). Ingawa Mikidadi alijua hatari iliyokuwako, alikata kauli kwenda kuyanywa yale maji, labda baada ya kusikia kuhusu utamu wa maji hayo.

Tashbihi nyingine imetumika kueleza sifa ya Mikidadi. Katika ubeti 282, Mikidadi amefananishwa na simba (*kama simba alokaa*). Mtunzi anasema kuwa sifa za Mikidadi zilienea kwa sababu ya tabia yake iliyofanana na tabia ya simba. Simba mara nyingi anasemekana kuwa ni mfalme wa wanyama wa porini. Hii ni kwa sababu ya ukali na ujasiri wake. Matumizi ya tashbihi hii basi ina maana kwamba tofauti iliyokuwako kati ya Mikidadi na simba ilikuwa finyu.

4.5.3 Matumizi ya Tashbihi katika UG

Lugha ya kijazanda imetumika aidha katika UG ili kusisitiza ujumbe uliokusudiwa.

Gilgamesh amefananishwa na fahali wa mwituni. Msimulizi anaeleza:

(...But who struts his power over the people lika a wild bull

Lakini atumiaye mamlaka yake kwa kiburi mithili ya fahali ya mwituni (Kibao1:5)

Tashbihi hii imetumiwa na kahaba anayemtahadharisha Enkidu asije akajiona kuwa na nguvu zaidi bali afahamu kwamba Gilgamesh anashinda watu wote. Ina maana kwamba Gilgamesh alikuwa na mamlaka yasiyopingika. Kwamba watu walikuwa chini ya uongozi wake. Tashbihi vilevile imetumika katika UG kuelezea dhiki ya Gilgamesh katika Kibao VII:25, Gilgamesh anatiririkwa na machozi anapomwona rafiki yake Enkidu akiwa mgonjwa (*...his tears flowing like canals, he (Gilgamesh) said...; ...machozi yake yakimbubujika kama mifereji, (Gilgamesh) akasema*). Machozi yanayobubujika kama mifereji yanaashiria ‘wingi’ wa machozi hayo sawa na huzuni aliyokuwa nayo mhusika. Gilgamesh na Enkidu walikuwa marafiki wa dhati, hivyo kuugua kwake Enkidu kulimhuzunisha sana Gilgamesh.

4.5.3.1 Matumizi ya Sitiari katika UG

Sitiari ni tamathali ya usemi ambayo inalingana na tashbihi. Inatumia lugha kiulinganishi pasipo kutumia vilinganishi kama vile ‘kama’ na ‘mithili ya’ jinsi ilivyo katika tashbihi. Maana inayokusudiwa huwa fiche, hivyo kuhitaji tafakari ya kina ili kuepukana na kupotosha maana. Inatumika kusisitiza ujumbe. UG umetumia sitiari kuelezea sifa za mhusika Gilgamesh. Msimulizi anasema kuwa Gilgamesh hawezi akafananishwa na binadamu yeyote kwani yeye ni kamilifu. *“Anu alimtunuku ukamilifu wa ufahamu wa Uruk, fahali mkali wa kuogofya”* (Kibao I:1). Gilgamesh amefananishwa na fahali mkali (wild bull) wa mwituni sawa na Liyongo aliyefananishwa na simba. Katika muktadha wa UG, fahali mkali ni mnyama wa

porini anayefanana na ng'ombe. Mtunzi anahimiza tofauti baina ya Gilgamesh na binadamu wa kawaida kwa kutumia sitiari hii.

Katika ukurasa wa kwanza pia, mtunzi ametumia sitiari katika ufafanuzi wa sifa za mhusika Gilgamesh. Katika mistari ifuatayo mtunzi anaeleza:

Mf 48

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(Mighty net, protector of his people</i>	Jamvi kuu, mlinzi wa watu wake
<i>Raging flood-wave who destroys even walls</i>	Wimbi kali la mafuriko, ambalo huangusha
<i>of stone!)</i> (Tablet 1:1)	hata kuta za mawe! (kibao 1:1)

Mtunzi wa UG ametumia sitiari kama vile kumwita Gilgamesh *Jamvi kuu, Wimbi kali la mafuriko*. Baada ya kutaja kwamba Gilgamesh ni *jamvi kuu*, mtunzi anafuatilia kwa kutoa maelezo *mlinzi wa watu wake*. Sitiari ya *jamvi* imetumiwa na msimulizi kuthibitisha ukuu wa Gilgamesh katika ulinzi wa watu wake. *Wimbi kali la mafuriko* aidha ni sitiari iliyotumiwa na mtunzi kueleza uthabiti wa Gilgamesh katika ulinzi wa watu wa Uruk. Mtunzi anaeleza kuwa yeye ni wimbi kali la mafuriko ambalo *huangusha hata kuta za mawe!* Kuta za mawe zinaweza kufasiriwa kama adui. Iwapo Gilgamesh analinganishwa na wimbi kali la mafuriko, basi ana sifa ya uharibifu. Kuharibu huku kunaelekezwa kwa adui. Katika muktadha huu, adui wa watu wa Uruk walioongozwa na Gilgamesh wangeharibiwa au kuuawa iwapo wangejaribu kuleta maafa ya aina yoyote.

Sitiari vilevile imetumika katika Kibao cha pili, ukurasa wa pili ambapo msimulizi anasifia Humbaba kwa kusema:

Mf 49

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>Humbaba's roar is a flood</i>	Mngurumo wa Humbaba ni mafuriko
<i>His mouth is fire</i>	Kinywa chake ni moto
<i>His breath is death</i> (Tablet II:2)	Pumzi zake ni kifo! (Kibao II:2)

Sifa za Humbaba, mlinzi wa Msitu wa Seda zimeelezwa kistiari. Mtunzi anasema kuwa *mngurumo wake ni mafuriko*. Mafuriko yanapotokea mara nyingi huosha kila kitu kinachopatikana njiani. Mtunzi anapotaja kuwa *mngurumo wa Humbaba ni mafuriko* anamaanisha kuwa anapozungumza, sauti yake inarindima na kusikika kwa mbali. Jambo hili pia humaanisha kuwa maumbile yake huenda yakawa ya kufananishwa na jitu.

Mtunzi anapoeleza kwamba *kinywa cha Humbaba ni moto*, anakusudia kuonyesha kuwa maneno ya mhusika yanawaka kama moto. Kuwaka huku kunahusiana na tabia yake ambako matamshi yake ni ya kufadhaisha mno. Sitiari ya pumzi za Humbaba kuwa kifo aidha huonyesha ukali wake. Inaonyesha sifa kuwa mhusika ni muuaji. Sitiari hizi zimetumiwa kufafanua zaidi hulka ya wahusika waliotajwa.

4.5.3.2 Matumizi ya Sitiari katika UMM

Katika UMM sitiari imetumika zaidi kuliko tashbihi. Katika ubeti wa 450, mtunzi ametumia sitiari kumsifu Mikidadi. Anasema:

Mf 50

UMM
 Simba huyu hali kitu
 hali manyama ya mwitu
 kila siku hula watu
 Sultani kamwambia (ub. 450:29)

Kwa kutaja kuwa mhusika *hali manyama ya mwitu bali kila siku hula watu*, mtunzi anaonyesha kwamba anayetajwa ni *mha watu* hivyo ni muuaji. Ana uwezo wa kuwaua watu kwa urahisi jinsi afanyavyo simba. Tunavyojua ni kuwa simba hula wanyama

wa mwituni. Tabia ya ukali wake ya uwindaji ilimfanya simba kuitwa mfalme wa mwituni. Vivyo hivyo, mtunzi wa UMM anamfananisha Mikidadi na simba kwa kuwa tabia yake inalandana na tabia ya simba. Aidha, Mikidadi amefananishwa na mnyama simba katika beti 295, 448, 449, 450, 455 na 458. Katika ubeti wa 295, kwa mfano, Mikidadi anajisifu kwa kusema “ni mimi simba wa mwitu”. Mbali na watu kumwita simba, yeye mwenyewe anasema kwamba ni simba wa mwituni kuonyesha kuwa hatishwi na mtu yeyote. Tashbihi imetumika katika ubeti ufuatao:

Mf 51 UMM

Khabarize Mikidadi
zikaenea biladi
kuwa wadi murtadi
kama simba alokaa (ub. 282:18)

Katika dondoo hii Mikidadi amepewa sifa ya mnyama simba sawa na mhusika Liyongo katika UFL. Mtunzi wa UMM anaeleza kuwa Mikidadi ana tabia zifananazo na za simba (*kama simba alokaa*). Habari za Mikidadi zilienea kote lakini jambo lililojulikana ni kwamba huyo mtu, Mikidadi, alikuwa anaogofya na alikuwa na tabia ya simba, anayejulikana hasa kwa mauaji ya wanyama wa pori na hata binadamu anapokutana naye.

4.5.3.3 Matumizi ya Sitiari katika SS

Simulizi ya Samsoni vilevile imetumia sitiari kumsawiri mhusika Samsoni. Dondoo lifuatalo linatupa maelezo zaidi:

Mf 52

SS

(5) Ndipo Samsoni na baba yake na mama yake wakatelemkia Timna wakafika mashamba ya mizabibu huko Timna. Na tazama, mwana simba akamngurumia; (6) Roho ya BWANA ikamjilia kwa nguvu, naye akampasua kana kwamba anampasua mwana mbuzi, wala hakuwa na kitu chochote mkononi mwake, lakini hakuwambia baba yake na mama yake aliyoyafanya (Waamuzi 14: 5-6).

Hapa mtunzi anaeleza kwamba Samsoni alimpasua mwanasimba ‘kana kwamba alikuwa ni mwanambuzi.’ Inavyoelezwa ni kuwa mhusika hakusumbuka kumwua huyo simba ingawa hakuwa na silaha yoyote. Ingawa Samsoni hakuwa na silaha yoyote, alitumia mikono yake kumwua mwanasimba. Hii inaonyesha kwamba Samsoni alikuwa na ushujaa tofauti na ule wa binadamu wa kawaida.

Sitiari na tashbihi zilizotumika katika matini teule zinahusisha simba. Inaonyesha kuwa wahusika wakuu wana tabia zinazolandana. Inaonyesha kuwa wana ujasiri wa kufananishwa na simba. Mifano iliyotolewa inabainisha kuwa kuna mwingilianomatini katika UFL, UG, UMM na SS katika matumizi ya lugha ya kijazanda. Kinachodhihirika ni kuwa wanyama wa porini, simba na fahali wa mwituni wametumika kuonyesha sifa za tabia za wahusika wakuu. Mbali na kuonyesha umwingilianomatini, tashbihi na sitiari zilizotumika kuwaelezea wahusika Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Samsoni zinaonyesha ukwasi wa lugha wa watunzi wa matini teule.

4.5.3.4 Maswali ya balagha katika UFL

Matini zilizochunguzwa katika utafiti huu zinaonyesha mwingiliano wa kimatini katika kipengele cha matumizi ya lugha. Moja kati ya mbinu za lugha zinazotumika katika matini teule ni maswali ya balagha.

Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, mtunzi ametumia maswali ya balagha kuonyesha kwamba hakuna anayeweza kumshinda Fumo Liyongo. Hayo tunapata katika ubeti ufuatao:

Mf 53

UFL

Wakanena kwa moyoni

“Amuwezao ni nyani

Hayuno hawezekani

Ni kutaka kwangamiya” (ub. 67:33).

Huu ni wakati ambapo Wasanye na Wadakhalo, walitaka Liyongo kuwatolea makoma yaliyokuwa kwenye miti mirefu mno. Kwa mujibu wa Mulokozi (1999), Wasanye na Wadakhalo ni makabila ya wawindaji yaishiyo Kaskazini Mashariki mwa Kenya. Mtunzi anaeleza kuwa watu hao walitembea kwa muda wakitafuta mkoma mrefu ambao walidhani Liyongo asingeweza kuyafikia makoma yake. Baadaye, alipoona kwamba Fumo Liyongo amewashinda, walishindwa kumshika kwa sababu waliogopa kuwa angewaua wote (ubeti 68).

Aidha, maswali ya balagha yametumika wakati mwana wa Liyongo alipokuwa akipanga jinsi ya kumwua baba yake. Mtunzi anamwonyesha mwanaye Liyongo akijiuliza maswali mengi katika beti zifuatazo:

Mf 54

UFL
Naye chenenda ndiani
una khaufu moyoni
*“Nifanye shauri gani
kwa baba kuisikiliya (ub.162)*

Yakamuiya matata
iye mimi kumpata
*kitokufa ni matata
taniuwa mara mmoja (ub.163)*

*“Ikiwa alonambiya ni
mzaha siyo niya
kasidi kunangaliya
ni khatari nacheleyea.” (ub.164)*

Katika mistari ya mlazo, inavyoonyeshwa katika beti 162, 163 na 164, kijana alijiuliza maswali ambayo hayakuhitaji kujibiwa na mtu yeyote isipokuwa yeye mwenyewe. Kwa mfano kusema, *nifanye shauri gani kwa baba kuisikiliya*. Ukweli ni kwamba hakuna yeyote anayeweza kujibu swali hilo ila yeye mwenyewe. Mbinu hii imetumika kikamilifu kuonyesha hofu iliyokuwa imemwingia kijana wa Liyongo. Mwenyewe

alijua hatari iliyokuwa mbele yake iwapo angeshindwa kutekeleza mipango yake ya kumwua babake. Anataja kwamba baba yake asipokufa atauawa mara moja (*kitokufa ni matata, taniuwa mara mmoja*). Mwana wa Liyongo alijua vizuri hatari iliyomkabili iwapo mipango yake ya kumwua baba yake ingefeli.

4.5.3.5 Maswali ya balagha katika UG

Katika *Utenzi wa Gilgamesh*, maswali ya balagha vilevile yametumika katika sehemu chache. Katika kibao cha kwanza, ukurasa wa pili, mtunzi anasema:

Mf 55

UG

M.A	M.T(tafsiri yangu)
<i>(Who can compare him in kingliness?</i>	Nani wa kulinganishwa naye katika Ufalme?
<i>Who can say like Gilgamesh: "I am King"!</i>	Nani anayeweza kusema kama Gilgamesh: "Mimi ni Mfalme"!
<i>Whose name from the day of his birth, was called "Gilgamesh"?(Tablet 1:2)</i>	Nani tangu kuzaliwa kwake aliitwa "Gilgamesh"? (Kibao 1:2)

Mistari hii imetumika kusisitiza ujumbe kuwa Gilgamesh alikuwa mtu wa kipekee. Alikuwa Mfalme wa kipekee aliyekuwa na sifa tofauti kabisa na Wafalme wengine. *Nani wa kulinganishwa naye katika Ufalme? Nani anayeweza kusema kama Gilgamesh: "Mimi ni Mfalme"!* Nani tangu kuzaliwa kwake aliitwa "Gilgamesh"? Maswali hayo yanaulizwa japo hakuna anayetoa jibu. Hata hivyo, maswali yayo hayo huenda yasijibiwe moja kwa moja. Ni maswali ya balagha ambayo yametumiwa na mtunzi kama mojawapo ya mbinu za lugha katika uandishi wake. Hii ndiyo sababu kwamba mhusika ametajwa kuwa na sifa ya kuwa nusu-mungu na nusu-binadamu (Mf 151). Aidha, katika Kibao cha 6, aya ya mwisho, Gilgamesh anajisifu kwa kutumia maswali ya balagha yafuatayo:

Mf 56

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(Gilgamesh said to the palace retainers: "who is the bravest of all the men Who is the boldest of all the males!)</i> (Tablet VI:25)	Gilgamesh akawaambia watumishi wa kasri: Nani shupavu zaidi ya watu wote Nani jasiri kati ya wanaume wote! (Kibao VI:25)

Mistari ya hapa juu inamwonyesha Gilgamesh kama mhusika anayependa kujisifu. Anajiona kuwa yeye pekee ndiye shupavu na kwamba anawashinda wanaume wote kwa kuuliza ‘*nani shupavu zaidi ya watu wote, nani jasiri kati ya wanaume wote!*’ Gilgamesh anajiona shupavu kuliko watu wote. Anadai kwamba yeye ndiye jasiri kuliko wanaume wote. Maneno haya yanaashiria kuwa mhusika anajiamini zaidi na huenda haamini kwamba kuna wanaume wengine ambao ni jasiri kumliko.

Mbali na kuwa maswali hayo yanatumika kama mbinu ya lugha, yanatumika pia kuendeleza usimulizi wa kisa cha Gilgamesh katika UG. Maswali ya balagha yaliyotumiwa katika UG yanatumika kama njia ya kusisitiza ujumbe unaokusudiwa kufikia hadhira.

4.5.3.6 Maswali ya balagha katika UMM

Katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*, maswali ya balagha yanatumiwa katika sehemu tofautitofauti. Katika muktadha wa beti zifuatazo, mhusika Mikidadi alikuwa akipigana na Waarabu waliokuja kumposa Mayasa. Watu walimshangaa jinsi alivyopigana bila silaha yoyote.

Mf 57

UMM
 Ni mtu gani huyule
 apiganaye hivile
 hatuoni tangu kale
 mtu kamaye mithaa (ub.88)

Au yule ni ruhani

au ni mwana wa jini
 aula ni sheitwani
 aula ni malakaa
 (ub.89)

Maswali ya balagha yaliyotumika katika beti 87- 89 yanadhihirisha kwamba mhusika alikuwa mtu wa ajabu. Watu walipomwona Mikidadi akipigana, walishangaa sana. Swali lililoulizwa; *Ni mtu gani huyule apiganaye hivile* halikuhitaji kujibiwa na yeyote ila ilikuwa ni ishara ya mshangao kwa waliomwona akipigana. Ilishangaza watu kuona Mikidadi akipigana hata wakasadiki kwamba huenda yeye ni mwana wa jini, shetani au basi Malaika kwa kuuliza; *Au yule ni ruhani, au ni mwana wa jini, aula ni sheitwani, aula ni malakaa.* Hayo ni maswali yaliyoulizwa na watu ila hakukuwa na mtu wa kuwajibu. Matumizi ya maswali haya yanasisitiza jambo kuwa Mikidadi ni hodari katika vita na kwamba hakujapatikana mtu mwengine wa kufananishwa naye (*Hatuoni tangu kale mtu kamaye mithaa*). Maswali ya balagha yanayotumika vilevile yanachangia kuendeleza hadithi ya Mikidadi na Mayasa.

Mf 58

UMM
 Mtu huyo awanaje
 upanga aushikaje
 aula autupaje
 naye ni mtu mmoja (ub. 52:23)

Katika Mf 58, askari jeshi wa Sultani walitumia maswali ya balagha kuusifu ushujaa wa Mikidadi. Walishindwa kuelewa jinsi Mikidadi alivyoweza kuwaua watu wengi ilhali yeye alikuwa mmoja tu. Swali la kwanza wanalojiuliza ni vipi mtu huyo anavyopigana (*mtu huyo awanaje*). Wanataka kujua jinsi anavyoushika upanga wake (*upanga aushikaje*) na jinsi anavyoutumia vitani kuwaua watu wengi ilhali yeye anapigana peke yake (*aula autupaje, naye ni mtu mmoja*). Maswali haya yanaonyesha mwingiliano wa matini katika kazi teule za utafiti huu. Watunzi wa matini teule wametumia mbinu ya usimulizi unaoelekea kufanana katika kazi zao.

4.5.3.7 Maswali ya balagha katika SS

Simulizi ya Samsoni katika *Biblia* imetumia maswali ya balagha katika sehemu chache. Katika Waamuzi 15:18, mhusika Samsoni anauliza swali lisilohitaji kujibiwa kwani swali lenyewe linaulizwa Mwenyezi Mungu. Samsoni anasema:

Mf 59

SS

Kwa kuwa alikuwa amesikia kiu sana, akamlilia Bwana akisema, “Umempa mtumishi wako ushindi huu mkuu. *Je, sasa nife kwa kiu na kuangukia mikononi mwa hawa watu wasiotahiriwa?*” (Waamuzi 15:18).

Muktadha wa mfano 59 ni baada ya Samsoni kuwaua watu 1,000 na ikawa kwamba alihisi kiu sana baada ya kutekeleza mauaji hayo. Hivyo, Samsoni aliona angeschindwa na Wafilisti, ambao katika mila na desturi zao, wanaume hawakuwa wanatahiriwa. Samsoni aliona kuwa jambo la fedheha sana iwapo angeschindwa na watu wasiotahiriwa. Samsoni hivyo anamsihi Mungu wake amwokoe kutoka kwa aibu hiyo kwa kuuliza; *Je, sasa nife kwa kiu na kuangukia mikononi mwa hawa watu wasiotahiriwa?* Ukweli ni kwamba swali hili limeulizwa Mungu na hatutarajii kupata jibu la hapo kwa hapo. Samsoni alijihisi kuwa dhaifu na kuona kuwa iwapo angepigana na Wafilisti angeschindwa na hii ingekuwa fedheha kwake na kwa jamii nzima kwa kushindwa na watu wasiotahiriwa.

Katika mahali pengine, maswali ya balagha yametumiwa wakati wa kutoa majibu ya kitendawili kilichotegwa na Samsoni kwa watu wa jamii ya mwanamke Mtimna.

Mf 60

SS

Nao watu wa mji wakamwambia siku ya saba kabla ya jua kuchwa;
Ni kitu gani kilicho kitamu kuliko asali?
Ni kitu gani kilicho na nguvu kuliko Simba? (Waamuzi 14:18)

Kwa kawaida katika kutegua kitendawili, ni nadra kutumia swali kulijibu swali. Katika muktadha huu, Wafilisti walitumia swali kutegua kitendawili kile kwa sababu

mkewe Samsoni ndiye aliyewapatia jibu. Hivyo, ilikuwa ni kama kumdhihaki Samsoni aliyekuwa ametoa masharti magumu iwapo wangeshindwa kutegua kitendawili chake. Maswali *ni kitu gani kilicho kitamu kuliko asali na ni kitu gani kilicho na nguvu kuliko Simba* yaliulizwa ili kumwonyesha Samsoni kuwa tayari alikuwa ameshindwa nao kwa kuwa mwanzoni alionyesha kuwa na kiburi akidhani kuwa hakungetokea mtu ambaye angetegua kitendawili hicho. Ukweli ni kwamba Wafilisti walipata jibu la kitendawili kutoka kwa Mtimna, aliyekuwa mke wa Samsoni wakati huo.

Matumizi ya lugha katika muktadha wa maswali ya balagha yanawiana katika matini teule za utafiti huu. Hili linabainisha kauli ya utafiti huu kuwa kuna mwingilianomatini katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni* katika kipengele cha matumizi ya lugha.

4.5.4 Taswira

Taswira katika fasihi ni picha fulani inayojengeka akilini mwa msomaji. Hutokea kutokana na uteuzi wa maneno ya mwandishi. Wamitila (2003) anaeleza kuwa kuna aina nyingi za taswira kutegemea kazi ya kifasihi. Cha msingi ni kwamba taswira ni kipengele kimoja kinachohusishwa na matumizi ya lugha katika kazi ya fasihi. Hivyo, maelezo ya mwandishi au msimulizi pamoja na uteuzi wa maneno kama vile tamathali za usemi, huchangia katika uundaji wa picha au taswira akilini mwa msomaji.

4.5.4.1 Taswira katika SS

Matini zilizoteuliwa kwa ajili ya utafiti huu zimeonyesha mwingiliano wa kimatini katika matumizi ya lugha kwa kuzingatia kipengele cha taswira. UFL na SS zina uwiano kwa namna ambavyo wahusika wakuu wamesawiriwa. Katika nukuu

zifuatazo, msomaji anapata picha ya Samsoni alivyokuwa akisaga ngano gerezani baada ya kung'olewa macho yake huku amefungwa kwa pingu za shaba.

Mf 61

SS

Basi Wafilisti *wakamkamata*,

Wakamng'oa macho yake wakamchukua

Wakamtelemsa mpaka Gaza

Wakiwa wamemfunga kwa pingu za shaba, *wakamweka* ili asage ngano huko gerezani (Waamuzi 16:21).

Maandishi ya mlazo yametumika kama msisitizo wa madhila aliyopitia Samsoni akiwa gerezani. Mwendelezo wa matendo ya kinyama aliyofanyiwa Samsoni yanajenga taswira ya kuwa na hisia za huruma kwa mhusika Samsoni. Msimulizi anakusudia hadhira kuwa na picha akilini mwao ya jinsi Samsoni alivyoteswa kwa kuradidi *-ka* ili kuisitiza vitenzi; *wakamkamata*, *wakamng'oa macho yake*, *wakamchukua*, *wakamtelemsa*... *wakamweka* ili asage ngano... Ni rahisi kwa hadhira kujenga taswira ya kumwona Samsoni akikamatwa, aking'olewa macho, akichukuliwa na kutelemshwa hadi kuwekwa mahali kusudi asage ngano. Hii ni mbinu ya kipekee inayogusa hisia za hadhira. Aidha, matumizi ya viambishi *...ka-...ka-...ka-* huakisi wakati uliopita na vilevile kuonyesha mfuatano wa matukio katika hadithi inayosimuliwa.

4.5.4.2 Taswira katika UFL

Katika UFL, taswira sawa na ile inayosawiriwa katika Mf 61 hujengeka kuhusiana na mhusika Liyongo alipotiwa gerezani. Huu ni wakati ambapo Sultani alikuwa na mpango wa kumwua Liyongo. Aliposhikwa, alifungwa kijumbani mle gerezani chini ya ulinzi mkali jinsi tunavyoelezwa hapa chini:

Mf 62

UFL
Wakanenda kwa utungo
 mafumo, zembe zigongo
wakamshika Liyongo
 gerezani akatiwa (ub. 86)

Akatiwa gerezani
kafungiwa kijumbani
 asikari mlangoni
 kwa zamu wachangaliya (ub. 87)

Maelezo ya kushikwa kwake Liyongo yanampa msomaji taswira fulani ya jinsi aliposhikwa. Hadhira hujenga taswira fulani akilini mwake anaposoma maneno katika Mf. 62. *Wakanenda kwa utungo, ...wakamshika Liyongo, ...akatiwa gerezani, kafungiwa kijumbani...* Viambishi -ka- vinaashiria mfuatano wa matukio na hali kadhalika kusesitiza utendaji wa matukio yenyewe.

Beti 86 na 87 zina maneno yanayowiana na maelezo ya jinsi Samsoni alivyokamatwa. Katika Mf. 62 yamkini Liyongo alikuwa jitu na hiyo inaeleza sababu ya watu waliomshika kuwa na silaha kama vile mikuki (mafumo), vigongo na mishale (zembe). Mtunzi anaeleza kuwa usiku ulipofika watu walishiriki ngoma na michezo iliyoandamana na tarumbeta kwa kusherehekea kushikwa kwake Liyongo. Hayo yanaelezwa katika beti 111 na 112:

Mf 63

UFL
 Hata usiku kufika
 matezo wakayandika
 kana ada wakaweka
 t'asa, pembe, siwa piya (ub. 111)

Na ngoma na nyingi kusi
 kusalie unasi
 ikawa kama harusi
 watu wakiangaliya (ub.112)

Ubeti wa 112 unaonyesha kwamba kila mtu (*kusisalie unasi*, yaani kusibaki mtu) alipiga makofi na ikawa kama sherehe ya harusi. Ukweli ni kwamba Wagala walikuwa na furaha kwa sababu walikuwa wamefaulu kumtia Liyongo nguvuni. Taswira hii inawiana na ya Samsoni alipokuwa gerezani katika mfano wa 61 uliotolewa hapo juu.

4.5.4.3 Taswira katika UMM

Aidha, katika UMM, msomaji anapata taswira sawa na ilivyokuwa katika simulizi za Samsoni na Liyongo wakati Mikidadi anahadaiwa na Jabiri. Jabiri anampa Mikidadi mvinyo kusudi lake alewe ili atiwe nguvuni (beti 686-691). Msimulizi anaeleza:

Mf 64

UMM
Ikampata sakara
kapotewa na fikira
 wakenenda na kambara
 ikawa kumtatia (ub. 689)

Ubeti 689 unaonyesha jinsi Mikidadi alivyopoteza fahamu baada ya kulewa na hivyo kushikwa mateka. Hii ni baada ya Mikidadi kupewa kileo kilichomlevya hata akapoteza fahamu (*kapotewa na fikira*). Alipopata fahamu alilia kwa huzuni alipogundua kuwa amefungwa kwa kamba na mapingu ya mnyororo. Msimulizi anaeleza katika ubeti 690:

Mf 65

UMM
 Hata zikija akili
 amefungwa silisili na
 mapingu ya rujuli
 Mikidadi akalia (ub. 690)

Maelezo hayo yanampa msomaji taswira ya dhiki za Mikidadi anapogundua kwamba amefungwa miguu yake hasa anapofahamu kuwa adui yake ndiye aliyemweka katika hali hiyo. Mikidadi anapopata fahamu anajiona amefungwa kwa kamba na mapingu

ya mnyororo (*amefungwa silisili na mapingu ya rujuli*). Msomaji anapata picha ya jinsi mhusika anavyolia baada ya kugundua kwamba amefungwa na yuko mikononi mwa adui zake huku akikosa namna yoyote ya kujinasua.

Katika kipindi kingine mtunzi wa UMM anatumia lugha inayomwezesha msomaji kuunda picha akilini mwake kuhusu Mikidadi akimenyana na askari jeshi katika vita vikali. Askari walimzunguka wakiwa wamejihami na silaha lakini hawakumshinda.

Kwa ghafla, Mikidadi akawaua watu mia moja:

Mf 66

UMM
Jamii wakamzinga
kwa mafumo na mapanga
muda punde kujitenga
ameua watu mia (ubeti 317)

Dondoo hili linatupatia picha ya watu wengi waliomzingira (Jamii wakamzinga) Mikidadi wakiwa wamejipanga kumwua (kwa mafumo na mapanga) ila hawakumweza. Badala yake Mikidadi aliwaua watu mia moja kwa ghafla papo hapo.

4.5.4.4 Taswira katika UG

Uwiano katika matumizi ya lugha unaonekana vilevile katika UG. Katika mazungumzo yake na Gilgamesh, Ishtar (binti ya Mfalme) anakereka kwa sababu ya kuambiwa ukweli kuhusu maovu yote aliyoyatenda. Hivyo basi, akapaa mbinguni na kumweleza baba yake, Anu, ambaye alimpa Fahali wa mbinguni ili amwue Gilgamesh. Katika mistari ifuatayo, tunapata maelezo yafuatayo katika UG:

Mf 67

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>Ishtar led the Bull of Heaven down to the earth</i>	Ishtar alimwongoza Fahali wa Mbinguni kuelekea duniani
<i>When it reached Uruk, it climbed down to the Euphrates...</i>	Fahali alipofika Uruk, aliteremka hadi mto Euphrates...
<i>the snort of the Bull of Heaven a huge pit opened up</i>	Fahali wa Mbinguni alipumua vikali na shimo kubwa likafunguka
<i>And 100 young men of Uruk fell in (Tablet VI:23)</i>	vijana 100 wa Uruk wakaanguka ndani (Kibao VI:23)

Ni rahisi na inashangaza kwa msomaji/msikilizaji kuchora picha ya fahali akipumua na shimo kubwa kufunguka akilini mwake. Zaidi ya hayo, ni kwamba vijana mia moja wa mji wa Uruk wanaanguka ndani ya shimo hilo. Taswira hii inawiana na maelezo ya Mikidadi anapoua watu mia moja pia (ubeti 317). Hivyo, watunzi wa matini teule wametumia lugha inayoingiliana katika kusuka simulizi zao.

4.5.5 Matumizi ya barua katika UFL na UMM

Kuna uwiano wa matumizi ya barua katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*. Watunzi wa tenzi hizi wametumia barua kama njia ya kufikisha ujumbe kwa walengwa wao kimakusudi. Katika UFL, barua iliandikwa na Mfalme kwa Liyongo (beti 18-19) kwa sababu Mfalme alikuwa na tamaa ya kumwona Liyongo ambaye sifa zake zilikuwa zimeenea kote. Baada ya Liyongo kupata na kusoma barua ya Mfalme, naye anamjibu kwa barua kwamba angetimiza matakwa yake (ubeti 21).

Mtunzi wa *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* vilevile ametumia barua katika simulizi yake. Barua imetumika katika beti 660-683. Jabiri aliona amwandikie Maliki barua kumjuza yaliyotokea na kumtaka alipize kisasi juu ya Mikidadi. Hii ni kwa sababu Mikidadi alikuwa amefaulu kumchukua Mayasa kama mke wake baada ya kupigana na jeshi la Alii. Tunaona ulinganisho huu katika beti zifuatazo:

Mf 68

UFL

Mfalme kaandika
waraka wake haraka
Mtu wake kampeka
Liyongo kampekeya (ub. 18:25)

Na Liyongo akajibu
kwa heshima na adabu
“Nitakuja kwa karibu
nitwiiye Maulaya” (ub. 21:26)

Ubeti wa 18 katika UFL, unaonyesha kuwa mfalme alimwandikia Liyongo barua na kumpa mtumishi wake kumpelekea. Vivyo hivyo, Liyongo alipopata waraka ule aliitikia maombi ya mfalme kwa kumjibu kuwa angeenda kumwona bila kukawia (*Nitakuja kwa karibu*). Barua vilevile imetumika katika UMM kama mojawapo ya mbinu za lugha. Kwa mfano:

Mf 69

UMM

Baadaye kaandika
akakutubu waraka
kwa mkwewe kaupeka
kumuarifu jamia (ub. 668)

Atukuzie kitabu
Kuwahimu waarabu
twaona hujatujibu
khati tulokuletewa (ub. 683)

Maneno katika beti mbili (668 na 683) yanathibitisha kuwa barua zilitumika katika mawasiliano yaliyohusiana na Mayasa. Barua hii iliandikwa na Jabir akimueleza Sheikh kuhusu mkewe (Mayasa) kwamba alitekwa nyara na Mikidadi ambaye pia aliwaua watu wake na kuwanyang'anya mali. Barua hii ilitumika kama njia ya mawasiliano ya faragha baina ya Jabir na Sultani kwa sababu ya ila ya kutaka kumwua Mikidadi. Mistari hii inaonyesha ulinganifu wa matumizi ya barua katika UFL na UMM. Kwa jumla, mifano iliyotolewa katika sura hii inaonyesha

mwingilianomatini katika mbinu ya usimulizi, muundo na matumizi ya lugha katika UFL, UG, UMM na SS.

4.6 Ulingano na Tofauti katika Mwingiliano wa Kisimulizi katika UFL, UMM, UG na SS

Mbinu ya usimulizi iliyotumika katika UFL, UG, UMM na SS inadhahirisha kuwa visa vinavyorejelewa vinawiana. Utafiti huu umeonyesha kuwa visa vya kiajabu vinavyobainika vimesimuliwa kwa kuzingatia mbinu za kisimulizi zinazowiana. UFL na UMM ni tenzi zinazohusisha mbinu ya usimulizi wa ki-Utendi. Katika mbinu hii, msimulizi anasimulia hadithi ambayo hajashiriki katika matendo yake. Katika UMM, msimulizi anasimulia yaliyotukia katika hadithi ya Mikidadi na Mayasa. Kisa kirefu cha Mikidadi kinahusisha matukio mengi ambayo msimulizi anayakusudia hadhira yake kusikiliza ingawa yeye si mshiriki katika matukio hayo. Mfanano wa mbinu ya usimulizi wa ki-Utendi katika UFL na UMM umeonyeshwa katika mifano 1,2, 3,4,5 na 6.

Tofauti na UFL na UMM, *Tenzi za Gilgamesh* (UG) na *Simulizi ya Samsoni* (SS) zimetumia usimulizi wa nafsi ya kwanza katika mawasilisho ya matukio yanayojiri katika visa vyao. Mbinu ya usimulizi wa nafsi ya kwanza inaonyesha msimulizi kama mhusika kwa sababu ya kutambulika kwake katika msuko wa hadithi. Mifano 8, 9, 10 na 11 zimefafanua ulinganifu wa mbinu ya usimulizi wa nafsi ya kwanza katika UG na SS.

Mbinu ya usimulizi wa nafsi ya tatu imetumika katika tenzi zote nne; UFL, UG, UMM na SS. Matumizi ya viambishi vya nafsi ya tatu (a), (wa) na (yeye) huashiria kwamba msimulizi hakushiriki katika hadithi. Mbinu hii imetumika kwa upana katika UFL, UG, UMM na SS kama inavyoelezwa katika mifano 12 hadi 29. Usimulizi

maizi umebainika katika SS pekee. Katika mbinu ya usimulizi maizi, msimulizi anaonekana kuelewa mhusika zaidi kiasi cha kujua yaliyomo katika mawazo yake. Mbinu hii imefafanuliwa katika mifano 30, 31 na 32.

Ulinganifu katika mwingiliano wa kimuundo umebainishwa kupitia mifano 33 hadi 46. Kuna ulingano katika kitangulizi katika UFL na UMM kwa sababu tendi zote mbili zimetambua ukuu wa Mwenyezi Mungu katika utunzi wa shairi. Tofauti na UFL na UMM, mianzo ya UG na SS inataja sifa za wahusika wakuu. UG umemfananisha mhusika mkuu (Gilgamesh) na Mungu ilhali SS imesisitiza kuwa mhusika Samsoni atakapozaliwa atakuwa mnadhiri wa Mungu. Katika UFL na UMM tashbihi imetumika kueleza sifa ya wahusika wakuu, Fumo Liyongo na Mikidadi mtawalia. Fumo Liyongo amesifiwa kuwa ni jasiri hivyo kufananishwa na Simba (mf. 47). Katika UMM vilevile, Mikidadi anaelezwa na msimulizi kuwa ana tabia za Simba kwa sababu ya ujasiri wake. Mbali na hayo, Mikidadi anajisifu mwenyewe kwa kusema kwamba yeye ni Simba (Mf. 50). Aidha, UMM, UG na SS zimedhihirisha matumizi ya sitiari kusifia tabia za wahusika wakuu. Tofauti na Fumo Liyongo katika UFL, Mikidadi katika UMM na Samsoni katika SS, waliohamishiwa tabia za Simba, Gilgamesh katika UG amefananishwa na fahali mkali wa mwituni. Gilgamesh pia amefananishwa na moto, mafuriko na hata kifo (Mf. 48,49).

Maswali ya balagha yametumiwa vilevile kuendeleza usimulizi katika UFL, UG, UMM, UG na SS. Taswira mbalimbali zimebainishwa kupitia maelezo yanayolenga kufafanua ama tukio au tabia fulani za wahusika katika miktadha tofautitofauti. Kuna ulinganishi wa matumizi ya barua katika UFL na UMM; mbinu isiyotumika katika UG na SS. Utafiti huu umebainisha kuwa kuna ulinganifu mwingi kuliko tofauti katika uendelezaji wa masimulizi katika UFL, UMM, UG na SS.

4.7 Hitimisho

Katika sura hii, tulichunguza mwingiliano wa kimatini katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni* katika viwango tofauti. Imebainika kwamba matini teule zinadhihirisha mtiririko wa matukio ya kiajabu hivyo kuwa na mwingiliano wa kisimulizi. Mbinu za kisimulizi, matumizi ya lugha, msuko wa hadithi na mahitimisho ya matini teule inafanana.

Simulizi ya Samsoni imechukuliwa kama moja ya simulizi za ki-utendi katika Biblia. Hadithi hii kama inavyojitokeza katika Biblia (Waamuzi 13-16), ina mtiririko wa matukio ambayo tumeweza kuyachambua kwa kuzingatia misingi ya kifasihi. Kwa misingi hiyo, UFL, UG na UMM ni baadhi ya matini zilizochota kwenye *Simulizi ya Samsoni* (SS) hivyo kudhihirisha mwingilianomatini katika kazi za fasihi na matini teule ya kidini katika utafiti huu. Katika sura inayofuata, mtafiti anahakiki mwingiliano wa sifa za wahusika katika UFL, UG, UMM na SS.

SURA YA TANO

MWINGILIANO WA SIFA ZA WAHUSIKA WAKUU KATIKA *TENZI ZA*

FUMO LIYONGO, MIKIDADI NA MAYASA, GILGAMESH NA

SIMULIZI YA SAMSONI

5.0 Utangulizi

Katika sura ya nne, tulifafanua mwingiliano wa kisimulizi kama ulivyotumika katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh na Simulizi ya Samsoni*. Ilibainika kwamba mwingiliano wa kisimulizi ulisababishwa na mbinu za usimulizi, matumizi ya lugha na mtiririko wa matukio katika tenzi teule. Sura hii imeshughulikia mwingilianomatini baina ya wahusika wakuu katika matini teule. Masuala ya ukatili, uongozi, ushujaa na majigambo yamejadiliwa kama baadhi ya vipengele vinavyoleta mwingilianomatini katika usawiri wa sifa za wahusika wakuu katika UFL, UMM, UG na SS. Aidha, tumeonyesha jinsi mwanamke kama mhusika alivyoathiri maisha ya wahusika wakuu katika matini teule.

5.1 Sifa za Wahusika Wakuu katika UFL, UMM, UG na SS

Wahusika wanachangia pakubwa katika kuendeleza na kufanikisha dhamira za mtunzi/ msimulizi wa kazi yoyote ya kifasihi. Pasipo wahusika, ni vigumu kuendeleza usimulizi wowote unaofikiriwa kuwa wa kifasihi. Hivyo basi, uhakiki wa wahusika katika matini teule ni muhimu kwa sababu ni kupitia kwa wahusika ambapo malengo ya mtunzi hukamilishwa. Mbali na ujenzi wa msuko wa hadithi, wahusika vilevile hukuza na kuendeleza maudhui yanayobainishwa katika kazi ya kifasihi.

Katika UFL, mhusika mkuu aliyechunguzwa ni Fumo Liyongo, Mikidadi katika UMM, Gilgamesh katika UG na Samsoni katika SS. Hata hivyo, kuna baadhi ya wahusika wajenzi ambao wanasaidia kukamilisha picha ya mhusika mkuu yeyote.

Utafiti umebainisha kwamba mapenzi na usaliti yanachangia kuanguka kwa wahusika wakuu katika UFL, UMM, UG na SS.

5.1.1 Sifa ya Ukatili katika UFL

Mwana wa Liyongo anasawiriwa kuwa na sifa ya ukatili katika UFL. Liyongo kama mhusika mkuu hajaonyeshwa kama mwenye sifa ya ukatili. Badala yake Liyongo ndiye aliyefanyiwa njama za kuuawa na mfalme kupitia kwa mtoto wake. Hivyo, mwana wa Liyongo anachukua sifa ya ukatili kwa sababu ya kumuua baba yake. Baada ya kumuua baba yake, mwanawe Liyongo anafurahia sana kitendo hicho kisha anarudi kwa mfalme ili atoe ‘habari njema’ ya kifo cha baba yake. Mwana wa Liyongo anaonyesha kuridhika moyoni mwake baada ya kufaulu kumwua baba yake. Hii ndiyo sababu yake ya kupeleka ‘habari njema’ kwa mfalme (Sultani) kuhusiana na kifo cha baba yake. Anakosa kumthamini baba yake na badala yake kuongozwa na tamaa. Mtunzi anaeleza:

Mf. 70

UFL

Kayuwa hana fahamu
Kijana aliazimu
Kwa ile yakwe hamumu
Mke kwenda kuzengenya (ub. 178)

Kamtiya kitovuni
Naye ulele kwa t’ani
Achamka hamuoni
Kiyana amekimbiya (ub. 179)

Kutokana na dondoo hili, mwana wake Liyongo ana hamu zaidi ya kwenda kusikia kuhusu mke aliyeahidiwa na Sultani. Mtunzi anasema, ‘*Kwa ile yakwe hamumu, mke kwenda kuzengenya.*’ Maneno hayo yanamsawiri mwanawe Liyongo kuwa mtu

asiyejali maisha ya baba yake mzazi. Ni ukatili kwake kumchoma baba yake kitovuni akiwa amelala chali na kukimbia ili asije akajulikana kuwa ni yeye aliyemwua.

Ingawa mwana wa Liyongo alitekeleza mauaji ya baba yake, chanzo hasa cha mauaji hayo ni Sultani. Mwana wa Liyongo anaonekana kumkera mfalme kwa sababu anacheka kifo cha baba yake badala ya kulia, jinsi inavyoelezwa katika beti 210 na 216. Mfalme basi anamvua vyote alivyoahidi na hatimaye kumfukuza kutoka himaya yake. Mwana wa Liyongo anaonyesha sifa ya ukatili kwa sababu ya kutokuwa na huruma kwa baba yake mzazi ila ana tamaa za kumwoa binti yake Sultani. Wahusika Samsoni, Mikidadi na Gilgamesh nao wamesawiri sifa za ukatili katika hali zinazolingana na kuingiliana.

5.1.2 Sifa ya Ukatili katika UMM

Katika UMM, tunapata taswira ya mhusika Mikidadi akiwa katili katika vipindi tofautitofauti. Kwanza kabisa, mhusika Mikidadi anaonyesha ukatili wake kwa kuwaua wanaume hamsini kama inavyodhihirika katika ubeti wa 216 hapa chini:

Mf 71

UMM
Kajipeka kati mwao
Kwa siaha na zomeo
Alotinda mwinda huo
Ni khamsini rijaa (ub. 216)

Ubeti 216 unaeleza kwamba Mikidadi aliwarukia wale wanaume (*kajipeka kati mwao*) kwa kelele na sauti ya juu (*kwa siaha na zomeo*) na wakati huo kuwaua wanaume hamsini (*alotinda mwinda huo, ni khamsini rijaa*). Hatimaye Mikidadi alimwua kiongozi wa watu wale, Luhani ambaye alimkejeli Mikidadi kwamba alikatazwa mke kwa sababu ya kukosa kulipa mahari. Hapo ndipo Mikidadi alimrukia na vita vikali vikaanza (beti 226-238). Baada ya mapigano makali, Mikidadi alifaulu kumwua

Luhani kwa kumkata kichwa chake hadi kikaanguka chini jinsi inavyoelezwa na msimulizi katika ubeti ufuatao:

Mf 72

Akamkamata ndevu
Akazivuta kwa nguvu
Akamshika mashavu
Kamtinda akamaa (ub. 237)

Akamkata na rasu
Kwa mkonowe na kisu
Akamuekea Kesu
Mbeleye kamuekea (ub. 238)

Ukatili wa Mikidadi unaonekana katika beti 237 na 238. Maneno katika ubeti wa 237 yanaonyesha kuwa Mikidadi alikuwa katili. Kitendo cha *kumkamata ndevu na kuzivuta kwa nguvu* kinaashiria ukatili. Inaonyesha kwamba mhusika hakuwa na huruma hata kidogo kwa adui wake. Isitoshe, *anamshika* tena *mashavu* ili aweze kumkata shingo. Ingawa Mikidadi anasawiriwa kama katili, mauaji aliyoyatekeleza katika ubeti 238 yalikuwa ya kumnusuru kijana Kesu ambaye alikuwa ametekwa nyara na Luhani. Luhani alikuwa amemfunga Kesu ili amchukue mkewe, Anasa, kuwa mke wake. Kwa sababu hiyo, Mikidadi alionyesha huruma kwa kijana Kesu aliyekuwa amefungwa miguu tayari kungojea kifo. Mtunzi anaeleza kuwa Mikidadi ‘*akamkata na rasu, kwa mkonowe na kisu*’ kuonyesha kuwa alimwua kwa urahisi bila usaidizi wa mtu yeyote. Hata hivyo, Mikidadi anaonyesha huruma kwake Kesu lakini ukatili kwake Luhani. Baada ya kumkata, anakipeleka kichwa kile hadi kwa Kesu ili kuthibitisha ukweli kwamba amemwua Luhani (*Akamuekea Kesu Mbeleye kamuekea*).

Katika mfano wa ubeti 216, 237 na 238, mauaji kwa Mikidadi kilikuwa kitu rahisi kwake mradi ametimiza malengo yake. Alipokejeliwa na Luhani, aliona aonyeshe umahiri wake kwa kumwua na kukipeleka kichwa chake kwa Kesu, ili kuthibitisha

kwamba yeye (Mikidadi) ni mtu hodari kama simba jinsi alivyoeleza katika ubeti wa 221.

Mfano mwingine unaodhihirisha kwamba mhusika Mikidadi alikuwa katili unapatikana katika masimulizi marefu ya beti 365 hadi 418. Katika beti 377 hadi 381, Mikidadi aliweka miadi na Sultani kwamba alihitaji kupigana na mashujaa elfu moja na iwapo angewashinda, Sultani angempa silaha za askari wale pamoja na farasi wao. Tunapata sehemu ya maagano hayo katika beti 379 na 381 hapa chini:

Mf 73

UMM
Nawatimue elifu
Mashujaa wasio khofu
Wawazao kita sefu
Wazoovu wa kitaa (ub. 379)

Tatwaa silaha zao
Na farasi walo nao
Sultani Kamba ndiyo
Ahadi imetimia (ub. 381)

Mhusika Mikidadi anamweleza Sultani kwamba alihitaji kupigana na askari, angalau elfu moja. Inabainisha kwamba alijiamini na alijua kuwa angewashinda wote “*Nawatimue elifu Mashujaa wasio khofu.*” Mikidadi anataja bila wasiwasi wowote kwamba yuko tayari kupigana na mashujaa elfu. Mbali na kupigana nao, Mikidadi anaonya kuwa atachukua silaha na farasi wao pia kwa kusema “*Tatwaa silaha zao na farasi walo nao.*” Kwa kweli, maneno ya Mikidadi yanatimia jinsi inavyoonyeshwa katika ubeti ufuatao:

Mf 74

UMM
Mikidadi kawakata
Asisaze mtu hata
Hata mwondoka wa vita
Sultani katongoa (ub. 414)

Kwa kuzingatia maneno “*Mikidadi kawakata, asisaze mtu hata...*” yaliyosemwa na msimulizi wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* maelezo katika ubeti 414 yanaonyesha kwamba Mikidadi aliwaua askari wote elfu moja waliopigana naye. Kitendo hiki aidha kinabainisha kuwa Mikidadi alikuwa muuaji katika hali nyingine tofauti na jeshi lililokuwa limeandamana na Mayasa. Jeshi hili lilitaka kujua ukweli iwapo Mayasa alitaka kuolewa na Mikidadi au Maliki. Hivyo, lilipigana vita vikali lakini mwishowe Mikidadi alishinda vita hivyo kwa kuwaua watu wote waliokuwa vitani. Hayo yanathibitishwa katika beti zifuatazo. Mikidadi anamjibu Mayasa kwamba atawaua wote na hakuna hata mmoja atakayebaki. Mtunzi anaeleza:

Mf 75

UMM
Akajibu Mikidadi
Hawa kwao hawarudi
Roho zao na jasadi
Haibudi kupotea (ub. 554)

Kawangia kati mwao
Asikhofu wingi wao
Kiwakata vitwa vyao
Asipumue kuuu (ub. 557)

Beti 554 na 557 zinabainisha ukweli kuwa Mikidadi alikuwa mhusika aliyejawa na hamaki zilizoishia kusababisha vifo kila alipoteteleza mauaji. Mikidadi aliwakata maadui wake vichwa. Tunaelezwa kwamba aliwakata vichwa vyao bila kupumzika “*kiwakata vitwa vyao, asipumue kuuu*”. Maneno hayo yanaashiria ukatili wa Mikidadi. Inaonyesha kwamba Mikidadi hakuwa na huruma wala hofu alipokuwa akitekeleza mauaji ya adui zake. Alikuwa katili. Utafiti huu unabainisha kuwa kuna mwingilianomatini baina ya SS na UMM unaoonekana kupitia wahusika wakuu, yaani Samsoni na Mikidadi. Wahusika wote wawili wana sifa ya ukatili hasa kupitia mauaji ya halaiki ya watu kama ilivyoelezwa katika mifano iliyotolewa. Samsoni na Mikidadi wanadhihirisha mauaji ya kuanzia watu wachache hadi maelfu. Simulizi

zote mbili zinatumia visa mbalimbali kueleza ukatili wa wahusika hao, Samsoni na Mikidadi.

5.1.3 Sifa ya Ukatili katika UG

Mhusika mkuu katika UG ni Gilgamesh. Sawa na UFL, UMM na SS, anwani ya matini inaashiria kuwa kisa kinachosimuliwa kinahusiana pakubwa na mhusika anayetajwa katika anwani. Mhusika Gilgamesh amesawiriwa kuwa na sifa ya ukatili katika visa vikuu viwili.

Katika kisa cha kwanza, Gilgamesh anaonekana akipigana na Humbaba, mlinzi katika Msitu wa Seda. Humbaba aliwekwa pale kimaksudi ili achunge msitu huo dhidi ya uvamizi wa binadamu. Msitu wa Seda ulikuwa ni makazi ya miungu na hivyo uliheshimika sana. Hakuna binadamu aliyethubutu kwenda pale. Kusudi la Gilgamesh kwenda kwenye Msitu wa Seda lilikuwa ni kukata miti ya seda ili ajenge kasri yake. Ingawa Gilgamesh alishirikiana na rafiki yake Enkidu katika uvamizi wa Msitu wa Seda, yeye aliongoza mapigano na Humbaba. Katika Kibao II:10 msimulizi anasema:

Mf 76

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(They will say) it was Gilgamesh who locked in battle with Humbaba the terrible!</i> <i>(Tablet II:10)</i>	(Watasema) Gilgamesh ndiye aliyepambana vitani na Humbaba anayeogofya! (Kibao II:10)

Mistari katika Mf 76 ni baadhi ya maneno yaliyosemwa na Enkidu akimtia moyo Gilgamesh asiogope kwenda kupigana na Humbaba. Anamhimiza kupigana vita ili hatimaye ijulikane kwamba ni yeye tu (Gilgamesh) aliyemwua Humbaba aliyeogopwa na kila mtu. Baada ya safari ndefu kuelekea msituni, Gilgamesh na Enkidu hatimaye walifika katika Msitu wa Seda. Njiani, Gilgamesh aliota ndoto tano ambazo zikitafsiriwa zilimpa moyo kuwa angefaulu katika vita vyake na Humbaba.

Maelezo ya vita baina ya Gilgamesh na Humbaba yanaonyeshwa katika Kibao cha V. Enkidu, rafiki wa Gilgamesh anachukua nafasi ya kumsaidia rafiki yake kukabiliana na Humbaba hadi kufa. Kabla ya vita vikali, majibizano ya kikejeli yalitangulia, kwa mfano katika Kibao V:18;

Mf 77

UG

M.A	M.T (Tafsiri yangu)
<i>(Humbaba spoke to Gilgamesh, saying; An idiot and a moron should give advice to each other, but you, Gilgamesh why have you come to me! ...You have brought Gilgamesh into my presence you stand....an enemy, a stranger. ...Gilgamesh, throat and neck I would feed your flesh to the screening vulture, ...the eagle, and the vulture!)</i> (Tablet V:18)	Humbaba alinena na Gilgamesh akisema; ...zuzu na punguani wanapenda kujipatia ushauri, Lakini wewe, Gilgamesh, kwa nini umekuja kwangu!umemleta Gilgamesh mbele yangu,...unasimama..., adui, mgeni ...Gilgamesh, koo na shingo, Nitawalisha tai nyama ya mwili wako! (Kibao V:18)

Katika mistari hii, kulikuwa na majibizano baina ya Humbaba, Gilgamesh na Enkidu. Kila mmoja alimchokoza au kumkejeli mwenzake kabla ya kuanza mapigano. Katika hali ya kawaida, uchokozi hutangulia vita baina ya watu wanaopigana. Muda mfupi baadaye, Gilgamesh na Enkidu walimkabili Humbaba, mlinzi wa Mstitu wa Seda. Majibizano baina ya Gilgamesh, Enkidu na Humbaba yanalingana na majibizano kati ya Samsoni, babake Mtimna na Wafilisti katika SS (Waamuzi 15:1-16). Mwingilianomatini unaonekana kupitia majibizano yanayoonyesha kuwa kila mhusika ana hasira juu ya mwenzake na kinachofuatia ni mapigano yanayosababisha vifo. Hivyo, maelezo ya Jilala (2016) kuwa hakuna matini yoyote katika fasihi inayoweza kuangaliwa peke yake na kwa kujitegemea yanabainika katika matini hii. Katika SS, babake Mtimna na Mtimna waliteketezwa na katika UG, Humbaba anashindwa na kuuawa.

Maelezo ya mazungumzo baina ya wahusika Gilgamesh, Enkidu na Humbaba yamechukua Kibao chote cha V. Hata hivyo, tutatoa mistari minne tu yanayoonyesha kuwa Gilgamesh ndiye aliyemwua Humbaba kwa ukatili.

Mf 78

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<p><i>“My friend Humbaba, Guardian of the forest, grind up, kill, pulverize (?) and destroy him! Erect an eternal monument proclaiming....how Gilgamesh killed (?) Humbaba”</i></p> <p><i>.....they pulled out his insides including his tongue.</i></p> <p><i>They tied together a raft... Enkidu streed it...</i></p> <p><i>While Gilgamesh held the head of Humbaba</i> (Tablet V:20)</p>	<p>Rafiki yangu Humbaba, mlinzi wa msitu wa mikangazi, <i>Msage, muue, mponde na umharibu!</i>Unda mnara utakaodumu milele <i>Kutangaza....jinsi Gilgamesh alivyomuua (?) Humbaba”</i></p> <p><i>...walinyofoa viungo vyote vya ndani ya mwili wake ikiwemo ulimi...</i></p> <p>Walifunga boya..Enkidu aliiendesha ...</p> <p>Huku Gilgamesh akishika kichwa cha Humbaba (Kibao V: 20)</p>

Katika maelezo hayo, usawiri wa mhusika Gilgamesh unaonyesha kwamba yeye ni katili na muuaji asiyeogopa hata miungu. Hii ni kwa sababu, Humbaba, aliyekuwa mlinzi katika msitu wa Seda alitumwa huko na mungu wa ulinzi, Shamash. “*Msage, muue, mponde na umharibu!*” ni maneno yaliyosemwa na Gilgamesh katika mapambano yake na Humbaba. Maneno haya yanaashiria ukatili aliokuwa nao Gilgamesh. Aidha, kwa msimulizi kueleza kwamba *...walinyofoa viungo vyote vya ndani ya mwili wake ikiwemo ulimi...* ina maana kuwa Humbaba aliuawa kinyama. Ni maneno yanayoonyesha ukatili wa Gilgamesh vilevile. Kitendo cha *kunyofoa viungo vyote ikiwemo ulimi* ni cha kusikitisha. Eliezer, F. K na wengine (2016) wanaeleza ‘kunyofoa’ kwamba ni kushika kitu na kukiachanisha na kingine kwa kuvuta. Kulingana na maelezo haya, Gilgamesh alikuwa katili mno ikichukuliwa kwamba baada ya kumuua Humbaba aliondoa viungo vyote vya ndani pamoja na ulimi. Kitendo hiki kinaonyesha kuwa Gilgamesh hakuwa na utu.

Mwanzoni, kabla ya kuanza safari yao, Gilgamesh na rafiki yake Enkidu walipeleka maombi yao kwa miungu (Ninsun na Shamash) ambao waliwapa baraka ya kuendelea na nia yao ya kuenda msituni. Hivyo basi, mauaji yaliyotekelezwa na Gilgamesh yalijulikana na miungu hiyo. Mhusika Gilgamesh katika kipindi kingine cha mauaji ya kikatili, anamwua Fahali wa Mbinguni kama afanyavyo bucha anapochinja mnyama. Maelezo hayo yanapatikana katika Kibao cha VI:24:

Mf. 79

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(Enkidu stalked and hunted down the Bull of Heaven.</i>	Enkidu alimwandama na kumwinda Fahali wa Mbinguni.
<i>He grasped it by the thick of its tail and held onto it with both his hands (?), while Gilgamesh,</i>	Alimfumbata kwa kuutumia mkia wake mnene. Aliushikilia kwa mikono yake miwili (?) <i>Naye Gilgamesh kama bucha hodari,</i>
<i>like an expert butcher, boldly and surely approached the Bull of Heaven.</i>	Kwa ujasiri na uhakika alimwendea Fahali wa Mbinguni
<i>Between the bape, the horns and ...he thrust his sword. After they had killed the Bull of Heaven, they ripped out its heart and presented it to Shamash) (Tablet VI:24)</i>	Baina ya ukosi, pembe na... alirusha upanga wake. Baada ya kumuua Fahali wa mbinguni. <i>Waliunyofoa moyo wake na kuupeleka kwa Shamash (Kibao VI:24)</i>

Maelezo katika kifungu hiki yanaonyesha ukatili wa Gilgamesh anapomuua Fahali wa Mbinguni. Msimulizi anaeleza kuwa Gilgamesh alikuwa *kama bucha hodari*. Isitoshe, “*waliunyofoa moyo wake na kuupeleka kwa Shamash.*” Mara nyingi baada ya kutekeleza mauaji, si kawaida kushughulika tena na kuchinja mhusika ili kutoa moyo wake. Kitendo cha kutoa au kunyofoa moyo wa maiti ni nadra sana. Hapa ndipo ukatili wa Gilgamesh unadhihirika. Aidha, kutoa moyo wa Fahali wa Mbinguni na kuupeleka kwa Shamash ni dhihirisho kwamba Gilgamesh alitaka kumhakikishia Shamash kwamba amemuua Fahali wa Mbinguni. Mauaji hayo yalikuwa ya kiwango cha juu kwa sababu kumwua Fahali wa Mbinguni, ambaye ni mmoja kati ya miungu, si jambo rahisi. Matendo yanayofanywa na Gilgamesh anapokabiliana na Humbaba

na Fahali wa Mbinguni yanatosha kumchora mhusika Gilgamesh kama mhusika katili.

5.1.4 Sifa ya Ukatili katika SS

Mhusika mkuu katika *Simulizi ya Samsoni* ni Samsoni. Samsoni amesawiriwa kama mhusika aliye na sifa tofautitofauti. Iliyotanguliwa kutajwa, Samsoni alikuwa kiongozi (Mwamuzi) wa Israeli kwa miaka ishirini (Waamuzi 16:31). Kwa wakati huu wote, Samsoni alikuwa na jukumu la kuwaongoza Waisraeli jinsi alivyoagizwa na Mwenyezi Mungu. Hii ndiyo sababu kuwa kuzaliwa kwake kuliwekewa masharti ambayo yalifaa kufuatwa na mama mzazi.

Katika kisa cha kwanza cha ukatili wake, Samsoni aliwaua wanaume thelathini katika mji wa Ashkeloni na kisha kuwanyang'anya mali yao pamoja na nguo (Waamuzi 14:19). Mauaji hayo hayakuwa ya kawaida kwa sababu msimulizi anaeleza kuwa “Roho wa Bwana ilimjia kwa nguvu” kisha akatekeleza mauaji hayo. Kitendo cha kuwaua na kisha kuwanyang'anya nguo maiti kinaonyesha ukatili wa Samsoni kwa binadamu wenzake. Haja yake Samsoni ilikuwa apate mali ya kuwapa watu waliofumbua kitendawili alichokuwa amewategea. Katika hali ya kawaida, kungekuwa na mapigano baina ya vikundi vinavyozozana kabla ya vifo au mauaji kutokea. Hata hivyo, hili halikufanyika katika kisa hiki cha mauaji yaliyofanywa na Samsoni.

Kisa kingine kinachoonyesha kwamba mhusika Samsoni alikuwa katili ni wakati alipolipiza kisasi juu ya Wafilisti waliokuwa wamewaua kwa kuwateketeza moto mwanamke Mtimna (mkewe Samsoni) pamoja na baba yake. Ukatili wa Samsoni katika kisa hiki huenda ulitokana na ukatili wa Wafilisti waliomchoma Mtimna pamoja na baba yake. Ingawa Samsoni alikuwa amechukuliwa na rafiki yake, kitendo

cha kuwaua watu wengi sana kama inavyoonyeshwa katika Waamuzi 15:8 kinaashiria kwamba bado alimpenda mke wake Mtimna. Wafilisti hata hivyo walifikiana kuwaua msichana Mtimna na baba yake baada ya kujua kwamba Samsoni alikuwa ameteketeza mashamba yao ya ngano na mizeituni. Mashamba hayo yaliteketezwa kwa njia ya ajabu kwa sababu Samsoni aliwashika mbweha mia tatu (300) na kuwafunga mikia yao wawili wawili. Baada ya kuwafunga hivyo, aliwasha mienge kwenye kila jozi ya mbweha na kuwaachia katika mashamba ya Wafilisti (Waamuzi 15:3-8). Kitendo hiki ndicho kilichochochea Wafilisti kuwaua Mtimna na baba yake, hivyo kumkasirisha Samsoni ambaye aliwashambulia kwa mapigo makuu na kuwaua watu wengi.

Ukatili wa Samsoni aidha unabainika katika mauaji ya watu elfu moja jinsi inavyorekodiwa katika Waamuzi 15:14-16. Wakati huu vilevile, msimulizi anasema kuwa “Roho wa Bwana alimjia kwa nguvu.” Jambo hili linaashiria kuwa nguvu aliyoitumia Samsoni katika mauaji yake ilitoka kwa “Bwana wake.” Msimulizi anataja kwamba alipojiwa na Roho, kamba zilizokuwa zimefunga mikono yake “zikawa kama katani iliyochomwa kwa moto na vifungo vyake vikaanguka chini toka mikononi mwake.” Vifungo vilipoanguka chini, Samsoni alipata nafasi ya kunyosha mkono wake na kuchukua mfupa mpya wa taya la punda na kua nao Wafilisti elfu moja. Mhusika alipokwisha kuwaua watu hao alijisifu kwa kusema:

Mf 80

SS

Kwa taya la punda

Malundo juu ya malundo

Kwa taya la punda

Nimeua watu 1,000 (Waamuzi 15:16).

Katika Mf 80, msimulizi anaeleza kuwa mhusika (Samsoni) aliutupa ule mfupa wa taya na mahali pale pakaitwa Ramath-Lehi, maana yake kilima cha Taya (Waamuzi

15:17). Mahali pale kuitwa baada ya *mfupa wa taya la punda* lililotumika kuwaua Wafilisti inamaanisha kwamba kitendo hicho kiliandika historia katika Kalenda ya Waisraeli.

Kipindi kingine kinachoonyesha kwamba Samsoni alikuwa katili ni wakati wa kufa kwake. Huu ni wakati alipokuwa amebembelezwa na mkewe Delila hadi akamfichulia siri ya nguvu zake zilizokuwa kwenye nywele zake ndefu. Delila alifaulu kujua siri za nguvu za mumewe na kumsaliti kwa Wafilisti. Baada ya kufaulu kuzinyoa nywele za Samsoni, aliwaita Wafilisti ambao walifika mahali pale upesi na kisha kumkamata na kumng'oa macho yake. Wafilisti baadaye walimpeleka Samsoni gerezani na kumsimanga. Hili lilimfanya Samsoni kumwomba Mungu wake amtie nguvu mara moja tu ili apate kulipiza kisasi juu ya Wafilisti. Hivyo basi, nywele zake zilimea tena na nguvu zikamrejea.

Watu na viongozi wa Wafilisti walifurahia sana kwa sababu ya ushindi dhidi ya adui wao Samsoni. Walimtoa gerezani na kumpeleka kwenye thieta ili waweze kufurahishwa naye. Msimulizi anasema kwamba jengo alilopelekwa Samsoni lilikuwa na watu 3,000 katika sakafu ya juu pasipo kuhesabu waliokuwa kwenye sakafu ya chini. Alipokuwa akijitayarisha kuwaburudisha watu waliokuwa pale, Samsoni alimwomba mtumishi aliyeshika mkono wake amweke mahali ambapo angeweza kuzigusa nguzo ambazo zilitegemeza jengo kusudi apate kuziegemea. Bila kusita, mtumishi alifanya jinsi alivyoagizwa na Samsoni. Muda mfupi baada ya kumwomba Mungu wake ampe nguvu angalau mara moja tena, Samsoni alizishika nguzo zile mbili na kuliangusha jengo hilo. Msimulizi anaeleza hivi katika Waamuzi 16:30:

Mf 81

SS

Basi nyumba ile ilikuwa imejaa watu waume kwa wake; na wakuu wote wa Wafilisti walikuwa- mo humo, na juu ya dari palikuwa na watu 3,000 waume kwa wake waliokuwa wakitazama, wakati Samsoni alipocheza... Samsoni akasema, “Nife pamoja na Wafilisti” Ndipo akazisukuma zile nguzo kwa nguvu zake zote, lile jengo likaanguka juu ya viongozi na watu wote waliokuwamo mle ndani yake. *Hivyo akawaua watu wengi wakati wa kufa kwake kuliko siku za uhai wake* (Waamuzi 16: 27-30).

Kutokana na maelezo katika Mfano 81, Samsoni *anawaua watu wengi* katika kufa kwake kuliko wakati wa uhai wake. Mauaji hayo yalifanywa kwa makusudi kwa sababu Samsoni, katika Waamuzi 16:28, anamwomba Mungu ampe nguvu za kutekeleza mauaji hayo juu ya Wafilisti. Watu waliokuwa katika jengo kubwa waliokuwa wakimtazama na kumdhihaki Samsoni walikuwa wengi ila waliokuwa katika sakafu ya juu ya jengo hilo wametajwa kuwa elfu tatu. Msimulizi anaeleza kwamba Samsoni *aliwaua watu wengi wakati wa kufa kwake kuliko siku za uhai wake*. Visa vilivyoratibiwa kuhusiana na watu wengi waliouawa na Samsoni vinampa mhusika Samsoni sifa ya kuwa mwaaji. Ingawa simulizi inaeleza kuwa mhusika alikuwa Mwamuzi wa Waisraeli, utafiti huu unadhihirisha kwamba ni kutokana na mauaji yake ya kiajabu ambapo Samsoni anasawiriwa kama katili.

5.2 Sifa ya Uongozi katika UFL, UG na SS

Wahusika wakuu katika matini teule wanasawiri sifa ya uongozi katika miktadha yao. Ili mhusika yeyote aitwe kiongozi, ni lazima aonyeshe kuwa na hulka fulani inayomfaa kiongozi. Ni lazima awe ameteuliwa na jamii au amejitolea mwenyewe kama kiongozi. Hata hivyo, kuna kiongozi atakayekuwa dhalimu na kuna yule atakayesifika katika uongozi wake jinsi tunavyoona kupitia wahusika Liyongo, Gilgamesh na Samsoni.

5.2.1 Sifa ya Uongozi katika UFL

Katika UFL, mhusika mkuu, Fumo Liyongo, anaonyesha sifa za kiongozi thabiti katika vipindi tofauti. Kwanza kabisa, Liyongo anasifika kwa sababu ya nguvu zake. Katika hali hiyo, Sultani wa Pate anamwandikia barua ya kumwita aende pale ili Wagalla nao wamwone. Liyongo anapopata barua, anakubali kwenda kwa Sultani. Matokeo yake ni kwamba Wagalla walivutiwa na umbo lake Liyongo na hivyo wakatamani kupata mbegu yake kwa kumwoza mke wa Kigalla kusudi awazalie mtoto wa kiume, mpango uliotimia. Sifa ya uongozi wa Fumo Liyongo vilevile inaonekana wakati anazidi kusifika, hivyo Sultani anahofia kwamba atamnyang'anya uongozi. Katika beti zifuatazo, tunapata maelezo hayo:

Mf 82

UFL
Na Sulutwani niseme
Alikuwa mwanamume
Tampoka ufalume
Dhana alimdhaniya (ub. 51)

“Anipoke ufalme
Kisa chanda nikiume
Kheri yangu mwanamume
Kumuuwa mara moya” (ub. 93)

Maelezo katika beti 51 na 93 yanaonyesha kwamba Fumo Liyongo alisifika kiasi cha kumshinda mfalme. Hiyo ndiyo sababu iliyomfanya Sultani kuhofia kwamba Liyongo angempokonya uongozi (*tampoka ufalme*). Sultani alifikiria zaidi na kuona heri kumwua Liyongo kuliko ajute baadaye. Mfalme anasema kuwa kuliko apokonywe uongozi na ajute baadaye (*kisa chanda nikiume*), ni heri amwue huyo mwanamume (Liyongo) mara moja. Uamuzi uliofikiwa na mfalme unaonyesha kuwa Liyongo alikuwa na sifa za uongozi hata kumshinda mfalme, ndiyo maana akataka kumwua mara moja. Katika UFL, kifo chake Liyongo kilionyesha kuwa alikuwa kiongozi

aliyesifika. Watu wengi walimlilia na kuhuzunika, wakisema kwamba Liyongo alikuwa silaha na ngao yao (UFL, ubeti 225).

5.2.2 Sifa ya Uongozi katika UG

Tofauti na Fumo Liyongo, mhusika Gilgamesh ameonyesha sifa ya kiongozi dhalimu. Sifa hii ya uongozi inadhihirika japo mwanzoni mwa simulizi, kwa mtazamo hasi na baadaye anageuka kuwa kiongozi mzuri. Gilgamesh anasifika kuwa kiongozi shupavu aliye na sifa ya uungu kando na kuwa binadamu (UG, Kibao I:2). Utafiti huu unashikilia kwamba huku kusifiwa kwake Gilgamesh kunamfanya kuwa dhalimu kwa watu wake. Kama kiongozi, Gilgamesh anafanya mambo kinyume na matarajio ya jamii. Ingawa alisifiwa na jamii kwamba yeye alikuwa mlinzi wa watu wake, aligeuka kuwanyanyasa na kuwadhulumu.

Katika kibao cha I:2, watu wa mji wa Uruk wanalalamika kwamba Gilgamesh anawanyanyasa kwa kuwa anamchukua kila mwanamwali na kulala naye kwanza kabla ya mume wake. Tafsiri ya Heidel (1949) imeweka wazi wazo hilo:

Mf 83

UG

M.A.	MT (Tafsiri yangu)
<i>And he is the shepherd of Uruk, (the enclosure</i>	Yeye ndiye mchungaji wa Uruk (mzunguko
<i>He is their shepherd, and yet he opposes them Strong, handsome (and) wisel...</i>	Ndiye mchungaji wao ilhali anawadhulumu Ana nguvu, mtanashati na mwenye hekima ...)
<i>Gilgamesh leaves no virgin to their lover</i> (Tablet I:2)	Gilgamesh <i>hamwachi bikira kwa mume wake</i> (Kibao I:2)

Mistari hii inaonyesha udhalimu wa Gilgamesh kwa watu wa Uruk. Gilgamesh alifaa kuwa kiongozi, mchungaji wa watu wa Uruk *ilhali anawadhulumu*. Ilikuwa kwamba Gilgamesh lazima afanye mapenzi na kila msichana aliyeolewa kabla ya kukutana na mume wake (*hamwachi bikira kwa mume wake*). Ni maneno yanayoonyesha kwamba

Gilgamesh alikuwa mbakaji. Katika ulimwengu wa sasa, ubakaji ni kosa ambalo linaadhibiwa vikali hasa kwa kuzingatia sheria dhidi ya ubakaji. Tendo la Gilgamesh la kuwabaka wanawake kabla ya kukutana na waume zao liliwachukiza watu wa Uruk ndipo wakapeleka malalamishi yao kwa miungu (Anu) ambao waliitikia maombi yao. Anu alimwumba Enkidu, aliyekuwa mpinzani wake aliyetumwa ili kushusha nguvu za Gilgamesh.

Enkidu alikuwa na sifa zilizolingana na za Gilgamesh na hivyo wakapigana mapigano makali. Hatimaye, hakuna aliyeshindwa na wakawa marafiki. Katika sehemu ya mwisho wa simulizi hii, Gilgamesh anageuza uongozi wake wa kidhalimu na kuwa kiongozi mzuri. Gilgamesh alibadilika na kuwa kiongozi mzuri jinsi utendi unavyoeleza katika mwanzo na mwisho wa simulizi.

5.2.3 Sifa ya Uongozi katika SS

Uongozi wa Samsoni ulitoka kwa Mwenyezi Mungu. Mungu alikusudia Samsoni kuwakomboa Waisraeli kutoka kwa utumwa wa Wafilisti. Samsoni aliteuliwa na Mungu kabla ya kuzaliwa kwake jinsi tunavyoelezwa na msimulizi katika Waamuzi 13:5:

Mf 84

SS

...kwani tazama, utachukua mimba, nawe utamzaa mtoto mwanamume; na wembe usipite juu ya kichwa chake; maana mtoto huyo atakuwa mnadhiri wa Mungu tangu tumboni; *naye ataanza kuwaokoa Israeli na mikono ya Wafilisti* (Waamuzi 13:5)

Mbali na masharti aliyopewa mama mzazi katika mfano 84 hapa juu, lengo kuu la kuzaliwa kwake Samsoni lilikuwa kuwakomboa Waisraeli kutoka kwa utumwa wa Wafilisti. Msimulizi anaeleza, *naye ataanza kuwaokoa Israeli na mikono ya Wafilisti*. Msimulizi anaweka wazi lengo la kuzaliwa kwake Samsoni, kwa kutumia neno

kuwaokoa. Katika utangulizi wa kitabu cha Waamuzi, tunapata maelezo kwamba Samsoni alizaliwa wakati Waisraeli walipokuwa wamemuasi Mungu na walipomrudia Mungu, naye Mungu aliwapatia Waamuzi, ambao ndio walioongoza makabila ya Israeli na kuwaokoa kutoka mikononi mwa adui zao (*Biblia Takatifu*, 2015). Katika uongozi wake, Samsoni anaonekana kutumia nguvu za kiajabu alizopewa na Mungu. Katika Biblia, Malaika anapotokea jamii fulani na mtoto kuzaliwa kwa njia ya kimiujiza, Mungu anawatumia watoto hao kwa njia ya kipekee kutimiza lengo lake. Henderson (2013) anaeleza kuwa matukio yaliyozingira kuzaliwa kwa Samsoni yanalingana na matukio yaliyozingira kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji katika Luka 1:1-25. Ijapokuwa Elizabethi (mama yake Yohana Mbatizaji), Sara (mama yake Isaka) na mama yake Samsoni walikuwa tasa, Mungu aliwajalia watoto wanaume ambao walitumiwa na Mungu kwa njia ya kipekee. Samsoni alikuwa kiongozi aliyejawa na ujasiri. Yeye pekee alikabiliana na taifa zima la Wafilisti. Katika SS, hakuna mhusika mwingine anayetajwa kuhusika na uongozi wa Wafilisti isipokuwa Samsoni.

Katika uongozi wake, Samsoni anaonyeshwa kuwa na imani kuu katika Mungu wake. Ana imani kwamba Mungu alikuwa pamoja naye kila wakati. Hili linadhihirika, kwa mfano katika Waamuzi 15:18-19. Samsoni anamlilia Bwana akisema, “*Umempa mtumishi wako ushindi huu mkuu. Je, sasa nife kwa kiu na kuangukia mikononi mwa hawa watu wasiotahiriwa?*” Samsoni anakuwa na uzungumzi nafsiya akijiuliza iwapo atakufa kwa sababu ya kiu baada ya kuwaua Wafilisti elfu moja. Maandishi yanaeleza kuwa **Bwana** alifunua shimo pakatoka maji na Samsoni alipoyanywa nguvu zikamrudia na kuhuika. **Bwana** hapa limetumika kwa maana ya Mwenyezi Mungu, Mungu wake Samsoni.

Ingawa Samsoni alikuwa kiongozi jasiri na mwenye imani alikuwa pia na udhaifu wake. Alikuwa kiongozi asiyetafakari kwa makini matokeo ya matendo yake. Aliongozwa na tamaa ya mwili wake. Katika SS, Samsoni amesawiriwa kuwa na tamaa ya wanawake, kahaba, ambao wanasababisha anguko lake. Hata hivyo, Biblia imenakili kuwa Samsoni alikuwa kiongozi wa Waisraeli kwa miaka ishirini.

Mf 85

Naye akawa *mwamuzi wa Israeli katika siku za Wafilisti muda wa miaka ishirini* (Waamuzi 15:20).

...Naye alikuwa *mwamuzi wa Israeli muda wa miaka ishirini* (Waamuzi 16: 31).

Matumizi ya maneno *...alikuwa mwamuzi wa Israeli muda wa miaka ishirini*, yanasisitiza uongozi wake. Katika uongozi wake, Samsoni anasifika kwa sababu ya nguvu zake za kiajabu zilizochangia katika ukombozi wa Waisraeli na urafiki wake wa kinafiki na Delila.

5.3 Sifa ya Ushujaa katika UFL, UMM, UG na SS

Katika jamii nyingi za Kiafrika, shujaa huonekana kuwa na sifa zisizo za kawaida. Ili kufikia kiwango cha mhusika kuitwa shujaa huwa amefanya mambo yasiyotendwa na binadamu wa kawaida katika jamii. Shujaa huonekana kutenda mambo makuu katika jamii ambayo huwa nadra sana kutendwa na wanajamii wa kawaida. Mara nyingi shujaa huwa mkombozi wa jamii hasa kutokana na vita. Aidha, mashujaa huwa na umbo la kutisha na nguvu zisizo za kawaida hivi kwamba kupigana na maadui huwa kitu rahisi kwake. Sifa ya ushujaa miongoni mwa wahusika Fumo Liyongo, Mikidadi, Gilgamesh na Samsoni zinalandana hivyo kuzua mwingilianomatini katika tendi teule za utafiti huu.

5.3.1 Sifa ya Ushujaa katika UFL

Utendi wa Fumo Liyongo umesifika kutokana na ushujaa wa mhusika mkuu, Fumo Liyongo. Ushujaa wake ulienea kwa sababu ya matendo yake yafikiriwayo kuwa ya ajabu. Sifa za ushujaa wa Liyongo zinadhihirika katika mifano ifuatayo:

Mf 86 UFL

Ni *mwanamume swahihi*
kama simba una zihi
 usiku na asubuhi
 kutembea ni mamoya (ub. 13)

Mhusika anaelezwa kuwa *ni mwanamume swahihi* aliyekuwa *kama simba*. Mtu anayefananishwa na simba ana uhodari fulani. Simba ni mnyama hatari porini na mara nyingi huchukuliwa kuwa mfalme wa porini. Fumo Liyongo anapofananishwa na simba anasawiri dhana ya ushujaa. Aidha, umbo lake lilionyesha kuwa alikuwa na nguvu (*kama simba una zihi*). Fumo Liyongo angetembea usiku na mchana bila woga. Katika hali ya kawaida, inaaminika kwamba usiku ni wakati wa giza, hivyo kutembea au kufanya kazi yoyote inakuwa vigumu. Kutembea kwake Fumo Liyongo usiku kunaashiria ushujaa kwa sababu hakutishwa wala kuogopa giza jinsi wafanyavyo binadamu wa kawaida.

Aidha, Fumo Liyongo anaonyesha ushujaa wake akiwa na Wagala. Tunapata hayo katika ubeti ufuatao:

Mf 87

UFL
 Ruhu zikenda kishindo
 zimo zao hukoma ondo
 huyo ni bwana wa kondo
 ashindaye jeshi niya (ub. 35)

Msimulizi anaeleza kuwa Wagala waliposikia habari za Fumo Liyongo, waliingiwa na hofu hivyo nyoyo zao zikadunda (*Ruhu zikenda kishindo*). Wagala walitambua kwamba Fumo Liyongo alikuwa hatari vitani (*huyo ni bwana wa kondo, ashindaye*

jeshi niya). Kutaja kwamba alikuwa bwana wa kondo (*vita*) ni dhahiri kwamba mhusika alijulikana hasa kutokana na ushujaa wake vitani, kwani angeshinda majeshi waliopigana naye (*ashindaye jeshi niya*).

Katika beti 67, 68 na 69, Wagala waliogopa kumshika Fumo Liyongo kwa sababu waliamini kwamba angewaua wote jinsi inavyoelezwa katika ubeti wa 68. Maelezo zaidi kuhusu ushujaa wake yanapatikana katika ubeti wa 69:

Mf 88

UFL
Sulutwani tumjibu
kumuuwa ni dharubu
kumshika ni taabu
hatuwezi kwa umoya (ub.69).

Katika Mf 88 hapa juu, Wagala walibaini kwamba kumwua Fumo Liyongo yalikuwa mapambano makali (*kumuuwa ni dharubu*). Aidha, walijua kwamba ilikuwa vigumu kumshika kwani angewashinda wote (*kumshika ni taabu, hatuwezi kwa umoya*). Maelezo hayo yanadhihirisha kuwa Fumo Liyongo alikuwa shujaa aliyesifika nyakati zake. Katika maelezo ya beti 67 hadi 69, inabainika kwamba Fumo Liyongo alikuwa na ushujaa uliomfanya mfalme (Sultwani) kumwonea wivu na kuogopa kuwa angemnyang'anya uongozi. Hiyo ndiyo iliyokuwa sababu ya mfalme kutaka kumwua. Alipokuwa gerezani, Fumo Liyongo alikuwa chini ya ulinzi mkali. Ilibidi azingirwe na majeshi kwa hofu kuwa chochote kingetokea kwa sababu ya ushujaa wake uliokuwa umeshangaza watu wengi. Katika ubeti ufuatao, uamuzi uliafikiwa kwamba Fumo Liyongo apelekwe vitani ili auawe. Msimulizi anaeleza:

Mf 89

UFL
Na tumfanye amiri
zikiya zita ni kheri
atakufa kwa uzuri
maana hatokimbiya (ub. 90)

Uamuzi uliafikiwa kwamba Fumo Liyongo afanywe amiri jeshi mkuu ili afe kwa urahisi akiongoza vita. Akiwa amiri, ilimaanisha kwamba Fumo Liyongo angekuwa mbele vitani na kufa kwake ilidhaniwa kuwa kungekuwa rahisi. Ni bayana kuwa yeyote anayewekwa kukaa mbele katika vita ana ushujaa na umahiri vitani. Hivyo, ushujaa wa Fumo Liyongo ulikuwa umekithiri kiasi cha kuogofya Mfalme wa Pate wakati huo.

5.3.2 Sifa ya Ushujaa katika UMM

Kisa cha Mikidadi na Mayasa kinaanza kwa kumsawiri Mikidadi kama mtu maskini. Anasutwa kwa kutorithi chochote kutoka kwa baba yake. Anakejeliwa kwa kukosa mali ya kupeana kama mahari ili apate mke (Mayasa). Hata hivyo, matukio ya kihadithi yanapoendelea, Mikidadi anajitokeza kama mhusika asiyepuuzwa. Anakabiliana na watu wengi ikiwa ni pamoja na majeshi ya Sultani katika vita vikali. Mikidadi anaonyesha ushujaa wake kwanza anapopambana na jini. Tukio hili limeonyeshwa katika beti 167 hadi 184 katika UMM.

Ushujaa wa Mikidadi vilevile unaonekana katika mashambulio yake na Luhani. Luhani alikuwa kiongozi katili aliyekutana na Mikidadi akiwatesa vijana wawili. Hapo ndipo Mikidadi alipowaokoa vijana wale kwa kumwua Luhani (beti 236-240). Baada ya kumwua Luhani, Mikidadi alikusanya mali yote na kumgawia Kesi (moja kati ya viongozi wa Sultani) sehemu yake. Ushujaa wa Mikidadi unadhihirika kwa namna alivyowanyang'anya watu mali yao kwa urahisi. Kwake kuwaua watu hamsini ilikuwa kazi rahisi, jinsi tunavyoelezwa katika ubeti ufuatao:

Mf 90

UMM
Na wane kamkamata
Na wa tano na wa sita
Hisabuye nilopata
Khamsini kawandoa (ub. 279)

UMM umewasawiri wahusika wawili, Mikidadi na Mayasa kama mashujaa wasiomithilika. Hata hivyo, utafiti huu umezingatia hasa Mikidadi kama mhusika mkuu. Mikidadi anaonyesha ujasiri wake kwa kuwaua majeshi ya askari na Sultani (beti 281 hadi 364). Mhusika Mikidadi anasema kwamba yeye si mwoga kamwe. Sultani alipomwona Mikidadi, alibainisha ukweli uliokuwa umeenea kote kwamba yeye ni shujaa. Tunapata haya katika beti mbili zifuatazo:

Mf 91

UMM
Mikidadi kajisifu
Waziri kumarifu
Mimi si mtu wa hofu.
Hata na wewe wajua (ub. 363)

Kumuonako shujaa
Sultani kafazai
Roho ikaingia mai
Kwani yakini ni shujaa (ub. 366)

Sultani alipomwona Mikidadi, alibainisha ukweli kuwa yeye alikuwa shujaa. Sultani alifadhaika sana (*Sultani kafazai, roho ikaingia mai*). Kwa kusema kwamba '*roho yake ikaingia mai*', msimulizi alikusudia kuonyesha hofu aliyosababisha Mikidadi kwa Sultani. Msimulizi anaposema *Kwani yakini ni shujaa*, ni kwa sababu ilikuwa imejulikana kwamba Mikidadi alikuwa shujaa.

Katika tukio jingine, Mikidadi anaonyesha sifa za ushujaa katika beti 365-418. Tukio hili linamwonyesha Mikidadi akipigana na askari elfu moja (1,000) waliotiwa alama nyekundu ya ngeu. Askari hao walikuwa wametengwa kimaksudi ili wapambane na Mikidadi. Wote walishindwa na Mikidadi na wakatoroka, wakirudi kwa Sultani. Jambo hili lilimkasirisha Sultani ambaye alitoa amri kwa Mikidadi kuwaua askari hao waliomfedhehesha kwa woga wao. Kwa amri ya Sultani, Mikidadi aliwaua wote asibakishe hata mmoja, jinsi inavyodokezwa katika ubeti ufuatao:

Mf 92

UMM
 Mikidadi kawakata
 Asisaze mtu hata
 Hata mwondoka wa vita
 Sultani katongoa (ub. 414)

Baada ya kuona ujasiri wa Mikidadi, Sultani alitoa amri Mikidadi apewe chochote alichohitaji. Hapa ndipo Mikidadi alipopata mali zaidi ya kupeleka kwa baba yake Mayasa kama mahari. Utafiti huu umebainisha kwamba ushujaa wa Mikidadi umeonyeshwa katika sehemu kubwa ya UMM. Aidha, ushujaa wake unaambatana na vita vinavyoishia kusababisha mauaji. Beti 528-639 zinaeleza mapigano makali yaliyotokea baina ya Mikidadi na jeshi lililoambatana na Mayasa kumsindikiza kwa mume aliyepangiwa, Malik. Katika ubeti ufuatao tunapata taswira ya Mikidadi akijibwaga katikati yao bila woga wowote.

Mf 93

UMM
 Kawangia kati mwao
 Asikhofu wingi wao
 Kiwakata vitwa vyao
 Asipumue kuua (ub. 557)

Mtunzi anaeleza kwamba Mikidadi aliingia katikati yao bila kuogopa wingi wa askari wale (*asikhofu wingi wao*) na *kuwakata vichwa vyao* bila kupumzika (*asipumue kuua*). Uteuzi wa maneno yaliyotumika unaendana na matendo yanayofanywa na mtu shujaa. Maelezo ya ubeti 557 yanalingana na tukio la Samsoni katika SS akiwaua Wafilisti kwa kutumia taya ya punda hivyo kudhihirisha mwingilianomatini. Tukio hili linamsawiri Mikidadi kama shujaa aliyetajika kwa wakati wake.

5.3.3 Sifa ya Ushujaa katika UG

Msimulizi katika UG anamsawiri Gilgamesh kama shujaa anayemithilishwa na mungu. Utangulizi wa utendi unamwonyesha Gilgamesh akiwa na sifa ya ujasiri.

Maneno ya msimulizi yanafafanua kuwa ujasiri wa Gilgamesh ulipita ujasiri wa wafalme wengine. Katika Kibao cha I:1 Gilgamesh anasemekana kuwa ndiye aliyekuwa kiongozi shujaa. Msimulizi anaeleza:

Mf 94

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>Supreme over other kings, lordly in Appearance he is the hero, born of Uruk, the giving wild bull (Tablet I:1)</i>	Mkuu zaidi ya wafalme wengine, mtawala mkuu. Ndiye shujaa, mzawa wa Uruk, fahali mkali wa kuogofya (Kibao I:1)

Inasadikika kuwa ushujaa wa Gilgamesh ulitokana hasa na maumbile yake. Hii ndiyo sababu msimulizi anataja kwamba mhusika alikuwa “fahali mkali wa kuogofya.” Mhusika anapomithilishwa na fahali ina maana kwamba alikuwa jitu kiasi cha kufananishwa na fahali mkali wa mwituni.

Muktadha mwingine unaomsawiri mhusika Gilgamesh kama shujaa upo katika Kibao I:2. Katika sehemu hii, kuna uradidi wa sifa ya ushujaa wa Gilgamesh. Msimulizi anasema kuwa hashindikiki. Hakuna mshindani aliyeweza kuinua silaha dhidi yake. Kwa sababu hiyo, inabainika kuwa mhusika Gilgamesh anaonyesha kuwa na sifa ya ushujaa. Kutokana na maelezo ya msimulizi, ushujaa wake ulikuwa bayana.

Sifa ya ushujaa wa Gilgamesh vilevile inabainika anapokabiliana na mlinzi wa Msitu wa Seda, Gilgamesh akisaidiana na mwenzake Enkidu. Alionyesha kuwa hakuwa na huruma hata kidogo katika makabiliano yake na Humbaba. Msimulizi anasema kwamba Enkidu na Gilgamesh walipomwua Humbaba, walivivuta viungo vyote vya ndani ya mwili wake ukiwemo ulimi. Kitendo hiki kinaonyesha kuwa Gilgamesh, ijapokuwa alikuwa shujaa, alikuwa katili pia.

Mhusika Gilgamesh anasawiriwa na sifa ya ushujaa pia anapokabiliana na Fahali wa Mbinguni. Tulivyotangulia kueleza, Fahali wa Mbinguni alikuwa mmoja kati ya

miungu iliyotajwa katika UG. Kumwua Fahali wa Mbinguni halikuwa jambo rahisi. Maumbile yake yalikuwa ya kuogofya vilevile. Alipopumua, ardhi ilipasuka na kufungua shimo kubwa jinsi inavyoelezwa katika kibao cha VI:23:

Mf 95

UG

M.A.	M.T (Tafsiri yangu)
<i>Ishtar led the bull of Heaven down to the earth.</i>	Ishtar alimwongoza Fahali wa Mbinguni kuelekea duniani.
<i>At the snort of the Bull of Heaven, a huge pit opened up (Tablet VI:23).</i>	Fahali wa Mbinguni alipumua vikali na shimo kubwa likafunguka (Kibao VI:23).

Mfano 95 unaonyesha kuwa Gilgamesh alikuwa na ujasiri wa hali ya juu ikiwa aliweza kupigana na hatimaye kumwua kiumbe cha maumbile yaliyotajwa. Msimulizi anaeleza kwamba Fahali wa Mbinguni *alipopumua vikali, shimo kubwa lilifunguka*. Hii ina maana kwamba kiumbe hiki kilikuwa pandikizi la fahali hivi kwamba kupumua kwake kulisababisha shimo kubwa kutokea. Katika hali nyingine, Gilgamesh anaonyesha sifa ya ushujaa anapoenda hadi Msitu wa Seda kwa lengo la kuukata mkangazi. Wakuu wa mji wa Uruk walimpa mawaidha asiende kwenye msitu huo kwa sababu ya hatari iliyohusishwa nao lakini akapuuza. Wazee wa Uruk walimwonyesha hatari iliyomkabili iwapo angeendelea na mpango wake wa kuzuru Msitu wa Seda. Mawaidha ya wazee yameonyeshwa katika kifungu kifuatacho:

Mf 96

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>The Noble counselors of Uruk a rose and delivered their advice to Gilgamesh; You are young, Gilgamesh, your heart carries you off.... Gave birth to you Humbaba's roar is a flood. His mouth is fire His breath death! He can hera any restling in his forest 100 leagues away! Who would go down into his forest! Who among (even!) the Igigi gods can confront him? (Tablet II :II)</i>	Washauri wadilifu wa Uruk walisimama na kutoa ushairi wao kwa Gilgamesh. "Ungali mdogo, Gilgamesh, moyo wako unakuongoza usijue kile unachokizungumzia....likuzaa Mngurumo wa Humbaba ni mafuriko Kinywa chake ni moto Pumzi zake ni kifo! Ana uwezo wa kusikia kelele zozote umbali wa maili 100 pale msituni! Nani atakayekwenda pale msituni! Nani hata miongoni mwa miungu wa Igigi anaweza kupambana naye? (Kibao II :II)

Washauri wakuu walijua fika kuwa Humbaba alikuwa hatari kwa Gilgamesh, aliyekuwa na umri mdogo (*ungali mdogo, Gilgamesh*). Washauri walijua kwamba yeyote aliye na umri mdogo bado anahitaji kusaidiwa hasa anapofanya maamuzi yanayoonekana kuwa hatari katika maisha yake. Gilgamesh alionywa kuwa pumzi za Humbaba ziliashiria kifo (*Pumzi zake ni kifo!*) lakini akapuuza. Gilgamesh alitaka kuonyesha uhodari wake na kujiongezea uthabiti. Alijisifu kwa kudai kuwa hakuna mtu aliyeweza kumshinda kwa sababu hata *miungu wa Igigi hawangeweza kupambana naye* (Humbaba).

5.3.4 Sifa ya Ushujaa katika SS

Simulizi ya Samsoni imemsawiri mhusika mkuu, Samsoni, kama shujaa aliyekabiliana na Wafilisti. Samsoni anapewa sifa za ajabu. Kwanza, nywele zake zilikuwa za kipekee kwani hazikunyolewa tangu utotoni mwake. Aidha, anaonyeshwa akiwa mtu mwenye nguvu nyingi sana. Kisa cha kwanza kinachoonyesha ushujaa wa Samsoni ni wakati anapomwua mwanasimba jinsi inavyoelezwa katika Waamuzi 14:5-6. Maandishi yanaeleza kwamba mwanasimba alipomngurumia, Samsoni alimpasua kana kwamba anampasua mwanambuzi.

Mf 97

SS

Ndipo Samsoni na baba yake na mama yake wakatelemkia Timna wakakafika mashamba ya mizabibu huko Timna; na tazama, mwanasimba akamngurumia

Roho ya BWANA ikamjilia kwa nguvu, naye akampasua kana kwamba anampasua mwanambuzi wala hakuwa na kitu cho chote mkononi mwake; lakini hakuwaambia baba yake na mama yake aliyoyafanya (Waamuzi 14:5-6).

Mtunzi anasema kuwa hakuwa na kitu chochote mkononi mwake na baada ya kumwua huyo simba, hakuwaeleza wazazi wake. Kitendo hiki kinaashiria kuwa mhusika alikuwa na ujasiri mkubwa. Si kila mtu anaweza kumwua simba. Kitendo cha Samsoni kumwua simba kinalingana na cha Mikidadi wakati alipomwua simba pia katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, beti 448 hadi 456.

Katika kisa kingine, Samsoni anaonyesha ushujaa wake alipowakamata mbweha mia tatu na kuwafunga mikia yao wawili wawili. Baada ya kuwafunga hivyo, akafungia mwenge wa moto kwenye mikia ya kila jozi ya mbweha kisha akawasha ile mienge na kuwaachia wale mbweha katika mashamba ya nafaka ya Wafilisti (Waamuzi 15:4-5). Kisa hiki kinastaajabisha. Inashangaza kufikiria jinsi mhusika alivyoshika mbweha mia tatu na hata baada ya kuwashika anawafunga wawili wawili. Isitoshe anachukua vienge vya moto na kuvifungia kwenye mikia ile halafu anawaachilia kwenda kuteketeza nafaka katika mashamba ya Wafilisti. Katika muktadha huu, utafiti unadhihirisha kwamba ujasiri wa Samsoni ulikuwa unapita ushujaa wa binadamu wa kawaida.

5.4 Sifa ya Majigambo katika UMM, UG na SS

Mikidadi katika UMM na Gilgamesh katika UG ni wahusika walio na majigambo katika tabia zao. Majigambo huhusisha masimulizi ya kujisifu hasa baada ya kutenda tendo lisilo la kawaida kama vile kumwua simba au adui katika vita. Hutokana na

tendo la kishujaa analolifanya mtu anayefikiriwa kuwa shujaa katika jamii. Katika fasihi simulizi, majigambo hudhihirika katika hadithi mbalimbali na simulizi za kiutendi. Utafiti huu umebainisha sifa ya majigambo kati ya wahusika wakuu katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa na Utendi wa Gilgamesh*.

5.4.1 Sifa ya Majigambo katika UMM

Katika UMM, beti kadhaa zimenakili majigambo ya mhusika Mikidadi. Katika beti 176-178, Mikidadi anajibizana na jini ambaye alikuwa ameteka nyara vijana wawili ambao hatimaye aliwaokoa. Mikidadi anamweleza jini kwamba kama angemjua vizuri alikuwa nani, asingesema alivyonena. Mikidadi alitaka kumwonyesha jini kuwa yeye hawezi akatishwa kamwe. Katika ubeti wa 221, Mikidadi anazidi kumwonyesha Luhani (jini) kwamba hakuwa na uoga wowote kwake kwa sababu yeye alikuwa simba. Ubeti ufuatao unafafanua wazo hilo:

Mf 98

UMM
Ewe Luhani adui
kamba huntambui
Ndimi simba ndimi tui
Nawe utajionea (ub. 221)

Mikidadi anaposema kwamba yeye ni simba (*Ndimi simba*) alikuwa anamwonyesha Luhani kuwa yeye ni hodari na kwamba angejionea pindi watakavyoanza kupigana. Katika hali ya kawaida, simba huwa mnyama hatari anayeogopwa. Hivyo, Mikidadi kujimithilisha na simba ni ishara kuwa alikuwa na majigambo. Ni kweli kwamba Mikidadi alikuja kumwua Luhani jinsi mtunzi anavyoeleza katika beti 236-238.

Majigambo ya Mikidadi vilevile yanaelezwa katika beti 363 na 364. Katika beti hizi, Mikidadi anajigamba kwamba yeye si mtu wa kuogopa chochote. Anajisifu kwa kusema “*Mimi si mtu wa khofu, hata na wewe wajua.*” Anamdhihirishia waziri

kwamba hata naye anajua vizuri kuhusu ushujaa wake. Hii ina maana kwamba Mikidadi ana hakika kuwa ushujaa wake ulikuwa unajulikana kote. Katika muktadha huu, Mikidadi alikuwa akimweleza waziri wa Sultani kwamba hakuwa na hofu rohani mwake. Katika ubeti wa 364 anafafanua kwa kusema *roho yangu sina shaka, kinitaka tamtaka*. Maneno hayo yanaonyesha kwamba Mikidadi alikuwa tayari kukutana na Sultani kwa vyovyote vile.

Mikidadi aidha anajisifu katika ubeti wa 438. Anasema kwamba yeye ni mtu hodari na kwamba anaweza kuchukua silaha na mali yote ya jamii. Mtunzi anaeleza:

Mf 99

UMM
Mikidadi kajisifu
Ndimi mtu maarufu
Mali hiyo na suyufu
Jamii nitazitwaa (ub. 438)

Sifa ya majigambo kwa Mikidadi imesheheni katika utendi huu. Katika mfano huu, tunapata kuelewa kwamba Mikidadi alikuwa mtu wa kujigamba (*Mikidadi kajisifu*). Alionyesha jamii kuwa yeye alikuwa mtu maarufu (*Ndimi mtu maarufu*) kwa sababu ya ushujaa wake. Aliwaeleza kuwa kwa sababu ya ushujaa wake, alikuwa na uwezo wa kuchukua mali ya jamii ikiwa ni pamoja na silaha zao (*Mali hiyo na suyufu, Jamii nitazitwaa*). Mikidadi anaonyesha uhakika wa ushujaa wake. Ingawa jamii ilimjua kuwa mtu maskini hapo mbeleni, Mikidadi alijitahidi hata akawa maarufu kwa sababu ya ushujaa wake. Katika jamii nyingi za Kiafrika, maskini hana heshima mbele ya watu. Mikidadi basi alipokejeliwa kwa sababu ya umaskini wake, alifanya bidii kujizolea mali na zaidi ya yote kujipatia mke (Mayasa) mrembo aliyeenziwa na kila mtu katika jamii. Yumkini Mikidadi alikuwa anaficha dosari yake ya umaskini kwa kujigamba kila wakati.

5.4.2 Sifa ya Majigambo katika UG

Mhusika Gilgamesh amechorwa kuwa na tabia ya kujigamba. Mwanzoni mwa utendi, Gilgamesh anajisifu kuwa yeye pekee ndiye mfalme ambaye theluthi mbili ya mwili wake ni mungu na theluthi moja ni binadamu:

Mf 100

UG

M. A	M.T (Tafsiri yangu)
<i>Who can compare with him in kingliness?</i>	Nani wa kulinganishwa naye katika ufalme?
<i>Who can say like Gilgamesh: "I am King!"</i>	Nani anayesema kama Gilgamesh: "Mimi ni Mfalme!"
<i>Two- thirds of him is god, one- third of him is human (Tablet 1:2).</i>	Theluthi mbili zake ni mungu na theluthi moja ni binadamu (Kibao I: 2).

Nafasi ya ufalme wa Gilgamesh inamfanya kuwa na majivuno kupita kiasi. Anataka kila mja ajue kwamba yeye ni mfalme kwa kusema *Nani anayesema kama Gilgamesh: "Mimi ni Mfalme!"* Matamshi hayo yanaonyesha majigambo kwa mhusika. Gilgamesh anatumia maumbile ya mwili wake kuonyesha kwamba yeye pekee ndiye aliyekuwa na sifa za uungu. Anaonyesha kwamba yeye alikuwa kiongozi ambaye alistahili heshima kutoka kwa watu wa Uruk kutokana na ujasiri wake, umaarufu wake na ufahamu wake wa busara. Mtunzi pia amemchora Gilgamesh kama mhusika anayejigamba katika Kibao cha VI: 25.

Mf 101

UG

M.A	M.T (Tafsiri yangu)
<i>Gilgamesh said to the palace retainers: "Who is the bravest of the men Who is the boldest of the males! Gilgamesh is the bravest of the men, The boldest of the males! (Tablet VI:25)</i>	Gilgamesh akamwaambia watumishi wa kasri; "Nani shupavu zaidi ya watu wote Nani jasiri kati ya wanaume wote! Gilgamesh ndiye shupavu zaidi, Shujaa zaidi ya wanaume wote! (Kibao VI:25)

Majigambo ya Gilgamesh yanaonyesha kuwa matendo yaliyofanywa naye yalikuwa ya kustaajibisha. Katika mfano wa hapa juu, Gilgamesh alikuwa amemwua Humbaba mlinzi wa Msitu wa Seda hivyo alitaka walinzi wa kasri wajue yaliyotendeka.

Matumizi ya maneno “*ndiye shupavu zaidi, shujaa zaidi ya wanaume wote*” yanamchora Gilgamesh kama mhusika anayejigamba. Katika hali ya kawaida mtu hajisifu ila anasifiwa. Hata hivyo, mhusika Gilgamesh, anachukua jukumu la kujisifu yeye mwenyewe. Anasisitiza kuwa yeye ni *shupavu zaidi ya watu wote na shujaa zaidi ya wanaume wote*.

5.4.3 Sifa ya Majigambo katika SS

Ingawa kuna sifa zinazolingiliana katika matini teule, Samsoni anasifika kwa sababu ya matendo yake ya kishujaa ila yeye haonekani kujisifu sana kama walivyo Mikidadi na Gilgamesh. Hata hivyo, Samsoni anajigamba baada ya kuwaua Wafilisti elfu moja kwa kutumia taya ya punda jinsi inavyoelezwa katika kifungu hiki:

Mf 102

SS

Naye akaona mfupa mbichi wa taya ya punda, akautwaa, akapiga watu elfu kwa mfupa huo. Samsoni akasema, Kwa taya ya punda chungu juu ya chungu, Kwa taya ya punda nimepiga watu elfu (Waamuzi 15:15-16)

Katika mfano huu, Samsoni anatumia *mfupa wa taya ya punda* kutekeleza mauaji. Hakuhitaji kutumia silaha hatari na ni kana kwamba Wafilisti walikuwa wamekaa mahali moja kila mmoja akingojea muda wake wa kwenda kuuawa na Samsoni. Samsoni anajigamba kwamba amewaua Wafilisti elfu kwa kutumia mfupa wa taya ya punda kwa kusema, *Kwa taya ya punda nimepiga watu elfu*. Ilikuwa ushindi mkuu kwake Samsoni. Ingawa Samsoni anajigamba, anatambua kwamba ushindi huo ulitokea kwa sababu ya uwezo wa Mungu wake (Waamuzi 15:18). Ingawa uwezo wa nguvu zake ulitoka kwa Mungu, Samsoni alijigamba kwa sababu ya nguvu zake mwenyewe.

Samsoni vilevile anaonyesha kiburi anapomwua mwana-simba (Waamuzi 14:6) na kunyamaza pasipo kuwaeleza wazazi wake kuhusu tendo hilo. Hatimaye, alichukua

asali iliyokuwa kwenye mzoga wa simba aliyemuua na kuwapa wazazi wake. Mutembei (2012) anaeleza kuwa kimya hakichukuliwi kama kutokuwapo kwa jambo tu, bali kukosekana kwa jambo jingine. Anasema kuwa kimya cha kifasihi sio ombwe, bali mahali pake kuna tukio la kifikra. Kutokana na maelezo ya Mutembei, kunyamaza kwa Samsoni kunaashiria kiburi. Samsoni ana tabia ya kufanya mambo yake jinsi anavyopenda. Hachukui mawaidha ya wazazi wake ila anataka kutimiza matakwa yake. Anajipenda hivi kwamba wakati huo wazazi wake walikuwa wanaandea posa kwa msichana Mtimna aliyempenda.

5.5 Sifa za Mwanamke kama Mhusika katika UFL, UMM, UG na SS

Baadhi ya wahusika wajenzi walioathiri wahusika wakuu katika matini teule ni wahusika wanawake. Sifa za wahusika wakuu katika UFL, UMM, UG na SS zimeathiriwa na mhusika mwanamke katika kila matini teule kwa njia hasi au chanya. Tangu kale ya Adamu na Hawa katika Biblia, mwanamke amekuwa akisawiriwa kama kiumbe aliye na udhaifu fulani, kwa mfano kuwa mdanganyifu, mnafikiri na pia msaliti. Katika *Utenzi wa Gilgamesh*, wanawake wachache (baadhi wakiwa miungu) wamewaathiri Gilgamesh na Enkidu kwa njia zote mbili, hasi na chanya. Mtimna na Delila katika *Simulizi ya Samsoni*, ni wanawake waliohusika katika anguko la mhusika mkuu, Samsoni, hivyo kuleta athari kubwa katika uhusika wake. *Tenzi za Fumo Liyongo* na *Mikidadi na Mayasa* zimesawiri wanawake husika kama waliowaathiri wahusika wakuu kwa njia chanya. Sehemu inayofuata inajadili sifa za mwanamke na athari yake kwa wahusika wakuu katika UFL, UMM, UG na SS.

5.5.1 Hekima ya Mwanamke katika UFL

Katika UFL, wanawake wanaoathiri maisha ya mhusika mkuu, Liyongo, ni mama yake Liyongo na kijakazi, Saada. Wanatumia hekima yao na kumwezesha Fumo Liyongo kutoroka gerezani. Fumo Liyongo alipotiwa gerezani, mama yake na kijakazi

walishirikiana hata Liyongo akatoka gerezani. Ushujaa wa Liyongo, sifa za maumbile na mienendo yake, ilimfanya awekwe chini ya ulinzi mkali. Katika ubeti ufuatao, tunapata habari hiyo:

Mf 103

UFL
 Akatiwa gerezani
 Kafungiwa kijumbani
 Askari mlangoni
 Kwa zamu wachangaliya (ub. 84)

Liyongo aliwekwa chini ya ulinzi mkali kwa sababu Sultani alihofia kwamba angetoroka. Sultani alikuwa amepanga kumuua Fumo Liyongo kwa hofu kuwa angemnyang'anya uongozi jinsi inavyoelezwa katika ubeti 93. Katika hali hiyo, Liyongo alipewa nafasi na Sultani kusema maneno yake ya mwisho kabla hajaaga dunia (ubeti 96). Kwa hekima yake mwenyewe, Liyongo aliomba nafasi ya kuandaliwa kwa ngoma ya sherehe ya kuaga kwake ili apate kuzungumza na mama yake. Kijakazi Sada aliyemletea Liyongo chakula gerezani, alitumwa kumweleza mama habari alizosema Liyongo. Habari hizi zimeelezwa katika beti zifuatazo:

Mf 104

UFL
 Kamba "Sada nakutuma
 Enda kamwambie mama
 Afanye mkate mwema
 Kati tupa aitiya (ub. 104)

Sada akabalighisha
 Mamake yakamwuwasha
 Akaufanya wa wishwa
 Mkate kampikiya (ub. 106)

Kupitia kwa kijakazi Sada, habari ilimfikia mamake Liyongo ambaye bila kusita alitimiza masharti ya mwana wake. Mkate uliopikwa ulikuwa wa wishwa na ulihitaji tupa kuwekwa katikati. Liyongo alijua kuwa askari hawangetamani mkate huo hivyo

angepata kifurushi chake ‘kizimakizima’ akijua silaha iliyokuwa ndani yake. Ukweli ni kwamba katika ubeti wa 108, askari walipoona kuwa mkate ulikuwa wa wishwa waliudhika wakisema “*wa wishwa hula watwana*” na kwamba Liyongo apelekewe chakula.

Ilipofika wakati wa kuuawa kwake Liyongo, sherehe kubwa kama harusi (ubeti 112) iliandaliwa na watu wengi wakakutanika. Ngoma ilipoendelea, Liyongo naye alizidi kukata pingu na minyororo aliyofungiwa. Maelezo haya yanapatikana katika beti za 114 hadi 118. Watu walipoinuka kucheza, Liyongo alitokea na wote wakaingiwa na hofu. Mtunzi anaeleza:

Mf 105

UFL
 Kwa wutie wakakimbiya
 Hapana alosaliya
 Liyongo kaitokeya
 Mabarani karejeya (ub. 118)

Kiini cha kutoroka kwake Liyongo hadi barani ni hekima ya mama. Kijakazi (Sada) na mama yake Liyongo waliweza kumwokoza Liyongo kutokana na mauaji ambayo alikuwa amepangiwa na Sultani. Hii inaonyesha kwamba, mama alichukua nafasi muhimu katika maisha ya mhusika Liyongo. Pasipo hekima ya mama ya kupika mkate wa wishwa na kuiweka tupa mle ndani kama alivyoagiza Liyongo, Liyongo angeuawa akiwa pale gerezani. Kutoroka kwake Liyongo gerezani kulisababisha Sultani kutafuta mbinu nyingine ya kuweza kumwua ambapo alifanikiwa kumtumia mwanawe. Hata baada ya Liyongo kuuawa na mwanawe, mama ndiye aliyeitwa kwenda kumbembeleza atoke kisimani ili watu wapate kuteka maji. Liyongo alikufa huku amepiga goti na kushika mshale karibu na kisima. Watu walikosa maji hata ikabidi mama atafutwe ili amshawishi Liyongo kuondoka kisimani ili watu wachote maji. Mama alisikia malilio ya jamii na bila kusita akaelekea alikokuwa Liyongo.

Mtunzi anasema:

Mf 106

UFL
 Na mamakwe kumwegema
 Alikicha tema tema
 Kwa mbali kintizama
 Na nasaha miya miya (ub. 193)

Mishororo hii inaeleza vile mama alivyomsongea Liyongo (*kumwegema*) huku akitetemeka (*alikicha tema tema*) na akiwa mbali akamsihi kwa maneno mengi (*na nasaha miya miya*). Ingawa mama hakujuu kwamba mwanawe alikuwa amekufa, alitumia hekima yake kama mama kuwajibika kwa kumsihi mwana wake ‘aondoke’ kisimani ili watu wapate nafasi ya kuteka maji. Baada ya siku chache, mwili wa Liyongo ulianguka na hapo watu wakatambua kuwa alikuwa amekufa (ubeti 202). Hata hivyo, mama yake Liyongo alikuwa na nafasi ya kipekee katika kukamilisha hulka na maisha ya mhusika mkuu katika UFL.

5.5.2 Hekima ya Mwanamke katika UMM

Utendi wa Mikidadi na Mayasa unasimulia kuhusu wahusika wawili: Mikidadi na Mayasa. Wao ni vijana ambao wanajenga kisa chao wenyewe. Tulivyotangulia kueleza, Mikidadi ni kijana chipukizi aliyepigana vita vikali kusudi amwoe Mayasa. Mayasa pia anachukua sehemu kubwa katika ujenzi wa sifa za mhusika mkuu ambaye ni Mikidadi.

Kwanza kabisa, katika uposi wake, Mayasa anaweka masharti ya mume atakayemwoa. Anasema kuwa sharti mwanamume atakayemshinda katika vita ndiye atakayekuwa mume wake (beti 38-40). Mtunzi anaeleza kuwa waposi wengi waliomtaka Mayasa hawakumridhisha. Jabiri, baba yake Mayasa anamsihi bintiye aolewe na Waarabu waliokuwa na mali nyingi, lakini Mayasa anakataa. Hatimaye,

Mikidadi ndiye aliyeibuka mshindi kwa sababu alionyesha ujasiri mkubwa katika vita vikali walivyopigana na Mayasa na kumvua taji lake. Hata hivyo, Jabiri alitia pingamizi uamuzi wa Mayasa wa kuridhishwa na Mikidadi kuwa mume wake. Mayasa anaonyesha hekima yake kwa kukataa kupangiwa mume. Anaonyesha msimamo wake kwa kukubali kuolewa na Mikidadi ingawa hakuwa na mali kama Maliki. Msimamo na ushujaa wa Mayasa katika vita ulimpendeza Mikidadi. Mtunzi anataeleza hayo katika beti zifuatazo:

Mf 107

UMM
Mikidadi kuonake
ghadhabu za mwanamke
ukarudi moyo wake
kwa mahaba kumngia (ub. 107)

Kawana naye kwa pole
mahaba yamzidile
na Mayasa amwambile
Mikidadi nisikia (ub. 108)

Katika beti 107 na 108, Mikidadi anapendezwa na Mayasa kwa namna anavyopigana. Hapo ndipo mapenzi yalipomwingia hivyo akapigana naye kwa upole huku mapenzi kwake yakimzidi, *“kawana naye kwa pole, mahaba yamzidile.”* Mishororo katika mfano 107 inaonyesha kuwa mapenzi ya Mikidadi yalizidishwa na ujasiri alioonyesha Mayasa katika vita. Katika kipindi kingine, Mikidadi anatiwa moyo kupigana na jeshi lililokuwa limeandamana na Mayasa kuelekea kwa Maliki bin Riyahi, mume aliyepangiwa Mayasa na Jabiri. Mikidadi alipojitambulisha kwa jeshi hilo, Mayasa alisikia na hapo hapo akatoa taji lake kichwani na kuzungumza na Mikidadi. Mayasa alitamka maneno yaliyomtia moyo Mikidadi. Mtunzi anaeleza:

Mf 108

UMM
 Sasa upijane nao
 uwashinde wende zao
 utwae na mali zao
 nami upate nitwaa (ub. 552)

Maneno katika mfano 108 yanaeleza kuwa Mayasa hakutaka kuandamana na jeshi hilo kwenda kwa Maliki. Anamweleza Mikidadi apigane nao (*sasa upijane nao*), awashinde (*uwashinde wende zao*) kisha achukue mali yao (*utwae na mali zao*) naye pia amchukue kama mke wake (*nami upate nitwaa*). Mikidadi aliposikia maneno ya Mayasa aliingiwa na mori na akamweleza kuwa askari hawangerudi nyumbani ila angewaua wote. Maneno yake Mayasa yaliathiri matendo ya Mikidadi. Ni mfano wa mwanamke anayetia moyo mume wake wakati kuna changamoto. Mayasa alichocha ujasiri wa Mikidadi. Maelezo haya tunapata katika beti mbili zifuatazo:

Mf 109

UMM
 Naapa kwa Moleo
 hawano hawendi kwao
 Mayasa akamba ndiyo
 nitakayo nitendea (ub. 555)

Mikidadi akanena
 minao hutindikana
 hata nawe utaona
 nitakavyowangilia (ub. 556)

Katika ubeti wa 555, mishororo ya kwanza na ya pili, Mikidadi anaapa kwamba watu hao hawangerudi kwao, huku Mayasa akiitikia kuwa ni hilo alilotaka atendewe (askari kuuawa). Ubeti wa 556 unaonyesha athari ya mawazo ya Mikidadi. Mikidadi anamhakikishia Mayasa kwamba atapambana na jeshi hilo vilivyo na kwamba angejionea jinsi atakavyowangilia (*minao hutindikana, hata nawe utaona nitakavyowangilia*). Kwa kuzingatia mifano iliyotolewa, inabainika kuwa Mikidadi anatiwa moyo wa kupigana zaidi na Mayasa. Hivyo, Mayasa anachukua nafasi ya

kipekee katika ujenzi wa sifa ya ujasiri wa Mikidadi. Anakuwa kichocheo cha ushujaa wa Mikidadi. Beti 557- 582 zinaeleza jinsi Mikidadi alivyowaua askari jeshi wale na hatimaye kukusanya mali aliyowanyang'anya na kuenda na mkewe Mayasa.

Katika vita vilivyofuatia, Mikidadi alipigana na Alii (Imam). Karibu Mikidadi ashindwe katika vita hivyo, lakini Mayasa anamsifu Alii ambaye analegeza mkono baada ya kumsikiliza. Ni dhahiri kuwa Imam aliishiwa nguvu baada ya kusikia sauti ya mwanamke, Mayasa. Mtunzi anaeleza:

Mf 110

UMM
Shairi akisha soma
Alii katabasama
akangiwa na huruma
Mayasa akamwambia (ub. 622)

Mayasa rejea kwako
utilize moyo wako
hana dhara mume wako
Mayasa akarejea (ub. 623)

Katika beti 622 na 623, sauti ya mwanamke ilimfanya Alii kushawishika katika vita kati yake na Mikidadi. Mtunzi anaeleza kuwa Alii aliingiwa na huruma na kumweleza Mayasa arejee kwake na atulize moyo wake kwa sababu hangemdhuru mume wake (*utilize moyo wako, hana dhara mume wako*). Hii ilitokana na sababu kwamba aliyesema naye alikuwa mwanamke. Katika hali hii, Alii hakumwua tena Mikidadi bali alimfanya kuwa Mwislamu. Kabla ya kusilimu, Mikidadi aliona apate ushauri wa mkewe aliyekubali na wote wakawa wafuasi wa dini ya Kiislamu jinsi inavyoelezwa katika beti 626 hadi 638.

Katika UMM, Mayasa amekuwa chanzo cha nguvu za Mikidadi. Katika vita vilivyopiganwa naye, amesimama na Mikidadi hadi mwisho waliposilimu na hatimaye kuandaa karamu ya ushindi baada ya wapinzani wao Jabiri na Malik kufa.

Mayasa ameonyesha upendo wa kweli kwa mume wake. Hii ndiyo maana kuwa katika mwisho wa utendi, Mikidadi na Mayasa wanapata kushinda mabaya waliyopangiwa na hatimaye kuishi maisha ya raha kama mke na mume. Mayasa ana hekima, ujasiri na msimamo thabiti katika maisha yake. Mapenzi yake kwa Mikidadi hayana unafiki kama yalivyo mapenzi ya Delila kwa Samsoni.

Athari ya mhusika mwanamke mwingine kwa mhusika mkuu yanatokana na mama mzazi. Mama yake Mikidadi, Tamima, ana sehemu yake katika msuko wa kisa cha Mikidadi. Tamima anakuja kama mwokozi wa Mikidadi aliposhikwa mateka na Jabir. Alipokuwa kwenye dhiki, Mikidadi alimlilia mama yake (ubeti 691) ambaye alifika upesi kusikiliza mahitaji yake. Uchungu wa mwana aujuaye ni mama kama tunavyosoma katika mfano ufuatao:

Mf 111

UMM
Mamaye keta matozi
ewe mwanangu mzazi
kukufungua siwezi
ulitakalo nambia (ub. 692)

Mama yake Mikidadi analia anapomwona mwanawe akiwa mikononi mwa Jabir kungojea kifo. Mikidadi tayari alikuwa amekata tamaa ndipo mama yake anasema “*kukufungua siwezi*” ila amweleze jambo alilotaka kufanyiwa. Mama alikuwa msaada kwa mwanawe kwa sababu alienda upesi kwa Mungu ili amwombee dua kama inavyoelezwa katika ubeti wa 694. Mama alijitakasa na kufanya hima kuelekea msikitini ili kupeleka malilio ya Mikidadi kwa Mungu. Maombi ya mama yanaonyesha hekima yake. Utendi unaeleza kuwa tayari malaika Jibrili alikuwa amemtangulia mama na hata alijua habari zilizoletwa naye. Maelezo hayo yamo katika beti 693 hadi 778. Kinachobainika ni kwamba maombi ya mama yalisikika. Mikidadi aliepuka kifo na badala yake adui zake, Maliki na Jabir ndio waliokufa.

Maelezo haya yanabainisha nafasi na umuhimu wa mama katika UMM. Mama yake Mikidadi akiwa mhusika mwanamke, aliweza kumwokoza mwanawe kutokana na kifo alichopangiwa. Aidha, maombi yake kwa Mungu yalikubalika ambapo malaika walitumwa kuwatia moyo wasikate tamaa kuhusiana na kifo chake Mikidadi. Katika kumwokoza Mikidadi baada ya ushawishi wa Tamima, Alii aliingia chumba alichofungwa Mikidadi na kufungua minyororo aliyofungwa nayo (ubeti 743). Hivyo, kutokufa kwa Mikidadi kulikuwa kwa sababu ya hekima ya wahusika wanawake, Mayasa na mama mzazi, Tamima.

5.5.3 Hekima ya Mwanamke katika UG

Baadhi ya wahusika wanaojenga mhusika mkuu katika UG ni wahusika wa jinsia ya kike. Aidha, UG haukamiliki pasipo kutaja Enkidu, mhusika ambaye ni rafiki wa karibu wa mhusika mkuu, Gilgamesh. Enkidu anatumwa na miungu ili kuwa mpinzani wa Gilgamesh kwa sababu alikuwa amewanyanyasa watu wa Uruk. Utendi unaeleza kuwa, mbeleni Enkidu alikuwa akiishi msituni na wanyama wa mwituni. Hivyo, tutamtaja kwanza mwanamke aliyesababisha Enkidu kuwa na sifa za kibinadamu na hatimaye kuwa rafiki yake Gilgamesh. Shamhat, kahaba ndiye aliyemfanya Enkidu kujua ngono. Mtunzi anaeleza hayo katika mistari ifuatayo:

Mf 112

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>Shamhat unclutched her bosom, exposed her took in her took in her, took in her voluptuousness She was not restrained but took his energy. She spread out her robe and he lay upon her.. She performed for the primitive the task of womankind... But when he turned his attention to his animals, the gazelles saw Enkidu and darted off. The wild animals distanced themselves from his body (Tablet I:5)</i>	Shamhat aliyaachilia. maziwa yake akaonyesha uchi wake. Naye akamteka kwa nyegereshi zake Hakujizuia, ila alizitwaa nguvu zake Alitandaza joho lake naye akajilaza juu. Alimtendea mshenzi huyo unyumba... Lakini alipogeza kwa wanyama wake makini yake, Swara walikurupuka walipomwona Enkidu. Wanyama wa porini walijitenga na mwili Wake (Kibao I:5)

Maneno katika Mf 112 hapa juu yanaonyesha athari ya mwanamke katika maisha ya Enkidu. Ni kutokana na kitendo cha ngono ambapo Enkidu aliwacha kuishi na wanyama wa porini na kuanza maisha ya kibinadamu. Haya yanadhihirishwa kwa maneno *Lakini alipogeuzwa kwa wanyama wake makini yake, Swara walikurupuka walipomwona Enkidu*. Nguvu za mwanamke, Shamhat, aliyekuwa kahaba, zilimfanya Enkidu kuacha makao yake msituni.

Mwanamke mwingine muhimu katika UG ni mama yake Gilgamesh. Mama yake Gilgamesh, jina lake Rimat-Ninsun, alikuwa na hekima. Yeye ndiye aliyetafsiri ndoto zote za Gilgamesh. Pia, alikuwa mmoja kati ya miungu wanaotajwa katika *Utendi wa Gilgamesh*. Kwa hekima aliyokuwa nayo Ninsun, anasikiliza ndoto za Gilgamesh na kumfunulia maana. Katika kusifia hekima ya mama yake Gilgamesh, mtunzi anaeleza:

Mf 113

UG

M.A	M.T (Tafsiri yangu)
<i>The mother of Gilgamesh, the wise, the all-knowing, said to her Lord; RimatNinsun, the wise, all-knowing said to Gilgamesh: (Tablet I:6)</i>	Mamaye Gilgamesh, mwenye busara, ajuaye yote, akamwambia bwana wake; Rimat-Ninsun, mwenye hekima, ajuaye yote, akamwambia Gilgamesh:(Kibao I:6)

Ninsun, alikuwa mwenye busara, hivyo aliweza kumwelekeza mtoto wake kwa njia iliyofaa. Katika hali ya kawaida, mara nyingi mama huwa hakosei. Mtunzi anasema kuwa mamake Gilgamesh alikuwa mwenye hekima na aliyejua mambo yote. Kwa sababu hiyo, mawaidha yake yalimfaa mwanawe Gilgamesh. Hii ndiyo sababu Gilgamesh alikuwa na ujasiri na nia ya kuenda msitu wa Seda kukabiliana na Humbaba, hata baada ya kukatazwa na wazee. Katika kibao cha III, Gilgamesh anaonyesha kuwa na imani kwa mama yake. Mtunzi anasema:

Mf 114

UG

M.A

M.T (Tafsiri yangu)

*Gilgamesh spoke to Enkidu saying:
Come on, my friend, let us go to the
Egalmah Temple, to Ninsun, the Great
Queen, Ninsun is wise, all-knowing, she
will put the advisable path at our feet”
(Tablet III: 12)*

Gilgamesh alinena na Enkidu akisema:
“Njoo rafiki yangu, twende kwenye hekalu
la Egalmah, kwake Ninsun, Malkia Mkuu,
Ninsun ana busara, anajua yote; atatuelekeza
katika njia ifaayo” (Kibao III: 12)

Ninsun anamwathiri mwanawe kwa njia chanya hivi kwamba Gilgamesh hana wasiwasi hata kidogo kuhusiana na safari yake kuelekea kwenye msitu wa Seda. Anasema kwa uhakika kwamba *Ninsun ana busara, anajua yote na atatuelekeza katika njia ifaayo*. Anaposema “*atatuelekeza*”, Gilgamesh anamaanisha yeye na rafiki yake Enkidu. Kwa kuwa Ninsun alikuwa mmoja kati ya miungu, aliweza kuzungumza na miungu wenzake ili kufanya safari ya Gilgamesh ya kwenda kupambana na Humbaba ifaulu. Ninsun alijitakasa na kupeleka maombi ya matambiko kwa Shamash ili amlinde Gilgamesh dhidi ya madhara yoyote. Kule kujitakaza kwa Ninsun kunaonyesha kuwa utakatifu ulihitajika kabla ya kuendeleza maombi ya matambiko kwa Shamash. Ninsun anaonyesha hekima yake kwa kujitakasa ili kuhakikisha kuwa maombi yake yanasikilizwa na mungu Shamash. Msimulizi anayaeleza haya katika kifungu kifuatacho:

Mf 115

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<p><i>She went up to the roof and set incense in front of Shamash, she offered fragrant cuttings and raised her arms to Shamash: "Why have you imposed...nay, inflicted!... a restless heart on my son, Gilgamesh!</i></p> <p><i>Now you have touched him so that he wants to travel a long way where Humbaba is!... Enkidu will protect the friend, will keep the comrade safe, In our Assembly we have entrusted the King to you, And on your return you must entrust the King back to us!" (Tablet III:12)</i></p>	<p>Alikwea kwenye paa na kuchana ubani mbele ya Shamash,</p> <p>Alitoa vipandikizi vyenye manukato na akainua mikono yake kwa Shamash: "Kwa nini umelazimisha ...la, umeambukiza!...moyo usiotulia ndani ya mwanangu Gilgamesh! Sasa umemgusa anataka kufunga safari ya mbali kuelekea aliko Humbaba! "Enkidu atamlinda rafikiye, atahakikisha mwenzi wake yu salama, Katika baraza letu tumekukabidhi mfalme mikononi mwako, Na utakaporejea sharti umrejeshe mfalme mikononi mwetu" (Kibao III:12)</p>

Ninsun anafanya matambiko ya kumwomba mwana wake Gilgamesh usalama. Aidha, anamwonya Enkidu amlinde rafiki yake dhidi ya hatari yoyote. Anaweka mikakati kabambe kabla ya kusali ili maombi yake yapokelewe na Shamash. Kwa mfano, *alitoa vipandikizi vyenye manukato na akainua mikono yake kwa Shamash.* Haya yote anafanya kwa ajili ya kuulinda usalama wa mwanawe Gilgamesh. Ninsun anasema kwamba katika baraza yao (ya miungu), wamemkabidhi Mfalme Gilgamesh mikononi mwa Enkidu na atakaporejea sharti amrejeshe mikononi mwao. Maelezo haya yanaonyesha kwamba Ninsun alikuwa na ushirika na miungu mingine kuhusiana na maisha ya Gilgamesh.

Katika kuhakikisha usalama wa mwanawe, Ninsun akiwa na miungu mingine aliona kuwa mmoja kati ya Enkidu na Gilgamesh alitakikana kufa. Kwa pamoja, walikubaliana kuwa Enkidu ndiye atakayekufa kama tunavyoelezwa na msimulizi katika mistari ifuatayo:

Mf 116

UG

M.A.	M.T. (Tafsiri yangu)
<p><i>“My friend, why are the great Gods in Conference? (In my dream) Anu, Enlil and Shamash held a council, and Anu spoke to Enlil:</i></p> <p><i>“Because they killed the Bull of Heaven and have also slain Humbaba, one of them who pulled up the cedar of the mountain must die!</i></p> <p><i>Enlil said: “Let Enkidu die, but Gilgamesh must not die!” (Tablet VII:25)</i></p>	<p>“Rafiki yangu, kwa nini miungu wakuu wana mkutano? (Katika ndoto yangu) Anu, Enlil na Shamash walifanya mkutano, Anu alinena na Enlil akisema:</p> <p>“Kwa kuwa walimuuu Fahali wa Mbinguni na pia wamemuuu Humbaba, mmoja wao aliyeung’oa msitu wa mkangazi sharti afe! Enlil akasema”</p> <p>“Mwache Enkidu afe, lakini Gilgamesh sharti asife!” (Kibao VII:25)</p>

Mf 116 unabainisha kuwa miungu ndio walioamua kuhusu kifo cha Enkidu. Ingawa inaonekana kuwa maneno hayo yalisemwa katika ndoto, kifo cha Enkidu kilitokea na Gilgamesh akaishi. Hivyo, Ninsun akiwa mhusika mwanamke (mama), alisimama kama mlinzi wa mtoto wake. Aliathiri miungu katika uamuzi wao dhidi ya mhusika aliyefaa kufa baina ya Enkidu na Gilgamesh. UG unaonyesha kuwa mbali na wahusika wengine, wanawake waliotajwa; Shamhat, Ninsun, Shamash, Enlil na Anu (ambao pia walichukua nafasi ya miungu) walikuwa na athari kubwa juu ya maisha ya wahusika wakuu, Gilgamesh na Enkidu. Maamuzi yao yaliathiri mikondo ya maisha ya Gilgamesh na Enkidu.

Kwa kuzingatia nadharia ya mwingilianomatini, mienendo ya wanawake waliotajwa katika matini teule inalingana. Wanawake waliotajwa katika UG, kwa mfano Ninsun, Shamash na Shamhat, wanatumia hekima yao kuona kwamba wamefaulisha malengo yao. Mwingilianomatini unabainika hasa tunapozingatia miktadha ya matendo yao. Ninsun anatumia hekima yake na kuwashawishi miungu wasimwue mwanawe Gilgamesh bali wamwue Enkidu. Shamhat kwa ujasiri na busara yake anamwingiza Enkidu katika mapenzi na kumfunza tabia na maisha ya kibinadamu, kitendo

kilichosababisha kifo chake hatimaye. Katika UFL, mama yake Liyongo na kijakazi Saada wanatumia hekima yao na kumwezesha Liyongo kutoroka gerezani.

Katika UMM, hekima ya Mayasa haina kifani. Ana msimamo thabiti na katika mahusiano yake na Mikidadi anampa moyo kila anapoonekana kushindwa vitani. *Simulizi ya Samsoni* imerekodi wanawake watatu, wawili wasiotajwa kwa majina na wa tatu, Delila. Wanawake hao wanahatarisha maisha ya Samsoni japo kwa mapenzi yao. Hata hivyo, ni bayana kuwa wanafaulu kutimiza matakwa yao juu ya maisha ya Samsoni. Delila kwa mfano anafaulu kujua siri ya nguvu za Samsoni kwa kumbembeleza na kutumia hila zake kama mwanamke. Mhusika Samsoni anaonyesha udhaifu wake ila Delila anatimiza malengo yake. Mwingilianomatini unabainika kati ya wanawake waliotajwa katika SS na baadhi ya wanawake katika UG, kwa mfano Shamhat na Delila. Shamhat katika UG anamhangaisha Enkidu kimapenzi sawa na Delila kwa Samsoni katika SS.

Ingawa kuna mwingilianomatini katika athari ya mwanamke kama mhusika katika matini teule, kuna tofauti kati ya wahusika Mayasa katika UMM na Delila katika SS. Tabia na mwenendo wa Mayasa kama mwanamke, ni tofauti ikilinganishwa na ya wanawake wengine (Shamash, Shamhat, Ninsun, Delila) katika matini teule. Mayasa ana ujasiri na hekima inayovutia wahusika kama vile Mikidadi na Alii katika UMM. Katika mfano 108, Mayasa anaonyesha hekima yake kwa kumshawishi Alii asimwue Mikidadi kwa kumsifu Alii kuwa yeye ni simba. Alii anaposikia matamshi yake Mayasa, anaingiwa na huruma na yanamfanya asimwue Mikidadi. Usawiri wa Delila kwa upande mwingine ni wa kinafiki akilinganishwa na Mayasa. Wakati Delila anapokubali kulipwa ili aseme siri za Samsoni, Mayasa anamwokoza Mikidadi kupitia hekima yake. Taswira za Mayasa na Delila zinaonyesha kwamba mwanamke ana uwezo wa kusaidia mtu/hali fulani ama kuharibu mtawalia.

5.5.4 Unafiki wa Mwanamke katika SS

Simulizi ya Samsoni imemchora mhusika mkuu kama jagina aliyeangushwa na mwanamke. Samsoni anaonyeshwa akiwa mhusika aliyejiingiza katika mapenzi na wanawake watatu; wa kwanza akiwa Mtimna, wa pili ametajwa kama Kahaba na wa tatu Delila.

Katika Waamuzi 14:1-4, Samsoni alimpenda mwanamke Mtimna kutoka kwa jamii ya Wafilisti. Wazazi wa Samsoni hawakuridhishwa na uamuzi huo lakini Samsoni aliwaeleza kuwa huyo *Mtimna ndiye aliyempendeza*. Maneno haya yanaonyesha kuwa Samsoni tayari alikuwa ameamua kumuoa Mtimna na kwamba hakuwa tayari kubadilisha mawazo yake. Wazazi hawakuwa na uamuzi mwingine ila kwenda kwa wazazi wa mwanamke Mtimna ili kumposa.

Baada ya posa, Samsoni na wazazi wake walirudi nyumbani na kumwacha mwanamke Mtimna kukaa chumbani kwa wazazi wake kama ilivyokuwa desturi yao. Ikawa tena baada ya siku chache Samsoni akaenda kumchukua. Karamu iliandaliwa na Samsoni. Vijana thelathini walioletwa karamuni waliburudika nao. Katika hafla hiyo, Samsoni akawategea kitendawili ambacho walishindwa kukitegua. Mke wake Samsoni (Mtimna) aliombwa kumbembeleza mumewe amweleze maana ya kitendawili kile. Hivyo, alilia mbele zake akisema:

Mf 117

SS

(16) Wewe wanichukia tu, wala hunipendi, wewe umewategea kitendawili hao wana wa watu wangu, nawe hukuniambia mimi.(17) Naye akalia mbele yake hizo siku saba wakati ulioendelea karamu yao, basi ikawa siku ya saba akamwambia, kwa sababu alikuwa akimsisitiza sana; naye akawaambia wale wana wa watu hicho kitendawili (Waamuzi 14:16-17).

Mistari 16 na 17 inaonyesha ushawishi ambao mke wa Samsoni alikuwa nao. Kule kulia kwake mbele yake siku saba kulisababisha ushawishi moyoni mwa Samsoni.

Mtimna hata hivyo alikuwa na unafiki. Mtimna alichangia uovu uliotendwa na Samsoni kwa Wafilisti. Samsoni alienda na kuwaua watu thelathini (Waamuzi 14:19) kutokana na hasira zake. Baada ya siku kadhaa, Samsoni alienda kwa mke wake akimchukulia mwana-mbuzi kama zawadi yake. Alitarajia kuingia chumbani mwake. Hata hivyo, baba mkwe alimkataza kwa sababu tayari alikuwa amemwoza kwa rafiki yake baada ya kulala naye. Iwapo Mtimna alimpenda Samsoni kwa dhati, hangekubali kuozwa mtu mwingine na baba yake.

Unafiki unabainika katika uhusiano wa Samsoni, Mtimna na baba mkwe. Baba mkwe alidhani kuwa Samsoni alikuwa amemchukia sana Mtimna na hakutarajia kwamba angerudi kumchukua jinsi inavyoelezwa katika Waamuzi 15:1-3. Samsoni aliudhika na kusema, *Safari hii nitakuwa sina hatia katika habari za hawa Wafilisti hapo nitakapowadhuru.* Hapo ndipo Samsoni alipoenda na kuchoma mashamba ya Wafilisti yaliyokuwa na ngano (Waamuzi 15:4-5). Chanzo cha kisa cha kuchoma mashamba ya ngano ya Wafilisti kilikuwa mwanamke. Iwapo mhusika Samsoni asingekasirishwa na mke wake aliyeozwa rafiki yake, asingechoma mashamba ya Wafilisti. Hivyo, unafiki wa mwanamke Mtimna ulichangia uovu uliotekelezwa na Samsoni kwa Wafilisti.

Mhusika mwingine ambaye ni mwanamke aliyechangia hulka na matendo ya Samsoni ni Delila. Delila anachukua sehemu kubwa katika maisha ya Samsoni kwa sababu yeye hasa ndiye aliyesababisha kuanguka kwake. Inabainika kwamba ijapokuwa Samsoni alikuwa jasiri, udhaifu wake ulitokana na mapenzi yake kwa wanawake, hasa Delila. Upendo wa Samsoni kwake Delila ulikuwa wa dhati lakini upendo wa Delila kwake Samsoni ulikuwa wa kinafiki. Kwa sababu ya ushawishi wake, Delila alipata kujua asili ya nguvu za mume wake. Alimbembeleza mara kadhaa bila kufanikiwa lakini hatimaye alifaulu. Mtunzi anaeleza kisa cha Delila na Samsoni katika sura ya

kumi na sita. Delila aliahidiwa fedha elfu na mia moja na Wafilisti iwapo angejua asili ya nguvu za mume wake (Waamuzi 16:5). Mwanamke basi akajitolea mhanga kuhakikisha kwamba amejua asili ya nguvu za mumewe. Aliongozwa na tamaa ya pesa alizoahidiwa. Hii inaonyesha kuwa mapenzi yake kwa Samsoni yalikuwa ya unafiki. Delila anasawiri sura ya mwanamke mnaofiki anayeonyesha mapenzi ya uongo kwa mume wake. Mistari ifuatayo inatupa maelezo ya maneno aliyoyatumia wakati wa kumshawishi Samsoni:

Mf 118

SS

1. Tafadhali uniambie asili za nguvu zako nyingi (Waamuzi 16:6)
2. Tazama umenidhihaki na kuniambia uongo; sasa tafadhali, niambie, waweza kufungwa kwa kitu gani? (Waamuzi 16:10)
3. Hata sasa umenidhihaki, umeniambia maneno ya uongo; niambie sasa tafadhali, niambie, waweza kufungwa kwa kitu gani?(Waamuzi 16:13)
4. Wawezaje kusema nakupenda, na moyo wako hauko pamoja nami? Umenidhihaki mara hizi tatu, wala hukuniambia asili ya nguvu zako nyingi (Waamuzi 16:15).

Lugha iliyotumiwa na Delila ilikuwa na ushawishi mno. Matumizi ya maneno kama vile *tafadhali, umenidhihaki, wawezaje kusema nakupenda, na moyo wako hauko pamoja nami* yana ushawishi mkubwa. Katika mistari wa nne (4), Delila anaonyesha kujua kuwa alikuwa amedanganywa mara tatu ndipo akamsihi Samsoni kumweleza ukweli. Katika mistari iliyofuata (Waamuzi 16:16-17), msimulizi anasema kwamba Delila alimsumbua kwa maneno yake ya kila siku na kumwudhi hata roho ya Samsoni ikadhikika hata kufa ndipo alipomwambia yote yaliyokuwa moyoni mwake. Samsoni alimfunulia siri kuhusu kunyolewa kwa nywele zake. Baada ya Delila kujua siri hiyo, aliwaita wakuu wa Wafilisti ambao walikuwa na fedha alizoahidiwa mikononi mwao.

Ni unafiki kwa Delila kukubali ‘kununuliwa’ kwa fedha elfu na mia moja kusudi ajue asili ya nguvu za mumewe na hatimaye kumwua.

Wahusika wawili wanawake, Mtimna na Delila, wametumika kumwangusha mhusika mkuu Samsoni. Hili linatimia kupitia uchu wa mapenzi yao kwa Samsoni. Katika visa vyao, Samsoni anaathirika ingawa pia naye anawadhuru Wafilisti. Samsoni anawaua Wafilisti wengi hasa anapokuwa gerezani (Waamuzi 15:14-17; 16; 25-30). Visa hivi vilevile vinaonyesha Mungu akiitikia maombi ya Samsoni na kumwokoza (Waamuzi 15:18-19, 16:28). Maneno ya Mtimna na Delila, kila mmoja akimbembeleza Samsoni yanalingana “*wewe wanichukia tu, wala hunipendi*” (14:16) na “*Wawezaje kusema, Nakupenda na moyo wako haupo pamoja nami?*” (16:15) Samsoni hatimaye alipomweleza Delila siri ya nguvu zake kifo chake kikatokea. Inabainika kwamba Mtimna na Delila walichangia pakubwa katika anguko la Samsoni. Mapenzi yao kwake Samsoni yalikuwa ya kinafiki. Ijapokuwa Samsoni alikuwa jasiri, uhusiano wake wa kimapenzi na wanawake Wafilisti ulimletea maafa yaliyosababisha kifo chake.

5.6 Sifa ya Tanzania katika UFL, UMM, UG na SS

Katika sehemu hii, tumejadili mwingilianomatini kwa kuzingatia kigezo cha Tanzania kaika matini teule. Tanzania ni kigezo muhimu kilichodhihirisha mwingiliano wa kimatini katika *tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa* na *Simulizi ya Samsoni*.

5.6.1 Tanzania katika UFL

Utendi wa Fumo Liyongo unasimulia kisa cha mhusika mkuu, Fumo Liyongo. Unaonyesha Fumo Liyongo akiwa binadamu aliyeonekana kukamilika katika hulka zake na aliyekuwa na sifa za kiajabuajabu kiasi cha kuogopwa na binadamu wenzake. Msuko wa epiki ya Fumo Liyongo unianza kwa kumwonyesha Liyongo kama mtu aliyekamilika, aliye na nguvu za kiajabu na anayetenda mambo ambayo hayangetendwa na binadamu wa kawaida. Kutokana na epiki hii, Fumo Liyongo

alikuwa shujaa wa wakati wake katika jamii ya Waswahili wa mwambao wa Kenya. Mhusika amesawiriwa kama shujaa anayeweza kukabiliana na hatari yoyote inayoweza kutokea katika jamii yake.

Beti za mwanzoni za utenzi huu zinamwonyesha mhusika Fumo Liyongo akiwa mtu tofauti na binadamu wa kawaida. Hii ni kwa sababu ya maumbile yake, ambayo kutokana na msimulizi alikuwa pandikizi la mtu. Hili lilimfanya kuwa tofauti hasa ikichukuliwa kwamba Fumo Liyongo *angekutokea kwa ghafla, ungejikojolea* (ubeti 14) na *angekukodolea macho ungezimia* (ubeti 15). Kwa sababu hiyo, watu wengi walitamani kumwona. Msimulizi anaeleza:

Mf 119

UFL
Wagala wakipulika
Kwa dhihaka wakateka
Wakanena “twamtaka
Na sisi kumwangaliya” (ub. 16)

Sifa za Liyongo zilikuwa zimeenea kote na ujumbe huu ulifikia Wagala ambao pia walitamani kumwona *“twamtaka na sisi kumwangaliya.”* Ubeti huu unasisitiza jinsi Wagala walivyomakinika kusikiliza sifa za Liyongo (*Wagala wakipulika*) ndipo wakawa na hamu ya wao kumwona ingawa hawakuwa na nia nzuri (*Kwa dhihaka wakateka*). Utendi unaeleza kuwa Wagala walikuwa watu wa kabila la Sultani ambao nao walikuwa mashujaa (ubeti 9). Yamkini sifa za Fumo Liyongo ziliwapiku mashujaa wao ndipo Wagala wakaonelea kuwa ni heri wajionee na kupeleka ujumbe kwa mfalme wao. Maelezo yapatikanayo katika beti za 7,12,13,15,16 na 17 yanatosheleza hoja kuwa Fumo Liyongo alikuwa shujaa katika jamii yake.

Baada ya kudhihirika kwamba Fumo Liyongo alikuwa shujaa wa kipekee, Sultani anamwonea wivu na kuanza kupanga jinsi ya kumwua. Alifanya hila hata akafaulu kumwoza Liyongo msichana wa Kigala kusudi lake waweze kuwa na uhusiano wa

karibu naye na kwa njia hiyo ingekuwa rahisi kwake kumwua Liyongo. Ingawa Fumo Liyongo aliitikia na kufurahia mke aliyepata kutoka kwa Wagala, hakujua kwamba alikuwa ameweka maisha yake hatarini. Haikuchukua muda Liyongo akajaliwa mtoto mwanamume. Msimulizi anaeleza kuwa, kadiri mtoto alipoendelea kukua ndipo alipozidi kufanana na baba yake (ubeti 48). Hali hii ilimfanya Mfalme kujawa na wivu hivyo kuudhika zaidi kiasi cha kukata kauli kwamba ilikuwa sharti Fumo Liyongo auawe. Msimulizi anaeleza katika beti zifuatazo:

Mf 120

UFL

Mke katukuwa mimba

Akazaa mwana simba

Mwanamume wa kutamba

Mwane Liyongo sikiya (ub. 46)

Fitina zikamngiya

Mfalme miya miya

Kwa hila kakusudiya

Kumuuwa fahamiya (ub. 49)

Katika mfano 120 ubeti 46, mtunzi anaeleza kuwa mtoto aliyezaliwa alikuwa mwanamume asiyeshindwa (*mwanamume wa kutamba*). Kuzaliwa kwa mtoto huyu kulizua hisia za uovu kwa mfalme. Hii ilitokana na sababu kwamba kuwa na mtoto mvulana au mwanamume, jinsi anavyoeleza msimulizi, ilikuwa dhihirisho kuwa sifa za baba mzazi, Fumo Liyongo, zingendelezwa na mwanawe. Mfalme aliona chuki kutokana na kuzaliwa kwa mwana wa Liyongo na kukata kauli kwamba ilikuwa bora Fumo Liyongo auliwe ili kukatiza kizazi cha ukoo wake.

Hofu ya Mfalme ilikithiri alipoona kuwa mwana wa Liyongo anachukua mkondo wa baba yake (*akazaa mwana simba, mwanamume wa kutamba*). Mfalme aliona kuwa utawala wake ulikuwa hatarini zaidi kuliko ilivyokuwa kabla ya kuzaliwa kwa mwana wa Liyongo. Msimulizi anapotaja katika ubeti wa 49 kwamba "*Fitina zikamngiya,*

Mfalme miya miya” ina maana kuwa watu wengi walimwendea Mfalme na kumweleza mambo kadha kuhusu Fumo Liyongo na mtoto wake. Matokeo ya fitina hizo ni kwamba mfalme aliamua kumwua Liyongo. Kosa alilolifanya Fumo Liyongo ni kukubali kuozwa mwanamke Mgala. Kunaswa kwake Liyongo kulikuwa rahisi sana. Haukuchukua muda Liyongo akagundua kwamba kulikuwa na hila za kumwua na kwa sababu hiyo akatorokea mwituni.

Mfalme anapogundua kuwa Fumo Liyongo hapatikani, anatoa ahadi ya pesa taslimu kwa yeyote atakayemwua na kumpelekea kichwa chake. Ufafanuzi huo unatolewa katika ubeti ufuatao:

Mf 121

UFL
Mfalme kawambiya
“Liyongo kunipatiya
Kitwa mukanieteya
Tawapa riale miya” (ub. 53)

Fumo Liyongo alikuwa mtu hodari aliyekuwa amemshinda hata mfalme kumwua. Maneno katika mfano 121, yanaonyesha kwamba Mfalme alihitaji tu kichwa chake Liyongo (*Liyongo kunipatiya, Kitwa mukanieteya*). Ili kurahisisha kazi ya ‘kukatwa kwa kichwa cha Liyongo’, mfalme alitoa ahadi ya fedha (*tawapa riale miya*) kama malipo ya kutekeleza mauaji hayo ambayo kwa kweli yalikuwa vigumu kutekelezeka. Mistari hii inalingana na kifungu katika Waamuzi 16:5 ambapo Delila anaahidiwa fedha, shekeli elfu na mia iwapo angeweza kumwua Samsoni. Katika hali nyingine katika Biblia, Liyongo analinganishwa na Yohana Mbatizaji aliyeamrisha kukatwa kichwa chake na Mfalme Herode jinsi inavyoelezwa katika Mathayo 14:1-12. Amri hii ilitolewa ili kichwa cha Yohana kipewe binti wa Herodia (Herodia alikuwa mke wake Filipu, ndugu yake Herode) kama zawadi kwa kucheza mbele ya umati mkubwa katika siku kuu ya kuzaliwa kwake Herode. Kukatwa kwa kichwa cha Yohana

kulitokana na sababu kwamba Yohana Mbatizaji alikuwa amemkemea mfalme Herode kwa kumchukua Herodia kuwa mke wake. Ahadi ya fedha ili kutekeleza mauaji katika *Utendi wa Fumo Liyongo* na *Simulizi ya Samsoni* inazua mwingilianomatini.

Mipango ya kumkamata Liyongo inaendelezwa na wazee wa Wagala kwa ushirikiano na Sultani. Hatimaye, wanafaulu kupanga ngoma ya kuwashirikisha wake kwa waume lakini nia ilikuwa ni kumshika Fumo Liyongo (ubeti 81). Beti za 92 na 93 zinaonyesha Mfalme aliyejawa na shauku ya kupokonywa uongozi na Fumo Liyongo. Ingawa ngoma iliandaliwa ili kumnasa Fumo Liyongo, aliweza kufaulu kukata minyororo aliyofungiwa kwa kutumia tupa iliyowekwa ndani ya mkate wa wishwa na ghafla kutokea dansini. Kitendo hiki kinawashangaza wote na kuafiki kuwa Fumo Liyongo kwa kweli alikuwa mtu wa ajabu asiyeweza kushindwa.

Mgogoro wa tanzia katika UFL unatokea wakati mwana wa Liyongo anatumiwa kumwua baba yake. Hii ni baada ya njama zote zilizotumiwa kumwua Liyongo kukosa kufaulu. Ili kuweza kumwua baba yake, mwana wa Liyongo anaahidiwa mambo mengi mazuri na Sultani; Sultani alimuahidi kumfanya waziri na kumwoza bintiye iwapo angemwua baba yake.

Kijana basi anafanya juhudi za namna ya kutekeleza wajibu wake mpya. Baada ya kukutana na baba yake na kufurahia chakula pamoja, mtoto anamwuliza baba swali la kutaka kujua kile kinachomwua. Hili linamtia Liyongo wasiwasi na hapo akamweleza mtoto wake kwamba amedanganywa na atakuja kuchekwa na kujuta yeye mwenyewe (ubeti 141). Hata hivyo, Fumo Liyongo anamweleza mwanawe siri za mauti yake. Msimulizi anaeleza:

Mf 122

UFL
 Nisikiya wangu baba
 Liniuwalo ni haba
 Ni msumari wa shaba
 Kitovuni nikitiya (ub. 143)

“Jamii silaha piya
 Haziniuwi swabiya
 Ila nimezokwambiya
 Ni ya kweli yote piya” (ub. 144)

Fumo Liyongo anamweleza mwanawe kuhusu namna ya kipekee ya kifo chake. Anaonyesha upendo kwa mwanawe kwa kumwita ‘baba’ (*Nisikiya wangu baba, ubeti 143*). Mapenzi haya hatimaye yalisababisha kifo chake. Utafiti huu unaamini kuwa mapenzi ya Fumo Liyongo kwa mwanawe yalikuwa udhaifu kwake na kisababishi cha kifo chake. Kosa lililotendwa na Fumo Liyongo ni kutoboa siri za kile kinachomwua jinsi inavyoelezwa katika beti za 143 na 144. Kifo chake kingetokea tu iwapo angedungwa kitovuni kwa kutumia msumari wa shaba. Ingawa mwana wa Liyongo alikuwa mtoto mdogo (*swabiya*) jinsi inavyoelezwa katika ubeti 144, baba yake anamweleza ukweli wote kuhusu kile kinachoweza kumwua. Umri mdogo wa mwana wa Liyongo aidha umetumika kama kichocheo cha kosa lililotendwa na shujaa na baadaye kusababisha kifo chake. Jambo linalodhihirika ni kwamba mwana wa Liyongo anamsaliti baba yake kwa kuahidiwa riale mia, uongozi na kuozwa binti wa mfalme. Uovu wa kijana huyu unatimia wakati anapomchoma baba yake kitovuni anapokuwa usingizini.

Mf 123

UFL
 Kamtiya kitovuni
 Naye ulele kwa t’ani
 Achamka hamuoni
 Kiyana amekimbiya (ub. 179)

Makosa aliyoyafanya Fumo Liyongo yalikuwa kumtobolea mwana wake kiini cha kifo chake. Analipia uzembe wake kwa njia hatari ya kifo. Hofu ya kutojua ni nini kingefuatia ilisababisha kijana kukimbilia maisha yake baada ya kutimiza matakwa ya kumwua baba yake. Ubeti 179 unaeleza kuwa Liyongo alidungwa kitovuni alipokuwa amelala chali (*naye ulele kwa t'ani*) na kwa haraka kijana akakimbiya (*achamka hamuoni, kiyana amekimbiya*). Wakati mwana Liyongo anafurahia kuwa ametimiza matakwa ya mfalme ya kumwua baba yake, anakuja kuhangaika baadaye kwa sababu ya kitendo hicho. Hili linazua sintofahamu kwa upande wa mwana Liyongo. Anatenda kosa la kumwua baba yake akitarajia kupokezwa utawala na mfalme lakini hili halikutimia. Badala yake, mfalme anamsuta kwa kukosa kuhuzunika kwa ajili ya kifo cha baba yake. Katika ubeti ufuatao, msimulizi anaeleza;

Mf 124

UFL
Mfalme kamwambiya
Mbona mwana hukuliya
Babako alikuyeya
Kwa anasa zote piya?" (ub. 211)

Hapa Mfalme anamsuta mwana wa Liyongo kwamba hajalia kwa sababu ya kifo cha baba yake (*Mbona mwana hukuliya*) aliyemlea kwa anasa kubwa. Ni anguko kwa upande wa mwana wa Liyongo kwa sababu Mfalme amemcheka na hata kumsuta badala ya kumzawadi jinsi alivyokuwa amemwahidi. Anajuta kutokana na kitendo kile cha kumwua baba yake badala ya kutunukiwa zawadi mzomzo alizoahidiwa na Mfalme. Adhabu anayopata mwanawe Liyongo ilikuwa kali. Ilibidi Mfalme amfukuze maskanini mwake kama inavyoelezwa katika beti za 213, 214 na 215. Hatimaye kabla ya kutoka kwa nyumba ya Mfalme, alihitajika kuvua nguo alizopewa na avalie matambara yake ya awali. Hayo ni maneno yaliyosemwa na Mfalme:

Mf 125

UFL
 “usiketi mui wangu
 Wewe adui ya Mungu
 Tena vua nguo zangu
 Vaa yako mezoweya (ub. 214)

Mfalme kamtowa
 Nguo zakwe kamvuwa
 Na watu akatukiwa
 Khabari ikaeneya (ub. 216)

Katika Mf 125, ubeti wa 214, Mfalme anamweleza kijana kwamba yeye ni adui ya Mungu kwa sababu ya kuuu. Inabainika kwamba kijana alimwua baba yake kwa maagizo ya Mfalme, ambaye sasa amemgeuka na kumwona adui mkubwa sana.

Mfalme hakutaka tena kuwa na uhusiano wowote na yeye, hivyo akamfukuza mjini humo (*usiketi mui wangu*). Ingawa mwana wake Liyongo alikuwa ameahidiwa zawadi nyingi na Mfalme, ahadi hizo zinageuka kuwa chuki kwake. Mfalme hataki kumwona tena katika mji wake. Isitoshe, mfalme anamwagiza avue nguo alizopewa kisha avalie nguo zake za awali kwa kusema *Tena vua nguo zangu, Vaa yako mezoweya*. Hali kadhalika, habari hizi zilienea na watu wakageuka na kumchukia huyu mwana wa Liyongo (*na watu wakatukiwa, khabari ikaeneya*). Majuto anayoyapata mwana wa Liyongo ni malipo ya matendo yake maovu ya kumsaliti baba yake. Msimulizi anaeleza:

Mf 126

UFL
 Kaingiya mayutoni
 Katindikia nyumbani
 Hata wenzi hawaoni
 Hamu imezomngiya (ub. 220)

Habari zilipoenea kwamba mwana wa Liyongo amefukuzwa na mfalme pasipo kutimiziwa ahadi zake, watu walimchukia na kutokana na hayo mwenyewe akaona

haya kutangamana na watu hao. Ilimlazimu ajifungie kwa nyumba (*katindikia nyumbani, hata wenzi hawaoni*) ili kuficha aibu yake. Haya yanaathiri maisha ya kisosholojia ya mhusika. Hii ilikuwa adhabu nyingine ya mwana wa Liyongo, kutengwa na jamii na kukosa kutangamana na jamii kwa sababu ya kumwua baba yake. Mwanawe Liyongo anadharauliwa na jamii kwa sababu ya kosa la kumwua baba yake. Ingawa alianza kutekeleza mpango wa mauaji hayo kwa furaha, anaishia kujuta. Alikuwa na matarajio mazuri ya kuchukua uongozi baada ya mfalme kumwahidi kumpa bintiye kuwa mke wake.

Moyo wa mwana wa Liyongo ulidanganyika. Tamaa yake ya kurithi uongozi ilipiku thamani ya baba mzazi. Ingawa sasa anajuta (*kaingiya mayutoni*), ni jambo ambalo alijitafutia mwenyewe. Huenda kijana hakutaka kutangamana na watu kusudi asiulizwe maswali kuhusiana na kifo cha baba yake. Katika muktadha huu, mwanawe Liyongo anapatwa na maradhi ambayo mtunzi hajaeleza yalikuwa ya aina gani. Kinachobainika ni kwamba maradhi mabaya yalimshika ambayo hatimaye yalisababisha kifo chake. Haijulikani iwapo alitafuta matibabu ili kujinusuru ila mwandishi anadokeza kuwa maradhi hayo yalimshika kwa muda mrefu. Mwandishi anafafanua zaidi katika ubeti ufuatao:

Mf 127

UFL
Siku chache kitimiya
Maradhi yakamniya
Yasiyomuondokeya
Naye kisa kaifiya (ub. 223)

Katika ubeti 223, mtunzi anaeleza kuwa mwana wa Liyongo aliugua kwa muda mrefu. Anasema *maradhi yakamngiya, yasiyomuondokeya* na hatimaye akaaga dunia (*naye kisa kaifiya*). Athari ya kuugua kwa muda mrefu ni kudhoofika kwa afya. Aidha, mgonjwa husononeka kutokana na uchungu anaouhisi mwilini. Masaibu

yaliyompata mwana wa Liyongo kutokana na ugonjwa yanalingana na masaibu yaliyomfika Enkidu katika UG. Enkidu aliugua kwa muda mrefu hata akajuta kukutana na Gilgamesh ambaye anasema kuwa alimwacha afe bila kumpa usaidizi wowote.

Anamlaani Gilgamesh akisema kwamba ingawa alimsaidia vitani, sasa amemwacha. Vipindi hivi vinazua ulinganifu hivyo mwingilianomatini katika UFL na UG. Uchungu alioupata mwana wa Liyongo ni ishara ya majuto yaliyotokana na kitendo cha kumwua baba yake. Masaibu yanayomfika yanazua tanzia katika kisa kizima cha *Utendi wa Fumo Liyongo*. Hata hivyo, hatima yake ilionekana pindi tu alipopeleka habari kwa mfalme kwamba amemwua baba yake. Katika ubeti wa 213, mtunzi anaeleza:

Mf 128

UFL
Mfalume kabaini
Kabisa huna imani
Epuka mwangu matoni
Na nyumbani nitokeya (ub. 213)

Maneno ya mfalme katika mfano 128 yanaashiria kuwa alikuwa anayafahamu mambo ambayo yangempata mwana wa Liyongo kwa kusema “*kabisa huna imani*” na kumfukuza kwa kumwambia *aepuke kwake machoni*. Ifahamike kwamba katika ubeti wa 157, mtunzi anaeleza kuwa mfalme alikaa na kijana siku kumi akimtunza kama ni bwana harusi ila alikuwa akimpumbaza (*kipumbaza mno ghaya*). Anasa alizofurahia mwana wa Liyongo zinageuka kuwa dhihaka. Laiti angalijua yaliyomngojea mbeleni, angaliwacha kabisa kushiriki mpango huo wa kumwua baba yake. Mfalme alikuwa anahitimisha mipango yake aliyokuwa amepanga tangu mwanzoni mwa wazo lake la kumuua Fumo Liyongo. Hili lilikuwa pigo kwa mwana wa Liyongo kwa sababu matarajio yake mazuri yalikatizwa kwa fedheha.

Matendo na matukio yanayotokea katika maisha ya wahusika wawili hasa, Fumo Liyongo na mwanawe yanatosheleza *Utenzi wa Fumo Liyongo* kuwa wa kitanzia. Fumo Liyongo anajutia hata kufa kwa sababu ya kukosa kuhifadhi siri za kile kiwezacho kumwua. Hili linalingana na udhaifu wa Samsoni wa kumfichulia Delila siri ya nguvu zake, jambo lililosababisha kifo chake. Udhaifu wa Fumo Liyongo wa kufichua siri ya kifo chake ulisababisha hasara ya kuuawa kwake ilhali mwana wake alikufa kwa sababu ya kumwua kutokana na tamaa na ahadi za uwongo kutoka kwa Mfalme. Mhusika mkuu, Fumo Liyongo, alikuwa shujaa aliyependwa katika jamii yake kwa sababu ya sifa za kipekee alizokuwa nazo. Hayo yanabainishwa na maelezo ya maneno yanayotumika katika mfano ufuatao;

Mf 129

UFL
 Liyongo silaha yetu
 Kwa wute khasimu zetu
 Alikuwa ngao yetu!”
 Wute wakinena haya (ub. 225)

Ubeti huu umebeba ujumbe mzito kwa kuzingatia lugha iliyotumika, *silaha yetu, ngao yetu!* Jamii inaomboleza kufuatia kifo cha Fumo Liyongo. Watu wote katika jamii wanalia kwa sababu ya kumpoteza mtu aliyekuwa tegemeo. Liyongo alikuwa na jukumu la kupambana na maadui (*khasimu*) wowote waliotishia maisha ya wanajamii. Katika ubeti wa 225, tunapata dhamira kuwa Fumo Liyongo alikuwa kielelezo cha ujasiri na mbabe wa kivita katika jamii yake. Hata hivyo, kifo kimeipokonya jamii hii tegemeo lao. Pengo lililoachwa kufuatia kifo chake halingeweza kuzibwa na mtu mwingine. Huzuni unaogubika *Utenzi wa Fumo Liyongo* ni kifo cha watu wawili, Fumo Liyongo na mwanawe, kwa sababu ya makosa yaliyotendwa na kila mmoja wao.

Tanzia katika UFL imedhihirika kwa sababu ya vigezo kama vile Mfalme kuingiwa na chuki kuhusiana na umaarufu wa Fumo Liyongo na hatimaye uamuzi wa hila ya mfalme kuwa Fumo Liyongo auawe. Mpango wa kumuua Liyongo uliendelezwa kupitia urafiki wa kinafiki baina yake na Wagala, Wadahalo na Waboni kwa nia ya kumuua akiangusha makoma. Wakati mwingine Fumo Liyongo alitiwa gerezani nia ikiwa ile ile ya kuuawa ila haikuwezekana kwa sababu Liyongo alitoroka (ubeti 118). Hata hivyo, hila ya mfalme kutumia mwanawe Liyongo kumuua baba yake ilifaulu baada ya kuahidiwa zawadi ya pesa, kumuoa binti ya mfalme na vilevile urithi wa ufalme.

Ingawa Fumo Liyongo alimpenda mwana wake, kilikuwa kitendo cha udhaifu kwake kutoboa siri ya kifo chake; kudungwa kitovuni kwa sindano ya shaba (ubeti 152). Mipango ya mahasidi wa Fumo Liyongo ya kuoia kutoka jamii ya Wagalla ili kupata namna ya kumteka nyara ilifaulu. Hata hivyo, majuto yalimpata mwanawe Liyongo baada ya kumuua baba yake na matarajio yake mazuri kukatizwa kwa kuwa hata naye alikufa baada ya kuugua kwa muda mrefu.

5.6.2 Tanzania katika UG

Msuko wa tamthilia ya kitanzia unaweka wazi utungo wake hivi kwamba kuna mwanzo, kati na mwisho. Mpangilio wa visa na matukio yamekusanywa hivi kwamba kitendo kimoja husababisha tukio katika kitendo kingine. *Utendi wa Gilgamesh* umefuata mpangilio wa tamthilia ya kitanzia uliopendekezwa na Aristotele. Mwanzoni mwa utendi, tunapata maelezo ya majigambo ya mhusika Gilgamesh ambaye anasawiriwa kuwa kamilifu, bila dosari. Gilgamesh anachukua nafasi ya shujaa katika utendi huu ambapo hatima yake mwishoni mwa utendi inatatanisha. Uchambuzi wa tanzia katika UG vilevile unahusisha mhusika Enkidu, aliyekuwa na sifa sawa na

Gilgamesh. Kisa cha mhusika Gilgamesh hakiwezi kukamilika bila kuhusishwa na Enkidu.

Katika kibao cha kwanza, ukurasa wa tatu, msimulizi anaeleza kuhusu Enkidu, ambaye anaishi na wanyama wa porini na hajastaarabika. Aidha, kifungu kinamtaja hawara ambaye anakutana na Enkidu kando ya bwawa la maji. Hawara, kwa kufuata masharti yaliyotolewa na Gilgamesh, anavua joho lake kufunua uchi wake ili kumvutia Enkidu. Katika hali hii Enkidu anajamiiana na Shamhat (hawara). Enkidu anashawishika kuandamana na Shamhat hadi kwa Gilgamesh huko mjini Uruk, akiwa tayari kukabiliana naye. Kifungu kifuatacho kina maneno matamu ya hawara Shamhat ambaye anamshawishi Enkidu kuandamana naye ingawa huu unakuwa mwanzo wa matatizo yaliyomkumba hadi kufa kwake. Msimulizi anaeleza:

Mf 130

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>The harlot said to Enkidu: "You are beautiful," Enkidu, you are become like a god.</i>	Yule hawara akamwambia Enkidu, "U mtanashati, Enkidu Wewe u sawa na miungu
<i>Why do you gallop around the wilderness with the wild beasts?</i>	Kwa nini wewe huchapuka ukiandamana na wanyama wa porini?
<i>Come, let me bring you into Uruk- Haven,</i>	Njoo, niruhusu nikuongoze twende Uruk- Haven,
<i>To the Holy Temple, the residence of Anu and Ishtar,</i>	Kwenye hekalu takatifu, makao ya Anu na Ishtar,
<i>The place of Gilgamesh, who is wise to perfection,</i>	Mahali pa Gilgamesh, mwenye hekima bila dosari,
<i>But who struts his power over the people like a wild bull" (Tablet 1:5)</i>	Lakini atumiaye mamlaka yake kwa kiburi mithili ya fahali mwituni) (Kibao I:5)

Katika kifungu hiki, hawara ametumika kumshawishi Enkidu afanye mapenzi naye, ingawa kitendo hiki kinakuja kuwa kiini cha kifo chake Enkidu. Ustaarabu na anasa anazopata Enkidu zinageuka kuwa majuto siku zake za baadaye. Kwa kumjibu Shamhat, Enkidu anatamka kwamba yuko tayari kupambana na Gilgamesh kwa kusema "*Nitapambana naye, niruhusu nipaaze sauti yangu huko Uruk nikisema:*

Mimi sishindiki!” Ingawa Enkidu anaonekana kupandwa na jazba ya kupambana na Gilgamesh, hakujua kwamba Shamhat alikuwa ametumika kama mtego ili amwongoze hadi kwa Gilgamesh. Tukio hili linalingana na tukio katika *Simulizi ya Samsoni* inavyoelezwa katika Waamuzi 16:1, ambapo Samsoni anajifurahisha na kahaba chumbani huku Wafilisti wakipazingira mahali pale wakimngojea ili kumwua. Mwingilianomatini unatokea kufuatia visa hivi viwili vinavyohusisha wahusika Enkidu na Samsoni wakijiburudisha kimapenzi na makahaba. Ashiki zao kwa wanawake makahaba zinawalemea na hatimaye kusababisha anguko lao. Enkidu hakujua kwamba Shamhat alimpenda Gilgamesh kumliko. Upendo wa Shamhat kwake Enkidu ulikuwa wa unafiki tu. Tunapata hayo kupitia maelezo yafuatayo:

Mf 131

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(Enkidu, it is your wrong thoughts you must change!</i>	(Enkidu, sharti uyabadili mawazo yako mabaya!
<i>It is Gilgamesh whom Shamhat loves, and Anu, Enlil and La have enlarged his mind. Even before you came from the mountain Gilgamesh in Uruk had dreams about you” (Tablet 1:6)</i>	Shamhat anampenda Gilgamesh, na Anu, Enlil na La wamepanua akili yake Hata kabla hujatoka milimani, Gilgamesh akiwa Uruk alikuwa ameota kukuhusu) (Kibao 1:6)

Kifungu hiki kinafafanua kwamba Enkidu alikuwa amedanganyika “*Enkidu, sharti uyabadili mawazo yako mabaya, Gilgamesh akiwa Uruk alikuwa ameota kukuhusu.*”

Shamhat, Gilgamesh na miungu walijua kwamba Enkidu angekufa baada ya kumwua Humbaba, ijapokuwa walikuwa na Gilgamesh. Ni kwamba Enkidu alikuwa amejitolea kwa kweli kupambana na Humbaba liwe liwalo huku Gilgamesh, Shamhat na miungu walikuwa na unafiki. Hayo yanadhihirishwa katika uneni wa Enlil akisema, “Mwache Enkidu afe, lakini Gilgamesh sharti aishi!” katika Kibao VII: 27. Kifo cha Enkidu kilitokea baada ya kuhadaiwa na hawara, Shamhat. Ingawa Enkidu alikuwa amevutiwa na Shamhat hata wakafanya mapenzi naye, hakujua kwamba

alikuwa amedanganywa. Kwake Enkidu, alikuwa amejitolea kupambana na Gilgamesh ili kupunguza makali ya udhalimu wake na amani iweze kupatikana Uruk. Hatima ya Enkidu tayari ilijulikana na miungu. Ingawa Enkidu alikuwa jasiri sawa na Gilgamesh, kifo chake kilitokana na udhaifu wake wa kumpenda Shamhat. Aidha, ilikuwa ni kwa sababu ya majaliwa ya miungu kwamba Enkidu ni sharti afe wala si Gilgamesh.

Mwingilianomatini unabainika katika *Utendi wa Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni* wakati mwanamke ametumika kumhadaa mhusika mkuu katika matini. Samsoni alivyohadaiwa kimapenzi na Delila inalingana na Enkidu alivyohadaiwa na Shamhat. Udhaifu wa Enkidu na Samsoni umechukua mkondo linganifu. Wanawake wametumika kama ‘chombo’ cha kuwaangusha mashujaa katika matini za UG na SS. Aidha, katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, udanganyifu na unafiki umetumika kupitia mwana wa Liyongo hata akamwua baba yake. Udhaifu wa Fumo Liyongo ulionekana kupitia upendo aliokuwa nao kwa mwanawe, ila hakuelewa kuwa kupitia huyo mwana wake angekutana na mauti yake.

Enkidu anajutia matendo yake na anawalaani mwindaji na hawara, ambao kwake, anaona kuwa wale ndio waliosababisha maafa yaliyompata. Hili linabainishwa katika kibao cha VII, ukurasa wa ishirini na sita. Ingawa Enkidu ametambua kwamba alifanya makosa kutagusana na mwindaji na hawara hana la kufanya sasa ila kukubali kukabiliana na mauti yanayomwandama. Matamshi ya maneno ya kulaani yanamfanya msomaji kusikitika na kumwonea Enkidu huruma kwa mfano, anaposema “Na paja lako chafu....naomba...liwe lake (?) kwa sababu yangu...kwa kuwa mimi, nisiye na hatia, umeni....dhidi yangu.” (Tafsiri yangu, kibao VII: 27). Enkidu anakiri kuwa hana hatia ilhali ukweli ni kwamba yeye mwenyewe ndiye aliyejiingiza katika mahaba na hawara, jambo linalobainisha udhaifu wake.

Tanzia vilevile katika UG imeendelezwa kupitia mhusika Gilgamesh. Gilgamesh ndiye mhusika mkuu ambaye anasifika kwa sababu ya sifa zake za kijasiri. Mbali na kusifiwa na jamii, Gilgamesh anajisifu mwenyewe. Hata hivyo, mambo yalimwendea mrama mwishoni mwa simulizi anapokosa kutimiza azimio lake la kupata uzima wa milele. Anatangazia watu wa Uruk kwamba alikuwa tayari kwenda nchi ya mbali kusudi apigane vita vikali hivyo alihitaji kupata baraka kutoka kwao. Maneno yake yalikuwa kama yalivyonakiliwa hapa chini:

Mf 132

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(Gilgamesh said to the men of Uruk: "Listen to me, men...</i>	(Gilgamesh alinena kwa watu wa Uruk akisema:
<i>You, men of Uruk, who know...</i>	Nisikilizeni, watu...
<i>I want to make myself more mighty, and will go on a distant (!) journey!</i>	Nyie watu wa Uruk, mjuao...
<i>I will face fighting such as I have never known,</i>	Nataka kujiongezea uthabiti, Nitafunga safari ya mbali!
<i>I will set out on a road I have never traveled!</i>	Nitajipata katika vita vikali zaidi ya nilivyowahi kupigana,
<i>Give me your blessings!</i>	Nitafuata njia ambayo sijawahi kuipitia!
<i>I will enter the city gate of Uruk...</i>	Nipeni baraka zenu!..
<i>I will perform the new Year's (ceremonies) in...</i>	Nitaingia lango la jiji la Uruk...
<i>The New Year's Festival will take place, celebrations...</i>	Nitajitenga kwa sherehe za mwaka mpya katika...
<i>They will keep shouting "Hurrah!" in...")</i>	Sherehe za mwaka mpya zitatukia, maadhimisho..
<i>(Tablet II:11)</i>	Watapaza sauti kwa riboribo katika..." (Kibao II:11)

Kifungu hiki ni muhimu katika kuelewa sifa za mhusika Gilgamesh. Anajigamba na kutangaza ushindi hata kabla ya kuanza safari yake, jinsi inavyoelezwa katika mistari mitatu ya mwisho. Katika fasihi, tanzia hutokea wakati mhusika mkuu anayesawiriwa na sifa za kishujaa, anaanguka kwa sababu ya kosa alilolitenda yeye mwenyewe. Vivyo hivyo, majisifu ya Gilgamesh yaliishia kuwa kilio wakati alirudi kwa watu wake bure, bila kuwa na sherehe za mwaka mpya jinsi alivyotangaza.

Katika tukio jingine, Gilgamesh alionekana kukaidi mawaidha ya wazee waliomkataza kwenda katika msitu wa Seda ili kupigana na Humbaba. Kutofanikiwa kwake Gilgamesh mwishoni mwa utendi kulitokana na ukaidi wake wa kutosikiliza mawaidha ya wazee katika nchi ya Uruk. Moja kati ya sababu za anguko la Samsoni katika SS ni Samsoni kutotii wazazi wake walipomkataza kumwoa mwanamke Mfilisti. Ulinganifu unabainika wakati Gilgamesh pia anakosa kutii mawaidha ya wazee na matokeo yake ni kwamba anakosa kitu cha thamani cha kuwaletea watu wa Uruk baada ya kusafiri kwenda safari ndefu na hatari.

Gilgamesh anahuzunika kutokana na kifo cha rafiki yake Enkidu. Urafiki wao ulikuwa wa dhati kwa sababu walitiana moyo kila walipokumbana na hatari yoyote hasa walipokuwa katika Msitu wa Seda. Kufa kwake Enkidu kunazua hofu nyingi kwake Gilgamesh kwa sababu alikuwa amejitolea mhanga kumsaidia Gilgamesh kukabiliana na Humbaba, mlinzi wa Msitu wa Seda. Kutokana na maelezo ya msimulizi, Humbaba alikuwa pandikizi la jitu, hivyo ilikuwa vigumu kwa mtu mmoja (Gilgamesh) kumwua. Gilgamesh anatambua msaada aliopewa na Enkidu. Msimulizi anaeleza:

Mf 133

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(Enkidu, whom I love deeply, who went through every hardship with me, The fate of mankind has overtaken him</i>	(Enkidu ninayempenda kwa dhati, aliyepitia magumu yote nami, Hatima ya binadamu imemchukua Jua lilichomoza mara sita, na mwezi ulichomoza mara saba,
<i>And would not allow him to be buried Until a maggot fell out of his nose, I was terrified by his appearance (!), I began to fear death, and so roam the wilderness</i>	Nilimwomboleza na singeruhusu azikwe Hadi buu likaanguka kutoka puani mwake Sura yake iliogofya (!) Nilianza kuogopa kifo, na sasa nazurura nyikani...
<i>The issue of my friend oppresses me, The issue of Enkidu, my friend, oppresses me, So I have been roaming long roads through the wilderness</i>	Suala la rafiki yangu linanisonga. Kwa hivyo nimekuwa nikizurura masafa marefu nyikani
<i>How can I stay silent, how can I be still! My friend whom I love has turned to clay.</i>	Nitawezaje kukaa kimya, nitawezaje kutulia! Rafiki yangu nimpendaye amegeuka udongo.
<i>Am I not like him? Will I lie down, never to get up again?" (Tablet X: 37)</i>	Kuna tofauti gani baina yangu na yeye? Nitalala siku moja, nisiwahi kuamka tena?" (Kibao X: 37)

Maneno katika Mf 133 yanaonyesha kwamba Gilgamesh anaelewa vizuri magumu yote aliyoyapitia akiwa na Enkidu, kwa mfano katika mistari mitatu ya kwanza (*Enkidu ninayempenda kwa dhati, aliyepitia magumu yote nami, hatima ya binadamu imemchukua*). Kifo cha Enkidu kinamfanya kuogopa kifo hivyo kumwomboleza kwa huzuni. Gilgamesh anahofu kwamba hata yeye atakufa kama rafiki yake Enkidu. Hisia za huruma zinamfika msomaji wakati msimulizi anapoeleza kwamba Gilgamesh alimwomboleza Enkidu na *asingeruhusu azikwe hadi buu likaanguka kutoka puani mwake*. Ina maana kuwa maombolezo yalichukua muda mwingi, kiasi cha mwili kuoza na wadudu (buu) kutokea kwa sababu ya uozo huo.

Kifo cha Enkidu kinamhangaisha Gilgamesh, hasa anapofikiria kwamba hata yeye siku moja atalala pasipo kuamka tena (*Kuna tofauti gani baina yangu na yeye? Nitalala siku moja, nisiwahi kuamka tena?"*). Katika mistari hii, Gilgamesh anajua

vizuri kuwa hamna tofauti yoyote kati yake na Enkidu na kwa sababu hiyo, kifo kwake pia kilikuwa kitu cha lazima. Enlil akasema: “Mwache Enkidu afe, lakini Gilgamesh sharti aishi!” Kwa vyovyote vile, Gilgamesh alishajua kwamba kifo kilikuwa kitu cha lazima kwa binadamu.

Ingawa Gilgamesh alikuwa mtu wa kiajabu kiasi cha kuitwa nusu-mungu na nusubinadamu, alionyesha udhaifu wa kibinadamu katika matendo yake, kwa mfano kulala na mwanamwali kabla ya kukutana na mume wake, kuogopa kifo hivyo kudhamiria kutafuta siri ya kuishi milele na kusononeka kwa sababu ya kifo cha rafiki yake Enkidu. Udhaifu mkubwa wa Gilgamesh ulikuwa kupoteza dawa ya kumwezesha kuishi milele. *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh na Simulizi ya Samsoni* zimewiana kwa kuonyesha ulinganifu wa matukio na hasa kwa kuzingatia hatima ya wahusika wakuu. Ingawa wahusika Liyongo, Gilgamesh na Samsoni walikuwa mashujaa katika jamii zao, makosa yaliyofanywa nao yaliwafanya kuwa mateka wa makosa yao wenyewe. Hili linaonyesha kuwa binadamu huwa na udhaifu unaolingana kote ulimwenguni.

5.6.3 Tanzania katika SS

Msuko wa kisa cha Samsoni ni wa kuhuzunisha. Samsoni alikuwa mtu aliyebarikiwa na Mungu kuwa na nguvu za kiajabu kupitia urefu wa nywele zake. Alipigana na Wafilisti wengi na kuwashinda kwa kuwaua (Waamuzi 14: 19, 16:30). Kwa sababu hiyo, Wafilisti walifanya juhudi za kutaka kujua zaidi kuhusu kiini cha nguvu zake.

Hatimaye, siri za nguvu zake zilijulikana kupitia kwa mke wake Delila (Waamuzi 16:18-20).

Katika sehemu ya utangulizi wa *Simulizi ya Samsoni*, inafahamika kuwa Samsoni hakuwa mtu wa kawaida bali alikuwa na sifa za kiungu. Kuzaliwa kwake

kulitanguliwa na shida kwa sababu mama yake alikuwa tasa (Waamuzi 13:2). Kwa kawaida, ni furaha kwa kila mwanamke, hasa aliyeolewa katika jamii za Kiafrika kupata mtoto. Mwanamke tasa hapewi heshima inayomfaa. Hivyo, tasa mara nyingi huishi maisha ya kusononeka. Wakati mwingine anakejeliwa kwa kukosa kuwa na watoto. Mfano mzuri ni kisa cha Hanna na Penina katika Biblia, 1Samweli 1:6-27. Hanna alimlilia Mungu kwa uchungu kwa sababu ya dhihaka alizopata kutoka kwa mke mwenza wake, Peninah. Kisa cha Hanna kinarekodi kwamba Hanna aliweka nadhiri na Mungu kuwa iwapo angemjalia mtoto, angemtoa kwake na wembe haungepita kichwani mwake, katika maelezo yafuatayo:

Akaweka nadhiri, akasema, Ee Bwana wa Majeshi, ikiwa wewe utaliangalia teso la mjakazi wako na kunikumbuka, wala usisahau mimi mjakazi wako, na kunipa mimi mjakazi wako mtoto mume, ndipo mimi nitakapompa BWANA huyo mtoto siku zote za maisha yake, wala wembe hautamfikilia kichwani kamwe (1 Samweli 1:11).

Kifungu hiki kinawiana na kifungu katika Waamuzi 13:5, kinachoeleza kuhusu kuzaliwa kwake Samsoni. Nywele ndefu ilikuwa ishara ya kuwekwa wakfu na kuwa mtumishi wa Mungu. Aidha, kuzaliwa kwa Samsoni kulitangazwa na malaika aliyemtokea mama yake na kumweleza kuhusu mtoto atakayezaliwa. Kwa sababu hii, Manoa (baba yake Samsoni) na mkewe waliingiwa na hofu. Katika Waamuzi 13:22, Manoa anamwambia mkewe kwamba hakika wangekufa kwa sababu walikuwa wamemwona Mungu.

Halikuwa jambo la kawaida kutokewa na malaika kwa ajili ya kuzaa. Hii ndiyo maana Manoa akasema kuwa hakika wangekufa kwa sababu wamemwona Mungu. Isitoshe, Malaika huyo alimpa mama masharti yaliyohitaji kufuatwa kabla ya kuzaliwa hadi kuzaliwa kwa mtoto jinsi inavyoelezwa katika Waamuzi 13:5-7. Inabainika kwamba, wazazi wake Samsoni walikuwa watu wa tabaka la chini kwa sababu malaika alipomtokea mama, alikuwa shambani, kama inavyoelezwa katika Waamuzi 13:9.

Maelezo haya yanaendana na ufafanuzi wa Lord Raglan (1956) anayesema kuwa matukio yanayozunguka kuzaliwa kwake shujaa yeyote si ya kawaida bali ni ya kushangaza.

Ujenzi wa ploti katika tanzia hutegemea usababishi. Kitendo kimoja husababisha kutokea kwa kitendo kingine. Katika maelezo ya tanzia, Aristole alieleza kwamba lengo kuu la kitendo ni kufikia kilele na kusababisha woga miongoni mwa hadhira. Samsoni alipokua kwa umri, ujasiri wake ulionekana kupitia kwa matendo yake. Kitendo cha kuwakamata mbweha mia tatu na kuwaachilia katika shamba la ngano ya Wafilisti hakikuwa kitendo cha kawaida. Katika historia ya binadamu, hakujatokea mtu aliyewakamata mbweha wengi hivyo. Hili linafanya *Simulizi ya Samsoni* kuwa ya kipekee. Maelezo hayo yamewasilishwa katika Waamuzi 15:4-5:

Mf 134

SS

Samsoni akaenda, akakamata mbweha mia tatu, kisha akatwaa vienge vya moto akawafunga mbweha mkia kwa mkia kienge ya kila mikia miwili....akawaachia mbweha kati ya ngano ya Wafilisti (Waamuzi 15:4-5).

Maneno katika kifungu hiki yanaonyesha ujasiri wa mhusika Samsoni na vilevile kusababisha hisia za woga na taharuki miongoni mwa hadhira. Kitendo cha Samsoni cha kuwakamata mbweha mia tatu kinachanganya hisia za mtazamaji ama msomaji. Ni vigumu kuamini ukweli kwamba jambo hili lilifanyika hasa ikifikiriwa kwamba mbweha hao walikuwa wamefungiwa vienge vya moto mikiani mwao! Kitendo cha kuwakamata mbweha mia tatu na kuwaachilia ili kuteketeza ngano ya Wafilisti kiliamsha hasira zao. Ilibidi Wafilisti kuchunguza jambo lililomfanya Samsoni kutenda kitendo hicho kiovu. Matokeo ni kwamba Wafilisti waliwateketeza mwanamke Mtimna na baba yake ambaye alikuwa baba mkwe wa Samsoni (Waamuzi 15:6). Tukio hili vilevile linasababisha mtu yeyote kuingiwa na hisia za

huruma na woga hasa ikizingatiwa kuwa kuua kwa kuteketeza ni kitendo cha kinyama kwa binadamu.

Baba mkwe wa Samsoni na binti yake hawakustahili kufa kwa kuchomwa. Tukio la kumchoma Mtimna na baba yake lilisababisha tukio jingine la kukamatwa kwa Samsoni na kutiwa katika mikono ya Wafilisti. Hata hivyo, Roho wa Bwana alipomjia Samsoni, kamba zilizotumiwa kumfunga zilikatika, zikawa kama katani iliyochomwa kwa moto. Hivyo, Samsoni aliweza kuwageukia Wafilisti na kuwaua kwa kutumia mfupa wa taya ya punda. Mtunzi anaeleza katika Waamuzi 15:16, “Naye akaona mfupa mbichi wa taya ya punda, akautwaa, akapiga watu elfu kwa mfupa huo”. Kifungu hiki kinataja watu elfu moja waliouawa bila sababu yoyote, ila walikufa kwa sababu ya makosa ya Mtimna aliyezini. Mhusika hakuhitaji kutumia silaha zozote hatari ila alichukua kile alichokiona karibu naye, yaani *mfupa mbichi wa taya ya punda* na hicho ndicho kilichotumiwa kuwaua watu elfu moja.

Katika tanzia, nguli anaanguka kutokana na kosa analolitenda mwenyewe. Udhaifu wa kimapenzi wa Samsoni ndio uliosababisha anguko lake. Delila, alimsaliti mume wake (Samsoni) kwa Wafilisti. Delila alitumiwa na Wafilisti kujua siri za nguvu zake Samsoni naye akamsihi mume wake mara kadha kumweleza chanzo cha nguvu hizo. Mtunzi anatoa maelezo hayo katika Waamuzi 16:16, “Ikawa kwa vile alivyomsumbua kwa maneno yake kila siku na kumwudhi, roho yake ikadhikika hata kufa.”

Delila alikuwa amembembeleza mume wake amweleze siri za nguvu zake bila kufanikiwa. Kifungu cha hapa juu kinadhihirisha usumbufu na kuudhika kwake Samsoni kwa sababu ya mke wake. Hii ilitokana na *maneno yake ya kila siku* kiasi cha kukosa utulivu. Samsoni “alichoka na maneno ya Delila” hivyo kumwambia siri yake yote. Uteuzi wa lugha ya Delila ulimfanya Samsoni kumfichulia siri zake. Alipofaulu kujua kiini cha nguvu za Samsoni,

Delila alituma mtu kuwaita wakuu wa Wafilisti ili awafichulie siri hizo, kama inavyoelezwa katika Waamuzi 16:18-20:

“Delila alipoona ya kuwa amemwambia yote yaliyokuwa moyoni mwake, akatuma mtu akawaita wakuu wa Wafilisti, akisema, Njooi huku mara hii tu, maana ameniambia yote aliyo nayo moyoni mwake. Ndipo wakuu wa Wafilisti wakamwendea wakachukua ile fedha mikononi mwao. Naye akamlaza usingizi magotini pake, kisha akamwita mtu akavinyoa vile vishungi saba vya nywele za kichwa chake; akaanza kumsumbua, nguvu zake zikamtoka. Kisha akasema, Samsoni, Wafilisti wanakujia. Akaamka katika usingizi wake, akasema, nitakwenda nje kama siku nyingine, akajinyosha, lakini hakujua ya kuwa BWANA amemwacha!

Mateso aliyopata Samsoni baadaye yalitokana na kosa kale la kumweleza Delila chanzo cha nguvu zake. Nguvu zake zilimtoka pindi tu aliponyolewa nywele zake ndefu. Anguko la Samsoni lilitokana na uamuzi wake wa kumweleza Delila kiini cha nguvu zake. Jambo hili lilikuwa chanzo cha mateso yake hadi kufa kwake. Aristotle (khj) anaeleza kuwa anguko la shujaa hutokana na uamuzi wake (mbaya) mwenyewe. Hata hivyo, Aristotle anasema kuwa hakuna kosa la bahati mbaya. Hivyo, adhabu anayopata mhusika inatokana na uamuzi wake mwenyewe na hapaswi kumlaumu yeyote. ‘Nemesis’ ni dhana iliyoibuliwa na Aristotle kuelezea hali hii. Baada ya Samsoni kunyolewa nywele zake ndefu na kupoteza nguvu zake, Wafilisti walipata nafasi ya kumkamata na kumtesa jinsi walivyotaka. Katika kifungu kifuatacho tunapata maelezo yafuatayo:

Mf 135

SS

Wafilisti wakamkamata, wakamng’oa macho, wakatelemka naye mpaka Gaza, wakamfunga kwa vifungo vya shaba, naye alikuwa akisaga ngano katika gereza (Waamuzi 16:21).

Kifungu hiki kinataja kwamba Samsoni aling’olewa macho yake akiwa hai. Kwa binadamu wa kawaida, kitendo hiki ni cha kusikitisha mno kiasi cha kumwonea huruma mhusika. Isitoshe, baada ya kung’olewa macho, Samsoni alihitajika kusaga ngano gerezani. Masaibu yanayomfika Samsoni yanatokana na kosa lake yeye mwenyewe. Wafilisti walifurahia kumwona Samsoni, adui wao akipitia dhiki hizo

zote. Kwao, Mungu wao (Dagoni) alikuwa amewajibu maombi yao ya kumweka adui wao Samsoni mikononi mwao.

Adhabu nyingine aliyoipata Samsoni kwa sababu ya kosa lake ni kifo. Akiwa gerezani, Samsoni aliagizwa na Wafilisti acheze mbele yao ili awaburudishe karamuni (Waamuzi 16:25). Jambo hili lilimkera Samsoni sana na akamwomba Mungu wake amrejeshee nguvu zake tena ili aweze kulipiza kisasi. Samsoni anapomwomba Mungu *amrejeshee nguvu zake tena* inaonyesha kwamba alikuwa amejuta. Ilikuwa njia ya kujisaka nafsi yake na kugundua kosa alilolifanya.

Mwandishi anaeleza:

Mf 136

SS

Samsoni akamwita Bwana, akasema,
Ee Bwana Mungu, unikumbuke, nakuomba,
Ukanitie nguvu, nakuomba, mara hii tu,
Ee Mungu, ili nipate kujilipiza kisasi
Juu ya Wafilisti kwa ajili ya macho yangu mawili (Waamuzi 16:28).

Samsoni alijutia makosa yake hivyo akachukua hatua ya kumwomba Mungu wake msamaha. Unyenyekevu wa Samsoni unahisika kupitia maneno "*Ee Bwana Mungu, unikumbuke, nakuomba, ukanitie nguvu, nakuomba, mara hii tu*". Taswira inayojengeka ni ile ya mtumwa na mwajiri. Samsoni anaonekana kujua nafasi yake kwamba hakuwa na uwezo wowote bali aliyekuwa na uwezo wa kumnusuru alikuwa ni Mungu wake tu. Ingawa alinyenyekea, bado alifanya hivyo kusudi lake alipize kisasi kwa ajili ya macho yake yaliyong'olewa (*ili nipate kujilipiza kisasi juu ya Wafilisti kwa ajili ya macho yangu mawili*). Maneno hayo yanaashiria kuwa Samsoni hakuamini kwamba alikuwa ameshindwa na Wafilisti. Hata hivyo, Mungu alisikia maombi yake na kumwezesha kutekeleza mauaji mengine:

Mf 137

SS

Samsoni akasema; na nife pamoja na hawa Wafilisti. Akainama kwa nguvu zake zote, ile nyumba ikawaangukia hao wakuu, na watu wote waliokuwa ndani yake. Basi wale watu aliowaua wakati wa kufa kwake walikuwa wengi kuliko wale aliowaua wakati wa uhai wake (Waamuzi 16:30)

Maneno ya Samsoni yanabainisha kwamba alikuwa amejua hatima yake kwa kusema, “*Na nife pamoja na hawa Wafilisti.*” Ukweli ni kwamba Samsoni alitekeleza mauaji ya watu wengi wakati wa kufa kwake kuliko wakati wa uhai wake. Alifanya hivyo kwa kuzisukuma nguzo zilizotegemeza jengo lile. Jengo lenyewe lilikuwa la ghorofa na mwandishi anaeleza kuwa watu waliokuwa katika sakafu ya juu walikuwa elfu tatu (Waamuzi 16:27). Hivyo maisha ya mhusika Samsoni, katika simulizi hii yameishia katika hali ya kitanzia. Kifo chake kilitanguliwa na mateso mikononi mwa adui zake, Wafilisti. Ingawa Samsoni alikuwa shujaa, akiwa na nguvu za kimwili, udhaifu wake kimapenzi ulisababisha kuanguka kwake.

Baadhi ya sifa zinazoifanya *Simulizi ya Samsoni* kuwa ya kitanzia ni pamoja na Samsoni kujiingiza katika mapenzi ya kinafiki na makahaba, kutoboa siri za nguvu zake kwa Delila mkewe, Wafilisti kupanga kumwua Samsoni mara kadhaa pasipo kufaulu na kufungwa gerehani na macho yake kung’olewa akiwa hai. Sawa na *Tenzi za Fumo Liyongo na Gilgamesh*, *Simulizi ya Samsoni* inadhihirisha mwingilianomatini wa udhaifu wa wahusika wakuu ambao wanaishia kufa kwa sababu ya makosa wanayoyatenda wao wenyewe. Ingawa wahusika *Fumo Liyongo*, *Gilgamesh na Samsoni* walikuwa mashujaa wa kutajika, miisho yao ilikuwa fedheha kwao na jamii zao hivyo kuzua mwingiliano wa kitanzia. Katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*, tanzia inayodhihirika ni tanzia-ramsa ambayo bado inazua mwingilianomatini katika matini teule.

5.6.4 Tanzania- ramsa katika UMM

Utendi wa Mikidadi na Mayasa ni utendi mrefu ulio na hadithi ndefu ya wahusika wawili wakuu, Mikidadi na Mayasa. Utendi unamchora Mikidadi kama kijana maskini ila anayejitahidi. Ingawa anakejeliwa kwamba hapaswi kumwoa Mayasa kwa sababu ya umaskini wake, anapigana vita vikali kusudi apate mali atakayotoa kama mahari. Mayasa kwa upande wake ni shujaa anayetoa masharti kwa yeyote anayetaka kumwoa. Anaeleza kuwa mume atakayemwoa sharti apigane naye na atakayemshinda ndiye atakayefaulu kuwa mume wake. Masharti hayo hayakuwa ya kawaida na ilikuwa mshangao kwa baba yake, Jabir. Ingawa Mikidadi alikuwa yatima na maskini asiyekuwa na mali, Mayasa alikuwa amependezwa naye kwa sababu ya ushujaa aliuonyesha. Hata hivyo, Jabiri hakutaka kamwe binti yake aolewe na maskini. Katika ubeti ufuatao, Jabir anamweleza bintiye:

Mf 138

UMM
 Huyu ni mwana yatima
 Hatimizi darahima
 Hapati hata kituma
 Cha maji kukutekea (ub. 123)

Jabir anamweleza bintiye kwamba anayetaka kumwoa ni yatima hivyo hana chochote. Anamwelimisha bintiye kuwa mtu kama huyo, (yatima) hana pesa za kukidhi mahitaji ya jamii. Anaeleza kuwa atakosa pesa (*hatimizi darahima*) za kumwajiri kijakazi atakayemsaidia katika shughuli za nyumbani (*hapati hata kituma, cha maji kukutekea*). Mistari hii inaonyesha juhudi za Jabir za kutia pingamizi uposaji wa Mikidadi kwa Mayasa. Kwa vyovyote vile, Jabir hakutaka msichana wake aolewe na Mikidadi. Tayari alikuwa amemweleza bintiye kuwa kuolewa kwake na Mikidadi hakungewezekana kwa sababu walitoka katika ukoo mmoja inavyoelezwa katika ubeti wa 120.

Katika muktadha huu, Jabiri anakuwa hasidi wa Mikidadi. Kinachomkera Jabir ni umaskini wa Mikidadi hali ndiye anayependwa na binti yake Mayasa. Jambo hili linampelekea Jabiri kumpangia Mayasa mume atakayemwoa. Mume wa kupangiwa Mayasa ni tajiri mmoja kwa jina Maliki Bin Riyahi, ijapokuwa Mayasa hamtaki. Kisa cha UMM kinapozidi kujengeka, Jabiri na Maliki ndio wanaoonekana kuwa adui wa Mikidadi. Wao wanapanga njama za Mikidadi kuuawa, wanapanga kumkaribisha Mikidadi na mkewe nyumbani kuwapongeza ila hayo yote ni unafiki. Katika ubeti wa 661, Jabiri anamweleza Mikidadi kwamba tangu alipopotea walikuwa wameingiwa na wasiwasi wakidhani kuwa alikuwa ameuawa. Katika ubeti ufuatao, msimulizi anaeleza:

Mf 139

UMM
Na leo umewasili
Zimepungua shughuli
Twamshukuru Jalali
Mke ulivyomtwa (ub. 662)

Jabiri anamweleza Mikidadi kuwa wanamshukuru Jalali kwa sababu ya kuwasili kwake na mke wake. Kuna mgeuko wa tabia ya Jabiri kwa kuwa katika ubeti huu, anafurahia Mikidadi ilhali tangu mwanzo amekuwa akimkataza bintiye Mayasa kuolewa naye. Makaribisho anayopewa Mikidadi ni ya kumhadaa tu ili kupatikane nafasi ya kumteka nyara na kuuawa. Mikidadi na Mayasa wanapokelewa vizuri na kila siku ilikuwa ni sherehe. Hata hivyo, mipango ya Jabiri ilikuwa tofauti kabisa kwani anamwandikia Maliki barua aende alipize kisasi kwa kuwa Mikidadi sasa alikuwa mikononi mwake. Katika hali ya kusherehekea, Mikidadi anapewa kileo na anapolewa anafungwa kisha Maliki anajulishwa. Katika ubeti wa 691 (Mf 18), mpango huu unatimia na Mikidadi anapogundua kwamba amedanganywa na kushikwa mateka, analaani jinsi dunia ya leo ilivyo mbaya. Katika msiba huo, anamtaja mama yake mzazi.

Ubeti 691 unaonyesha jinsi Mikidadi anavyolaani dunia ya sasa (*hino dunia ya lewe*). Analaani dunia ya sasa kwa sababu ya unafiki wa Jabiri. Kwake yeye (Mikidadi), alikuwa anaona amefurahiwa na Jabiri kwa sababu ya karamu aliyomfanyia na mkewe ilhali alikuwa na nia tofauti. Mara nyingi mtu anapokuwa katika shida anamkumbuka mama mzazi (*Ee msiba wa kuwe, mamaye kamililia*). Mikidadi anamlilia mamake angalau apate kumwona katika hali hiyo na labda kumwoko. Mama anapopata habari hii, hali ya majonzi inampata kwa sababu ya ukweli kuwa Mikidadi angeuawa. Mateso anayopitia Mikidadi yana uzito katika kisa hiki. Msomaji anaingiwa na hofu hasa inapoonekana kuwa Mikidadi amenaswa na anaenda kuuawa na Maliki jinsi inavyoelezwa katika ubeti ufuatao:

Mf 140

UMM
 Maliki bin Riyahi
 Angojewa asubuhi
 Kesho atamdhabih
 Mdirikini jamaa (ub. 718)

Mtunzi anaeleza kuwa Maliki alikuwa anangojewa ili atimize lengo lao la kumuua Mikidadi (*angojewa asubuhi, kesho atamdhabih*). Maneno hayo yana maana kwamba Mikidadi “angechinjwa” na atolewe kafara. Maliki alikuwa amejipanga kwa ajili ya kutekeleza uovu wake. Alikuwa na hamu ya kukamilisha jambo la mauaji ya Mikidadi hata kabla ya muda uliopangiwa, *asubuhi*, kufika. Hata hivyo, hayo hayakutimia kwa sababu Maliki ndiye aliyekuja kuuawa na Mikidadi baada ya kuokolewa na Ali. Uovu uliopangiwa Mikidadi ulimrudia Maliki kwani Mikidadi mwenyewe alimua. Tukio hili linathibitisha sifa ya tanzia-ramsa kuwa uovu haulipi chochote. Ingawa Maliki alitarajia kumwua Mikidadi, hakufaulu na badala yake yeye anakufa kupitia upanga uliopangiwa Mikidadi. Katika beti 751 na 752, tunapata maelezo yafuatayo:

Mf 141

UMM
 Akampa Mikidadi
 Na maguuni kuyudi
 Kumtinda asibudi
 Kamkata saa moya (ub. 751)

Kamtinda binafusi
 Kamkata yake rasi
 Roho yake kwa upesi
 Motoni ikenda tiwa (ub. 752)

Mistari 1 na 2 katika ubeti wa 751 inaeleza jinsi Maliki alivyofungwa mguu na Ali kisha kuwekwa katika mikono ya Mikidadi. Mikidadi alihitajika kumwua Maliki pasipo kukosea na kwa kweli anamkata mara moja (*kumtinda asibudi, kamkata saa moya*). Msimulizi anafafanua katika ubeti 752 kuwa Mikidadi binafsi ndiye aliyemwua Maliki kwa kumkata kichwa (*Kamtinda binafusi, kamkata yake rasi*). Mara hiyo hiyo roho yake ikaenda motoni (*roho yake kwa upesi, motoni ikenda tiwa*). Upanga uliokuwa utumiwe kumwua Mikidadi ndio uliotumiwa na Mikidadi mwenyewe kumwua hasidi wake, Maliki ambaye anapofurahi kuwa amempata Mikidadi ili aweze kumwua, furaha hiyo ghafla inageuka na kuwa kifo chake yeye mwenyewe. Kitendo hiki kinasababisha tanzia-ramsa katika UMM. Aliyetarajiwa kuuawa (Mikidadi), ndiye anayemwua hasidi, Maliki.

Adui mwingine wa Mikidadi ni bwana Jabir, baba yake Mayasa. Katika mwanzo wa utendi, Jabir anajaribu awezavyo kumshawishi bintiye asiolewe na maskini asiye kuwa hata na urathi wa baba yake (ubeti 15). Baada ya kufanya ushauri, aliona aweke mahari ya mali nyingi mno kwa kutarajia kwamba Mikidadi angeshindwa kulipa. Jabiri hapati amani moyoni mwake anapogundua kuwa bintiye ameolewa na maskini Mikidadi. Anafanya juu chini kuona kwamba Mayasa kamwe haolewi na Mikidadi.

Kwa sababu hiyo, Jabiri anaona njia pekee ya kumwoza bintiye kwa tajiri Maliki ni kumwua Mikidadi. Anafaulu kumhadaa Mikidadi na hatimaye anamteka nyara na kumfanyia sherehe kubwa, akiwa na mkewe, Mayasa. Hapa ndipo anapomlevya Mikidadi kusudi lake apate kumwua. Mpango huu haukufaulu, kwani aliyepangiwa kuuawa mwishowe anakuwa mwaaji. Beti 760 na 761 zinaeleza jinsi Jabiri anavyouawa baada ya kukataa kujiunga na dini ya Kiislamu. Mtunzi anaeleza:

Mf 142

UMM
 Katamka Haidari
 Akamwambia Jabiri
 Ni kumkiri Jabbari
 Na mtumewe pamoya (ub. 760)

Jabiri asikubali
 Kumfuata Jalali
 Kamkata pande mbili
 Sawasawa kamtwaa (ub. 761)

Jabiri anapokataa kumfuata Jalali, anauawa mara hiyo kwa kukatwa katika pande mbili (*kamkata pande mbili, sawasawa kamtwaa*). Mtunzi anapotaja “kamkata pande mbili” anaonyesha ukatili aliofanyiwa Jabiri katika mauaji yake. Ingawa mwandishi wa utendi hajafafanua zaidi kuhusu kufa kwake Jabiri, inayumkinika kuwa kuuawa kwake kulifanyika kwa njia rahisi mno. Katika ubeti wa 756, mwandishi anaeleza kuwa Ali na Mikidadi waliingia katikati ya jeshi la Jabiri pasipo kuogopa kifo na kwamba kua kwao kulikuwa sawa na kula matikiti (*wakangia katikati, wasikukhofu mauti, kama kula matikiti, hali walivyowangia*). Aidha, inaashiria kuwa nguvu walizokuwa nazo Ali na Mikidadi hazikuwa za kawaida ndipo wakaweza kumkata Jabiri pande mbili mara moja.

Vifo vya Jabir na Maliki viliashiria ushindi kwa Mikidadi. Baada ya vifo vyao, Ali na Mikidadi waliwaongoza maelfu ya watu waliosilimishwa kukusanya mali mjini ili

wagawanye. Mikidadi anaishia kuwa na furaha baada ya patashika na misukosuko ya vita baina yake na majeshi kadhaa ya Jabiri na Maliki. Kama njia ya kuonyesha shukrani zake, Mikidadi anaamua kwenda hadi Medina ili kupigana vita vitakatifu vya Jihad kwa niaba ya Mtume Muhamadi. Anakaribishwa na malaika Gabrieli na hatimaye kuandaliwa karamu kubwa akiwa na mkewe Mayasa. Hayo yanadhihirishwa na maneno katika beti zifuatazo:

Mf 143

UMM
 Yakisa hayo kutimu
 Tuma kafanya karamu
 Wali mwingi na lahamu
 Muyini wote kenea (ub. 774)

Kawapa karamu wote
 Vipofu hata viwete
 Kwa kila mtu apate
 Hapo asiye kwenea (ub. 775)

Maneno katika beti 774 na 775 yanaashiria ushindi wa Mikidadi baada ya kuandaliwa karamu kubwa na mtume Mohammed. Chakula kilikuwa tele (*wali mwingi na lahamu, muyini wote kenea*) kiasi cha kumtosha kila mtu mjini pasipo kubagua vipofu na hata viwete. *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* unasawiri tanzia-ramsa kulingana na namna Mikidadi anavyofurahi na mkewe Mayasa baada ya kupitia dhiki. Uovu uliopangiwa Mikidadi haukufaulu. Mahasidi wake Jabiri na Maliki wanakufa kwa mikono yake. Kulingana na utafiti huu, hili linasababisha utendi huu kuwekwa katika kategoria ya tanzia-ramsa.

Furaha inayoonekana mwishoni mwa utendi inapiku changamoto alizopitia Mikidadi tangu mwanzo. Jitihada zake zinazaa matunda kwa sababu anakuwa mshindi kwa kupata mke aliyempigania na vilevile kupata mali chungu nzima. Ingawa Mikidadi alikuwa maskini mwanzoni mwa utendi, mwishowe anaishia kuwa tajiri

huku waliomkejeli wakifa kifo cha kusikitisha. Hata hivyo, baadhi ya sifa zinazoonyesha matendo ya kitanzia katika UMM ni kama vile masharti ya mahari aliyowekewa Mikidadi ili kumwoa binti yake Jabiri (Mayasa) kwa nia ya kumkatiza tamaa kwa madai kuwa angeshindwa kulipa mahari hiyo, kutiwa mbaroni kwa Mikidadi na kulindwa na askari kusudi lake auawe, mahasidi wa Mikidadi (Maliki na Jabir) kupanga njama za kumwua ambazo hazikufaulu na kifo cha Maliki na Jabir.

5.7 Mfanano na Tofauti baina ya Wahusika Wakuu katika UFL, UMM, UG na SS

Ulinganishaji wa wahusika wakuu katika UFL, UMM, UG na SS umeonyesha kuwa wahusika wana sifa nyingi zinazofanana. Wahusika waliochunguzwa wanasawiri tabia zinazowiana zaidi kuliko kutofautiana. Mikidadi katika UMM, Gilgamesh katika UG, na Samsoni katika SS wote wanasawiri sifa ya ukatili. Kwa mfano, Mikidadi kuwakatakata watu (Mf. 74, 75), Gilgamesh alivyomuua Humbaba (Mf. 78) na Samsoni alivyowaua watu elfu moja kwa kutumia taya ya punda (Mf. 80). Tofauti na Gilgamesh, Mikidadi na Samsoni, Fumo Liyongo hajasawiriwa kuwa na sifa yoyote ya ukatili ila ukatili unaobainika katika UFL ni ukatili wa mwanawe akimdungu baba yake kitovuni kwa kutumia sindano ya shaba.

Sifa ya uongozi aidha imedhihirika miongoni mwa wahusika wakuu katika UFL, UG, na SS. Katika UMM, sifa ya uongozi wa Mikidadi haijabainika waziwazi. Sifa nyingine zinazolingana miongoni mwa wahusika wakuu katika UFL, UMM, UG, na SS ni sifa za ushujaa na majigambo. Fumo Liyongo, Mikidadi, Gilgamesh na Samsoni wamesawiri sifa ya ushujaa kupitia matendo yao ya ujasiri kama inavyoelezwa katika mifano 86, 87, 90, 91, 94, 96, 97.

Mikidadi na Gilgamesh wanawiana katika usawiri wa sifa ya majigambo. Kila mmoja wao anajigamba kuwa ni hodari katika vita na kwamba hakuna anayeweza kuwashinda. Sawa na Gilgamesh, Mikidadi anajisifu mbele ya luhani (jini) kwamba hana woga wowote kwake kwa sababu yeye ni simba (Mf. 98) huku Gilgamesh akijigamba kuwa hakuna anayelinganishwa naye kwa kuwa theluthi mbili ya mwili wake ni Mungu na theluthi moja ni binadamu (Mf.100). Maumbile yake yanamfanya kujigamba. Katika Mf. 86, Fumo Liyongo hajasawiri sifa ya majigambo ila anasifiwa na msimulizi kwamba yeye ni shujaa.

Utafiti huu ulichunguza sifa za mwanamke kama mhusika katika UFL, UMM, UG na SS. Mwanamke amechukua nafasi ya kipekee katika matini zilizoteuliwa. Katika UFL, Mama yake Liyongo na kijakazi Saada wanatumia hekima yao na hatimaye kumwezesha Fumo Liyongo kutoroka gerezani. Wanapanga kumtumia Liyongo mkate wa wishwa uliotiwa tupa katikati. Tupa hiyo ilitumiwa na Liyongo kukata minyororo aliyofungiwa. Hekima ya mwanamke pia inabainika katika UMM kupitia Mayasa. Mayasa ni mwanamke aliye na msimamo thabiti katika kauli zinazogusia maisha yake na Mikidadi. Mayasa anaonyesha hekima yake kwa kukataa mume aliyepangiwa na baba yake. Anaeleza kuwa ingawa Mikidadi alikuwa hana mali yoyote, alikuwa amependezwa naye na kwamba angekuwa mume wake.

Mienendo ya wanawake waliotajwa katika UG inalingana na mienendo ya wanawake waliotajwa katika UMM na UFL. Katika UG, wanawake kama vile Ninsun, Shamhat na Shamash wanahakikisha kwamba Gilgamesh yu salama msituni. Ninsun, kwa mfano anajitakasa na kufanya maombi ya matambiko kusudi Gilgamesh asiawe na miungu. Maombi yake yalisikilizwa na miungu na Enkidu anakufa huku Gilgamesh

akibaki salama. Hivyo, kuna ulinganifu wa mienendo ya wanawake waliotajwa katika UFL, UMM na UG.

Tofauti na *Tenzi za Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Mayasa, Simulizi ya Samsoni* imemsawiri mwanamke kuwa na sifa ya unafiki. Unafiki wa Delila, mkewe Samsoni, unadhihirika katika miktadha tofautitofauti akimbembeleza Samsoni kumweleza siri ya nguvu zake ilhali nia yake ilikuwa ni kumweka katika mikono ya Wafilisti. Ilikuwa ni unafiki kwa Delila kukubali kuchukua fedha alizoahidiwa na Wafilisti badala ya ama kumficha au kutotambulisha siri ya nguvu za Samsoni, mumewe.

Mfanano mwingine unaobainika katika UFL, UMM, UG na SS ni uwiano wa sifa ya tanzia. Katika UFL, UG na SS, udhaifu wa wahusika wakuu, Fumo Liyongo, Gilgamesh na Samsoni ulisababisha kuanguka kwao. Fumo Liyongo anafichua siri kwa mwanawe ya kile kilichoweza kumwua huku Samsoni akifichua siri ya nguvu zake kwa mkewe Delila. Gilgamesh anapoteza uzima wa kuishi milele kwa sababu ya uzembe wake wa kukosa kutunza dawa alizopewa na Mvushaji Feri. Ingawa kuna ulinganifu wa tanzia katika UFL, UG, na SS, aina ya tanzia inayotokea katika UMM ni tanzia ramsa hivyo kuleta tofauti katika ulinganifu wa kipengele hiki.

5.8 Hitimisho

Katika sura hii, tumehakiki mwingiliano wa sifa za wahusika wakuu katika UFL, UMM, UG na SS. Aidha, tumejadili mwingilianomatini kwa kuzingatia kipengele cha tanzia. Fumo Liyongo katika UFL, Mikidadi katika UMM, Gilgamesh katika UG na Samsoni katika SS wameonyesha kuwa sifa zao kama wahusika wakuu zinaingiliana katika miktadha tofauti. Utafiti unabainisha kuwa wahusika hao wameonyeshwa kuwa na sifa za ukatili, uongozi, ushujaa na vilevile majigambo katika milki zao. Tofauti na

UMM, UG, na SS, UFL umemwonyesha mwana wa Fumo Liyongo kama katili anayemuua baba yake. Uchunguzi wa mwingiliano baina ya wahusika wakuu umeonyesha vilevile athari ya mhusika mwanamke katika matini teule. Kila mmoja wa wahusika wakuu anaathiriwa ama na hekima au unafiki wa mhusika mwanamke kwa njia moja ama nyingine.

Kuhusu sifa ya tanzia, kifo cha Fumo Liyongo katika *Utendi wa Fumo Liyongo* kinasababishwa na kosa lake la kumweleza mwana wake kiini cha kile kinachoweza kumwua. Hali sawa na hii inatokea katika *Simulizi ya Samsoni*. Kufa kwake Samsoni kulitokea kwa sababu ya udhaifu wake wa kumweleza mkewe Delila siri za nguvu zake. Kosa hili lilifanya adui zake Wafilisti kupata nafasi ya kumnasa, kumtesa, kumdhihaki na hatimaye kufa. Tanzia katika *Utendi wa Gilgamesh* vilevile inatokana na hatima ya Gilgamesh kukosa maisha ya uzima baada ya uzembe wake wa kukosa kuweka dawa ya maisha ya milele vizuri. Gilgamesh anajuta kwa kutokamilisha azma yake ya kutafuta urithi wa maisha ya milele. Aina ya tanzia inayobainika katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa ni* tanzia-ramsa. Mahasidi wa Mikidadi ambao ni Jabiri na Maliki wanakufa baada ya kupanga kumwua Mikidadi aliyefaulu kumposa Mayasa kinyume na matarajio yao. Sura inayofuata inahusu mwingiliano wa kikale cha safari katika UFL, UMM, UG na SS.

SURA YA SITA

MAINGILIANO YA MOTIFU YA SAFARI KATIKA *TENZI ZA FUMO*

LIYONGO, MIKIDADI NA MAYASA, GILGAMESH NA SIMULIZI YA

SAMSONI

6.0 Utangulizi

Katika sura ya tano tulijadili mwingilia no wa sifa za wahusika wakuu katika matini teule. Utafiti ulionyesha kuwa wahusika wakuu wana sifa zinazoingiliana katika miktadha mbalimbali. Sura hii imehakiki maingiliano ya motifu ya safari katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh na Simulizi ya Samsoni*. Tumeonyesha mwingilianomatini katika UFL, UMM, UG na SS kwa kuzingatia urudiaji wa kikale cha safari kinachobainika katika matini teule.

6.1 Motifu ya Safari kwa Ujumla

Matini teule za utafiti huu zimeonyesha kuwa na ruwaza ya urudiaji wa kikale cha safari. Safari katika miktadha ya utafiti huu ni za aina mbili. Kwanza, ni safari halisi ambapo mhusika anafunga safari ya kusafiri kutoka mahali pamoja hadi pengine. Pili, safari inayohusishwa na maisha ya mhusika tangu kuzaliwa hadi kufa kwake.

Utafiti huu umefungamanisha aina hizi mbili za safari kwa pamoja ili kuleta uwiano, hivyo kujadili maisha ya mashujaa Fumo Liyongo, Mikidadi, Gilgamesh na Samsoni kwa kuonisha na motifu ya safari kama inavyoelezwa na Campbell (2008). Ingawa kuna hatua kumi na mbili za safari zilizoordheshwa, tutaweka hatua hizo katika hatua nne kuu. Hatua ya kwanza ambayo itakuwa chini ya anwani ‘Mwanzo wa Safari’ ambazo ni ulimwengu wa kawaida, mwito wa ziara, kukataa mwito wa ziara na kukutana na mshauri. Katika hali ya maisha ya kawaida, hizi ni hatua za kuzaliwa na vilevile utotoni.

Hatua ya pili chini ya anwani ‘Kivuko cha Kizingiti’ inaweka pamoja majadiliano kuhusu kivuko cha kizingiti, majaribu, maadui na marafiki, kisha hatua ya safari kuelekea pangoni. Hatua hizi zinalinganishwa na maisha ya ujana.

Mgogoro wa Safari umejadiliwa kwa kuzingatia vipengele vinavyohusu tatizo, kutuzwa na kurudi nyuma. Hatua hizi tatu zinajadiliwa kama ‘Tatizo’. Hizo ni hatua ambazo zinamwonyesha shujaa akikabiliana na changamoto nyingi katika safari yake. Katika hali ya maisha ya binadamu, hizi ni hatua zinazorejelea utu-uzima. Hatimaye, katika kujadili motifu ya safari, tumeangazia hatua mbili za mwisho ambazo ni ufufuo na kurudi na zawadi, chini ya anwani ‘Ufufuo’. Hizi ni hatua zinazoashiria mwisho wa safari. Katika maisha ya kawaida, tumechukua hatua hizi kurejelea kifo ambapo kikale cha safari kinafikia mwisho.

6.1.1 Hatua za Mwanzo wa Safari

Kikale cha safari ya shujaa huanzia kuzaliwa hadi kufa kwake. Mara nyingi, shujaa hukumbwa na matatizo mengi katika maisha yake, japo anakabiliana nayo kwa ujasiri. Aidha, mazingira yanayozunguka kuzaliwa kwa shujaa huwa ya kiajabu. Miujiza hutokea kuashiria kuwa mtoto atakayezaliwa atakuwa na upekee fulani anapolinganishwa na watoto wengine wa kawaida. Ingawa shujaa anaishi katika ulimwengu wa kawaida, anaonekana kuwa na sifa za kipekee zinazomfanya kujiona tofauti na watu wengine.

Katika hali ya kujiandaa kwa ajili ya Mwito wa Ziara/Safari, shujaa huenda akaondolewa katika mazingira yake ya kawaida. Campbell (2008) anaeleza kwamba shujaa anahitajika kwenda katika nchi ya mbali, msituni, mlimani, ziwani au kuota ndoto ili kukutana na watu wasio wa kawaida. Hatua hii humfanya shujaa kuitikia au kukataa kuitikia mwito wa ziara. Kinachomfanya shujaa kukataa kuitikia mwito ni

woga, ukosefu wa usalama na changamoto mbalimbali zinazomkabili. Hatua hii ni muhimu kwa sababu inabashiri hatari zinazongoja shujaa katika ziara inayotarajiwa. Vilevile, shujaa huenda akakutana na mshauri (hata katika ndoto) ambaye atakuwa wa msaada kwake katika ziara. Mshauri anampa shujaa mawaidha mbalimbali na mashauri yenye hekima kulingana na safari yake. Hivyo, shujaa na mshauri wanaanzisha uhusiano wa kipekee kiasi kwamba uhusiano wao unakuwa tofauti kabisa na wahusika wengine katika simulizi.

6.1.2 Hatua ya Kivuko cha Kizingiti

Katika hatua hii, tunajadili hatua tatu ambazo ni Kivuko cha Kizingiti, Majaribu, Marafiki/Maadui na pia hatua ya Kuelekea Pangoni. Katika hatua hizi, shujaa anaonekana akiwa tayari kuvuka mlango unaotenganisha ulimwengu wa kawaida na ulimwengu mpya. Shujaa anatakiwa kukabiliana na tukio lenye nguvu za kiajabu ili aweze kuingia katika ulimwengu wake mpya pasipo kurudi nyuma. Shujaa aidha anapata majaribu mengi na kukutana na marafiki na maadui vilevile. Katika hatua hii, shujaa anatarajiwa kufanya uamuzi wa busara na kutambua nani kati ya marafiki wake anaweza kuaminika. Uamuzi usiofaa huenda ukamweka shujaa katika hatari, hivyo kukosa kuafiki lengo lake. Mbali na kukutana na majaribu, marafiki na maadui, shujaa anapaswa kujifunza kanuni na sheria za ulimwengu mpya. Hatua hii inampa msomaji nafasi ya kutambua tabia ya shujaa na jinsi anavyokabiliana na changamoto au hatari mbalimbali katika ulimwengu mpya.

Katika hatua hii vilevile, shujaa anapaswa kujitayarisha kwa makabiliano ya hofu na migongano inayomwandama, kwa kuelekea pangoni. Miyamoto (2020) anaeleza kuwa dhana ya pango katika motifu ya safari imetumika kurejelea mahali halisi ambapo hofu, hatari na changamoto nyingi zinatokea. Ni hatua ya kitovu cha

mgogoro katika simulizi yenyewe. Hii ni hatua inayomwezesha shujaa kujisaili, kutathmini na kupanga upya namna ya kukabiliana na tatizo lake. Ni hatua inayozua hofu na taharuki miongoni mwa hadhira. Miyamoto anaeleza kuwa zana kuu ya mtunzi yeyote katika hatua hii ni kushika makini ya hadhira kwa kusababisha msisimko na taharuki huku ‘akichezea’ hisia zao kupitia matukio mbalimbali hatari. Wasiwasi hutanda miongoni mwa hadhira iwapo shujaa ataweza kuikabili changamoto inayomkumba au la.

6.1.3 Hatua ya Tatizo

Katika kuendeleza motifu ya safari katika utafiti huu, tumefafanua hatua tatu tulizoweka pamoja katika sehemu hii ya ‘Tatizo’ nazo ni Tatizo, Kutuzwa na hatua ya Kurudi Nyuma. Katika motifu ya safari, hatua hizi zinaonyesha shujaa akikabiliana na tatizo lake kuu katika safari. Shujaa anakabiliana na tatizo lake na washauri wa karibu wa shujaa huenda wakauawa. Hata hivyo, shujaa anajitahidi kadri ya uwezo wake ili kuibuka mshindi. Safari ya shujaa katika hatua hii imefika nusu na tatizo analokabiliana nalo linaonekana kuwa kilele japo sivyo.

Mapambano makali yanayohatarisha maisha ya shujaa yanashuhudiwa. Shujaa anahitaji kutuzwa na anapotuzwa kwa sababu ya kushinda changamoto iliyomkabili, anapata nguvu zaidi ya kukabiliana na hatari nyingi katika safari yake. Vogler (2003) anaeleza kwamba shujaa huweza kutuzwa kwa kupewa maarifa zaidi, kurudiana na mpenzi wake, kupata tajriba ya kiajabu, kupata zana ya kiajabu au kupata dawa ya kiajabu.

Baada ya kupata tajriba za kiajabu, shujaa anaonyeshwa akikabiliana na mapambano makali. Mapambano hayo yanamfanya kuamua kurudi katika ulimwengu wake wa kwanza (wa kawaida). Hatua hii inamwonyesha shujaa akikabiliana na hatari kubwa

zaidi na maisha yake yakiwa hatarini. Hii ni hatua inayoonyesha safari ya shujaa ikielekea kufika kileleni. Kuna dalili kwamba safari au igizo linafikia mwisho.

6.1.4 Hatua ya Ufufuo

Hatua hii ni kilele cha safari ya shujaa. Baada ya kuibuka mshindi katika mapambano makali na changamoto nyingi alizokabiliana nazo, shujaa anaibuka akiwa mwenye sifa tofauti kabisa. Shujaa amegeuzwa kuwa kiumbe wa kiajabu zaidi na anaonekana kama aliyezaliwa upya, kwa sababu ya mabadiliko mengi yaliyomtokea. Shujaa anaonyesha ujasiri wake zaidi na iwapo kuna changamoto inayokabili jamii, anaamua kujitoa kafara na kuwaokoa walio wanyonge katika jamii. Anafanya hivyo pasipo kujali hatari ya kifo inayomkabili. Hapa ndipo hadhira inasisimuliwa kumwonea huruma shujaa.

Hatua ya Kurudi na Zawadi ni hatua ya mwisho katika safari ya shujaa. Ni hatua iliyo na tuzo ya kumpongeza shujaa. Ni hatua inayomwonyesha shujaa akiwa na ufufuo kana kwamba amezaliwa upya. Hali hii inamfanya kuwa na kibali na ari ya kutaka kurudi katika ulimwengu wake wa kwanza na kuigawa zawadi aliyopata safarini mwake. Hatua hii inamwezesha shujaa kukamilisha safari ya maisha yake, hivyo kukamilisha duara ya safari ya shujaa. Vogler (khj) anaeleza kuwa hatua hizi si lazima kufuatwa moja kwa moja bali kuna uwezekano visa mbalimbali vikawa na hatua zote kumi na mbili, zaidi au visifikishe hatua hizi kumi na mbili. Muhimu ni kwamba duara ya safari ya maisha ya shujaa inakamilika kwa kuzingatia muundo wa kimsingi wa motifu ya safari.

6.2 Hatua ya Mwanzo wa Safari katika UFL, UMM, UG na SS

Utenzi wa Fumo Liyongo ni simulizi inayoonyesha visa vya ajabu vilivyofanywa na Liyongo, shujaa tajika katika jamii ya Waswahili. Ndani ya hadithi hii, Fumo

Liyongo anafanya ziara ya safari kutoka Shaka hadi Pate, kwa mwaliko wa Mfalme. Anapogundua kwamba Mfalme alikuwa na nia ya kumwua, anafunga safari nyingine ya kutorokea Barani. Hata hivyo, Liyongo anawindwa na maadui wake na baada ya majaribio mengi wanafaulu kumwua, hivyo kukamilisha safari yake maishani. Masimulizi haya yamesheheni hatua za kimsingi zinazoambatishwa na motifu ya safari ya shujaa katika fasihi.

Mikidadi akiwa mhusika mkuu katika UMM, anatazamia kumwoa Mayasa, bintiye Jabiri. Azimio lake linazua safari halisi ya kuenda kutafuta mahari. Safarini, Mikidadi anapaswa kupigana vita vikali ili kupata mali ya mahari. Vilevile, anapigana vita vya kimawazo vya kuona kwamba amefaulu katika azimio lake la kumwoa Mayasa. UMM unabainisha hatua zinazozingatiwa katika motifu ya safari.

Motifu ya safari katika UG inabainika kupitia kwa mhusika mkuu Gilgamesh. Akiwa na mshauri wake wa karibu, Enkidu, anaanza safari kuelekea msitu wa Seda kwa nia ya kupambana na Humbaba, mlinzi wa msitu huo ili aweze kukata miti ya mikangazi iliyokatazwa na miungu. Njiani, Gilgamesh anakutana na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na kufa kwa rafiki yake, Enkidu. Sawa na UFL, UMM na UG, safari ya Gilgamesh inahusisha baadhi ya hatua za kimsingi katika motifu ya safari.

SS vilevile inabainisha hatua mbalimbali za motifu ya safari. Motifu hii inadhihirika kupitia kwa maisha ya mhusika mkuu Samsoni kuanzia kuzaliwa hadi kufa kwake. Samsoni anakabiliana na changamoto za kimapenzi na hatimaye kufa hivyo kutamatisha safari yake maishani. Aidha, Samsoni anaanza safari halisi nchini Israeli, paitwapo Sora kuelekea katika nchi ya Wafilisti kusudi atafute mke atakayemwoa. Duara ya safari yake inakamilika anapokufa na kurudi kuzikwa katika shamba la baba

yake katikati ya Sora na Eshtaoli. Kisa cha Samsoni kinafuata baadhi ya hatua za kimsingi katika motifu ya safari ya shujaa yeyote.

6.2.1 Hatua ya Mwanzo wa Safari katika UFL

Katika UFL, safari ya Fumo Liyongo, ambaye ni mhusika mkuu inianza kuangaziwa katika ubeti wa sita, anapoonyeshwa akiwa mwanamume aliyebaleghe. Kuzaliwa kwake hakujaangaziwa katika utendi ila hadithi inianza Liyongo akiwa kijana aliyekwisha baleghe, aliye na nguvu nyingi hivyo kusifiwa na jamii. Mtunzi anaeleza:

Mf 144

Liyongo kitakamali
Akabalighi rijali
Akawa mtu wa kweli
Na haiba kaongeya (ub.6)

Mfano 144 unaonyesha mhusika Liyongo akiwa katika ulimwengu wa kawaida. Mtunzi anaeleza kuwa Liyongo '*kitakamali*' maana yake, alipokamilika. Kukamilika kwake Liyongo kunaonyesha kwamba yeye sasa alikuwa ametoka utotoni na kuwa rijali aliyebaleghe (*akabalighi rijali*). Mistari hii inaonyesha hali ya kawaida kwamba mtoto anazaliwa na baada ya miaka kadhaa anafikisha umri wa kuzaa mtoto baada ya mabadiliko ya kihomoni katika mwili wake. Katika muktadha huu, safari ya Fumo Liyongo (katika utendi) imeanza akishakuwa mwanamume.

Mtunzi anaeleza kuwa Liyongo alikuwa *mtu wa kweli na haiba kaongeya*. Maneno haya yanatupatia dhana kuwa sura yake Liyongo ilikuwa ya kuvutia. Inaonyesha kuwa Liyongo alikuwa mtu aliyependeza na msema kweli ndipo akajulikana kuwa *mtu wa kweli*. Aidha, hatua hii inamwonyesha shujaa akiwa na sifa tofauti na walimwengu wa kawaida. Ubeti ufuatao unatoa maelezo yanayodhihirisha dai hili:

Mf 145

Kimo kawa mtukufu
 Mpana sana mrefu
 Majimboni yu marufu
 Watu huya kwangaliya (ub. 7)

Mistari katika ubeti 7 inafafanua maumbile ya mhusika Liyongo. Kwanza, kimo chake kilikuwa *mtukufu*. Neno *mtukufu* linatumika mara nyingi kuonyesha mojawapo ya sifa za Mwenyezi Mungu au mtu anayeheshimiwa kama vile Rais. Liyongo alikuwa mrefu (*mpana sana mrefu*) kiasi cha kulinganishwa na Mungu. Maumbile yake yalimfanya kuwa maarufu (*majimboni yu marufu*) na watu kutoka sehemu mbalimbali walienda kumwalia (*watu huya kwangaliya*). Maelezo katika mfano huu yanatosha kuthibitisha kuwa japo Liyongo alikuwa katika ulimwengu wa kawaida, alikuwa na sifa zisizo za kawaida za binadamu wa kawaida.

Mwito wa Ziara au safari ya Fumo Liyongo inaelezwa katika beti 23 na 24. Liyongo anafunga safari kuelekea Pate. Safari hii inatokea baada ya barua iliyoandikwa na Sultani akimwomba Liyongo kuzuru Pate ili Wagala nao wapate kumwona kufuatia sifa zake. Msimulizi anasema:

Mf 146

Liyongo siku ya pili
 Ndiye aikabili
 Kainenda tasihili
 Ndiya akaiemeya (ub.23)

Kaifunga kwa sitawa
 Silaha za kuteuwa
 Panda tatu katukuwa
 Kaziwangaa pamoya (ub.24)

Katika ubeti 23, msimulizi anaeleza kwamba Fumo Liyongo alianza safari yake siku ya pili. Safari hii ilikuwa ndefu hivyo alihitaji kutembea upesi (*kainenda tasihili*). Aidha, Liyongo alijitayarisha kikamilifu ili kuikabili safari iliyomngoja. Katika

mistari ya ubeti 24, msimulizi anataja kwamba alijifunga vizuri na kutafuta silaha za kubeba (*kaifunga kwa sitawa, silaha za kuteuwa*). Kwa kuzingatia nadharia ya vikale, shujaa anahitaji kuondoka katika mazingira yake ya kawaida ili kuweza kuanza safari yake ya kuingia katika ulimwengu mpya, ulimwengu unaoweza kuhatarisha au kufanikisha maisha yake. Mbali na silaha alizochukua, Liyongo pia alipanga na kuchukua baragumu tatu (*panda tatu katukuwa*). Maelezo hayo yanatupatia taswira ya mtu ambaye amefunga mzigo mkubwa tayari kuanza safari inayochukua muda mrefu. Ikilinganishwa na maisha ya Fumo Liyongo, hatua hii inasawiri maisha magumu yaliyomngoja, hasa kwa kuzingatia silaha alizoziteua kwa ajili ya safari. Ni hatua inayoonyesha kwamba safari ya shujaa Liyongo imeng'oa nanga.

Mwanzoni mwa safari vilevile, utafiti umejumuisha hatua ya shujaa kukutana na mshauri. Shujaa anakutana na mshauri ambaye atamsaidia katika safari yake. Katika utafiti huu, tumechukua Sultani na Wagala kuwa washauri wa Fumo Liyongo. Mshauri anapaswa kuanzisha uhusiano wa kipekee na shujaa. Katika mfano unaofuata, Sultani na Wagala wanaanzisha urafiki na Liyongo.

Mf 147

Wagala wakabaini
 Kumwambia Sulutwani
 “Twamtaka kwa thamani
 Kijana kutuweleza (ub. 40)

Wagala na Sultani wanachukua nafasi ya kuwa washauri wa Fumo Liyongo. Wao wanaanzisha uhusiano wa kipekee na Liyongo. Katika Mfano147, mshororo wa tatu, Wagala wanamweleza Sultani “*Twamtaka kwa thamani.*” Wagala walitamani kuwa na mtu wao aliyekuwa na sifa sawa na Liyongo. Kwa sababu hiyo, waliona njia ya kipekee ni kuanzisha urafiki na Liyongo wakiwa na njama ya kumwoza msichana wa

jamii ya Wagala. Kwa hekima yao, Wagala wanamhusisha Sultani (*Sulutwani*) katika mpango wao wa kutafuta urafiki na Fumo Liyongo.

Ingawa shujaa anapaswa kutafuta ushauri kutoka kwa rafiki, kwake Fumo Liyongo ni tofauti. Sultani na Wagala wanahusishwa katika safari ya shujaa Liyongo ili kuendeleza mtiririko wa hadithi na vilevile kuendeleza maudhui na vipengele vingine vya kifasihi. Uhusiano unaoanzishwa baina ya mshauri na shujaa ni muhimu. Uhusiano huu huweza kumfaidi shujaa kwa kumtayarisha kwa safari inayomngoja au kusababisha mikinzano kati yake na mshauri. Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, Sultani na Wagala wako kwenye kitovu cha mikinzano katika safari ya shujaa Liyongo.

6.2.2 Hatua ya Mwanzo wa Safari katika UMM

Katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*, shujaa Mikidadi anaonyesha taswira ya umaskini. Katika ulimwengu wa kawaida, Mikidadi anasawiriwa akiwa kijana maskini hivi kwamba hakurithi chochote kutoka kwa baba yake kwa sababu ya umaskini. Msimulizi anabainisha hayo katika beti mbili zifuatazo:

Mf 148

Urathi wa baba yake
Mikidadi asishike
Hakuwa hata na mke
Kwa unyonge kumngia (ub. 15)

Ila ana mjombawe
Etwa Turadi mtuwe
Akenda kukaa naye
Mbuzi akimtungia (ub.16)

Mistari katika ubeti 15 inaonyesha kuwa baba yake Mikidadi alikuwa maskini kiasi kwamba hakuwa na chochote cha kumrithisha mwanawe (*urathi wa baba yake, Mikidadi asishike*). Hali hii inalinganishwa na maisha ya kawaida, ambapo kuna

vikundi viwili vya watu, tajiri na maskini. Isitoshe, msimulizi anaeleza kuwa umaskini wa Mikidadi ulikuwa umekithiri hivi kwamba ilikuwa hata vigumu kwake kupata mke (*hakuwa hata na mke, kwa unyonge kumngia*).

Taswira inayosawiriwa ni kuwa Mikidadi alikuwa amesengenywa na jamii kwa sababu ya umaskini wake. Hii ni hali inayodhihirika vilevile katika ubeti 16. Mikidadi aliishi na mjomba wake na akiwa pale akawa anachunga mbuzi (*akenda kukaa naye, mbuzi akimtungia*). Mara nyingi, inachukuliwa kwamba mtu anayechunga mifugo kama vile kondoo, mbuzi au ng'ombe ni mtoto ama mtumwa. Hata hivyo, mtoto au mtumwa huyo huenda akawa na kipawa fulani kisichoonekana kwa uwazi ila hugunduliwa baada ya tukio fulani linalomhusisha.

Mikidadi alichunga mbuzi wa mjomba wake na alipobaleghe aliweza kumwua Jabiri na kumchukua bintiye (Mayasa) kuwa mke wake. Mikidadi anaonyesha kuwa yuko tayari kuanza safari yake anapokata kauli kwamba atapigana vita hadi afaulu kumwoa Mayasa. Katika mfano ufuatao, msimulizi anaeleza:

Mf 149

Muda huo Mikidadi
Kaondoka kwa juhudi
Kamuendea turadi
Mjombawe kamwambia (ub. 80)

Mjomba nipe farasi
Unazime na **libasi***
Nimtokee Mayasi
Napenda kumtokea (ub. 81)

Katika Mf 149, Mikidadi anaamua kumwendea mjomba wake Turadi ili kumweleza kuhusu azimio lake la kumwoa Mayasa. Hali yake ya umaskini ilimlazimu aombe farasi na hata nguo kusudi aonekane nadhifu vile msimulizi anavyoeleza, *mjomba*

*nipe farasi, unazime na libasi**². Kwa vyovyote vile, Mikidadi alikuwa tayari kuandama azimio lake la kumwoa Mayasa. Hii ndiyo sababu ya kumwomba mjomba wake farasi, nguo na silaha.

Mikidadi anakatazwa na mjombawe kwenda kupigana vita hivyo kwa dai kuwa alikuwa angali kijana mdogo (ubeti 82). Hata hivyo, anamwomba mjomba asimkataze kwenda au kumwona akiwa mdogo sana kwa sababu angeenda na arudi kesho yake vile inavyoelezwa katika ubeti 83. Hii ilikuwa mwanzo wa safari ya Mikidadi. Alikuwa tayari kujitenga na ulimwengu wa kawaida na kujiunga na ulimwengu mpya, anaanza kuonyesha sifa tofauti katika hulka yake. Mwenendo wake unaanza kubadilika na kuwa tofauti kabisa na binadamu wa kawaida.

Mikidadi hakatai mwito wa ziara kama ilivyo katika hatua ya tatu ya motifu nyingi za safari ya shujaa. Kile ambacho kingemzuia Mikidadi kuendelea na ziara yake ni madai ya mahari ya kiasi kikubwa sana. Hata hivyo, Mikidadi hakutishika na jambo la mahari ila tangu mwanzo anaonekana kuwa na matumaini ya kupata mali yote iliyoitishwa na baba yake Mayasa. Hatua ya nne ni Kukutana na Mshauri. Shujaa anakutana na mshauri ili kumsukuma kuendelea katika safari. Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, Mayasa anachukua nafasi ya mshauri. Mshauri anapokutana na shujaa, anatakiwa kumpa maneno ya hekima, wosia, ujumbe maalum au zana zozote muhimu kwa ajili ya safari inayomsubiri. Mshauri aidha anaanzisha uhusiano wa kipekee na shujaa. Katika ubeti ufuatao, msimulizi anaonyesha kuwa Mayasa anafurahia ushujaa wa Mikidadi.

Mf 150

² **Libasi* (1) Katika utafiti huu, tumetumia istilahi hii kumaanisha *lebas* (*mavazi*), maelezo ya *A Standard Swahili- English Dictionary*, 2002, (uk.244). (2) Tafsiri ya istilahi hii katika *Tendi: Six examples of a Swahili classical verse form with translations and notes*, (uk. 284) ni *armour*, maana yake silaha.

Mayasa kuona hivyo
 Mikidadi awanavyo
 Na upanga apigavyo
 Kamjua ni shujaa (ub. 116)

Mf 150 unatangiwa na mapigano baina ya Mikidadi na Mayasa. Baada ya mapigano haya, Mayasa anaridhika kuwa Mikidadi anatosha kuwa mume wake. Hivyo basi, uhusiano wa karibu unaanza kati ya Mayasa na Mikidadi. Mayasa anaona ushujaa wa Mikidadi kufuatia mapigano baina yao, ndipo anasema.....*na upanga apigavyo, kamjua ni shujaa.*

Uhusiano wa karibu baina ya Mikidadi na Mayasa unaanzia tukio hili hadi mwisho wa utendi. Katika motifu ya safari, shujaa anahitaji mshauri atakayemsaidia. Shujaa anapokabiliwa na hatari, anahitaji mshauri wa kumpa moyo. Mayasa anachukua nafasi hii katika utendi huu. Hii ndiyo sababu moja ya kuwa na anwani *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* kwa sababu wawili hao hawatenganishwi. Matukio ya Mikidadi kama shujaa wa utendi hayakamiliki pasipokuwa na Mayasa.

6.2.3 Hatua ya Mwanzo wa Safari katika UG

Motifu ya safari katika Utendi wa Gilgamesh inaingiliana na motifu za safari katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa* na vilevile *Simulizi ya Samsoni*. Matini hizi zimeonyesha mashujaa katika visa husika wakiwa na safari fulani halisi mbali na safari inayohusisha maisha yao tangu kuzaliwa hadi kufa kwao. Katika *Utendi wa Gilgamesh*, Gilgamesh anafunga safari ndefu kuelekea msitu wa Seda ambako anakutana na miungu wanaomshauri kuhusiana na matendo yake kama mfalme wa Uruk. Katika *Utendi* hamna habari zozote kuhusu kuzaliwa kwa shujaa (Gilgamesh) ila tunapata maelezo kuhusu sifa zake. Gilgamesh ni mzawa wa Uruk na

ametunukiwa sifa za ushujaa. Msimulizi anaeleza kuhusiana na sifa hizo katika kifungu kinachofuata:

Mf 151

M.A	M.T (Tafsiri yangu)
Anu granted him the totality of knowledge of all	Anu alimtunuku ufahamu wa yote.
He is the hero, born or Uruk, the goring wild bull	Ndiye shujaa, mzawa wa Uruk, fahali mkali wa kuogofya
Two-thirds of him is god, one-third of him is human (Tablet 1:1)	Theluthi mbili zake ni mungu, na theluthi moja ni binadamu. (Kibao 1:1)

Gilgamesh yuko katika ulimwengu wake wa kwanza, ulimwengu wa kutosheka na yaliyomo. Maneno katika Mf 151 yanaashiria ulimwengu wa kawaida katika maisha ya Gilgamesh. Ingawa hakuna habari kuhusu kuzaliwa kwake na wazazi wake, Gilgamesh anaelezwa kuwa ni mzawa wa nchi ya Uruk na kwamba yeye ni shujaa. Aidha, maumbile yake ni ya kuogofya hivi kwamba amefananishwa na fahali mkali. Gilgamesh ni tofauti na binadamu wa kawaida kwa sababu theluthi mbili zake ni mungu na theluthi moja ni binadamu. Msimulizi anapotoa maelezo kuhusu maumbile yake, anafanya hivyo kimaksudi ili kutoa kisababishi cha kuendeleza matukio mbalimbali katika safari ya Gilgamesh.

Katika hatua ya pili ambayo ni Mwito wa Ziara, Gilgamesh anazungumza na mama yake mzazi katika ndoto. Ndoto hii inahusu mtu jasiri anayeishi mlimani. Hivyo, shujaa Gilgamesh anafunuliwa ziara yake kupitia ndoto, jinsi inavyodokezwa katika maneno yafuatayo:

Mf 152

M.A	M.T (Tafsiri yangu)
Mother <i>I had a dreamlast night</i>	Mama <i>jana usiku niliota ndoto</i>
Stars of the sky appeared, and some kind of meteorite (?)	Nyota ya angani zilichomoza, na aina fulani ya kimondo (?)
Of Anu fell next to me...(Tablet 1:6)	Cha Anu kinaanguka kando yangu ...(Kibao 1:6)

Ndoto ya Gilgamesh inahusu aina fulani ya kimondo kilichoanguka kando yake. Katika nadharia ya vikale, Jung (khj) anaeleza kwamba ndoto ni njia moja ya kueleza vikale vya kibinadamu. Hivyo, ziara ya Gilgamesh inaanza kupitia ndoto. Katika kutafsiri ndoto hii, mama yake Gilgamesh anaeleza kwamba kutatokea mwanamume mwenye nguvu ambaye atamwoko katika changamoto atakazopata safarini mwake.

Mwanamume anayezungumziwa ni Enkidu ambaye anafanya kazi na Gilgamesh kwa karibu hadi kufa kwake. Gilgamesh alipaswa kusafiri kwenda kwenye msitu wa Seda ili kupigana na Humbaba, mlinzi katika msitu huo. Hata hivyo, wazee wanamkataza asifunge safari hiyo kwa sababu ya hatari iliyofahamika kuhusu Humbaba. Ingawa Gilgamesh anakiuka ushauri wa wazee na kuanza safari yake kwenda msituni, hatua hii inajumuisha hatua ya Kukataa Mwito wa Ziara. Baada ya kuzungumza na wazee, wanakubaliana Gilgamesh aandamane na Enkidu katika safari. Hii ni kutokana na madai kwamba msitu wa Seda ulikuwa hatari sana. Mbali na Enkidu kuwa rafiki wa Gilgamesh, anachukua nafasi ya kuwa mshauri wake katika safari. Msimulizi anaeleza:

Mf 153

M.A	M.T (Tafsiri yangu)
Enkidu will protect the friend, will keep the comrade safe....	Enkindu atamlinda rafikiye, atahakikisha mwenzi wake yu salama...
In our assembly, we have entrusted the King to you, and on your return you must entrust the King back to us! (Tablet III:13)	Katika baraza letu tumekukabidhi Mfalme mikononi mwake, na utakaporejea sharti umrejeshe Mfalme mikononi mwetu! (Kibao III:14)

Maneno katika Kibao III:14 yalisemwa na wazee ambao waliona vigumu kumwacha Gilgamesh peke yake katika safari waliyojua kuwa ni hatari. Kwa sababu hiyo basi, wazee wanakubaliana kwamba Gilgamesh sharti aandamane na Enkidu. Jukumu la Enkidu lilikuwa kumlinda rafikiye. Alihitaji vilevile kuona kwamba anarudi kwa wazee (...*Sharti umrejeshe Mfalme mikononi mwetu!*). Ili kutimiza masharti haya

yote, ilibidi Enkidu kuanzisha uhusiano wa kipekee na shujaa, kwa kuwa yeye ndiye aliyekuwa mshauri mkuu wa shujaa. Katika hatua nne za kwanza katika utafiti huu, hatua hii ya Kukutana na Mshauri inafunga jumla ya hatua katika mwanzo wa safari ya shujaa.

6.2.4 Hatua ya Mwanzo wa Safari katika SS

Mwanzo wa Safari inayoshuhudiwa katika *Simulizi ya Samsoni* imechukuana na hatua za Mwanzo wa Safari katika UFL, UMM na UG. Kikale cha safari kinadhihirika kupitia kwa shujaa Samsoni. Mwanzo wa Safari, Samsoni anaonyeshwa akiishi maisha ya kawaida akiwa na wazazi wake. Hata hivyo, kuzaliwa kwake kulikuwa na upekee fulani hivi kwamba mama mzazi alihitaji kutimiza masharti maalum aliyowekewa na Malaika wa Mungu. Mtoto aliyetarajiwa angekuwa mnadhiri wa Mungu, hivyo mama akatakiwa kujiweka ‘safi’ wakati alipokuwa amebeba mimba yake. Aidha, kabla ya kuzaliwa kwake Samsoni, mama yake alikuwa tasa (Waamuzi 12:2-3).

Mwito wa ziara ya shujaa unafuatia maisha katika ulimwengu wa kawaida. Shujaa anatakiwa kujitenga na dunia halisi kwa matayarisho ya ziara. Katika *Simulizi ya Samsoni*, shujaa anaonekana kutengwa kwa ajili ya ziara hata kabla ya kuzaliwa kwake. Hii ni kwa sababu ya upekee wa kuzaliwa kwake. Katika Waamuzi 13:4-5, Malaika wa Mungu anamwomba mkewe Manoa afuate masharti anayompa kwa kusema “...*Basi sasa, jihadhari, nakuomba, usinywe divai wala kileo wala usile kitu kilicho najisi, kwani tazama, utachukua mimba, nawe utamzaa mtoto mwanamume, na wembe usipite juu ya kichwa chake...*” Maneno hayo yanaashiria kwamba tangu tumboni mwa mama yake, shujaa alikulia katika mazingira tofauti, hasa kupitia kwa chakula alichogizwa mama yake kutumia. Mazungumzo yaliyoendelea kati ya

wazazi wa Samsoni na Malaika yalionyesha ulimwengu wa kiroho au kimiujiza ambapo mambo hayangeeleweka kikawaida na binadamu wa kawaida.

Katika hatua ya Mwanzo wa Safari, kila mhusika anafunga safari ‘fulani’. Fumo Liyongo anafunga safari kuelekea Pate kwa ajili ya kumwona Sultani, Mikidadi anaanza safari ya kutafuta mali ya mahari, Gilgamesh anasafiri kuelekea msituni, msitu wa Seda na Samsoni kusafiri kwenda kwa Wafilisti. Katika maandalizi ya safari, Fumo Liyongo na Mikidadi wanajihami na silaha za vita kama vile mkuki na baragumu. Aidha, wahusika wanapojiandaa kwa ajili ya ziara zao, wanakatazwa na miungu au jamii zao. Gilgamesh anakatazwa hasa na mama yake kuzuru msitu hatari wa Seda ila anapositiza kwamba ni lazima aende, miungu wanampa rafiki Enkidu aandamane naye na kuagizwa na miungu kwamba sharti amrejeshe Gilgamesh kwao.

Samsoni anakatazwa na wazazi wake kwenda kwa Wafilisti ili kujitafutia mke ila anakaidi amri zao na kuendelea na mwito wake. Vilevile, azimio la Mikidadi kumwoa Mayasa linakataliwa na mjomba wake, sababu ikiwa kwamba haingewezezana kupata kiwango cha mahari kilichoitishwa na wazazi wa Mayasa. Isitoshe, Mikidadi alikuwa maskini wa kufahamika katika jamii. Kati ya hao wahusika, ni Fumo Liyongo pekee asiyekuwa na masharti au pingamizi zozote katika maandalizi ya safari yake. Wahusika wakuu Fumo Liyongo, Mikidadi, Gilgamesh na Samsoni wote wanaanza safari zao wakiwa vijana ambao walikuwa wamebaleghe. Hivyo, kinachobainika katika hatua ya Mwanzo wa Safari ni safari halisi inayohusishwa na kila mhusika mkuu katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh na Simulizi ya Samsoni*.

6.3 Hatua ya Kivuko cha Kizingiti

Kivuko cha kizingiti ni hatua inayojumuisha hatua nyingine mbili ambazo ni hatua ya Kukutana na Majaribu, Marafiki na vilevile Maadui. Shujaa analikabili tukio linalomfanya kuingia katika ulimwengu mpya pasipo kurudi nyuma. Pia, kunayo hatua ya Kuelekea Pangoni ambapo shujaa anapaswa kukabiliana na hofu katika safari yake.

6.3.1 Kivuko cha Kizingiti katika UFL

Katika hatua hii, shujaa anatakiwa kukabiliana na changamoto kadhaa baada ya kuanza safari yake. Katika UFL, shujaa Liyongo anapokutana na Sultani na Wagala, wanaanzisha uhusiano unaoendelea hadi kufikia kileleni wakati Fumo Liyongo anapouawa. Uhusiano huu unakuwa lango la kuingia katika ulimwengu mpya wa shujaa Liyongo. Katika mfano unaofuata Liyongo amekubali kumwoa msichana Mgala:

Mf 154

Sharuti wakatimiza
Liyongo wakamuoza
Kwa furaha na kuteza
Nyumbani akaingiya (ub. 45)

Mke katukuwa mimba
Akazaa mwane simba
Mwanamume wa kutamba
Mwane Liyongo sikiya (ub.46)

Katika mfano huu, Wagala wamefaulu kumuoza Liyongo msichana wao kama inavyoelezwa katika mistari *sharuti wakatimiza, Liyongo wakamuoza*. Msimulizi anaonyesha furaha ya Wagala kwa kusema, “*Kwa furaha na kuteza, nyumbani akaingiya.*” Ina maana kwamba Liyongo alikuwa amekubali azimio la ndoa baina yake na msichana kutoka katika jamii ya Wagala. Msimulizi anaeleza, “*Mke katukuwa mimba akazaa mwane Simba.*” Maneno hayo yanaashiria kuwa Liyongo

alikuwa amekwisha kuanza maisha mapya katika ulimwengu mpya. Kizingiti alichokivuka Liyongo ni kule kukubali kumwoa Mgala ilhali Wagala hatimaye ndio waliosababisha kuanguka kwake.

Katika hatua ya Kivuko cha Kizingiti vilevile, shujaa anakabiliwa na majaribu, marafiki na maadui. Shujaa anapata majaribu mengi, anapata marafiki na maadui pia. Katika ubeti 46, mishororo miwili ya mwisho, msimulizi anaeleza kuwa mtoto aliyezaliwa alikuwa mwanamume aliyesifika (*mwanamume wa kutamba*). Hapa ndipo kitendawili cha kifo cha shujaa Liyongo kilipoanzia kwa sababu mwana aliyezaliwa ndiye aliyekuja kumwua baba yake.

Kati ya marafiki zake, shujaa anatakiwa kutambua ni nani kati yao ni rafiki wa kweli. Anahitaji kutambua nani kati ya marafiki anaweza kuaminika. Katika mistari ifuatayo, msimulizi anabainisha hatua hii.

Mf 155

Fitina zikamngiya
Mfalume miyamiya
Kwa hila kakusudiya
Kumuuwa fahamiya (ub. 49)

Liyongo akatambuwa
Huzengea kuuwawa
Pale Pate kayepuwa
Barani akitembeya (ub. 50)

Maneno katika mfano 155 yanaonyesha kwamba Liyongo alikuwa na marafiki wa kinafiki ila ametambua kuwa kulikuwa na njama za kumwua (*Liyongo akatambua, huzengea kuuwawa*). Inahitaji shujaa kufanya uamuzi wa busara wakati anateua marafiki zake. Hata hivyo, Liyongo aliweza kuhepa mauaji yaliyokuwa yamepangwa dhidi yake na kutoroka Pate kwenda Barani (*Pale Pate kayepuwa, Barani akitembeya*). Kutoroka kwa Liyongo kulitokana na hila za Mfalme za kutaka kumwua.

Urafiki aliouanzisha Mfalme na Liyongo ulikuwa wa kinafiki. Mfalme (Sultani) alikuwa na nia mbaya ya kupanga kumuua Liyongo. Katika mfano 155 ubeti 50, msimulizi anabainisha hayo kwa kusema “...*kwa hila kakusudiya, kumuuwa fahamiya.*” Msimulizi anatahadharisha kuwa ingawa Mfalme alikuwa ameanzisha urafiki na Fumo Liyongo, urafiki huo haukuwa wa kuaminika kwa sababu alikuwa na kusudi la kumwua. Msimulizi anataka hadhira kufahamu kwamba Mfalme alikuwa na nia mbaya kwa kusema “...*kwa hila kakusudiya, kumuuwa fahamiya.*” Hatua ya Liyongo kutoroka baada ya kugundua hila za Mfalme ilikuwa ya busara.

Wasanye, Wadahalo na Mfalme ambao pia walijifanya marafiki wa Fumo Liyongo ni maadui wake. Mfalme anakusudia kumwua Liyongo kwa kutumia Wasanye na Wadahalo. Hata hivyo, uhodari wa Liyongo ulipiku mipango na hila zao. Msimulizi anaeleza:

Mf 156

Na yeye una hadhari
 Kilala huwa tayari
 Awayuwa wana shari
 Wute piya kwa umoya (ub. 64)

Msimulizi anaonyesha kwamba kila wakati Liyongo yu tayari (*kilala huwa tayari*) hata wakati anapolala. Liyongo aliweza kutambua hila zao (*awayuwa wana shari*) ila aliweza kutumia ujuzi wake wakati wa kuangusha makoma mtini. Katika hatua ya kivuko cha kizingiti, weledi wa shujaa unawekwa katika mizani. Fumo Liyongo anaonyesha uhodari wake. Iwapo ilikuwa ni mtihani, basi Fumo Liyongo ‘alipita’ mtihani huo wa kuangusha makoma.

Ndani ya hatua ya kivuko cha kizingiti, tumejadili pia hatua ya kuelekea pangoni. Hii ni hatua inayomwandaa shujaa kukabiliana na hofu na migongano inayomwandama njiani. Ni hatua inayosawiri changamoto nyingi zinazomfanya shujaa kuwa na hofu.

Taharuki inatanda miongoni mwa hadhira iwapo shujaa ataweza kukabiliana na changamoto na hatari zinazomkabili au la. Katika mfano ufuatao, msimulizi anasema:

Mf 157

“Watamani jambo gani
Menituma Sulutwani
Utapowa kwa yakini
Ili uwage duniya (ub. 96)

“Mekwambia Bwana wetu
Menituma mimi mtu
Muhula wa siku tatu
Fahamu utauwawa.” (ub. 97)

Katika mfano huu, msimulizi anasababisha hofu miongoni mwa hadhira. Maisha ya Fumo Liyongo yamo hatarini. Katika ubeti 96, shujaa anatakiwa kusema maneno yake ya mwisho kabla ya kuaga dunia (*watamani jambo gani...ili uwage duniya*). Huu ni wakati Fumo Liyongo alikuwa tayari ameshikwa na adui wake. Anapatiwa nafasi ya kusema maneno yake ya mwisho ila kwa siku tatu...*muhula wa siku tatu, fahamu utauwawa*. Maisha ya shujaa Liyongo yalikuwa hatarini. Ni wazi kwamba shujaa anakabili kifo ana kwa ana.

Hali hii inasababisha wasiwasi mwingi. Hata hivyo, hatua hii inampa shujaa muda wa kutafakari kikamilifu. Anaelezwa kwamba Sultani ameamuru kwamba kwa muda wa siku tatu angeuawa. Hizo siku tatu zilitosha Fumo Liyongo kupanga namna ya kujinasua katika mtego uliokuwa tayari umemnasa. Ingawa maisha yake yalikuwa hatarini katika hatua hii, msimulizi pia anampa nafasi ya kuweza kutoroka mikononi mwa adui zake. Fumo Liyongo anaonyesha hekima yake kwa kuitisha mkate wa wishwa na kuwekewa tupa ndani ili aweze kuitumia kukatia minyororo aliyokuwa amefungiwa. Anafanya hivyo wakati wa maandalizi ya ngoma. Nyimbo na ngoma zilipozidi, Liyongo naye alikuwa akizikata pingu na minyororo upesi. Shujaa anapojitokeza, msimulizi anaeleza:

Mf 158

Wakiinuka kuteza
 Liyongo akatokeza
 Khaufu zaliwakaza
 Mbiyo zikawapoteya (ub. 117)

Mistari katika ubeti 117 inadhihirisha ushindi wa shujaa Liyongo dhidi ya kifo alichokuwa amepangiwa na Sultani. Watu waliokuwa wakicheza walishangaa kumwona Liyongo aliyekuwa amefungwa jela (*wakiinuka kuteza, Liyongo akatokeza*). Hili halikuwa jambo la kawaida. Msimulizi anaeleza kuwa hofu iliwapata kiasi cha kushindwa kukimbia, (*khaufu zaliwakaza, mbiyo zikawapoteya*). Hata hivyo, watu hawa wote baadaye waliweza kukimbia kama inavyoelezwa katika ubeti 118 “...*kwa wote wakakimbiya, hapana alosaliya....*” Katika hatua ya nane ya motifu ya safari, shujaa anatakiwa kuonyesha kuwa ana uwezo wa kukabiliana na changamoto na hatari ambazo anatarajia kuzipata njiani. Hadhira inabakia kujiuliza maswali mengi iwapo Fumo Liyongo angeweza kukabiliana na changamoto hizo au la. Ni hatua inayojenga mchanganyiko wa hisia miongoni mwa hadhira hasa ikizingatiwa kwamba shujaa alikuwa amefikia nusu ya safari yake.

6.3.2 Kivuko cha Kizingiti katika UMM

Kivuko cha kizingiti katika motifu ya safari ina maana kwamba shujaa yuko tayari kukabiliana na hatari inayomkabili. Yuko tayari kuvuka mlango unaotenganisha ulimwengu wa kawaida na mpya. Hatua hii vilevile inampa shujaa fursa ya kupitia majaribu makali na kutambua kwamba katika safari, kuna marafiki na maadui. Shujaa aidha anaonyeshwa akielekea kufika pangoni ambapo anakabiliana na hofu kuu maishani au safarini mwake. Katika UMM, mapenzi ya Mikidadi kwake Mayasa yanamtoa Mikidadi kutoka katika hatua moja hadi nyingine. Katika ubeti ufuatao, msimulizi anaeleza tabia ya Mikidadi kuhusiana na Mayasa:

Mf 159

Mikidadi kuonake
 Ghadhabu za mwanamke
 Ukarudi moyo wake
 Kwa mahaba kumngia (ub. 107)

Kawana naye kwa pole
 Mahaba yamzidile
 Na Mayasa amwambile
 Mikidadi nisikia (ub. 108)

Beti 107 na 108 zinawasilisha mazungumzo ya kimapenzi baina ya Mikidadi na Mayasa. Kwanza kabisa, Mikidadi anapendezwa na jinsi Mayasa anavyopigana (...*ukarudi moyo wake, kwa mahaba kumngia*). Mikidadi anachukuliwa mateka na uhodari wa Mayasa katika vita. Aidha, msimulizi anaeleza kuwa Mikidadi anapigana naye kwa upole (*kawana naye kwa pole*) kwa sababu ya mapenzi yaliyomzidi (*mahaba yamzidile*). Hii inamfanya Mikidadi kuanza ukurasa mpya wa kimapenzi kati yake na Mayasa. Mikidadi analenga kumwoa Mayasa kwa kuwa ana sifa zinazomvutia. Hii ndiyo sababu kuu ya Mikidadi kupigana vita vikali ili apate mali ya mahari yanayoitishwa na Jabiri, babake Mayasa. Katika utafiti huu, hali hii inalinganishwa na hatua ya Kivuko cha Kizingiti katika motifu ya safari.

Ingawa mapenzi ya dhati yanadhihirika kati ya Mikidadi na Mayasa, Jabiri anaazimia kukatisha uhusiano wao kwa kuitisha mahari ya kiwango cha juu zaidi. Hii ilikuwa ni majaribu kwake Mikidadi hasa inapokumbukwa kwamba hakurithi chochote kutoka kwa baba mzazi. Jabiri ni kizingiti anayefanya bidii kuona kwamba Mikidadi anakata tamaa na kuwacha azma yake ya kumwoa Mayasa. Anamshurutisha bintiye kutokubali kuolewa na Mikidadi kwa sababu ya kile alichosema kuwa wana uhusiano wa kinasaba. Msimulizi anaeleza:

Mf 160

Babaye akamjibu
 Huyuno ni Muarabu
 Na tena mna nasabu
 Na jadi yenu ni moya (ub.120)

Jabiri anamweleza bintiye kuwa wana uhusiano wa kinasaba na Mikidadi kwa kusema; ... *na tena mna nasabu, na jadi yenu ni moya*. Hii ilikuwa njia ya kumzuia Mayasa kuolewa na Mikidadi. Katika hatua ya Kivuko cha Kizingiti, Jabiri anadhihirika kuwa kizingiti na adui mkuu katika safari ya shujaa. Hivyo, Mikidadi anahitaji kutambua maadui na marafiki zake kadiri anavyoendelea na safari yake.

Katika mfano 160, ubeti 120, Mayasa anaonyesha msimamo wake kwa kumwambia babake (Jabiri) awarudishe watu wake na mali yao kwa kuwa alishahitimisha kuwa Mikidadi ndiye angekuwa mume wake. Kwake shujaa Mikidadi, Mayasa ni rafiki wa dhati. Kila mmoja wao ameonekana kuridhika na mwenzake.

Ingawa Jabiri anajaribu kila njia kumzuia Mayasa asiolewe na Mikidadi, Mikidadi anakubali masharti yote anayopewa. Anamweleza ataje yote yaliyo moyoni mwake naye atatimiza. Hata hivyo, changamoto inatokea wakati Jabiri anaitisha mahari inayoonekana kukithiri mipaka ya mahari ya kawaida. Hatua hii inaleta wasiwasi hasa kwa mjombawe Mikidadi. Mahari aliyoitisha Jabiri ilikuwa ngamia mia moja na arobaini walio na afya bora, ngamia hamsini waliofungiwa mzigo wa ambari, muski na kafuri, nguo za dibaji za kisomali mia saba na nguo za kuvaliwa mia mbili, farasi mia moja weusi na wasichana (watumwa) wa Mayasa hamsini. Mbali na hayo, Mikidadi alihitaji pia kuleta kipimo cha dhahabu cha kuridhisha (beti 147-152). Hata hivyo, Mikidadi anaitikia yote yaliyosemwa na Jabiri. Mjomba wake Mikidadi (Turadi) anashangaa ni vipi Mikidadi angetimiza masharti hayo ilhali hakuwa na

chochote, ndipo anamweleza kuwa ameingiwa na kichaa (ubeti 155). Kwa kumjibu mjomba wake, Mikidadi anasema;

Mf 161

Tafanya juhudi yangu
Hata awe mke wangu
Haolewi na mwenzangu
Illa mimi kumuoa (ub. 158)

Mbali na kanuni na masharti ya mahitaji ya mahari, umaskini wa Mikidadi ni kizingiti kingine cha kipekee katika safari yake. Mistari katika mfano 161 ni maelezo tosha kwamba Mikidadi anajitahidi kuvuka kizingiti alichowekewa. Anaeleza kwamba angefanya juhudi yake yeye mwenyewe hadi Mayasa awe mke wake. Katika kuzingatia motifu ya safari ya shujaa, hadhira huenda wakaingiwa na wasiwasi kuhusu vipi Mikidadi ataweza kupata mahari aliyoitishwa hasa ikizingatiwa kuwa yeye ni maskini asiyekuwa na chochote. Ni hali inayoifanya hadhira kuwa na taharuki kuhusu hatua itakayofuata. Swali linalojiri ni je, Mikidadi ataweza kuikabili changamoto inayomkumba au la?

6.3.3 Kivuko cha Kizingiti katika UG

Katika *Utendi wa Gilgamesh*, shujaa anavuka kizingiti wakati anaamua kwamba ataenda kwenye msitu wa Seda ili kukabiliana na Humbaba, mlinzi wa msitu huo. Hii ni hatua muhimu kwa sababu shujaa anajitenga na ulimwengu wa kawaida na kuzuru ulimwengu mpya. Msitu wa Seda haukuwa msitu wa kawaida. Ulikuwa msitu wa kuogofya kwa kuwa kulikuwa na hatari nyingi. Shujaa anaonyesha kuhusu hatari iliyomngoja katika msitu wa Seda kupitia ndoto. Shujaa anashindwa kutafakari na kupata maana ya ndoto lakini Enkidu ambaye ni mshauri wake mkuu anafafanua maana ya ndoto ya Gilgamesh:

Mf 162

M.A	M.T
<i>Enkidu, my friend, I have had a dream...</i>	Enkidu rafiki yangu, nimeota ndoto...
<i>And the dream I had was deeply disturbing</i>	Ndoto niliyoota imenihangaisha sana Katika mabonde ya mlima, Mlima uliniangukia (sisi?)
<i>In the mountain gorges, The mountain fell down on me (us?)</i>	Enkidu aliitafsiri ndoto ya rafiki yake:
<i>Enkidu interpreted the dream for his friend:</i>	
<i>The dream is extremely important, my friend, The mountain which you saw in the dream is Humbaba</i>	Rafiki yangu, ndoto hii ni muhimu sana, Mlima uliouona kwenye ndoto ni Humbaba
<i>It means we will capture Humbaba and kill him and throw his corpse into the wasteland (Tablet IV:14)</i>	Inamaanisha, tutamnasa Humbaba, kumwua na kuirusha maiti yake kwenye ardhi kavu. (Kibao IV:14)

Ndoto ya Gilgamesh katika mfano 162 ilionyesha kuwa shujaa angekabiliana na hatari katika safari yake. Hii ni baada ya Gilgamesh kukiri kuwa ndoto aliyoiota ilikuwa ya kutatiza sana. Enkidu anatafsiri kuwa mlima aliouona Gilgamesh katika ndoto ni Humbaba na kwamba wangemnasa, kumwua na kuirusha maiti yake kwenye ardhi kavu. Ilikuwa kutimbia kuwa Gilgamesh na Enkidu hatimaye walimwua Humbaba. Hatua hii ni muhimu katika motifu ya safari ya shujaa kwa sababu inamweka shujaa katika ulimwengu mpya ambapo hakukuwa na nafasi ya kurudi nyuma kwenda katika ulimwengu wa kwanza (wa kawaida).

Shujaa akishavuka kizingiti na kuingia katika ulimwengu mpya, anakutana na majaribu mengi. Aidha, anapatana na marafiki na maadui vilevile. Katika hatua hii ya safari, shujaa anahitaji kutambua nani kati ya marafiki wake ni wa kuaminika. Anapaswa kuwa makini katika matendo yake akishauriana na marafiki ili asidanganywe na kukosa kutimiza lengo lake. Katika kifungu kifuatacho, Gilgamesh amekutana na wahusika wapya, mmoja wao akiwa Ishtar binti wa mfalme akisema:

Mf 163

M.A	M.T
<i>Gilgamesh addressed Princess Ishtar saying:</i>	“Gilgamesh alinena na binti Mfalme, Ishtar akisema:
<i>“What would I have to give you if I married you!</i>	“Ningekupa nini iwapo nitakuoa!
<i>Where are your bridegrooms that you keep forever”</i>	Wako wapi mabwana harusi ambao umewaweka milele”
....
<i>See here now, I will recite the list of your lovers</i>	Tazama hapa sasa, nitaghani orodha ya wapenzi wako,
<i>And then hit him breaking his wing...</i>	Kisha ukamgonga ukamvunja ubawa...
<i>And now me! It is me you love and you will ordain for me as for them!</i>	Na sasa mimi! Ni wewe nikupendaye na utaamuru iwe kwangu kama ulivyowatendea! (Kibao VI:22-23)

Katika mfano 163 hapo juu Gilgamesh anamsuta Ishtar, ambaye ana uchu wa mapenzi kwake. Hata hivyo, Gilgamesh, kama shujaa tayari amejua tabia yake. Ameelewa kwamba Ishtar ana tabia ya kuwapenda mabwana hao hatimaye kuwadhulumu. Ameelewa kwamba Ishtar si rafiki wa kuaminika, ndipo anamwambia, *wako wapi mabwana harusi ambao umewaweka milele...Kisha ukamgonga ukamvunja ubawa...* Ingawa Ishtar anaonyesha kuwa anampenda Gilgamesh, hana nia nzuri kwa sababu ya uovu ambao anampangia, sawa na wale wapenzi wa mbeleni, kwa mfano; Tamuz, aliyevunjwa ubawa, Simba Mkuu, aliyechimbiwa mashimo saba, Ishullani aliyegongwa na kugeuzwa mbilikimo.

Katika hatua hii, inabainika kuwa Gilgamesh amejifunza kanuni na sheria za ulimwengu mpya. Amekutana na wahusika wengi na kuelewa mienendo yao. Hii ndiyo maana anachukua tahadhari kuhusiana na urafiki wa Ishtar. Hataki kutendewa unyama waliofanyiwa wenzake. Ishtar alijua kuwa angemwangamiza Gilgamesh pindi atakapokubali kufanya mapenzi naye. Hatua hii inapisha hatua ya saba ambayo ni Kuelekea Pangoni.

Hatua ya Kuelekea Pangoni inamsawiri shujaa akikabiliana na hatari safarini. Pango katika motifu ya safari huenda ikawa mahali halisi, kama vile msituni ambapo changamoto nyingi hutokea. Baada ya Gilgamesh kupuuzwa urafiki wa Ishtar, hapendezwi naye hivyo kufoka maneno yafuatayo kwa baba yake Anu. Katika kifungu kifuatacho, msimulizi anaeleza:

Mf 164

M.A	M.T
<i>Ishtar spoke to her father Anu, saying:</i>	Ishtar alinena na baba yake, Anu akisema:
<i>Father, give me the Bull of Heaven, so he can kill Gilgamesh in his dwelling....(Tablet VI:23)</i>	“:Baba, nipe Fahali wa Mbinguni, ndipo amuue Gilgamesh katika makao yake...(Kibao VI:23)

Fahali wa Mbinguni anayetajwa katika mfano 174 ni Humbaba, mlinzi wa msitu wa Seda. Ishtar ambaye amekereka kwa sababu Gilgamesh alikataa kufanya urafiki naye anakusudia kumwua. Kwa sababu hiyo, Ishtar anamwomba baba yake, Anu, kumwachilia Fahali wa Mbinguni kwenda kumwua Gilgamesh katika makao yake. Maelezo hayo yanaonyesha kwamba Gilgamesh alikuwa katika hatari kubwa. Iwapo vita vyake vinapangwa na miungu, basi vita vilivyokuwa vinamngoja Gilgamesh vilikuwa vya kuhatarisha maisha yake. Hatua hii inamtayarisha shujaa kukabiliana na changamoto zaidi zinazotarajiwa katika hatua ya nane ya kukabiliana na tatizo kuu.

6.3.4 Kivuko cha Kizingiti katika SS

Baada ya Samsoni kuzaliwa na kukua, Biblia inarekodi katika Waamuzi 13:25 kwamba Roho ya Bwana ikaanza kumtaharakisha katika Mahame-dani, katikati ya Sora na Eshtaoli. Matukio ya Samsoni yanazungukia mahali hapa (katikati ya Sora na Eshtaoli). Safari ya Samsoni inaendelea kujengeka anapokua kwa umri na kutaka kuo. Anakutana na msichana kutoka Timna na anapendezwa naye, hivyo kupanga kumwoa. Anatafuta ushauri kutoka kwa wazazi wake ila wao wanapinga hatua hiyo.

Hali hii inapisha hatua nyingine katika motifu ya safari ya Samsoni ambayo ni Kivuko cha Kizingiti.

Hatua ya Kivuko cha Kizingiti inaashiria kwamba shujaa ameanza safari yake na kwamba yuko tayari kukabiliana na changamoto zozote njiani. Changamoto ya kwanza ya Samsoni ni wazazi kupinga azimio lake la kumwoa Mtimna. Baba yake Samsoni anamkashifu mwanawe kwa kusema:

Mf 165

Je! Hapana mwanamke hata mmoja katika
Ndugu zako, au katika jamaa zangu zote,
Hata uende kumwoa mwanamke kwa hawa
Wafilisti wasiotahiriwa? (Waamuzi 14:3a)

Maneno haya yanaonyesha kuwa mhusika hana furaha hata kidogo. Baba yake Samsoni hasa anakerwa na jambo kuwa mwanawe anataka kuoa kutoka kwa jamii ya Wafilisti ambao hawatahiri (*...hata uende kumwoa mwanamke kwa hawa Wafilisti wasiotahiriwa?*). Samsoni anapoenda kwa Wafilisti, anakaidi agano la Mungu na Waisraeli ambao ni sharti watahiri wana wao wa kiume kama ilivyoandikwa katika Biblia, kitabu cha Mwanzo 17:10-14. Samsoni hivyo basi anakejeliwa na baba yake. Mbali na hayo, lilikuwa jambo la aibu kutafuta uhusiano na watu wasiotahiriwa. Ingawa baba yake Samsoni anajaribu kumzuia, Samsoni anatamani kutimiza lengo lake la kuoa Mtimna.

Katika Waamuzi 14:3b Samsoni anasema, “...*Mnipatie huyo, kwa maana ananipendeza sana.*” Kwake Samsoni, anapita mipaka ya mila ya ukoo na tamaduni za watu wa jamii yao. Muhimu kwake ni kupata kipenzi cha roho yake pasipo kutilia maanani masharti ya jamii yake.

Hatua ya Kivuko cha Kizingiti vilevile ni sharti kuonyesha shujaa akikabiliana na tukio lenye nguvu za kiajabu kusudi aingie kwenye ulimwengu mpya. Katika Waamuzi 14:5-6, Samsoni anamrarua mwana simba aliyemngurumia. “...*Roho ya Bwana ikamjilia kwa nguvu, naye akampasua kana kwamba anampasua mwana-mbuzi.*” Kukutana na simba pia ilikuwa ishara ya mambo magumu yajayo. Aidha, simba ametumika kijazanda kuashiria Wafilisti ambao wanashindana na Samsoni hadi mwisho wa safari yake.

Matukio yaliyojadiliwa katika hatua ya Kivuko cha Kizingiti katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni* yanafanana kwa kiwango fulani. Fumo Liyongo katika UFL amekubali kumwoa msichana kutoka jamii ya Wagala. Tukio hili linamfanya kuingia katika ulimwengu mpya ambapo hakuna nafasi ya kurudi nyuma. Ni sharti Fumo Liyongo akabiliane na mambo yote magumu ambayo yangemfika maishani akiwa na wakwe zake, Wagala. Sawa na Fumo Liyongo, Mikidadi pia katika UMM anaamua kupigania azma yake ya kumwoa Mayasa hadi kufikia mwisho, ishara kwamba ameingia katika ulimwengu mpya. Ingawa hana mali ya mahari, anajitoa mhanga kupigana vita vikali ili apate mali atakayopatia wakwe zake kama mahari.

Katika UG, Gilgamesh anavuka kizingiti anapokaidi ushauri wa mama yake mzazi na kuingia kwenye msitu hatari wa Seda. Ingawa miungu hatimaye ilimkubalia kuingia katika msitu wa Seda, Gilgamesh anapatiwa rafiki wa kuandamana naye hadi mwisho wa safari yake. Kwa upande wake, Samsoni katika SS anakatazwa na wazazi wake kuoja kutoka jamii ya Wafilisti.

6.4 Hatua ya Tatizo

Katika hatua za Kivuko cha Kizingiti na hatua ya Kuelekea Kufika Pangoni, shujaa anaonyeshwa akiwa amekabiliana na hatari ya kifo ijapokuwa anaepuka kifo hicho. Mashujaa Fumo Liyongo, Mikidadi, Gilgamesh na Samsoni wote wanafaulu kuingia katika ulimwengu mpya katika safari zao hivyo kuendelea na hatua inayofuata. Katika utafiti huu, Hatua ya Tatizo ni hatua ya nane katika motifu ya safari ya shujaa. Ni hatua inayoonyesha shujaa akikabiliana na tatizo lake kuu katika safari. Aidha, hadithi ya shujaa imefikia nusu.

6.4.1 Hatua ya Tatizo katika UFL

Katika hatua hii, shujaa anakabiliwa na changamoto nyingi zinazoathiri maisha yake. Baada ya Fumo Liyongo kukabiliana na hofu ya kuuawa gerezani na kutoroka, mahasidi wake wanapanga upya jinsi ya kumwua. Wanatumia mwanawe Liyongo kama mbinu mpya na hakika mbinu hii ilifaulu.

Mf 166

“Kwa baba enda sikhini
 Umuulize yakini
 Kimuuwacho ni n’ni
 Nakuomba hili moya (ub. 126)

Mfalme anamuomba mwana wa Liyongo kumwuliza baba yake kile kinachoweza kumwua kama inavyoelezwa katika mistari ya kwanza na pili katika mfano 166. Mfalme anataka kujua siri ya kifo chake Liyongo, inavyoelezwa kwa maneno ‘*kimuuwacho ni n’ni, nakuomba hili moya*’ (moja). Maneno yanayosemwa na Mfalme katika ubeti 126, yanatia woga na wasiwasi. Hatua hii basi inatuelekeza kufikia katika kilele cha igizo. Uamuzi uliofanywa na Mfalme ni hatari kwa maisha ya Fumo Liyongo. Kitendo cha kuamua kutumia mwanawe kumwua baba mzazi kinazua tatizo hivi kwamba ni lazima kuwe na mipango kabambe ili mpango wa mauaji uweze kufaulu.

Msimulizi anaeleza kuwa mwana wa Liyongo amekuwa na mazungumzo na baba yake. Fumo Liyongo anamjibu mwanawe kwa kumwambia “Nayuwa kijana umefundiwa, na wewe utahadawa, hayo wamezokwambiya” (ub. 140). Liyongo anamweleza mwanawe kwamba amefundishwa na watu wengine kwa kusema ‘*Nayuwa kijana umefundiwa*’ maana kuwa Liyongo amefaulu kujua hila za mwanawe ila anaelewa fika kuwa amedanganywa (*na wewe utahadawa, hayo wamezokwambiya*). Katika hali ya kawaida, inatatanisha kujua kwamba mtoto wako anapanga kukuua. Vivyo hivyo, Fumo Liyongo anashushwa moyo kujua kwamba mwanawe ametumiwa ili kumwua. Sehemu ya tatizo katika motifu ya safari inamsawiri shujaa akiwa ameshushwa moyo kwa sababu ya jaribio la kifo chake, mshauri au rafiki wake wa karibu.

Katika ubeti 141 Fumo Liyongo anazidi kumweleza mwanawe kuwa amedanganywa (*baba umehadaika*) na kwamba baadaye atakuja kuchekwa (*wao kisa watateka*). Liyongo anamfafanulia mwanawe kuwa atadhihakiwa (*na kuzifanya dhihaka*) kisha yeye mwenyewe atajuta (*kisa utaiyutiya*). Fumo Liyongo kama shujaa yeyote anajua ni nani atakayemuua au kumsaliti. Ameelewa kwamba mwanawe ametumwa ili kumuua. Ilimchukua mwana wa Liyongo mwezi mmoja kupanga kifo cha baba yake kama inavyoelezwa katika ubeti 174 wa UFL. Hakika, hatua hii ni hatua inayomwonyesha shujaa akiwa chini kihisia. Ni hatua inayoweza kusemwa kuwa ni ya kutamausha. Hata hivyo, kuna nafasi ya shujaa kuendelea na safari yake kwa sababu ya kupata tuzo inayompa moyo kuendelea na safari. Katika UFL, Fumo Liyongo anajihami na mkuki wake kwa nia ya kumkabili adui wake (mwanawe). Katika mfano ufuatao, msimulizi anaeleza:

Mf 167

Babake akishutuka
 Chembe uta akashika
 Kwa haraka akatoka
 Nde mui kayendeya (ub. 180)

Fumo Liyongo anapodungwa kitovuni na mwanawe, anagutuka kutoka usingizini. Anashika mshale wake (*chembe uta akashika*) na kutoka upesi kwenda nje ya mji (*kwa haraka akatoka, nde mui kayendeya*). Katika hali hiyo, mshale unakuwa silaha yake muhimu. Ni tuzo anayopata ili kuendeleza safari yake. Silaha hii ni muhimu kwa sababu ndiyo inayotumika kuendeleza hadithi katika UFL. Liyongo anashika mshale wake kwa nia ya kupigana na adui wake. Ingawa hakumpata, aliweza kumfuata haraka akielekea nje ya mji. Hali hii inapeleka kisa hiki cha safari katika Hatua ya Kurudi Nyuma.

Hatua ya kurudi katika ulimwengu wa kawaida katika UFL inahusisha Fumo Liyongo kumfuata adui wake na vilevile mwana wake kumrudia mfalme na kupeleka habari kuhusu kifo cha baba yake. Mwana wa Liyongo anafurahi baada ya kufaulu kumwua baba yake. Anajua kwamba atapatiwa zawadi yake ya kumwoa msichana wa Mfalme na kurithi uongozi kutoka kwake. Hata hivyo, azimio hili halikufaulu. Mwana Liyongo anapofika kwa Mfalme, anadhihakiwa kwa kumwua baba yake. Anafukuzwa maskani mwa Mfalme baada ya kunyang'anywa nguo zote alizokuwa amepatiwa. Kitendo hiki kinamrudisha mwana wa Liyongo katika hali aliyokuwa mwanzoni, ulimwengu wa kawaida. Aidha, Fumo Liyongo anapotoka mjini na kuelekea barani, ni ishara ya kurudi katika ulimwengu wake wa kwanza, hali ya kawaida maishani.

6.4.2 Hatua ya Tatizo katika UMM

Hatua hii inaonyesha safari ya shujaa ikiwa imefika nusu. Ni hatua inayosawiri changamoto nyingi. Shujaa anakabiliana na hatari nyingi ikiwa ni pamoja na kifo. Katika UMM, Mikidadi anapigana vita vikali kusudi apate mahari aliyoitishwa na Jabiri. Katika mfano unaofuata, Mikidadi anakutana na jini na kabla ya kupigana naye, kila mmoja anajaribu kuonyesha umahiri wake katika vita. Katika mfano unaofuata, msimulizi anaonyesha mazungumzo kati ya jini na Mikidadi.

Mf 168

Mikidadi akanena
Ewe jini maleuna
Kama wanijua sana
Hayo usengenambia (ub. 178)

Jini akajikutua
Akajikuza kwa kuwa
Pumzi akazitoa
Huona moto kuwaa (ub. 179)

Katika mf. 168 hapa juu, Mikidadi anamjibu jini aliyemshauri arudi nyumbani kwao (*rejea kwetu urudi, waama utapotea* (ubeti 177)). Mikidadi anaonekana kughadhibishwa na maneno yake ndipo anamjibu katika ubeti 178 kuwa laiti angalijua anayeongea naye, asingalinena alivyonena kwa kumwambia; *kama wanijua sana, hayo usengenambia*. Maneno haya yanatupatia picha kuwa Mikidadi ni mtu jasiri ndiposa ana uwezo wa kukabiliana na jini. Muktaadha wa mazungumzo hayo unaonyesha ghadhabu na hasira za shujaa akihisi kugandamizwa na jini. Kwa upande wake, jini anaonyesha ushupavu wake kwa kujitingisha (*akajikutua*) na kutoa pumzi zilizowaka moto (*pumzi akazitoa, huona moto kuwaa*). Kitendo cha jini kutoa pumzi zinazowaka moto, kinatarajiwa kumweka shujaa katika hali ya kusononeka, ili labda akate tamaa. Hata hivyo, Mikidadi hakukata tamaa ila alipigana na jini, akamwua na kisha kuchukua mali yao kama inavyoelezwa katika ubeti 240. Katika muktaadha

mwingine, shujaa anahitajika kupambana na simba kama inavyodokezwa katika mfano ufuatao:

Mf 169

Wewe una simba wako
Hula watu kila siku
Tumwambie ende huko
Akenda nae taliwa (ub. 448)

Maneno katika ubeti 448 yanasemwa na waziri wa Sultani ambaye anajua sifa za Mikidadi. Anamweleza Sultani kuhusu ujasiri wake wa kuweza kumwua hata jini pasipo kuogopa. Kwa sababu hiyo, waziri anamshauri Sultani kumwachia Mikidadi apambane na simba wake ambaye anasemekana kwamba hula nyama ya watu tu (*...wewe una simba wako, hula watu kila siku*). Wao walijua kuwa safari hii bila shaka Mikidadi ataliwa na simba huyo (*...tumwambie ende huko, akenda nae taliwa*). Hali hii inaleta wasiwasi miongoni mwa hadhira ambao wanaona kwamba safari ya shujaa inafika mwisho. Hata hivyo, shujaa anang'ang'ana na tatizo hili (la kupigana na simba) na hatimaye anaibuka mshindi.

Baada ya kupigana vita vingi kwa ajili ya kutafuta mali ya mahari, Mikidadi anapata habari za kuhuzunisha. Akikaribia mjini kwao, anapata habari kuwa kuna harusi ya Mayasa kuozwa Maliki Bin Riyahi. Habari hii ilikuwa ya kushusha moyo. Katika kueleza hatua ya tatizo katika safari ya shujaa, ni sharti hatua hii imsawiri shujaa akikabiliana na changamoto kuu kimwili na kimawazo. Hali hii inafanya hatua ya Tatizo kuonekana kuwa kilele cha igizo japo sivyo.

Safari ya shujaa inakumbwa na hatari zaidi ila anajitahidi hata kupata tuzo. Tuzo yenyewe inapatikana kwa ncha ya upanga. Katika mfano unaofuata, Mikidadi analikabili jeshi lililoandamana na Mayasa.

Mf 170

Jeshi kuonake vita
 Mikidadi kiwakata
 Mayasa wakamuata
 Mikidadi kamwendea (ub. 546)

Maneno yanayotumiwa na msimulizi katika Mf 170 yanaonyesha kwamba vita vilikuwa vikali. Jeshi lilipoona jinsi Mikidadi alivyokuwa akipigana na kuwaua (*jeshi kuonake vita, Mikidadi kiwakata*), liliwachana na Mayasa na Mikidadi akamwendea (*Mayasa wakamuata, Mikidadi kamwendea*). Ingawa kulikuwa na hatari ya Mikidadi kuuawa na jeshi hilo, msimulizi anamtuza ili kupata nguvu zaidi anapokabiliana na changamoto za mwisho katika safari yake.

Baada ya kukabiliana na changamoto nyingi njiani na kuibuka mshindi hivyo kutuzwa, shujaa anarudi katika ulimwengu wa kawaida. Katika UMM, hatua hii inamwonyesha Mikidadi akiwa amepatana na mpenzi wake Mayasa. Anaona kuwa amefikia azma yake ya kumwoa Mayasa. Hata hivyo, anakumbana na hatari kubwa zaidi huku safari yake ikielekea kufikia kileleni. Hatua hii basi inatupisha katika hatua ya mwisho wa safari ya shujaa.

6.4.3 Hatua ya Tatizo katika UG

Katika hatua ya Tatizo, safari ya shujaa imefika katikati. Ni hatua muhimu kwa kuwa inaonyesha sifa chanya za shujaa anapokabiliana na changamoto yake kuu katika safari. Katika UG, shujaa anafikia nusu ya safari yake anapofika katika msitu wa Seda ambako anakabiliana na Humbaba, mlinzi wa msitu huo.

Gilgamesh anaandamana na rafiki yake Enkidu hadi kufikia msitu wa Seda. Enkidu ndiye rafiki wa Gilgamesh na vilevile mshauri wake. Safarini, Enkidu anampa moyo Gilgamesh anapoonekana kuchoka na kudhamiria kukata tamaa. Mhusika Ishtar anafaulu kumshawishi baba yake, Anu, amtume Fahali wa Mbinguni kumwua

Gilgamesh. Anamwongoza Fahali wa Mbinguni kufika ardhini. Anapofika chini, Fahali wa Mbinguni ananguruma na madhara yanatokea. Mara ya kwanza, kunatokea vifo vya wanaume mia moja na katika mngurumo wa pili, vifo vya wanaume mia mbili vinatokea. Katika mngurumo wa tatu, Enkidu anaangukia katika shimo lililochimbuka na hapo ndipo wanapoamua kumkabili huyu Fahali wa Mbinguni. Hatua hii basi inaonyesha mapigano baina ya Humbaba, Gilgamesh na Enkidu. Enkidu anafaulu kuruka na kutoka katika shimo kisha kusaidiana na Gilgamesh kumkabili Humbaba jinsi inavyoelezwa katika mfano ufuatao:

Mf 171

M.A	M.T
Then Enkidu jumped out and seized the Bull of Heaven by its horns.	Kisha Enkidu akaruka nje ya shimo na kuzikamata pembe za Fahali wa Mbinguni.
The Bull spewed his spittle in front of him...	Fahali akayarusha mate mbele yake.....
Enkidu addressed Gilgamesh saying: “My friend, we can be bold (?) I and you we must share (?) I shall grasp the Bull..... (Tablet VI:24)	Enkidu alinena na Gilgamesh akisema: “Rafiki yangu, tunaweza kuwa jasiri (?) Mimi na wewe sharti tugawane (?) Nitamkamata Fahali.... (Kibao VI:24)

Kutokana na kifungu kilichotajwa katika Mf 171, Enkidu na Gilgamesh wanajitahidi na kuzikamata pembe za Fahali wa Mbinguni (Humbaba) lakini anaonyesha ukali wake kwa kuyarusha mate mbele ya Enkidu. Hii ilikuwa hatari kwao kwa sababu ya nguvu alizokuwa nazo Humbaba, hivi kwamba mngurumo wake pekee ungechimba shimo kubwa ardhini. Huyu ndiye mnyama aliyetarajiwa kupigana na Gilgamesh. Hata hivyo, Gilgamesh na Enkidu wanajipa moyo. ...*“Rafiki yangu, tunaweza kuwa jasiri (?) Mimi na wewe sharti tugawane...* Wanasema kuwa watakuwa jasiri na kugawana majukumu kusudi wafaulu kumwua Humbaba.

Hatua ya Tatizo (The Ordeal) katika safari ya shujaa huonyesha makabiliano makali yanayoonekana kuwa na nguvu za kiajabu. Madai hayo yanachukuana na

makabiliano baina ya Enkidu, Gilgamesh na Humbaba. Kila mmoja wao anaonekana kuwa na nguvu za kipekee zinazopiku nguvu za kawaida za binadamu.

Mara nyingi katika hatua ya Tatizo, mhusika mkuu hukumbana na kifo ana kwa ana, ila anaepukana na kifo hicho kimiujiza. Gilgamesh na Enkidu wanabahatika kumwua Humbaba. Wanaonyesha ujasiri wao zaidi kwa kutoa moyo wake kama thibitisho la mauaji hayo na kuupelekea Shamash. Msimulizi anaeleza kuwa baada ya kumwua Fahali wa Mbinguni waliunyofoa moyo wake na kuupeleka kwa Shamash (Mf 79). Ushindi huu ulimfanya Gilgamesh kuandaa karamu ya kipekee katika makao yake. Mauaji ya Humbaba yanakasirisha miungu ambao wanaitisha mkutano ili kujadiliana kuhusu kitendo hicho. Wao wanaafikiana kwamba ni sharti Enkidu afe badala ya shujaa Gilgamesh. Baada ya siku kadhaa, afya ya Enkidu inadhoofika na hatimaye kufa.

Kufa kwake Enkidu kunatimiza madai ya Volger (khj) kuwa hatua ya Tatizo katika safari ya shujaa huweza kubainisha mwisho wa mahusiano kati ya shujaa na (ma)rafiki wake wa karibu. Gilgamesh anasononeka sana kwa sababu ya kifo cha rafiki yake ambaye anamwomboleza kwa siku nyingi. Hata hivyo, Gilgamesh anatumwa (ilivyo katika hatua ya kutuzwa). Baada ya kukabiliana na changamoto za kutembea katika msitu ulioogopwa na watu wote, baada ya kusafiri mwendo mrefu kupitia milima na mabonde, baada ya kumwua Humbaba na hasa baada ya kuvuka bahari pana katika maji ya kifo, Gilgamesh anakutana na Urshanabi, mvushaji-feri katika bahari ya Maji ya Kifo. Urshanabi anamwelekeza Gilgamesh kukutana na Utnapishtim ambaye anajua siri ya kifo.

Mf 172

M.A	M.T
<i>Utnapishtim spoke to Gilgamesh saying:</i> <i>“Gilgamesh, you come here exhausted and worn out.</i> <i>What can I give you so that you can return to your land?</i> <i>There is a plant like a boxthorn,</i> <i>Whose thorn will prick your hand like a rose.</i> <i>If your hands reach that plant, you will become a young man again.</i> (Tablet XI : 52)	Utnapishtim alinena na Gilgamesh, akisema “Gilgamesh, ulikuwa hapa ukiwa umechoka na dhaifu. Nikupe nini ili urejee katika nchi yako? Kuna mmea unaofanana na ‘mwibamraba’ Miiba yake itachoma mikono yako kama vile waridi. Iwapo mikono yako itafikia mmea huo, utarudi kuwa kijana tena. (Kibao XI :52)

Kifungu katika Mf 172 kinamwonyesha Gilgamesh akiwa na Utnapishtim. Msimulizi anaeleza kwamba Gilgamesh anaonekana kudhoofika lakini baada ya mazungumzo yake, anapata suluhu kuhusu kile kilichokuwa kimemsumbua. Tangu kufa kwa rafiki yake Enkidu, Gilgamesh amekuwa na tatizo la kupata dawa ya kuzuia kifo. Anaona kifo kama tatizo kuu maishani mwa binadamu. Msako wake wa dawa ya kifo umemfanya akutane na Utnapishtim ambaye anampa dawa itakayomfanya kuwa kijana tena, hivyo kuepukana na kifo.

Hatua ya Kutuzwa ni muhimu katika motifu ya safari ya shujaa kwa sababu ni thibitisho la ujasiri wake. Ina maana kwamba shujaa amekabiliana na changamoto kadhaa na baada ya kufaulu anatumizwa. Gilgamesh anatumizwa na Utnapishtim ili anaporejea katika nchi yake, arejee akiwa na kitu cha thamani kwa raia wake.

6.4.4 Hatua ya Tatizo katika SS

Baada ya kuvuka kizingiti na kuingia katika ulimwengu mpya, Samsoni anapata majaribu zaidi. Anapata marafiki na maadui vilevile. Katika karamu ya ndoa kati ya Samsoni na Mtimna, Samsoni anakutana na marafiki wengi. Karamu ya ndoa

iliendelea na kama ilivyokuwa desturi ya Wafilisti, Samsoni anapatiwa vijana thelathini ili kujumuika naye. Hata hivyo, hofu inatokea wakati Samsoni amemwacha ‘mkewe’ na anaporudi kutoka nyumbani kwao, anapata kwamba rafiki yake wa dhali amemchukua. Katika kifungu kifuatacho, tunapata maelezo yafuatayo:

Mf 173

Baba yake akasema, hakika mimi nalidhani ya kuwa
umemchukua kabisa, basi nalimpa rafiki yako... (Waamuzi 15:2)

Katika mf 173 hapa juu, baba mkwe wa Samsoni anageuka kuwa adui. Hii ni kwa sababu anatoa msichana wake kwa rafiki ya Samsoni ilhali tayari alikuwa amemwoza, hali inayozua mtafaruku. Rafiki yake Samsoni anaonyesha unafiki. Samsoni anapandwa na hasira na kuchoma mashamba ya ngano ya Wafilisti, kama njia ya kulipiza kisasi. Hatimaye, Wafilisti wanapogundua yaliyotendeka, wanawageukia msichana na baba yake na kuwateketeza kwa moto pia. Katika motifu ya safari, hatua hii ni muhimu kwa kuwa shujaa anatambua marafiki wake wa kuaminika na wasioaminika.

Ndani ya Kivuko cha Kizingiti katika utafiti huu, tunapata hatua ya Kuelekea Pangoni. Katika hatua hii, shujaa anakumbana na hatari na changamoto zaidi. Shujaa anajipata katika hali ya mvutano wa kihisia akijaribu kujinasua kutoka changamoto inayomkabili. Ili kutimiza hatua hii ya safari, Samsoni anakumbwa na hatari ya kifo wakati ameshikwa na watu wake wa Yuda kwa sababu ya kosa la kuchoma mashamba ya ngano. Watu wa Yuda (Waisraeli) walikuwa na hofu ya kulipizwa kisasi na Wafilisti juu ya mashamba yao yaliyoteketezwa. Isitoshe, Wafilisti ndio waliokuwa katika mamlaka ya uongozi wa Israeli wakati huo. Hivyo, wanamshika Samsoni na kumkabidhi Wafilisti. Kifungu kifuatacho kinaonyesha wasiwasi wa Samsoni.

Mf 174

Wakamwambia, tumeshuka ili kukufunga,
 Tupate kukutia katika mikono ya Wafilisti,
 Samsoni akawaambia, niapieni ya kwamba
 Ninyi wenyewe hamtaniangukia (Waamuzi 15:12)

Suala la Tatizo katika SS limejitokeza vizuri katika Mf 174. Samsoni amezongwa na mawazo juu ya maisha yake anaposema;...*niapieni ya kwamba ninyi wenyewe hamtaniangukia.*” Inaonekana kana kwamba anajua jinsi atakavyojinasua akiwa mikononi mwa Wafilisti mradi tu watu wake wasimwue. Kuna taharuki miongoni mwa hadhira iwapo Samsoni ataweza kukabiliana na changamoto hii na kufaulu. Katika muktadha huu, tatizo linalotokea ni kwamba Samsoni anafungwa mikono yake hivi kwamba ilikuwa vigumu kwake kufanya chochote. Muktadha huu unapisha hatua ya tatizo katika motifu ya safari.

Samsoni anafungwa mikono kwa kamba mbili mpya na kupelekwa hadi Lehi ili kukutana na Wafilisti. Ingawa walifurahi kwa kumpata Samsoni akiwa amefungwa, hawakufaulu kumwua kwa sababu anakata kamba hizo kiajabu. Katika Waamuzi 15:14, msimulizi anaeleza kwamba roho ya Bwana ilimjia kwa nguvu na zile kamba zilizokuwa juu ya mikono yake zikawa kama kitani iliyoteketezwa kwa moto na vile vifungo vyake vikaanguka mikononi mwake. Tukio hili linamfanya Samsoni kuondoka kwa hasira na kwenda kuwaua Wafilisti zaidi ya elfu moja (Waamuzi 15:16). Baada ya kuwaua Wafilisti hao, Samsoni anahisi kiu, ishara ya kuishiwa na nguvu zake.

Mara nyingi, shujaa anaonekana kushushwa moyo au hata kuonekana kukata tamaa katika hatua ya tatizo kwenye motifu ya safari. Hata hivyo, anapata tuzo kama zawadi ya bidii yake katika kukabiliana na tatizo lake kuu. Kwake Samsoni, anapata nguvu mpya baada ya kumwomba Mungu wake kumpa maji ya kukata kiu aliyokuwa nayo.

Katika nadharia ya vikale, maji ni moja kati ya ishara zinazotumika kuashiria uhai. Eliade (1959) akizungumzia ubia wa ishara ya maji katika dini mbalimbali, anaeleza kuwa maji huashiria maisha mapya, yana uwezo wa kusafisha na kutakasa hasa yanapotumika katika muktadha wa ubatizo. *Simulizi ya Samsoni* inaeleza katika Waamuzi 15:19 kuwa Samsoni alipokwisha kunywa maji katika Lehi, roho yake ilimrudia naye akaburudika. Hii inaonyesha umuhimu wa maji katika maisha na vilevile maji kama ishara ya uhai na/au kuzaliwa upya hivyo kuashiria shujaa kupata nguvu mpya ili kuendelea na safari yake.

Tatizo lingine linalomkumba Samsoni ni hali yake ya kushindwa kudhibiti hisia zake za kimapenzi kwa wanawake. Samsoni anakutana na kahaba na wanapokuwa pamoja katika nyumba yake, Wafilisti wanagundua na kupanga kumwua. Aidha, anakutana na mwanamke mwingine kwa jina Delila. Delila anatumiwa na Wafilisti kujua siri ya nguvu za Samsoni. Anamrairai Samsoni mara kadha ili amweleze siri ya nguvu zake lakini hakufalu. Kwa wakati mwingine, Wafilisti wanaahidi kumpa Delila fedha elfu na mia kila mmoja iwapo angepata kujua asili ya nguvu za Samsoni (Waamuzi 16:5). Ingawa Samsoni anafungwa kwa kamba saba ambazo hazijakauka na kufungwa tena kwa kamba mpya mikononi, anazikata zote kwa urahisi. Matukio hayo yanaonyesha safari ya shujaa ikielekea kufika kileleni. Katika matukio yote mawili, Samsoni anakabiliwa na hatari ya kifo ila anaibuka mshindi na kuwaacha adui zake Wafilisti wakishangaa.

6.5 Hatua ya Ufufuo

Katika motifu ya safari, Hatua ya Ufufuo ni hatua ya mwisho. Ni kilele cha safari ya shujaa. Shujaa anakamilisha mapambano makali na kuibuka mwenye sifa tofauti baada ya kuepuka kifo na hatari nyingine nyingi, hivyo kuimarika zaidi. Shujaa

‘anakufa’ na kukamilisha duara ya safari yake kwa kurudi katika ulimwengu wake wa kwanza, ulimwengu wa kawaida palipo na watu wake.

6.5.1 Hatua ya Ufufuo katika UFL

Katika UFL, safari ya shujaa Liyongo inafika mwisho wakati yeye na mwanawe wanakufa. Fumo Liyongo anauawa akiwa amelala usingizi. Msimulizi anaeleza kuwa Liyongo alidungwa kitovuni akiwa amelala chali na anapogutuka mwanawe alikuwa tayari ametoweka (ubeti 179). Hata katika kifo chake, Liyongo analeta matumaini kwa watu wake kwa kuelekea kisimani, mahali pa kuteka maji. Msimulizi anaeleza kuhusu tukio hilo katika ubeti 184:

Mf 175

Kuwa Liyongo mekwima
Uko nde ya kisima
Sasa watu wamekoma
Mai hawapati ndiya (ub. 184)

Katika ubeti 184, kifo cha Liyongo kilisababisha watu kukosa maji (*sasa watu wamekoma, mai hawapati ndiya*). Hata hivyo, kisima kimetumika kijazanda kuashiria uhai hivyo kuleta matumaini miongoni mwa jamii. Kwa sababu kisimani mnapatikana maji, maji huashiria pia kuzaliwa upya. Kifo cha Fumo Liyongo basi kinasawiri uhai miongoni mwa watu wake wa jamii. Inaonyesha kwamba hata baada ya kufa kwake Liyongo, roho yake ingali ilikuwako. Hii ndiyo sababu ya kusema kwamba katika kisasili cha safari, shujaa hafi ila anasafiri na kurudi tena.

Tofauti na baba yake, kifo cha mwana wa Liyongo kinaonyesha dhiki. Hii ni kutokana na maradhi yaliyompata. Mwanawe Liyongo alikufa baada ya kuugua kwa muda mrefu (*maradhi yakaingiya, yasiyomuondokeya*). Mistari hii inaonyesha kwamba mwanawe Liyongo aliugua kwa muda mrefu kabla ya kufa. Kifo chake kinapofananishwa na kifo cha baba yake (Fumo Liyongo), kuna tofauti kubwa. Kifo

cha shujaa kina uajabu fulani unaoambatanishwa nacho. Fumo Liyongo anakufa huku amepiga magoti akiwa ameshika mshale wake kando ya kisima. Maji ni uhai, hivyo kufa kwake Liyongo kisimani kuliashiria kwamba alikuwa angali anaishi. Kitendo hiki kinakamilisha safari ya shujaa Liyongo.

6.5.2 Hatua ya Ufufuo katika UMM

Katika UMM, karibu kila hatua inahusisha vita kati ya Mikidadi na vikundi tofauti tofauti. Mikidadi anajikakamua kupigana ili kupata mali ya mahari. Katika mfano unaofuata, anapigana na Alii ambaye anamwangusha chini tayari kumkatakata.

Mf 176

Alii akamrudi
Kamba ewe Mikidadi
Walionapi asadi
Akaepuka na baa (ub. 604)

Ikawa kumkamata
Pale tini kumuata
Tiati akamuata
Na kisu kamkalia (ub. 619)

Msimulizi katika ubeti 604 analinganisha mapigano kati ya Alii na Mikidadi na mtu ambaye amemwona simba, kwa sababu anaelewa kuwa hakika kuna hatari (*walionapi asadi, akaepuka na baa*). Maneno hayo yalikuwa ya kumtahadharisha Mikidadi kwa mapigano makali. Katika hali ya kawaida, ni kwamba huwezi ukakutana na simba kisha ukose kujeruhiwa. Katika ubeti 619, Mikidadi anaangushwa chini (*pale tini kumuata*) na Alii alikuwa tayari kumkata (*tiati akamuata, na kisu kamkalia*). Hapa ndipo Mikidadi kama shujaa alipaswa kuonyesha umahiri wake vitani. Katika hatua ya ufufuo, shujaa anahitajika kuonyesha kwamba yeye ni tofauti sasa akilinganishwa na wakati wa kuanza safari yake. Vita baina ya Ali na Mikidadi viliisha kwa kumfanya Mikidadi mfuasi wa dini ya Kiislamu. Changamoto iliyomkabili Mikidadi ni kuamua iwapo angejiunga na dini ya Kiislamu ama afe, kama inavyoelezwa katika

ubeti 628 kwa maneno yafuatayo “...*Ewe yakhi Mikidadi, ni kukiri Muhamadi, na wewe ukashadidi, ndipo nitakondokea.*” Mbali na kukabiliana na changamoto ya nguvu za kimwili, Mikidadi pia alikuwa katika mkanganyiko wa kihisia. Hii ni kwa sababu anafanya ushauri na Mayasa kabla ya kukata kauli kuwa wafuasi wa dini ya Kiislamu (ub. 629).

Kilele cha safari ya Mikidadi kinatokea wakati Jabiri anamkaribisha nyumbani kwake lakini Mikidadi anakosa kujua hila zake potovu. Nia yake ilikuwa ni kumwita Maliki ili aje alipize kisasi juu ya Mikidadi ‘aliyemnyang’anya’ Mayasa ‘mke wake’. Karamu kubwa iliyoandaliwa ilikuwa ya kumfunga macho Mikidadi asijue mipango ya Jabiri. Katika ubeti ufuatao, msimulizi anaeleza jinsi Mikidadi alivyopatiwa kileo na baadaye kutiwa nguvuni.

Mf 177

Hata zikija akili
Amefungwa silisili
Na mapingu ya rujuli
Mikidadi akalia (ub. 690)

Katika **Mf 177**, msimulizi anaeleza kuwa Mikidadi anaporudiwa na *fahamu* ya ulevi, anajipata katika hali tatanishi baada ya kugundua kuwa amefungwa (*amefungwa silisili, na mapingu ya rujuli*). Uyakiniifu wa hali alimokuwa Mikidadi ulimfanya kufikiria mama yake tu ili apate usaidizi aliohitaji sana. Hali hii inaleta wasiwasi hasa miongoni mwa hadhira ambao wanaona kuwa shujaa atauawa. Hata hivyo, miujiza inatokea wakati malaika Jibrili, Tamima (mamake Mikidadi) na vilevile Mikaili wanashughulika kuona kwamba Mikidadi anaachiliwa. Mikaili anatumwa na Mungu akunje nchi ili Tamima aweze kufika Medina upesi (ub. 698) kwa kusudi la kutafuta ushauri na usaidizi kutoka kwa Nabii. Hatua hii inaleta mchanganyiko wa kimawazo

miongoni mwa hadhira iwapo kweli itawezekana nchi kukunjwa ili kupunguza umbali wa mwendo wa safari ya Tamima hadi Medina.

Wakati mipango ya kumwokoza Mikidadi ikiendelea, Jabiri na Maliki wanafanya mpango wa kumuoza Mayasa kwake Maliki huku wakimdhulumu Mikidadi. Msimulizi anaeleza kuwa Mikidadi alisikika akilia kwa dhiki ya kamba (ub. 732). Hata hivyo, Mikidadi anaokolewa kwa wakati ufaao na Alii. Ingawa nyumba alimofungiwa Mikidadi ilikuwa imezungukwa na watu wengi, Ali anaingia ndani na kumfungua. Mara tu anapofunguliwa, Mikidadi anauliza mahali aliko Mayasa na anapoonyeshwa, anajitosa ndani pasipo kubisha hodi (ub. 745). Kitendo hiki kinamkasirisha Maliki ambaye alikuwa anajifurahisha na Mayasa, na mara hiyo vita vinaanza kati yake na Mikidadi. Tunapata maelezo yafuatayo kuhusiana na vita kati ya Maliki na Mikidadi.

Mf 178

Maliki akabaini
Kwani kungia nyumbani
Usipopawa idhini
Maliki kamuawia (ub. 747)

Kamtinda binafusi
Kamkata yake rasi
Roho yake kwa upesi
Motoni ikenda tiwa (ub.752)

Mistari ya ubeti 747, inarejelea Maliki ambaye analalamika kwa sababu ya kumwona Mikidadi chumbani mwake bila idhini yoyote kwa kusema, “...*kwani kungia nyumbani, usipopawa idhini...*” Ifahamike kwamba Mikidadi kwa wakati huu ana nguvu mpya, amepata sifa nyingine zinazomfanya kuwa tofauti na wakati wa mwanzo wa safari yake. Hii ndiyo maana Mikidadi anaonekana kutotishwa na Maliki. Katika ubeti 752, tunaelezwa kuwa Mikidadi anamkata kichwa Maliki yeye mwenyewe (*kamtinda binafusi, kamkata yake rasi*) na mara hiyo Maliki anakufa na

roho yake kutiwa motoni (*roho yake kwa upesi, motoni ikenda tiwa*). Hatua hii imeonyesha ushujaa wa Mikidadi ambaye hajali hatari ya kifo inayomkabili.

Ili kukamilisha safari ya shujaa, kuna haja ya kumwonyesha akiwa amepata tuzo/zawadi. Katika utafiti huu, hatua hii ni ya mwisho, chini ya Hatua ya Ufufuo. Shujaa akishazaliwa upya anapata kibali cha kurudi katika ulimwengu wa kawaida na kuigawa zawadi aliyopata safarini. Baada ya kumwua Maliki na Jabiri, Mikidadi anaungana na mkewe (Mayasa) kwa furaha. Mikidadi anajitoa kupigana vita vya Jihad kama njia ya kumshukuru Muhamed kwa kumpa ushindi dhidi ya hila za Jabiri na Maliki. Kwa kuzingatia motifu ya safari, kauli ya shujaa kujitoa kama kafara ili kuokoa watu walio katika ulimwengu wa kawaida ni muhimu. Mikidadi anapoamua kupigana vita vya jihad, anatimiza kanuni na sheria za motifu ya safari kwa kujitoa kafara ili kuokoa wanyonge katika jamii au watu wake.

Mikidadi anahitimisha safari yake kwa kufanya harusi ya kufana na Mayasa. Hivyo, tuzo au zawadi anayopata safarini mwake ni kutimiza azma yake ya kumwoa Mayasa. Anafanya karamu kubwa mjini ambapo kila mja anafurahia. Msimulizi anaeleza;

Mf 179

Kawapa karamu wote
Vipofu hata viwete
Kwa kila mtu apate
Hapo asiye kwenea (ub.775)

Karamu iliyofanywa na Mikidadi kama inavyoelezwa katika **Mf 179** ilikuwa ya kuhusisha watu wote pasipo kubagua hata vipofu na viwete. Msimulizi anafafanua kwamba Mikidadi hakuwabagua watu (*kawapa karamu wote, vipofu hata viwete*). Hali hii inaonyesha kwamba shujaa amepigana vita vikali na kushinda. Kwa sababu hiyo, amepata kibali cha kurudi katika ulimwengu wake wa kawaida. Shujaa sasa

yuko tayari kuanza maisha mapya yanayotokana na athari ya safari aliyosafiri. Baada ya karamu ya harusi yao, Mikidadi na Mayasa wanaishi kama mume na mke. Mikidadi anaanza maisha mapya na mpenzi wa roho yake, hivyo kukamilisha duara ya safari yake.

6.5.3 Hatua ya Ufufuo katika UG

Baada ya kupata tuzo, Gilgamesh anarudi katika nchi yake, Uruk-Haven ambayo ni ulimwengu wake wa kawaida. Anarudi pale akiwa na furaha. Anaandamana na mvushaji feri (Urshanabi) katika safari hiyo ya mbali. Njiani, Gilgamesh anatamani kuoga kwa sababu ya uchovu aliokuwa nao. Hata hivyo, anapatwa na janga jingine baada ya nyoka kuunyemelea mmea ule wa uhai. Msimulizi anaelezea hayo katika kifungu kifuatacho:

Mf 180

M.A	M.T
Gilgamesh spoke to Urshanabi the ferryman saying; Urshanabi, this plant is a plant against decay (!) By which a man can attain his survival (!)	Gilgamesh alinena na Urshanabi, mvushaji akisema; Huu ni mmea unaopinga kudhoofika (!) Kupitia kwake binadamu atapata kuishi (!)
Seeing a spring and how cool its waters were, Gilgamesh went down and was bathing in the water. A snake smelled the fragrance of the plant. Silently came up and carried off the plant (Tablet XI : 50)	Alipoona Kisima na jinsi maji yake yalivyokuwa tulivu, Gilgamesh alijitosa ndani kuoga katika maji hayo. Nyoka alinusa harufu nzuri ya mmea ule. Taratibu aliunyemelea na kuubeba mmea (Kibao XI : 50)

Tukio la Gilgamesh la kupata dawa iliyoziua kifo linalinganishwa na hatua ya ufufuo katika motifu ya safari. Ni tukio lililohatarisha maisha yake japo matokeo yake yangefaidi watu wa Uruk-Haven. Mbali na kwamba nia ya shujaa ilikuwa kujiokoa kutokana na janga la kifo, dawa hii ingetumika pia kuokoa watu wa nchi yake hasa kutokana na kifo cha rafiki yake Enkidu.

Ingawa Gilgamesh alikuwa amepata suluhisho la kifo, anapoteza kipawa hicho kutokana na uzembe wake. Kama shujaa, alihitaji kuwa makini katika kila hatua aliyoichukua. Kisa hiki cha nyoka kuunyemelea mmea wenye siri ya kuwa kijana tena, kinaeleza kwa nini nyoka hubambua gamba lake. Gilgamesh anapoteza dawa hii muhimu, ndipo anasononeka na kulia kwa uchungu. Anajuta na kuendelea tu na safari hadi Uruk-Haven, nchi yake.

Kisa cha Gilgamesh kupoteza kipawa alichopewa na miungu (Utnapishtim) kinamsawiri kwa njia hasi. Inaonyesha udhaifu wake akiwa shujaa, hivyo kuanguka kwake. Ingawa alikuwa amekaribia kupata uzima wa milele aliokuwa amesaka kwa muda mrefu, anapokonywa na ibilisi wake nyoka. Kitendo hiki kinasababisha mageuzi ya mwelekeo wa safari ya Gilgamesh. Mwenendo wa Gilgamesh unabadilika na anarudi katika nchi yake akiwa na huzuni.

Safari ya shujaa Gilgamesh inafika mwisho anapofika nchi yake na kujiliwaza kwa kumwonyesha Urshanabi maendeleo aliyoyafanya nchini humo. Anatembea katika makao yake huku akiusifu ujuzi wa ujenzi wake. Maneno yanayosemwa na Gilgamesh ni yale yale aliyoyasema mwanzoni mwa utendi kama inavyobainika kupitia mfano unaofuata:

Mf 181

M.A	M.T
<i>Go up on the wall of Uruk and walk around! Examine its foundation, inspect its brickworks thoroughly. Is not (even the core of) the brick structure made of kiln-fired brick (Tablet I : 1)(a)</i>	Kwea ukuta wa Uruk na uzunguke! Chunguza msingi wake, kagua uashi wake kwa makini. Thibitisha kuwa matofali yake ni ya kukaushwa ndani ya tanuri (Kibao I : 1)(a)
<i>Go up, Urshanabi, onto the wall around, Examine its foundation, inspect its brickwork thoroughly.... Is not (even the core of) the brick structure of kiln-fired brick. (Tablet XII :50)(b)</i>	Kwea juu Urshanabi, kwenye ukuta wa Uruk na utembe pale, Chunguza msingi wake, kagua uashi wake kwa makini.... Je, matofali yake si ni ya kukaushwa ndani ya tanuri. (Kibao XII : 50)(b)

Mazungumzo ya Gilgamesh katika (a) ambao ni mwanzo wa safari yake ni sawa na mazungumzo yake katika (b), mwisho wa safari yake. Hayo yanaashiria kuwa safari yake imefikia mwisho. Baada ya shujaa kukabiliana na changamoto zote alizokutana nazo njiani, ni sharti arudi katika ulimwengu wake wa kwanza ili kukamilisha duara ya safari yake. Mfano katika (a) na (b) ni ishara kuwa Gilgamesh amehitimisha safari aliyoianza mwanzoni mwa utendi. Katika hatua hii ya mwisho, shujaa ameshapata ujuzi wa nguvu za kimiujiza na kimwili. Shujaa kwa sasa amebainisha ujuzi na umahiri wake. Ujuzi alioupata shujaa utatumika kwa manufaa ya watu wake. Hii inathibitisha madai ya nadharia ya vikale kuwa shujaa hafi ila anazaliwa upya.

6.5.4 Hatua ya Ufufuo katika SS

Hatua ya ufufuo katika SS inasawiriwa na nywele za Samsoni kumea upya baada ya kunyolewa na Delila. Kilele cha safari ya Samsoni kinafika wakati ambapo mhusika amechoka kusumbuliwa na Delila kuhusu asili ya nguvu zake. Katika utafiti huu, tumechambua kisa hiki katika hatua za Ufufuo na Kurudi na Zawadi.

Wakati Wafilisti walipokuwa wamefurahi kwamba wamefaulu kumshika adui wao Samsoni, nywele zake zilikuwa zinamea tena. Kumea tena kwa nywele za Samsoni ilikuwa ishara ya ufufuo, kwamba shujaa hajashindwa kamwe. Ingawa alikuwa ameng'olewa macho, Samsoni 'anzaliwa upya' kwa sababu ya mabadiliko yaliyomtokea. Katika kifungu kufuatacho, tunapata maelezo yafuatayo:

Mf 182

Samsoni akamwita BWANA akasema,
Ee Bwana MUNGU, unikumbuke, nakuomba,
Ukanitie nguvu, nakuomba, mara hii tu,
Ee Mungu, ili nipate kujilipiza kisasi juu ya Wafilisti
Kwa ajili ya macho yangu mawili (Waamuzi 16:28).

Maneno katika kifungu hiki yanaonyesha kwamba shujaa ameshushwa moyo kwa sababu ya kitendo cha kung'olewa macho. Anaomba Bwana Mungu ampe nguvu tena ili aweze kulipiza kisasi juu ya macho yake. Wakati huu, Samsoni alikuwa gerehani akidhulumiwa na wapinzani wake, Wafilisti. Katika Hatua ya Ufufuo, shujaa anatakiwa kuonyesha kwamba hajashindwa. Anatakiwa kuonyesha upekee wa ushujaa wake baada ya kudhaniwa kuwa ameshindwa. Katika **Mf 182**, Samsoni anamwomba Mungu ampe nguvu mpya ili kuangamiza adui zake. Ili kukamilisha safari yake, Samsoni anachagua kufa na adui zake. Katika Waamuzi 16:30, Samsoni anasema, “...*Na nife pamoja na hao Wafilisti...Basi wale watu aliowaua wakati wa kufa kwake walikuwa wengi kuliko wale aliowaua wakati wa uhai wake.*”

Ingawa Samsoni anaamua kufa na adui zake, anadhihirisha upekee wa ushujaa wake kwa kuwaua watu wengi zaidi. Hii pia ilikuwa kama zawadi kwake, kwa kuwa tayari alikuwa ameangukia mikononi mwa adui zake (Wafilisti). Isitoshe, akawa ameng'olewa macho. Shujaa alihitaji kuwaonyesha kuwa sherehe walizofanya Wafilisti katika Waamuzi 16:24 hazikuwa halali mbele ya Mungu na ushujaa wa Samsoni ulihitaji kubainika waziwazi.

Safari ya Samsoni inafikia mwisho wakati jamaa zake wanapochukua mwili wake na kwenda kuuzika (Waamuzi 16:31). Mahali anapozikwa Samsoni ni mahali katikati ya Sora na Eshtaoli. Hapa ni mahali palipotajwa katika mwanzo wa hadithi yake kwamba Roho ya Bwana ilianza kufanya kazi katika maisha yake.

Mf 183

Roho ya Bwana ikaanza Kumtaharakisha katika Mahane-dani, Katikati ya Sora na Eshtaoli (Waamuzi 13:25) (a)	Wakamchukua, wakamzika kati ya Sora na Eshtaoli, katika kiwanja cha kuzikia cha Manoa baba yake... (Waamuzi 16:31) (b)
--	---

Vifungu hivi viwili katika **Mf 183** vinaonyesha mwanzo na mwisho wa safari ya Samsoni. Safari ya shujaa imerudi katika ulimwengu wake wa kwanza. Hii ni baada ya kushuhudia kuzaliwa, kukua, kuimarika na kuanguka kwake Samsoni. Kifungu katika (a) kinaonyesha kuwa roho ya BWANA Mungu ilianza kufanya kazi ndani ya maisha ya shujaa Samsoni katikati ya Sora na Eshtaoli. Matukio yake mengi yalitendeka mahali pale. Safari yake inapofikia mwisho katika (b), shujaa anaenda kuzikwa mahali palepale panapotajwa mwanzoni mwa Simulizi, katikati ya Sora na Eshtaoli. Katika motifu ya safari, hatua hii ni muhimu ili kukamilisha hadithi ya shujaa. Kurudi kwa shujaa katika ulimwengu wake wa kwanza kunakamilisha duara ya safari ya shujaa Samsoni.

6.5.5 Ulingano na Tofauti ya Motifu ya Safari katika UFL, UMM, UG na SS

Tukilinganisha hatua ya Mwanzo wa Safari katika UFL, UMM, UG na SS, kuna sifa ambazo zinawiana katika matini zote. Wahusika wakuu ambao ni Fumo Liyongo, Mikidadi, Gilgamesh na Samsoni wana sifa za ushujaa. Kila mmoja wao ana sifa tofauti na binadamu wa kawaida. Gilgamesh, kwa mfano, ana maumbile ya kiajabu kwa vile theluthi yake moja ni binadamu na theluthi mbili ni mungu. Aidha, amefananishwa na fahali mkali. Fumo Liyongo ana kimo cha urefu mkubwa, mpana na macho makali hivi kwamba akikuangalia unazimia. Samsoni na Mikidadi vilevile

wanasawiriwa kuwa na nguvu za kiajabu, kwamba wana uwezo wa kupigana na simba. Wahusika Fumo Liyongo, Mikidadi, Gilgamesh na Samsoni vilevile wanafunga safari halisi inayosuka hadithi yenye visa mbalimbali katika UFL, UMM, UG na SS.

Hatua ya Kivuko cha Kizingiti imewasawiri wahusika Fumo Liyongo, Mikidadi, Gilgamesh na Samsoni wakiwa na vizuizi kadha vilivyoelekea kutinga safari zao. Wasiwasi inatanda miongoni mwa mashujaa na vilevile hadhira iwapo shujaa ataweza kukabiliana na hatari inayomzonga. Hata hivyo, wote wanafaulu na kila mmoja kuendelea na safari aliyokuwa ameianza.

Hatua ya Tatizo katika UFL, UMM, UG na SS imeonyesha kwamba wahusika wakuu katika matini wanakumbana na changamoto nyingi katika safari zao. Kwa mfano, Fumo Liyongo anadungwa sindano ya shaba kitovuni na mwanawe, Mikidadi anapigana na jeshi kubwa, simba na hata jini. Gilgamesh anakabiliana na Humbaba (Fahali Mkali) huku Samsoni akishikwa na kufungwa mikono na Wafilisti kwa nia ya kuuawa. Isipokuwa Fumo Liyongo, wote wanaepuka kifo kilichokuwa kimewaandama. Hatua hii ya Tatizo imefichua nguvu za kiajabu zinazomilikiwa na kila shujaa katika matini teule. Aidha, hadhira inahadaiwa kufikiria kwamba hatua hii ni kilele cha igizo ingawa sivyo.

Hatua ya Ufufuo ni kilele cha safari ya shujaa. Katika hatua hii, shujaa anatarajiwa kukamilisha duara ya safari yake. Hatua ya Ufufuo ya shujaa Liyongo inafika mwisho kwa kuuawa na mwanawe na kufia kisimani. Hata hivyo, kifo chake kisimani ni ishara ya kijazanda kwamba ingawa Liyongo amekufa, 'anaishi' miongoni mwa jamii hasa ikichukuliwa kuwa maji ni ishara ya uhai. Hatua ya ufufuo katika UMM inaishia kwa furaha kwa sababu Mikidadi na Mayasa wanafaulu

kufunga ndoa baada ya Mikidadi kuepushwa na kifo kilichopangwa na mahasidi wake, Jabiri na Maliki. Safari ya Gilgamesh inafikia mwisho baada ya kukabiliana na changamoto nyingi. Gilgamesh anarudi katika ulimwengu wake wa kwanza baada ya kupoteza dawa ambayo ingemwezesha kuishi milele. Anarudi katika nchi yake akiwa na ujuzi mpya ambao alitumia kwa manufaa ya watu wa nchi ya Uruk.

Katika hatua ya Ufufuo, kuna uwiano wa matukio katika UFL na SS. Fumo Liyongo katika UFL anapatikana amekufa karibu na kisima baada ya kudungwa sindano ya shaba na mwanawe. Samsoni katika SS anakufa pamoja na watu wengi waliokuwa katika jengo alimokuwa amefungiwa, kukejeliwa na kuteswa kwa sababu ya nguvu zake zilizokuwa zimeisha. Tofauti na UFL na SS, Mikidadi katika UMM anakamilisha duara ya safari yake kwa furaha. Hivyo, Mikidadi na Gilgamesh wanakamilisha duara ya safari zao kwa kurudi katika jamii zao huku Fumo Liyongo na Samsoni wakikamilisha safari zao kupitia mauti.

6.6 Hitimisho

Katika sura hii, tumeonyesha maingiliano ya motifu ya safari katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni*. Matini teule zimeonyesha kuwa na ruwaza ya urudiaji wa kikale cha safari. Katika utafiti huu, tumezifinyanga hatua kumi na mbili katika motifu ya safari ya shujaa na kuzijadili hatua hizo ndani ya hatua nne kuu ambazo ni Hatua ya Mwanzo wa Safari, Kivuko cha Kizingiti, Tatizo na Hatua ya Ufufuo. Tumeonyesha ulinganifu wa hatua hizi kwa kuzingatia matendo ya wahusika wakuu ambao ni Fumo Liyongo katika UFL, Mikidadi katika UMM, Gilgamesh katika UG na Samsoni katika SS.

Motifu ya safari katika UFL, UMM, UG na SS inaonyesha ulinganifu wa kimwingilianomatini. Safari halisi inayodhihirika katika kila utenzi inabainisha safari

kama moja kati ya vikale vinavyotajwa na Carl Jung katika nadharia ya vikale. Wahusika wakuu wanadhihirisha kuwa na safari halisi katika maisha yao ya kishujaa. Kila mmoja wao anajihusisha na safari inayoanza utotoni hadi kufa kwake, huku wakidumisha hatua za kimsingi zinazobainika katika motifu ya safari ya shujaa. Mbali na kubainisha kuwa matini teule zinasawiri ubia wa kikale cha safari, kuna mwingiliano wa kimatini katika visa vya safari za mashujaa katika UFL, UMM, UG na SS. Sura ya saba inahusu muhtasari wa tasnifu, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

SURA YA SABA

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

7.0 Utangulizi

Sura ya sita ilishughulikia mwingilianomatini katika UFL, UMM, UG na SS kwa kuzingatia motifu ya safari iliyodhihirika katika matini husika. Katika sura hii tumeangazia muhtasari wa tasnifu kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti, kutoa hitimisho ya utafiti na hatimaye kutoa mapendekezo ya utafiti huu.

7.1 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii imegawanywa katika sura saba. Utafiti ulichunguza mwingilianomatini katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni*. Sura ya kwanza ilitupa msingi wa masuala yote yaliyoibuliwa katika utafiti huu. Masuala haya yalijadiliwa kwa kuzingatia mada ya utafiti ya kuonyesha mwingilianomatini katika matini zilizoteuliwa.

Katika sura ya pili mtafiti ameonyesha mapitio ya maandishi na nadharia iliyoongoza utafiti. Sehemu hii ilianguzia maandishi mbalimbali yaliyoana na mada pamoja na malengo ya utafiti. Maandishi yaliyoandikwa kuhusu usimulizi katika tenzi, sifa za wahusika wakuu na kikale cha safari yalichunguzwa. Nadharia za mwingilianomatini na nadharia ya vikale ndizo zilizotumika katika uhakiki wa kazi hii.

Sura ya tatu imejadili mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti ikiwa ni pamoja na eneo la utafiti, ukusanyaji wa data, sampuli, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Kazi mahususi zilizochunguzwa katika utafiti huu ni *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni*, ambapo tulikusanya data kutoka katika matini hizi. Data iliyohakikiwa imeonyeshwa katika kurasa za viambatisho vya utafiti huu.

Katika sura ya nne tulifafanua mwingilianomatini unavyodhihirika kisimulizi katika *Utenzi wa Fumo Liyongo, Utenzi wa Mikidadi na Mayasa, Utenzi wa Gilgamesh na Simulizi ya Samsoni*. Tulihakiki mwingiliano wa kisimulizi kwa kuzingatia vipengele vya mtiririko wa matukio katika mbinu za kisimulizi kama vile usimulizi wa nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu. Aidha, tulionyesha mwingiliano katika muundo na matumizi ya lugha katika UFL, UMM, UG na SS. Katika muktadha huu, mwingiliano wa kisimulizi katika matini zilizohakikiwa ulibainishwa.

Sura ya tano ilihusu uchanganuzi wa kina wa sifa za wahusika wakuu katika UFL, UMM, UG na SS. Mtafiti alionyesha mwingilianomatini baina ya wahusika wakuu. Utafiti ulionyesha kuwa kuna ulinganifu wa sifa za wahusika wakuu, ambao ni Fumo Liyongo, Mikidadi, Gilgamesh na Samsoni katika miktadha mbalimbali. Katika sura hii vilevile tulichunguza athari ya mwanamke kama mhusika katika matini zilizohakikiwa. Ilibainika kwamba mwanamke kama mhusika mjenzi anaathiri pakubwa hulka na maisha ya mhusika mkuu katika matini teule. Katika sura hii, vilevile, tulichanganua mwingiliano wa sifa ya kitanzia katika UFL, UMM, UG na SS. Ni katika muktadha wa sura hii ambapo mihimili ya nadharia ya mwingilianomatini ilizidi kudhihirika katika UFL, UMM, UG na SS.

Sura ya sita ilihakiki mwingiliano wa kikale cha safari katika UFL, UMM, UG na SS. Ilibainika kwamba kuna urudiaji wa kikale cha safari ya shujaa katika matini teule. Ubia wa kikale cha safari ya shujaa unadhihirika katika visa vya wahusika wakuu hivyo kuleta maingiliano katika ruwaza ya motifu ya safari katika UFL, UMM, UG na SS. Iidhihirika kwamba urudiaji wa kikale cha safari ni kipengele kingine kilichosababisha mwingilianomatini katika matini teule za utafiti huu. Sura ya saba

ndiyo sehemu ya mwisho ya utafiti huu na imeshughulikia muhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

7.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulihusu uhakiki wa mwingilianomatini katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi za Samsoni*. Utafiti umeonyesha kuwa mwingilianomatini unadhihirika katika vigezo vya usimulizi, uhusika na kikale cha safari. *Utendi wa Fumo Liyongo* na *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* ni tenzi zilizotungwa katika miktadha ya jamii za Kiafrika. *Utendi wa Gilgamesh* una misingi yake katika jamii ya Wababiloni huku *Simulizi ya Samsoni* imeibuliwa katika miktadha ya jamii ya Waisraeli. Licha ya tofauti za misingi ya kijamii, matini zilizohakikiwa zinaonyesha ulinganifu katika usimulizi, usawiri wa wahusika wakuu na kigezo cha kikale cha safari ya shujaa.

7.2.1 Mwingiliano wa Kisimulizi katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni*

Kuhusu mwingilianomatini wa kisimulizi ulivyojitokeza, utafiti umebainisha kuwa ingawa watunzi wa kazi teule wamekulia katika mazingira tofauti, utunzi wao unashabihiana kwa kiwango fulani. Utafiti umebainisha kuwa visa vya kiajabuajabu vinasimuliwa katika matini. Kuna mtiririko wa matukio ya kiajabu yanayotokea katika UFL, UMM, UG na SS. Jambo hili ndilo linalopelekea tungo teule kusemwa kuwa ni za kisimulizi. Aidha, mbinu zilizotumika katika usimulizi wa visa katika matini teule zinashabihiana. Utafiti ulibainisha kuwa mbinu za usimulizi wa nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu zilitumika katika kazi zote. Mbinu nyingine zilizotumika katika usimulizi ni usimulizi wa ki-utendi na usimulizi maizi. *Simulizi ya Samsoni* imechukuliwa kama moja ya simulizi za ki-utendi katika Biblia hivyo kudhihirisha mwingilianomatini katika kazi za fasihi na matini teule ya kidini katika utafiti huu.

Katika kiwango kingine, mwingiliano wa kimuundo unabainika katika UFL, UMM, UG na SS. Muundo unaingiliana katika tungo hizi hivi kwamba tangulizi, msuko wa hadithi na miisho ya matini teule ilifanana. Katika UFL na UMM, mianzo yao inatambua ukuu na uwezo wa Mwenyezi Mungu katika utunzi. Tofauti inaonekana katika tangulizi za UG na SS. Matini hizi zinatanguliza hadithi kwa kutaja sifa za uungu za wahusika wakuu, Gilgamesh na Samsoni mtawalia. Desturi ya Waislamu kulitanguliza jina la Mwenyezi Mungu kabla ya kulifanya jambo lolote inawiana na Wakristo. Hata hivyo, mtindo wa kutaja Utatu wa Mungu (Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu), hutumika hasa katika mwanzo wa sala za Wakristo.

Utafiti ulibainisha kuwa dhamira za watunzi wa UFL, UMM, UG na SS zinaingiliana. Watunzi wanaweka wazi madhumuni yao ya kusimulia visa vya ajabu. Ni ugunduzi wa utafiti huu kuwa msuko na mpangilio wa matukio yanayopatikana katika visa vilivyosimuliwa huwiana. Vilevile, muundo wa tungo teule huingiliana hivi kwamba tangulizi, msuko ya hadithi na hitimisho za matini teule zinalingana. Tangulizi za UFL na UMM zimetaja ukuu wa Mungu katika utunzi wa tenzi ilhali UG na SS zimetoa sifa za wahusika wakuu na jinsi walivyo tofauti na wanadamu wa kawaida. Katika kiwango cha matumizi ya lugha, mwingiliano wa kimatini hudhihirika katika vipengele kama vile tashbihi, sitiari, maswali ya balagha na taswira. Kwa mfano, kuna ulinganisho wa wahusika wakuu na wanyama kama vile simba na fahali ambao unadhihirika katika matini zote. Katika UFL, Fumo Liyongo amelinganishwa na simba (*Ni mwanamume swahihi, kama simba una zihi*) katika ubeti 13, ukurasa 24. Katika UMM, Mikidadi amefananishwa na simba na hali kadhalika yeye mwenyewe anasema kwamba yeye ni simba (*Ni mimi simba wa mwituni*) (ubeti 295).

Katika SS, Samsoni hajafananishwa na simba ila yeye mwenyewe anamwua simba kwa kumrarua akitumia mikono yake (Waamuzi 14:5-6). Katika UG, Gilgamesh amelinganishwa na fahali mkali wa kuogofya (Kibao I: 1). Utafiti huu umebaini kwamba mwingilianomatini wa kisimulizi katika UFL, UMM, UG na SS umesababishwa na miktadha ya kijamii na mitindo ya kisimulizi ya watunzi husika.

Kwa mujibu wa utafiti huu, mjadala ulioendelezwa kuhusiana na mwingilianomatini katika UFL, UMM, UG na SS umedhihirisha kuwa matini za kifasihi zinategemeana na kukamilishana. Matini teule zimeonyesha kuwa kuna vipengele kadha ambavyo vinaingiliana hivyo kubainisha kuwa kuna mwingilianomatini baina yazo. Kutokana na utafiti huu, tuligundua kuwa kuna mwingilianomatini katika vipengele vya usimulizi, uhusika na kigezo cha kikale cha safari ya shujaa.

Ingawa usimulizi umehusishwa zaidi na kazi za kinathari katika fasihi, tenzi zilizohakikiwa zimedhihirisha usimulizi kwa kuhusisha visa vyenye matukio ya kiajabu. Hivyo, kilichobainika ni kwamba visa vya kiajabu katika UFL, UMM, UG na SS vilisababisha matini hizi kuwa za kisimulizi. Hii ni kwa sababu hakuwezi kukatokea usimulizi pasipo kisa ama hadithi ya kusimuliwa. Aidha, mbinu za kisimulizi, muundo wa uandishi na matumizi ya lugha katika matini teule yanashabihiana hivyo kuwa na mwingiliano wa kimatini. Iwapo jamii ya sasa itatilia maanani kazi za kale kama vile *Tenzi za Fumo Liyongo*, *Mikidadi na Mayasa*, *Gilgamesh* na *Simulizi ya Samsoni* basi itajifunza mengi kutokana na sanaa hii muhimu.

7.2.2 Mwingiliano wa Wahusika Wakuu katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh na Simulizi ya Samsoni*

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa kuonyesha sifa za wahusika wakuu katika UFL, UMM, UG, na SS. Utafiti ulizingatia hulka na sifa mbalimbali za kila mhusika mkuu. Sifa zao zinashabihiana katika miktadha mbalimbali. Kwanza kabisa, wahusika hao wamesawiriwa kuwa viongozi waliotajika katika jamii zao. Kwa mfano, Fumo Liyongo katika UFL anasifiwa na jamii yake kuhusiana na uongozi wake, jambo linalomkera Sultani na kupanga kumwua Liyongo. Haya yamefafanuliwa katika beti 51 na 93. Katika UG, Gilgamesh amesawiriwa kuwa kiongozi, japo aliyewadhulumu watu wake. Hata hivyo, Utendi unamwonyesha Gilgamesh kama kiongozi aliyeheshimika katika jamii yake. Samsoni katika SS ni kiongozi aliyeteuliwa na Mwenyezi Mungu hata kabla ya kuzaliwa kwake. Mikidadi kwa upande wake alisifika kama kiongozi kupitia jitihada zake za kumchukua Mayasa kuwa mkewe.

Kuhusu sifa ya ushujaa, utafiti umethibitisha kuwa wahusika Fumo Liyongo, Gilgamesh, Mikidadi na Samsoni, wote walikuwa mashujaa katika nyakati zao. Ushujaa huo, vilevile, uliandamana na maumbile yao hivi kwamba walikuwa ‘majitu’. Visa vyao vinawasawiri kama mashujaa waliofanya mambo makuu katika jamii. Kwa mfano, Gilgamesh akisaidiana na rafiki yake Enkidu anamwua Humbaba, mlinzi hodari wa msitu wa Seda. Mbali na matukio mengine, ushujaa wa Fumo Liyongo nao ulidhihirika alipofananishwa na mnyama simba na kwamba kutembea kwake usiku na mchana kulikuwa sawa, giza kwake halikumfanya awe mwoga wa kutembea usiku. Mikidadi kwa upande wake anapambana na luhani (jini) na hatimaye anamwua huku Samsoni akimrarua simba kwa mikono yake. Yote haya yanaonyesha sifa ya ushujaa miongoni mwa wahusika.

Ingawa Fumo Liyongo hajaonekana kuwa na ukatili katika UFL, utafiti ulibainisha kuwa wahusika wakuu, Gilgamesh katika UG, Mikidadi katika UMM na Samsoni katika SS wote wana sifa ya ukatili. Wao wanaua halaiki ya watu pasipo na huruma. Isitoshe, wahusika hao wanafurahia na kujigamba baada ya kuuu. Majigambo baina ya wahusika wakuu Fumo Liyongo, Mikidadi, Gilgamesh na Samsoni ni sifa inayobainika katika matini zote teule, UFL, UMM, UG na SS.

Utafiti huu vilevile umejadili kuhusu athari ya mwanamke kama mhusika mjenzi katika matini teule. Mwanamke kama mhusika katika matini zilizohakikiwa ameonyeshwa kuwa na athari kuu katika maisha ya wahusika wakuu. Katika UFL na UMM, athari ya mwanamke kama mhusika ni chanya ilhali athari katika UG na SS ni hasi. Mwanamke kama mhusika ameathiri mhusika mkuu katika matini teule, kwa njia hasi ama chanya. Hivyo, ni muhimu kila wakati kuchunguza kwa makini nafasi ya mwanamke katika kazi yoyote ya fasihi. Katika UFL, mama yake Fumo Liyongo na kijakazi Saada wanachangia katika kumwezesha Liyongo kutoroka gerezeni. Mama yake Mikidadi vilevile katika UMM anachangia katika kumwokoza Mikidadi kusudi asiuliwe na Jabiri. Mayasa aidha katika UMM ni mwanamke shujaa ambaye anakuwa pia kichocheo cha ushujaa wa Mikidadi.

Maisha ya Gilgamesh na Enkidu katika UG yanaathiriwa pakubwa na wahusika wanawake. Ninsun, mama yake Gilgamesh anamwelekeza mwanawe katika njia iliyofaa. Ninsun ni mwanamke mwenye hekima ambaye anasikiliza ndoto za Gilgamesh na kumfunulia maana. Hatimaye, anamlinda mwanawe asiuliwe baada ya kumwua Humbaba. Ninsun anawashawishi miungu wenzake (yeye pia alikuwa mmoja ya miungu) wasimwue Gilgamesh bali Enkidu, “*Let Enkidu die but Gilgamesh must not die!*” (Tablet VII:25). Hivyo, Ninsun anasimama kama mlinzi wa mtoto

wake. Shamhat ni mwanamke kahaba aliyemfanya Enkidu kujua mambo ya ngono ambapo aliwacha kuishi na wanyamapori na kuanza maisha ya ubinadamu. Shamhat ndiye aliyemfanya Enkidu kujuana na Gilgamesh hivyo kusababisha hatima ya kufa kwake.

Katika SS, wanawake watatu wanaoonekana katika maisha ya Samsoni wametajwa, nao ni Mtimna, wa pili akitajwa tu kama Kahaba (Waamuzi 16:1-2) na wa tatu Delila. Wanawake hao wanatumika katika kumwangusha Samsoni. Mapenzi yao ya kinafiki yanamfanya Samsoni kushikwa na kuhangaishwa na Wafilisti. Mtimna ndiye aliyechangia hasira za Samsoni hadi akachoma mashamba ya Wafilisti. Delila naye ndiye anayefaulu kumshawishi Samsoni hata akafunuliwa siri za nguvu zake. Hatimaye anawaita wakuu wa Wafilisti ambao wanamteka nyara Samsoni. Inabainika kwamba Mtimna na Delila walichangia pakubwa katika anguko la Samsoni.

Sifa nyingine inayosababisha mwingilianomatini katika UFL, UMM, UG na SS ni sifa ya kitanzia. Fumo Liyongo, Gilgamesh na Samsoni wanakufa kutokana na uzembe na udhaifu unaolingana ama kufanana. Kwa mfano, Fumo Liyongo anamtobolea mwanawe siri ya kile kinachoweza kumwua. Samsoni vilevile anapumbazwa na Delila ambaye hatimaye anagundua siri ya chanzo cha nguvu zake hivyo kufanya njama ya kumnasa na hatimaye kufa mikononi mwa Wafilisti. Gilgamesh kwa upande wake anajuta kwa sababu ya uzembe wake baada ya kupoteza uzima wa milele na badala yake nyoka kunufaika na dawa alizopewa. Gilgamesh basi anahangaika na kujuta kwa kutokamilisha azma yake ya kutafuta maisha ya milele. Tofauti na UG, UFL na SS, tanzia-ramsa inadhihirika katika UMM. Ingawa anafanyiwa njama ya kuuliwa, Mikidadi anashinda kwa kuwaua mahasidi wake, Jabiri na Maliki. Mikidadi anaokolewa na anaishi kwa raha na mpenzi mke wake Mayasa.

Kwa jumla, mwingilianomatini katika kipengele cha sifa za wahusika wakuu katika UFL, UMM, UG na SS unabainika. Utafiti ulibainisha kuwa wahusika wakuu katika UFL, UMM, UG na SS wanasawiri sifa zinazoelekea kufanana. Wahusika Fumo Liyongo, Mikidadi, Gilgamesh na Samsoni wamesawiriwa kama watu wenye nguvu za kiajabu, yaani majitu na wenye kutenda mambo ya kuogofya. Wahusika hao walichukuliwa kuwa mashujaa katika jamii zao. Aidha, walikuwa viongozi katika enzi zao. Hata hivyo, utafiti umebainisha kuwa wahusika hao walikuwa katili na wenye kujigamba katika uongozi wao.

7.2.3 Mwingiliano wa Kikale cha Safari katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh na Simulizi ya Samsoni*

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa kuhakiki maingiliano ya motifu ya safari kama kigezo muhimu kinachodhihirika katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh na Simulizi ya Samsoni*. Utafiti huu ulionyesha kuwa kuna mwingiliano wa kikale cha safari katika matini teule. Kazi tulizozirejelea zinasawiri wahusika wakuu kama mashujaa katika jamii zao. Matukio yanayozungukia maisha yao yanahusisha safari halisi inayofungwa kuelekea mahali fulani na kila mmoja wa wahusika wakuu katika matini teule.

Watunzi wa kazi husika wameonyesha kuwa jamii kote ulimwenguni zina ubia katika sifa za kibinadamu. Kila jamii ina ngano zake za majitu na kishujaa ambazo zinapokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mtagusano baina ya wanadamu vilevile husababisha simulizi mbalimbali kuenea katika jamii tofautitofauti. Utafiti huu umebainisha kuwa mwingilianomatini katika kikale cha safari umetokana na ubia wa ishara zilizoenea na kutambulika katika kazi za kisanii na jamii za binadamu kote ulimwenguni. Aidha, utafiti umedhihirisha kuwa Biblia inaweza kutumika kama

matini rejea katika kazi za kifasihi. Tunaamini kwamba tumetimiza malengo yote matatu ya utafiti huu hivyo kutoa mchango wa kitaaluma katika fasihi ya Kiswahili.

Utafiti huu ulibainisha kuwa tungo za kifasihi huingiliana, huhusiana na kutegemeana ili kuzalisha maana. Utafiti umebainisha kuwa mwingiliano wa kisimulizi katika UFL, UMM, UG na SS unadhihirika. Ilibainika kwamba visa vya Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh na Samsoni vinaonyesha mwingiliano wa matini kwa kuzingatia mtiririko wa matukio yanayotokea katika matini teule. Aidha, utafiti ulibainisha kwamba binadamu kote ulimwenguni wana ruwaza za kvikale zinazofanana. Hivyo, motifu ya kikale cha safari ya shujaa inayorudiwarudiwa katika UFL, UMM, UG na SS ni ishara ya vikale bia vilivyoenea na kutambulika katika kazi za kisani. Kwa sababu hii, ilibainika kwamba hakuna matini yoyote ya kifasihi inayoweza kuangaliwa peke yake na kwa kujitegemea.

Ni dhahiri kuwa matini zilizohakikiwa ni za kale mno. UFL, UMM, UG na SS zinaangazia hali ya maisha yalivyokuwa wakati huo. Hata hivyo, matini teule zina mafunzo ambayo yanapita mipaka ya nyakati za ukale na usasa. Ni muhimu kuelewa kuwa hakuna ukongwe katika mafundisho tunayoyapata katika kazi za kifasihi. Kwa misingi hii, kizazi cha Karne ya Ishirini na Moja, kinapewa changamoto kuchunguza na kujinufaisha kutokana na mafundisho yanayopatikana katika kazi hizi za kijadi.

7.3 Hitimisho

Utafiti huu umebainisha kwamba mwingilianomatini unadhihirika katika *Tenzi za Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa, Gilgamesh na Simulizi ya Samsoni* katika vipengele vya usimulizi, wahusika na kikale cha safari. Utafiti umeonyesha kuwa visa vya kiajabu vinavyowasilishwa katika UFL, UMM, UG na SS vinasababisha

usimulizi katika matini teule. Aidha, kuna mwangwi unaohisika katika vipengele vya wahusika wakuu na kigezo cha kikale cha safari.

Utafiti huu una mchango mkubwa katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili. Tasnifu inaongezea maandishi ya kitaaluma yanayohusu mwingilianomatini katika tenzi. Wapenzi, wasomaji na hasa wahakiki wa mashairi kwa jumla watanufaika katika kuzielewa mada za usimulizi, uhusika na kigezo cha vikale katika ushairi. Utafiti huu ni rejea muhimu kwa kazi na tafiti za baadaye zinazohusiana na tenzi mbalimbali.

Aidha, inasadikika kutaja kwamba baadhi ya maandishi ya Biblia kama vile *Simulizi ya Samsoni* yamechangia katika ukuaji wa kazi za kifasihi katika Kiswahili. Kwa kuongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini na Vikale, imebainika kwamba *Biblia* ina fasihi inayohitaji kuhakikiwa zaidi ili kurutubisha fasihi ya Kiswahili.

Utafiti huu ni mchango kwa kizazi cha Karne ya 21 kuelimika kutokana na mafunzo yapatikanayo katika matini teule ambazo ni baadhi ya kazi za kijadi. Mabadiliko ya kijamii na ujio wa utandawazi umesababisha asasi muhimu katika tamaduni za Kiafrika kusahaulika. Utafiti huu umeonyesha kuwa kazi za kijadi kama vile tenzi zina mafunzo muhimu hivyo zinahitaji kuhifadhiwa kwa kuzifanyia utafiti.

7.4 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu umeonyesha kuwa kazi zilizohakikiwa zinaingiliana na kuathiriana hivyo kuwa na mwingilianomatini. Vipengele vilivyochunguzwa vilihusu usimulizi, sifa za wahusika wakuu na kikale cha safari. Ni muhimu kutambua kuwa kuna vipashio vingi ambavyo vinahitaji kufanyiwa utafiti zaidi kimwingilianomatini, navyo ni vipashio kama vile maudhui na dhamira.

Mwingiliano wa kisimulizi katika UFL, UMM, UG na SS ulidhihirisha msuko wenye matukio ya kiajabu hivyo kuhalisi usimulizi. Pendekezo letu ni kuwa tafiti za baadaye

zizingatie usimulizi katika tenzi kwa kutumia nadharia kama vile naratolojia ili kuhusisha vipashio vingi katika usimulizi. Kwa kutumia nadharia ya Naratolojia, vipashio kama vya kiwakati, kitendo cha usimuliaji, hadithi na msuko vinaweza kuangaziwa kwa kina.

Ingawa utafiti huu ulishughulikia sifa za wahusika, ni wahusika wakuu hasa walioangaziwa. Utafiti ulichunguza sifa za wahusika wakuu peke yake na kuonyesha namna walivyofanana na kulingana. Wahusika na uhusika ni mada pana ambayo inaweza kuchunguzwa zaidi katika matini teule. *Utenzi wa Gilgamesh*, kwa mfano, una wahusika wengi baadhi yao wakiwa miungu, hivyo utafiti unaweza kufanywa ili kuchunguza sifa na taathira ya uungu.

Ingawa matini zilizohakikiwa ni za jadi, kuna mambo mengi ambayo tunaweza kujifunza. Tenzi nyingi zinaeleza historia ya jamii husika. Ni pendekezo la utafiti kuwa matini zilizotafitiwa zichunguzwe ili kuangazia kwa undani masuala ya kihistoria na kijamii. Kupitia katika *Simulizi ya Samsoni*, utafiti huu ulibaini kuwa *Biblia Takatifu* ina vipashio vingi vya fasihi ambavyo vinaweza kuhakikiwa na kulinganishwa na matini nyingine za kifasihi.

MAREJELEO

Vitabu

- Abdulaziz, H. M. (1979). *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Poetry*. Nairobi: KLB
- Allen, G. (2000). *Intertextuality*. New York: Routledge.
- Allen, J.W.T (1971). *Tendi: Six examples of a Swahili classical verse form with translations and notes*. Nairobi: Heinemann.
- Barker, K.L. (Ed.) (1973). *New International Study Bible*. Michigan: USA.
- Bashir, A. (1972). *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Nairobi: Heinemann Educational Books
- Biblica-Africa. (2015). *Neno: Biblia Takatifu*. Nairobi: Biblica Inc.
- Bradley, A. (2008). *Derrida's of Grammatology: An Edinburgh Philosophical Guide*. Edinburgh University Press.
- Campbell, J. (1949). *The Hero with Thousand Faces*. Pantheon Books, USA
- Campbell, J. (2008). *The Hero with Thousand Faces*(3rd Ed.). Novato, C.A: New World Library.
- Cuddon, J. A. (1997). *A Dictionary of Literary Terms* (4th Ed.). New York: Penguin.
- Davidson, A.B (2011). *Biblical and Literary Essays*. London: Hodder and Stoughton.
- Dobie, A. (2002). *Theory into Practice: An Introduction to Literary Criticism*. New York: Thomson Heinle.
- Dorsch, T. (1965). *Aristotle, Poetics Aristotle/Horace/Longinus: Classical Literary Criticism*. Harmondsworth: Penguin.
- Eagleton, T. (1983). *Literary Theory: An Introduction*. Cambridge: Blackwell.
- Eliade, M. (1959). *The Sacred and the Profane*. Harcourt: Harcourt Books Inc. USA.
- Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Oxford: Oxford Library of African Literature.
- Fludernik, M. (2009). *An Introduction to Narratology*. London: Routledge.
- Gabel, J. (1996). *The Bible as Literature: An Introduction*. Oxford: Oxford University Press.
- Genette, G. (1980). *Narrative Discourse*. New York: Cornell University Press.
- George, A .(2002). *The epic of Gilgamesh: The Babylonian Epic poem and other texts in Akkadian and Sumerian*. Penguin Publishers.

- Heidel, A. (1949). *The Gilgamesh Epic and Old Testament Parallels*. Chicago: The University of Chicago Press.
- Henderson, L. (2013). Folk Belief and Scottish Traditionl Literatures, in S. Dunningan, and S. Gilbert (eds). *The Edinburgh Companion to Scottish Literature*. Edinburg University Press pp. 26-34.
- Jahadhmy, A. (1975). *Anthology of Swahili Poetry*. Nairobi: Heinemann.
- Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Company.
- Jung, C.G. (1972). Translated by Hull, R.F.C. (2017). *Mandala Symbolism*. Princeton: Princeton University Press
- Jung, C.G. (1959). *Archetypes of the Collective Unconciuous*. London:Uk.Routedge B. Kegan Paul.
- King'ei, K. G., & Kisovi, C. N. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Knappert, J. (1992). *Utenzi wa Kalevala (The Kalevala)*. Dar es Salaam: TUKI.
- Kombo, D., & Tromp, D. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Paulines Publications Africa.
- Kovacs, M. G. (1998). *The epic of Gilgamesh*. Toronto: Stanford University Press.
- Kristeva, J. (1980). *Desire In Language:A Semiotic Approach to Literature and Art*. New York: Columbia University Press.
- Kristeva, J. (1986). *Word, Dialogue and Novel, In: Toril Moi ed. The Kristeva Reader*. Oxford: Blackwell, uk. 35-61.
- Madumulla, S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Mazrui, A.M., & Syambo, B.K. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mbogo, E. (2009). *Fumo Liongo*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Metzger, B., & Coogan, M. (1993). *The Oxford Companion to the Bible*. Oxford University Press.
- Mulokozi, M. M. (2002). *The African Epic Controversy: Historical, Philosophical and Aesthetic Perspectives on Epic Poetry and Performance*, Dar es Salaam: Mkuki Na Nyota Publishers.
- Mulokozi, M.M. (Mh.) (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.

- Mutembei, A. (2012). *Korasi katika Fasihi: Nadharia Mpya ya Uhakiki*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mwaruka, R. (1976). *Utenzi wa Jamhuri ya Tanzania*. Dar es Salaam: EALB.
- Mwita, M. B. (2017). Uhakiki wa Taswira ya Mwanamke kama Chombo na Kitega Uchumi Katika Ichingero za Wakuria katika Lugha na Fasihi Katika Karne ya Ishirini na Moja. Eldoret: Moi University Press, uk. 187-197.
- Nabea, W., Mwangi, J.N., & Mayaka, G. (2017). Matendo ya Wahusika Wakuu katika Tendi za Kiswahili: Ushujaa au Uhayawani? katika Lugha na Fasihi Katika Karne ya Ishirini na Moja. Eldoret: Moi University Press, uk. 101-111.
- Njogu, K., & Wafula, R. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Njogu, K., na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Raglan, L. (1956). *The Hero*. New York: New American Library Inc.
- Ruo, K.R. (1989). *Nguzo za Ushairi wa Kiswahili*. Nairobi: Macmillan.
- Schmitz, T.A. (2007). *Modern Literary Theory and Ancient Texts: An Introduction*. Malden: Blackwell Publishing.
- Shitemi, N. L. (2010). *Ushairi wa Kiswahili Kabla ya Karne ya Ishirini*. Eldoret: Moi University Press.
- Sofokile, S. M. (1969). *Mfalme Edipode*. (Tafsiri ya S. Mushi). Nairobi: Oxford
- Soseleje, M. (1946). *Safari ya Msafiri*. (Tafsiri ya Pilgrims Progress). Dodoma: Central Tanganyika press.
- Thomas, I. B. (1930) *The Autobiography of Segilola: The Lady with the Delicate EyeBalls*. Lagos: C. M. S Bookshops.
- Unger, M. F. (1967). *Unger's Bible Handbook: An Essential Guide to Understanding the Bible*. Chicago: Moody Press.
- Vogler, C. (2007) (3rd ed.). *The Writer's Journey: Mythic Structure for Writers*. Studio City: Michael Wiese Productions, USA.
- Wafula, R. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wafula, R., na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Walvoord, J.F., & Zuck, R.B (Ed.) (1985). *The Bible Knowledge Commentary: An Exposition of the Scriptures*. Dallas Seminary Faculty, Canada SP Publications.

- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
- Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications.

Tasnifu

- Achieng, O. B. (2012). Sifa za Mashujaa na Umuhimu Wao kwa Jamii Zao: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Lwanda Magere. *Tasnifu ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Arege, T I. (2012). *Narration In Swahili Narrative Poetry: An Analysis of Utenzi wa Rasi'Lghuli*. *Tasnifu ya Uzamifu (Phd)*, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Clemence, S. M. (2015). Kuchunguza Mbinu za Kitanzia za ki-Aristotle katika Tamthilia za Fumo Liyongo na Sundiata. *Tasnifu ya Uzamili*, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Gathara, F. K. (2015). *Taswira ya Jagina Katika Tendi: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Nabii Isa*. *Tasnifu ya Uzamili*, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).
- Gimode, J. (2006). *The Language of The Church*. *Tasnifu ya Uzamili*, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).
- Kyamba, A.N. (2018). *Mchango wa Mathias Mnyapala Katika Maendeleo ya Ushairi wa Kiswahili*. *Tasnifu ya Uzamifu*, Chuo Kikuu cha Moi (Haijachapishwa).
- Mningo. R. (2015). Mwingilianomatini katika Utunzi wa Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Tamthilia ya Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liyongo. *Tasnifu ya Uzamili*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
- Omboga, J. Z. (2006). *Siting Text, Culture, Context and Pedagogy in Literay Translation: A Theorization of Translation in Cultural Transfer with Examples from Selected Texts in Kiswahili*. *Tasnifu ya Uzamifu*, Chuo Kikuu cha Kenyatta, (Haijachapishwa).
- Shitemi, N. L. (1997). *Uaminifu Katika Tafsiri: Uhakiki wa Tafsiri za Ushairi wa Jadi wa Kiswahili: Utenzi wa Inkishafi, Utenzi wa Mwanakupona na Mashairi ya Muyaka*. *Tasnifu ya Uzamifu*, Moi University. (Haijachapishwa).

Tuglu, U. (2011). A Bakhtinian analysis of William Goldings Rites of Passage: Heteroglossia, Polyphony and the Carnavalesque in the Novel (M.A. Thesis). Middle East Technical University.

Majarida

Burundi, R.N. (2014). Usimulizi katika Utenzi wa Swifa ya Nguvumali katika *Kioo cha Lugha* Vol. 12. No.1 pp. 73-87.

Davidson, J. (1993). Bakhtin as a Theory of Reading. Illinois: University of Illinois, Centre For the Study of Reading, Technical Report No. 579.

De Villiers, G. (2006). The Epic of Gilgamesh and the Old Testament: Parallels beyond the Deluge in Old Testament Essays, Vol.19 (1), 26-34.

Gijo, D., & George, K. (2021). Archtypal Criticism: A Brief Study of the Discipline and the Sempiternal Relevance of its Pioneers. *International Journal of English Literature and Social Sciences* Vol.6.No.2pp. 054-060.

Kehinde, A. (2003). Intertextuality and the Contemporary African Novel. *Nordic Journal of African Studies* Vol.12 (3) uk.372-386.

Kwame, S, F. (2013). Ruwaza za Shujaa na Uibuaji wa Dhamira: Mifano kutoka *Utendi wa Gilgamesh Katika Kiswahili Juzuu* Na. 76 uk: 1-13.

Mohochi, E.S (2000). Usimulizi wa Riwaya ya Nyongo Mkalia Ini katika *Nordic Journal of African Studies* vol.9 (2) uk.44-59.

Mwamzandi, I. (2013). Riwaya Teule za Karne ya Ishirini na Moja na Udurusu wa Nadharia za Fasihi, Katika *Swahili Forum* 20. uk 48-66.

Raj, P.E (2015). Text/Texts: Interrogating Julia Kristeva's Concept of Intertextuality" In *Ars Artium: An International Peer Reviewed-Cum-Refereed Research Journal of Humanities and Social Sciences*. Vol.3, uk. 77-80.

Wanyama, A. Chimerah, R.M., Karisa, B.S. (2017). Muundo wa Utenzi wa Wabukusu wa Khuswala Kumuse katika *Mulika* Na. 34 uk. 99-115.

Mtandao

Miyamoto, K. (2020). Exploring the 12 stages of the Hero's Journey. <https://screencraft.org/2020/04/03/Free-download> Tarehe 12/7/2021

Vanwesenbeeck, I. (2017). Translating Gilgamesh: A Conversation with Benjamin Foster. *World Literature Today*. Kutoka <https://www.worldliteraturetoday.org/blog/translation-tuesday/translating-gilgamesh-conversation-benjamin-foster> Tarehe 18/9/2019

VIAMBATISHO

Kiambatisho 1A: Usimulizi katika *Utendi wa Fumo Liyongo* (UFL)

Mf 1 UFL

Hadithi niwandikiye
Ya ajabu musikiye
Yalojiri amriye
Mupate kufahamiya (ub. 4)

Niweleze kwa utungo
Hadithi yake liyongo
Niweleze na mazinga
Mambo yalomzingiya (ub. 5)

Mf 2

UFL
Wagala wakabaini “Huyu
Liyongo ni nyani Kwetu
hayusilikani
Wala hatuyasikiya” (ub. 11)

“Ni mwanamume Swahihi
Kama simba una zihi
Usiku na asubuhi
Kutembea ni mamoya (ub. 12)

Mf 12

UFL
Liyongo akikabili
Ndiye kenenda rijali
Alikwenda siku mbili
Na ya pili ni kungiya (ub. 26)

“Twaitaka mbeu yake
Nasi kwetu tuipeke
Kwa furaha tumuweke
Apate kutuzaliya” (ub. 41)

Mf 13

UFL
Sharuti wakatimiza
Liyongo wakamuoza
Kwa furaha na kuteza
Nyumbani akaingiya (ub. 45)

Mke katukuwa mimba
Akazaa mwane simba
Mwanamume wa kutamba
Mwane Liyongo sikiya (ub. 46)

Mf 33

UFL
 Bismillahi nabutadi
 Kwa ina la Muhammadi
 Nandikie auladi
 Nyuma watakaokuya (ub.1:23)

UMM
 Bismillahi Mbuyaza
 awali ya kujifunza
 sijui taufawaza
 au vitanichachia
 (ub.1:1)

Mf 47

UFL
 Ni mwanamume swahihi
 kama simba una zihi
 usiku na asubuhi
 kutembea ni mamoya (ub.13:24)

Mf 53

UFL
 Wakanena kwa moyoni
 “Amuwezao ni nyani
 Hayuno hawezekani
 Ni kutaka kwangamiya” (ub. 67:33).

Mf 54

UFL
 Naye chenenda ndiani
 una khaufu moyoni
 “*Nifanye shauri gani
 kwa baba kuisikiliya* (ub.162:48)

Yakamuiya matata
 iye mimi kumpata
*kitokufa ni matata
 taniuwa mara mmoja* (ub.163:48)

“*Ikiwa alonambiya
 ni mzaha siyo niya
 kasidi kunangaliya
 ni khatari nacheleyea.*” (ub.164:48)

Mf 62

UFL
 Wakanenda kwa utungo
 mafumo, zembe, zigongo
 wakamshika Liyongo
 gerezani akatiwa (ub.86:36)

Akatiwa gerezani
 kafungiwa kijumbani
 asikari mlangoni
 kwa zamu wachangaliya (ub.87:36)

Mf 63

UFL
 Hata usiku kufika
 matezo wakayandika
 kana ada wakaweka
 t'asa, pembe, siwa piya (ub.111:40)

Na ngoma na nyingi kusi
 kuisalie unasi
 ikawa kama harusi
 watu wakiangaliya (ub.112:40)

Mf 68

UFL
 Mfalme kaandika
 waraka wake haraka
 Mtu wake kampeka
 Liyongo kampekeya (ub.18:25)

Na Liyongo akajibu
 kwa heshima na adabu
 “Nitakuja kwa karibu
 nitwiiye Maulaya” (ub.21:26)

Mf. 70

UFL
 Kayuwa hana fahamu
 Kijana aliazimu
Kwa ile yakwe hamumu
Mke kwenda kuzengenya (ub. 178)

Kamtiya kitovuni
Naye ulele kwa t'ani
 Achamka hamuoni
 Kiyana amekimbiya (ub.179)

Mf 82

UFL
 Na Sulutwani niseme
 Alikuwa mwanamume
 Tampoka ufalume
 Dhana alimdhaniya (ub. 51)

“Anipoke ufalme
 Kisa chanda nikiume
 Kheri yangu mwanamume
 Kumuuwa mara moya” (ub. 93)

Mf 86

UFL
 Ni *mwanamume swahihi*
kama simba una zihi
 usiku na asubuhi
 kutembea ni mamoya (ub. 13)

Mf 87

UFL
 Ruhu zikenda kishindo
 zimo zao hukoma ondo
 huyo ni bwana wa kondo
 ashindaye jeshi miya (ub.35)

Mf 88

UFL
 Sulutwani tumjibu
 kumuuwa ni dharubu
 kumshika ni taabu
 hatuwezi kwa umoya (ub.69)

Mf 89

UFL
*Na tumfanye amiri
 zikiya zita ni kheri
 atakufa kwa uzuri
 maana hatokimbiya (ub.90)*

Mf 103

UFL
 Akatiwa gerezani
 Kafungiwa kijumbani
 Askari mlangoni
 Kwa zamu wachangaliya (ub.84)

Mf 104

UFL
 Kamba 'Sada nakutuma
 Enda kamwambie mama
 Afanye mkate mwema
 Kati tupa aitiya (ub.104)

Sada akabalighisha
 Mamake yakamuwasha
 Akaufanya wa wishwa
 Mkate kampikiya (ub.106)

Mf 105

UFL
 Kwa wutie wakakimbiya
 Hapana alosaliya
 Liyongo kaitokeya
 Mabarani karejeya (ub.118)

Mf 106

UFL
 Na mamakwe kumwegema
 Alikicha tema tema
 Kwa mbali kimitizama
 Na nasaha miya miya (ub.193)

Mf 119

UFL
 Wagala wakipulika

Kwa dhihaka wakateka
Wakanena “twamtaka
Na sisi kumwangaliya” (ub.16)

Mf 120

UFL
Mke katukuwa mimba
Akazaa mwana simba
Mwanamume wa kutamba
Mwane Liyongo sikiya (ub. 46)

Fitina zikamngiya
Mfalme miya miya
Kwa hila kakusudiya
Kumuuwa fahamiya (ub. 49)

Mf 121

UFL
Mfalme kawambiya
“Liyongo kunipatiya
Kitwa mukaniyeteya
Tawapa riale miya” (ub. 53)

Mf 122

UFL
Nisikiya wangu baba
Liniuwalo ni haba
Ni msumari wa shaba
Kitovuni nikitiya (ub.143)

“Jamii silaha piya
Haziniuwi swabiya
Ila nimezokwambiya
Ni ya kweli yote piya” (ub. 144)

Mf 123

UFL
Kamtiya kitovuni
Naye ulele kwa t’ani
Achamka hamuoni
Kiyana amekimbiya (ub. 179)

Mf 124

UFL
Mfalme kamwambiya
Mbona mwana hukuliya
Babako alikuyeya
Kwa anasa zote piya?” (ub. 211)

Mf 125

UFL
“usiketi mui wangu
Wewe adui ya Mungu
Tena vua nguo zangu
Vaa yako mezoweya (ub. 214)

Mfalme kamtowa
 Nguo zakwe kamvuwa
 Na watu akatukiwa
 Khabari ikaeneya (ub. 216)

Mf 126

UFL
 Kaingiya mayutoni
 Katindikia nyumbani
 Hata wenzi hawaoni
 Hamu imezomngiya (ub. 220)

Mf 127

UFL
 Siku chache kitimiya
 Maradhi yakamniya
 Yasiyomuondokeya
 Naye kisa kaifiya (ub. 223)

Mf 128

UFL
 Mfalume kabaini
 Kabisa huna imani
 Epuka mwangu matoni
 Na nyumbani nitokeya (ub. 213)

Mf 129

UFL
 Liyongo silaha yetu
 Kwa wute khasimu zetu
 Alikuwa ngao yetu!"
 Wute wakinena haya (ub. 225)

Kiambatisho 1B: Usimulizi katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* (UMM)**Mf 3**

UMM
 Simba awele kuruka
 Ili kutaka mshika
 Upanga ukamtoka
 Mikidadi katwaa (ub.455)

Alipokwisha mkataa
 Simba akamkukuta
 Na shairi akaleta
 Kujisifu ushujaa (ub.456)

Mf 4

UMM
 Huwaje mgeni wako
 ukampa taji lako
 lililo kitwani mwako
 ukamvika kavaa
 (ub.467)

Mimi naona aibu
 Ndipo hufanya ghadhabu
 Mgeni mja gharibu
 Uyasidi kumwatia (ub.470)

Mf 5

UMM
 Wakanioza Maliki
 Wala mimi simtaki
 Illa nafuata haki
 na idhini ya abia (ub. 551)

Sasa upigane nao
 uwashinde wende zao
 utwae mali zao
 nami upate nitwae (ub. 552)

Mf 6

UMM
 Akatamka Mayasa
 Ewe samba mnafisi
 Simtinde kwa upesi
 Laala akalekea (ub. 620)

Mayasa rejea kwako
 utilize moyo wako hana
 dhara mume wako
 Mayasa akarejea (ub.623)

Mf 14

UMM
 Urathi wa baba yake
 Mikidadi asishike
 Hakuwa hata na mke
 Kwa unyonge kumngia (ub.15)

Mf 15

UMM
 Aliambia shuruti
 Mume mtaka binti
 Akhitarie mauti
 Ndiyo aliyonambia (ub.31)

Shoti apigane naye
 Hiyo ndiyo shartiye
 Na mtu amshindaye
 Ndiye mume wa kuoa (ub.32)

Mf 16

UMM
 Mayasa kuona hivyo
 Mikidadi aanavyo
 Na upanga apigavyo
 Kamjua ni shujaa (ub. 116)

Kawambie Warabuo
 Warudi na mali yao
 Mume wangu nitakao
 Ni huyu nimekwambia (ub. 126)

Mf 17

UMM
 Mtu huyo awanaje
 Upanga aushikaje
 Aula autupaje
 Naye ni mtu mmoja (ub.352)

Awanaje mtu huyo
 Hata mkatoka mbiyo
 Silaha mlio nayo
 Jamii kawatwalia (ub.353)

Mf 18

UMM
 Hata zikija akili'
 amefungwa silisili na
 mapingu ya rujuli
 Mikidadi akalia (ub.690)

Akalia kwa mayowe
hino dunia ya lewe
ee msiba wa kuwe
mamaye kamlilia (ub.691)

Mf 19

UMM
Ali akisafika
Mikidadi kamshika
mikufu aliyovikwa
jamii akaivua(ub.743)

Mf 20

UMM
Kisa utendi wavita
simulia yaliopita
hijazi yenyematata
jamaa nimewambia (ub. 777)

Nami mwenye kuradidi
Ismu yangu Saidi
wa Abdalla Masudi
Jina langu nawambia (ub. 778)

Mf 34

UMM
Sasa nitatawakali
Bismillahi awali
yu pweke Rabi Jalali
ndiye pwekeye mmoya(ub.7:1)

Mf 39

UMM
Akamkamata ndevu
akazivuta kwa nguvu
akashika mashavu
kamtinda akamaa (ubeti 237:15)

Akamkamata na rasu
kwa mkonowe na kisu
akamuekea kesu
mbele ye kamuekea (ub.238:15)

Mf 42

UMM
Tumeziya kukhitimu
hapo ndio wasalamu
Illahi tatukirimu
kwa baraka na afiya (ub. 228:15)

Mf 43

UMM
Kaletewa Jibrili
akamwambia Rasuli
akusalimu Jabbari
na mengine akamwambia (ub. 769:49)

Mf 44

UMM
 Nami mwenye kuradidi
 Ismu yangu Saidi
 wa Abdalla Masudi
 jina langu nawambia (ub. 778:49)

Mf 50

UMM
 Simba huyu hali kitu
 hali manyama ya mwitu
 kila siku hula watu
 Sultani kamwambia (ub. 450:29)

Mf 51

UMM
 Khabarize Mikidadi
 zikaenea biladi
 kuwa wadi murtadi
 kama simba alokaa (ub.282:18)

Mf 57

UMM
 Ni mtu gani huyule
 apiganaye hivile
 hatuoni tangu kale
 mtu kamaye mithaa (ub.88:6)

Au yule ni ruhani
 au ni mwana wa jini
 aula ni sheitwani
 aula ni malakaa (ub.
 89:6)

Mf 58

UMM
 Mtu huyo awanaje
 upanga aushikaje
 aula autupaje
 naye ni mtu mmoja (ub. 352:23)

Mf 64

UMM
Ikampata sakara
kapotewa na fikira
 Wakenenda nkambara
 Ikawa kumtatia
 (ub.689)

Mf 65

UMM
 Hata zikija akili
 amefungwa silisili
 na mapingu ya rujuli
 Mikidadi akalia (ub. 690)

Mf 66

UMM
 Jamii wakamzinga
 kwa mafumo na mapanga
 muda punde kujitenga
 ameua watu mia (ub. 317)

Mf 69

UMM
 Baadaye kaandika
 akakutubu waraka
 kwa mkwewe kaupeka
 kumuarifu jamia (ub. 668:42)

Atukuzie kitabu
 kuwahimu Waarabu
 twaona hujatujibu
 khati tulokuleteya (ub. 683: 43)

Mf 71

UMM
 Kajipeka kati mwao
 Kwa siaha na zomeo
 Alotinda mwinda huo
 Ni khamsini rijaa (ub. 216)

Mf 72

Akamkamata ndevu
 Akazivuta kwa nguvu
 Akamshika mashavu
 Kamtinda akamaa (ub. 237)

Akamkata na rasu
 Kwa mkonowe na kisu
 Akamuekea Kesu
 Mbeleye kamuekea (ub. 238)

Mf 73

UMM
 Nawatimue elifu
 Mashujaa wasio khofu
 Wawazao kita sefu
 Wazoevu wa kitaa (ub. 379)

Tatwaa silaha zao
 Na farasi walo nao
 Sultani Kamba ndiyo
 Ahadi imetimia (ub. 381)

Mf 74

UMM
 Mikidadi kawakata
 Asisaze mtu hata
 Hata mwondoka wa vita

Sultani katongoa (ub. 414)

Mf 75

UMM
Akajibu Mikidadi
Hawa kwao hawarudi
Roho zao na jasaki
Haibudi kupotea (ub. 554)

Kawangia kati mwao
Asikhofu wingi wao
Kiwakata vitwa vyao
Asipumue kuua (ub. 557)

Mf 90

UMM
Na wane kamkamata
Na wa tano na wa sita
Hisabuye nilopata
Khamsini kawandoa (ub. 279)

Mf 91

UMM
Mikidadi kajisifu
Waziri kumuarifu
Mimi si mtu wa hofu.
Hata na wewe wajua (ub. 363)

Kumuonako shujaa
Sultani kafazai
Roho ikaingia mai
Kwani yakini ni shujaa (ub. 366)

Mf 92

UMM
Mikidadi kawakata
Asisaze mtu hata
Hata mwondoka wa vita
Sultani katongoa (ub. 414)

Mf 93

UMM
Kawangia kati mwao
Asikhofu wingi wao
Kiwakata vitwa vyao
Asipumue kuua (ub. 557)

Mf 98

UMM
Ewe Luhani adui
kamba hunitambui
Ndimi simba ndimi tui
Nawe utajionea (ub. 221)

Mf 99

UMM
Mikidadi kajisifu

Ndimi mtu maarufu
Mali hiyo na suyufu
Jamii nitazitwaa (ub. 438)

Mf 107

UMM
Mikidadi kuonake
ghadhabu za mwanamke
ukarudi moyo wake
kwa mahaba kumngia (ub.107)

Kawana naye kwa pole
mahaba yamzidile
na Mayasa amwambile
Mikidadi nisikia (ub. 108)

Mf 108

UMM
sasa upijane nao
uwashinde wende zao
utwae na mali zao
nami upate nitwaa (ub. 552)

Mf 109

UMM
Naapa kwa Moleo
hawano hawendi kwao
Mayasa akamba ndiyo
nitakayo nitendea (ub. 555)

Mikidadi akanena
minao hutindikana
hata nawe utaona
nitakavyowangilia (ub. 556)

Mf 110

UMM
Shairi akisha soma
Alii katabasama
akangiwa na huruma
Mayasa akamwambia (ub. 622)

Mayasa rejea kwako
Utilize moyo wako
Hana dhara mume wako
Mayasa akarejea (ub. 623)

Mf 111

UMM
Mamaye keta matozi
ewe mwanangu mzazi
kukufungua siwezi
ulitakalo nambia (ub. 692)

Mf 138

UMM

Huyu ni mwana yatima
 Hatimizi darahima
 Hapati hata kituma
 Cha maji kukutekea (ub. 123)

Mf 139

UMM
 Na leo umewasili
 Zimepungua shughuli
 Twamshukuru Jalali
 Mke ulivyomtwaa (ub. 662)

Mf 140

UMM
 Malik bin Riyahi
 Angojewa asubuhi
 Kesho atamdhabihi
 Mdirikini jamaa (ub. 718)

Mf 141

UMM
 Akampa Mikidadi
 Na maguuni kuyudi
 Kumtinda asibudi
 Kamkata saa moya (ub. 751)

Kamtinda binafusi
 Kamkata yake rasi
 Roho yake kwa upesi
 Motoni ikenda tiwa (ub. 752)

Mf 142

UMM
 Katamka Haidari
 Akamwambia Jabiri
 Ni kumkiri Jabbari
 Na mtumewe pamoya (ub. 760)

Jabiri asikubali
 Kumfuata Jalali
 Kamkata pande mbili
 Sawasawa kamtwaa (ub. 761)

Mf 143

UMM
 Yakisa hayo kutimu
 Tuma kafanya karamu
 Wali mwingi na lahamu
 Muyini wote kenea (ub. 774)

Kawapa karamu wote
 Vipofu hata viwete
 Kwa kila mtu apate
 Hapo asiye kwenea (ub. 775)

Kiambatisho 1C: Usimulizi katika Utendi wa Gilgamesh (UG)**Mf 7**

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(He who has seen everything I will make known to the lands I will teach about him who experienced all things alike Anu granted him the totality of knowledge of all No later king or man ever equaled) (Tablet 1:1)</i>	“Nitaifahamisha nchi yote, kumhusu yeye aliyeyaona yote Nitatoa mafundisho kumhusu yeye aliyeyapatia mambo yote Anu alimtunuku ukamilifu wa ufahamu wa yote Hakuna mtu au mfalme wa baadaye aliyefikia utukufu wake (Kibao I:1)

Mf 8

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(They (Gilgamesh and Enkidu)... They lunge at each other like raging wild bulls.... One name he bellowed full of..... The guardian of the forest bellowed...Humbaba like..... “one alone cannot” Strangers..... A slippery path is not feared by two people who help each other” Twice, three times... (Tablet IV: 17a)</i>	Wao (Gilgamesh na Enkidu) wanarukiana kama fahali mwitu walioghadhabika Jina moja alinguruma akijawa na... mlinzi wa msitu alinguruma... Humbaba kama... ...“Mmoja pekee hawezi” wageni... Njia yenye utelezi haiogopwi na watu wawili wanaosaidiana’ Mara mbili, mara tatu... (Kibao IV: 17a)

Mf 9

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(I fell to my knees and sat weeping, Tears streaming down the side of my nose... When a seventh day arrived, I set forth a dove and released it..... I sent forth a swallow and released it... I sent akimwomboleza Rafiki yake Enkiduforth a raven and released it.....(Tablet XI: 46)</i>	Nilipiga magoti na kukaa nikiomboleza Machozi yalinibubujika na kuteremka kando ya pua yangu ...siku ya saba ilipofika, nilimtuma njiwa na kumwaachilia... nilimtuma mbayuwayu na nikamwachilia... nilimtuma kunguru na nikamwachilia... (Kibao XI: 46)

Mf 21

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>...They stood at the forest’s edge ... gazing at the top of the Cedar Tree, gazing at the entrance to the forest, where Humbaba would walk there was a trail...(Tablet V:18)</i>	(Walisimama pembeni mwa msitu, wakitazama kilele cha mti wa mkangazi, wakitumbulia macho kiingilio cha msitu. Palikuwa na alama kila ambapo Humbaba alitembea...) (Kibao V:18)

Mf 22

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(Enkidu lies down a first day, a second day, That Enkidu....in his bed;</i>	(Enkidu analala chini siku ya kwanza, ya pili,
<i>A third day and fourth day, that Enkidu...in his bed;</i>	Siku ya tatu na ya nne, Yule Enkidu...kitandani mwake;
<i>A fifth, a sixth, and seventh, that Enkidu...in his bed;</i>	Siku ya tano na sita na ya saba, Yule Enkidu...kitandani mwake;
<i>An eighth, a ninth, a tenth, that Enkidu...in his bed</i>	Siku ya nane, ya tisa, ya kumi, Yule Enkidu...kitandani mwake
<i>Enkidu's illness grew ever worse...(Tablet VII:28)</i>	Maradhi ya Enkidu yalizidi kuwa mabaya... (Kibao VII:28)

Mf 35

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(Anu granted him the totality of knowledge of all... supreme over other Kings, Lordly in appearance, Mighty net, Protector of His people) (Tablet 1:1)</i>	Anu alimtunuku ukamilifu wa ufahamu wote... Mkuu wa Wafalme wengine, mtawala mkuu. Jamvi kuu, mlinzi wa watu wake (Kibao 1:1)

Mf 36

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(Offspring of Lugalbanda, Gilgamesh is strong to perfection,</i>	Mzawa wa Lugalbanda, Gilgamesh, Hodari siye dosari,
<i>Son of the august cow, Rimat-Ninsun., Gilgamesh is awesome, Gilgamesh is strong to perfection,</i>	Mwana wa ng'ombe adhimu, Rimat...Ninsun..
<i>Son of the august cow, Rimat-Ninsun., Gilgamesh is awesome to ssperfection) (Tablet 1:1)</i>	Gilgamesh anapendeza hana dosari (Kibao 1: 1)

Mf 38

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(They pulled out his insides including his tongue).</i>	...Walinyofoa viungo vyote vya ndani ya mwili ikiwemo ulimi

Mf 45

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(Go up on the wall of Uruk and walk around,</i>	Kwea ukuta wa uruk na uzunguke,
<i>Examine its foundation, inspect its brickwork thoroughly.</i>	Chunguza msingi wake, kagua uashi wake kwa makini
<i>Is not even the core of the brick structure made of kiln fired brick</i>	Thibitisha kuwa matofali yake ni ya kukaushwa ndani ya tanuru...
<i>The Ishtar Temple) (Tablet 1:1)</i>	<u>Ukumbi wa hekalu la Ishtar (Kibao 1:1)</u>

Mf 46

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(Go up, Urshanabi, onto the wall of Uruk and walk around. kwenye ukuta wa Uruk na utembe pale,</i>	Kwea juu Urshanabi
<i>Examine its brickwork thoroughly...</i>	Chunguza msingi wake, kagua uashi wake kwa makini...
<i>Is not (even the core of) the brick structure of kiln-fired brick...</i>	Je, si matofali yake si ni ya kukaushwa ndani ya tanuru...
<i>The Ishtar Temple) (Tablet XI: 51)</i>	Ukumbi wa hekalu ya Ishtar Thibitisha kuwa matofali yake ni ya kukaushwa ndani ya tanuru... Ukumbi wa hekalu la Ishtar (Kibao cha XI: 51)

Mf 48

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(Mighty net, protector of his people</i>	Jamvi kuu, mlinzi wa watu wake
<i>Raging flood-wave who destroys even walls of stone!) (Tablet 1:1)</i>	Wimbi kali la mafuriko, ambalo huangusha hata kuta za mawe! (Kibao 1:1)

Mf 49

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>Humbaba's roar is a flood</i>	Mngurumo wa Humbaba ni mafuriko
<i>His mouth is fire</i>	Kinywa chake ni moto
<i>His breath is death (Tablet II:2)</i>	Pumzi zake ni kifo! (Kibao II:2)

Mf 55

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(Who can compare him in kingliness?</i>	Nani wa kulinganishwa naye katika Ufalme?
<i>Who can say like Gilgamesh: "I am King"!</i>	Nani anayeweza kusema kama Gilgamesh: "Mimi ni Mfalme"!
<i>Whose name from the day of his birth, was called "Gilgamesh"?) (Tablet I:2)</i>	Nani tangu kuzaliwa kwake aliitwa "Gilgamesh"? (Kibao 1:2)

Mf 56

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(Gilgamesh said to the palace retainers: "who is the bravest of all the men Who is the boldest of all the males!) (Tablet VI:25)</i>	Gilgamesh akawaambia watumishi wa kasri: Nani shupavu zaidi ya watu wote Nani jasiri kati ya wanaume wote! (Kibao VI:25)

Mf 67

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>Ishtar led the Bull of Heaven down to the earth</i>	Ishtar alimwongoza Fahali wa Mbinguni kuelekea duniani
<i>When it reached Uruk, it climbed down to the Euphrates...</i>	Fahali alipofika Uruk, aliteremka hadi mto Euphrates...
<i>the snort of the Bull of Heaven a huge pit opened up</i>	Fahali wa Mbinguni alipumua vikali na shimo kubwa likafunguka
<i>And 100 young men of Uruk fell in (Tablet VI:23)</i>	vijana 100 wa Uruk wakaanguka ndani (Kibao VI :23)

Mf 76

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(They will say) it was Gilgamesh who locked in battle with Humbaba the terrible! (Tablet II:10)</i>	(Watasema) Gilgamesh ndiye aliyepambana vitani na Humbaba anayeogofya! (Kibao II:10)

Mf 77

UG

MA	MT (Tafsiri yangu)
<i>(Humbaba spoke to Gilgamesh, saying; An idiot and a moron should give advice to each other, but you, Gilgamesh why have you come to me!</i>	Humbaba alinena na Gilgamesh akisema; ...zuzu na punguani wanapenda kujipatia ushauri, Lakini wewe, Gilgamesh, kwa nini umekuja kwangu!
<i>...You have brought Gilgamesh into my presence you stand....an enemy, a stranger.</i>umemleta Gilgamesh mbele yangu,...unasimama..., adui, mgeni
<i>...Gilgamesh, throat and neck I would feed your flesh to the screening vulture, the eagle, and the vulture!) (Tablet V:18)</i>Gilgamesh, koo na shingo, Nitawalisha tai nyama ya mwili wako! (Kibao V:18)

Mf 78

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<p><i>("My friend Humbaba, Guardian of the forest, grind up, kill, pulverize (?) and destroy him! Erect an eternal monument proclaiming....how Gilgamesh killed (?) Humbaba")</i></p> <p><i>.....they pulled out his insides including his tongue.</i></p> <p><i>They tied together a raft... Enkidu stried it...</i></p> <p><i>While Gilgamesh held the head of Humbaba) (Tablet V:20)</i></p>	<p>Rafiki yangu Humbaba, mlinzi wa msitu wa mikangazi, Msage, muue, mponde na umharibu!Unda mnara utakaodumu milele Kutangaza....jinsi Gilgamesh alivyomuua (?) Humbaba"</p> <p><i>...walinyofoa viungo vyote vya ndani ya mwili wake ikiwemo ulimi...</i></p> <p>Walifunga boya..Enkidu aliendesha ...</p> <p>Huku Gilgamesh akishika kichwa cha Humbaba (Kibao V: 20)</p>

Mf. 79

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<p><i>(Enkidu stalked and hunted down the Bull of Heaven.</i></p> <p><i>He grasped it by the thick of its tail and held onto it with both his hands (?), while Gilgamesh,</i></p> <p><i>like an expert butcher, boldly and surely approached the Bull of Heaven.</i></p> <p><i>Between the bape, the horns andhe thrust his sword. After they had killed the Bull of Heaven, they ripped out its heart and presented it to Shamash)</i></p> <p><i>(Tablet VI:24)</i></p>	<p>Enkidu alimwandama na kumwinda fahali wa mbinguni.</p> <p>Alimfumbata kwa kuutumia mkia wake mnene. Aliushikilia kwa mikono yake miwili (?) Naye Gilgamesh kama bucha hodari,</p> <p>Kwa ujasiri na uhakika alimwendea fahali wa mbinguni</p> <p>Baina ya ukosi na pembe, na alirusha upanga wake. Baada ya kumua Fahali wa mbinguni. Waliunyofoa moyo wake na kuupeleka kwa Shamash (Kibao VI:24)</p>

Mf 83

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<p><i>(And he is the shepherd of Uruk,(the Yeye ndiye mchungaji wa Uruk (mzunguko) enclosure)</i></p> <p><i>He is their shepherd, and yet he opposes ndiye mchungaji wao ilhali anawadhulumu them Strong, handsome (and) wisel...</i></p> <p><i>Gilgamesh leaves no virgin to their lover)</i></p>	<p>Ana nguvu, mtanashati na mwenye hekima (...)</p> <p><u>Gilgamesh hamwachi bikira kwa mume wake.</u></p>

Mf 94

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<p><i>Supreme over other kings, lordly in Appearance he is the hero, born of Uruk, the giving wild bull (Tablet I:1)</i></p>	<p>Mkuu zaidi ya wafalme wengine, mtawala mkuu.</p> <p>Ndiye shujaa, mzawa wa Uruk, fahali mkali wa kuogofya (Kibao I:1)</p>

Mf 95

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>Ishtar led the bull of Heaven down to the earth.</i> <i>At the snort of the Bull of Heaven, a huge pit opened up (Tablet VI:23)</i>	Ishtar alimwongoza Fahali wa Mbinguni kuelekea duniani. Fahali wa Mbinguni alipumua vikali na shimo kubwa likafunguka (Kibao VI:23)

Mf 96

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>The Noble counselors of Uruk a rose and delivered their advice to Gilgamesh; You are young, Gilgamesh, your heart carries you off.... Gave birth to you Humbaba's roar is a flood. His mouth is fire His breath death! He can hera any resting in his forest 100 leagues away! Who would go down into his forest! Who among (even!) the Igigi gods can confront him? (Tablet II :II)</i>	Washauri wadilifu wa Uruk walisimama na kutoa ushairi wao kwa Gilgamesh. "Ungali mdogo, Gilgamesh, moyo wako unakuongoza usijue kile unachokizungumzia...likuzaa Mngurumo wa Humbaba ni mafuriko Kinywa chake ni moto Pumzi zake ni kifo! Ana uwezo wa kusikia kelele zozote umbali wa maili 100 pale msituni! Nani atakayekwenda pale msituni! Nani hata miongoni mwa miungu wa Igigi anaweza kupambana naye? (Kibao II :II)

Mf 100

UG

M.A	M.T (Tafsiri yangu)	M. A
<i>Who can compare with him in kingliness? Who can say like Gilgamesh: "I am King!" Two- thirds of him is god, one- third of him is human (Tablet 1:2).</i>	Nani wa kulinganishwa naye katika ufalme? Nani anayesema kama Gilgamesh: "Mimi ni Mfalme!" Theluthi mbili zake ni mungu na theluthi moja ni binadamu (Kibao I: 2).	

Mf 101

UG

M.A	M.T (Tafsiri yangu)
<i>Gilgamesh said to the palace retainers: "Who is the bravest of the men Who is the boldest of the males! Gilgamesh is the bravest of the men, The boldest of the males!</i>	Gilgamesh akamwaambia watumishi wa kasri; "Nani shupavu zaidi ya watu wote Nani jasiri kati ya wanaume wote! Gilgamesh ndiye shupavu zaidi, Shujaa zaidi ya wanaume wote!

Mf 112

UG

M.A.	M.T. (Tafsiei yangu)
<i>Shamhat unclutched her bosom, exposed her sex, and he took in her voluptuousness.</i>	Shamhat aliyaachilia maziwa yake, akaonyesha uchi wake.
<i>She was not restrained but took his energy.</i>	Naye akamteka kwa nyegereshi zake.
<i>She spread out her robe and he lay upon her.</i>	Hakujizuia, ila alizitwaa nguvu zake.
<i>She performed for the primitive the task of womankind</i>	Alitandaza joho lake naye akajilaza juu.
<i>But when he turned his attention to his animals, the gazelles saw Enkidu and darted off.</i>	Alimtendea mshenzi huyo unyumba...
<i>The wild animals distanced themselves from his body.</i>	Lakini alipogeza makini yake kwa wanyama wake.
	Swara walikurupuka walipomwona Enkidu
	Wanyama wa porini walijitenga na mwili wake.

Mf 113

UG

M.A	M.T (Tafsiri yangu)
<i>The mother of Gilgamesh, the writer, all-knowing, said to her Lord; RimatNinsun, the wise, all-knowing said to Gilgamesh:</i>	Mamaye Gilgamesh, mwenye busara, ajuaye yote, akamwambia bwana wake; Rimat-Ninsun, mwenye hekima, ajuaye yote, akamwambia Gilgamesh:

Mf 114

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>Gilgamesh spoke to Enkidu saying: Come on, my friend, let us go to the Egalmah Temple, to Ninsun, the Great Queen, Ninsun is wise, all-knowing, she will put the advisable path at our feet” (Tablet III: 12)</i>	Gilgamesh alinena na Enkidu akisema: “Njoo rafiki yangu, twende kwenye hekalu la Egalmah, kwake Ninsun, Malkia Mkuu, Ninsun ana busara, anajua yote; atatuelekeza katika njia ifaayo” (Kibao III: 12)

Mf 115

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>She went up to the roof and set incense in front of Shamash, she offered fragrant cuttings and raised her arms to Shamash: “Why have you imposed...nay, inflicted!... a restless heart on my son, Gilgamesh! Now you have touched him so that he wants to travel a long way where Humbaba is!... Enkidu will protect the friend, will keep the comrade safe, In our Assembly we have entrusted the King to you, and on your return you must entrust the King back to us!” (Tablet III:12)</i>	Alikwea kwenye paa na kuchana ubani mbele ya Shamash, Alitoa vipandikizi vyenye manukato na akainua mikono yake kwa Shamash: “Kwa nini umelazimisha ...la, umeambukiza!...moyo usiotulia ndani ya mwanangu Gilgamesh! Sasa umemgusa anataka kufunga safari ya mbali kuelekea aliko Humbaba! “Enkidu atamlinda therafikiye, atahakikisha mwenzi wake yu salama, Katika baraza letu tumekukabidhi mfalme mikononi mwako, Na utakaporejea sharti umrejeshe mfalme mikononi mwetu” (Kibao III:12)

Mf 116

UG

M.A	M.T. (Tafsiri yangu)
<p><i>“My friend, why are the great Gods in Conference? (In my dream) Anu, Enlil and Shamash held a council, and Anu spoke to Enlil:</i></p> <p><i>“Because they killed the Bull of Heaven and have also slain Humbaba, one of them who pulled up the cedar of the mountain must die!</i></p> <p><i>Enlil said: “Let Enkidu die, but Gilgamesh must not die!” (Tablet VII:25)</i></p>	<p>“Rafiki yangu, kwa nini miungu wakuu wana mkutano? (Katika ndoto yangu) Anu, Enlil na Shamash walifanya mkutano, Anu alinena na Enlil akisema:</p> <p>“Kwa kuwa walimuua Fahali wa Mbinguni na pia wamemuua Humbaba, mmoja wao aliyeung’oa msitu wa mkangazi sharti afe! Enlil akasema”</p> <p>“Mwache Enkidu afe, lakini Gilgamesh sharti asife!” (Kibao VII:25)</p>

Mf 130

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<p><i>The harlot said to Enkidu:</i></p> <p><i>“You are beautiful,” Enkidu, you are become like a god.</i></p> <p><i>Why do you gallop around the wilderness with the wild beasts?</i></p> <p><i>Come, let me bring you into Uruk- Haven,</i></p> <p><i>To the Holy Temple, the residence of Anu and Ishtar,</i></p> <p><i>The place of Gilgamesh, who is wise to perfection,</i></p> <p><i>But who struts his power over the people like a wild bull” (Tablet 1:5)</i></p>	<p>Yule hawara akamwambia Enkidu,</p> <p>“U mtanashati, Enkidu</p> <p>Wewe u sawa na miungu</p> <p>Kwa nini wewe huchapuka ukiandamana na wanyama wa porini?</p> <p>Njoo, niruhusu nikuongoze twende Uruk-Haven,</p> <p>Kwenye hekalu takatifu, makao ya Anu na Ishtar,</p> <p>Mahali pa Gilgamesh, mwenye hekima bila dosari,</p> <p>Lakini atumiaye mamlaka yake kwa kiburi mithili ya fahali mwituni) (Kibao I:5)</p>

Mf 131

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<p><i>(Enkidu, it is your wrong thoughts you must change!</i></p> <p><i>It is Gilgamesh whom Shamhat loves, and Anu, Enlil and La have enlarged his mind.</i></p> <p><i>Even before you came from the mountain Gilgamesh in Uruk had dreams about you” (Tablet 1:6)</i></p>	<p>(Enkidu, sharti uyabadili mawazo yako mabaya!</p> <p>Shamhat anampenda Gilgamesh, na Anu, Enlil na La wamepanua akili yake</p> <p>Hata kabla hujatoka milimani, Gilgamesh akiwa Uruk alikuwa ameota kukuhusu) (Kibao 1:6)</p>

Mf 132

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(Gilgamesh said to the men of Uruk: "Listen to me, men...</i>	(Gilgamesh alinena kwa watu wa Uruk akisema: Nisikilizeni, watu...
<i>You, men of Uruk, who know...</i>	Nyie watu wa Uruk, mjuao...
<i>I want to make myself more mighty, and will go on a distant (!) journey!</i>	Nataka kujiongezea uthabiti, Nitafunga safari ya mbali!
<i>I will face fighting such as I have never known,</i>	Nitajipata katika vita vikali zaidi ya nilivyowahi kupigana,
<i>I will set out on a road I have never traveled!</i>	Nitafuata njia ambayo sijawahi kuipitia!
<i>Give me your blessings!</i>	Nipeni baraka zenu!..
<i>I will enter the city gate of Uruk...</i>	Nitaingia lango la jiji la Uruk...
<i>I will perform the new Year's (ceremonies) in...</i>	Nitajitenga kwa sherehe za mwaka mpya katika...
<i>The New Year's Festival will take place, celebrations...</i>	Sherehe za mwaka mpya zitatukia, maadhimisho..
<i>They will keep shouting "Hurrah!" in..."</i> (Tablet II:11)	Watapaza sauti kwa riboribo katika..." (Kibao II:11)

Mf 133

UG

M.A	M.T(Tafsiri yangu)
<i>(Enkidu, whom I love deeply, who went through every hardship with me, The fate of mankind has overtaken him</i>	(Enkidu ninayempenda kwa dhati, aliyepitia magumu yote nami, Hatima ya binadamu imemchukua
<i>And would not allow him to be buried Until a maggot fell out of his nose, I was terrified by his appearance (!), I began to fear death, and so roam the wilderness</i>	Nilimwomboleza na singeruhusu azikwe Hadi buu likaanguka kutoka puani mwake Sura yake iliogofya (!) Nilianza kuogopa kifo, na sasa nazurura nyikani...
<i>The issue of my friend oppresses me, The issue of Enkidu, my friend, oppresses me, So I have been roaming long roads through the wilderness</i>	Suala la rafiki yangu linanisonga. Kwa hivyo nimekuwa nikizurura masafa marefu nyikani
<i>How can I stay silent, how can I be still! My friend whom I love has turned to clay. Am I not like him? Will I lie down, never to get up again?"</i> (Tablet X: 37)	Nitawezaje kukaa kimya, nitawezaje kutulia! Rafiki yangu nimpandaye amegeuka udongo. Kuna tofauti gani baina yangu na yeye? Nitalala siku moja, nisiwahi kuamka tena?" (Kibao X: 37)

Kiambatisho 1D: Usimulizi Katika Simulizi ya Samsoni (SS)**Mf 10**

SS
 Samsoni akawaambia,
 Mimi nitawategea ninyi kitendawili, Kama mnaweza kunionyesha katika hizo siku saba za karamu, na kukitambua, ndipo hapo nitawapa mavazi thelathini ya kitani na mavao mengine thelathini (Waamuzi 14: 12).

Mf 11

SS
 Wewe wanichukia tu, wala hunipendi, wewe umewategea kitendawili hao wana wa watu wangu, nawe hukuniambia mimi....

Mf 23

SS
 Palikuwa na mtu mmoja wa sora, wa jamaa ya wadani, jina lake akiitwa Manoa, na mkewe alikuwa tasa, hakuzaa watoto

Mf 24

SS
 Malaika wa BWANA akamtokea yule mwanamke, akamwambia, Tazama, wewe sasa u tasa, huzai, lakini utachukua mimba, nawe utamzaa mtoto mwanamume (Waamuzi 13:3)

Mf 25

SS
 Ndipo huyo Manoa akamwomba BWANA akisema, Ee Bwana, nakuomba, Yule mtu wa Mungu uliyemtuma na aje kwetu mara ya pili, atufundishe hayo yatupasayo kumfanyia huyo mtoto atakayezaliwa (Waamuzi 13:8).

Mf 26

SS
Alipokwisha kuviwasha moto vile vienge akawaachia mbweha kati ya ngano ya Wafilisti, akayatekeleza matita na ngano, hata na mashamba ya mizeituni (Waamuzi 15:5).

Mf 27

SS
 1) Samsoni akaenda Gaza, akaona huko mwanamke kahaba, akaingia kwake. 2) Watu wa gaza wakaambiwa, ya kwamba, huyo Samsoni amekuja huku. Wakamzingira, wakamvizia usiku kucha, penye lango la mji, wakanyamaza kimya usiku kucha, wakisema, Na tungoje mpaka mapambazuko ndipo tutamwua. 3) Basi Samsoni akalala hata usiku wa manane, akaondoka katikati ya usiku, akaishika milango ya lango la mji, na miimo yake miwili, akaing'oa pamoja na komeo lake, akajitwika mabegani, akavichukua hata kilele cha mlima ule unaokabili Hebroni (Waamuzi 16:1-3).

Mf 28

SS

Ndipo alipomwambia yote yaliyokuwa moyoni mwake, akamwambia, wembe haukupita juu ya kichwa changu kamwe; maana mimi nimekuwa mnadhiri wa Mungu, tangu tumboni mwa mama yangu, nikinyolewa, ndipo nguvu zangu zitanitoka, name nitakuwa dhaifu, nitakuwa kama wanadamu wenzangu (Waamuzi 16:17).

Mf 29

SS

Kisha Samsoni akazishika nguzo mbili za katikati ambazo nyumba ile ilikaa juu yake, akazitegemea, moja kwa mkono wake wa kiume na moja kwa mkono wake wa kushoto...Akainama kwa nguvu zake zote, ile nyumba ikawaangukia hao wakuu, na watu wote waliokuwa ndani yake (Waamuzi 16:29).

Mf 30

SS

Lakini baba yake na mama yake hawakujua ya kuwa jambo hili ni la BWANA; maana alitaka kisa juu ya Wafilisti (Waamuzi 14:4).

Mf 31

SS

Roho ya BWANA ikamjilia kwa nguvu, naye akampasua kana kwamba anampasua mwana mbuzi, wala hakuwa na kitu chochote mkononi mwake, lakini hakuwaambia baba yake na mama yake aliyofanya (Waamuzi 14:6).

Mf 32

SS

Akaamka katika usingizi wake, akasema, nitakwenda nje kama siku nyingine, na kujinyosha. *Lakini hakujuu ya kuwa BWANA amemwacha* (Waamuzi 16:20b).

Mf 37

SS

Basi sasa, jihadhari, nakuomba usinywe divai wala kileo, wala usile kitu kilcho najisi, kwani tazama, utachukua mimba, nawe utamzaa mtoto mwanamume; na wembe usipite juu ya kichwa chake; maana mtoto huyuatakuwa mnadhiri wa Mungu tangu tumboni; naye ataanza kuwaokoa Israeli na mikono ya Wafilisti (Waamuzi 13:4-5)

Mf 40

Naye akaona mfupa mbichi wa taya ya punda, akautwaa, akapiga watu elfu kwa mfupa huo (Waamuzi 15:15)

Mf 41

SS

Delila alipoona ya kuwa amemwambia yote yaliyokuwa moyoni mwake, akatuma mtu akawaita wakuu wa Wafilisti, akisema, njooni huku mara hii tu, maana ameniambia yote aliyo nayo moyoni mwake.

Mf 52

SS

(5) Ndipo Samsoni na baba yake na mama yake wakatelemkia Timna wakafika mashamba ya mizabibu huko Timna. Na tazama, mwana simba akamngurumia; (6) Roho ya BWANA ikamjilia kwa nguvu, naye akampasua kana kwamba anampasua mwana mbuzi, wala hakuwa na kitu chochote mkononi mwake, lakini hakuwambia baba yake na mama yake aliyoyafanya (Waamuzi 14: 5-6).

Mf 59

SS

Kwa kuwa alikuwa amesikia kiu sana, akamlilia Bwana akisema, “Umempa mtumishi wako ushindi huu mkuu. Je, sasa nife kwa kiu na kuangukia mikononi mwa hawa watu wasiotahiriwa?” (Waamuzi 15:18).

Mf 60

SS

Nao watu wa mji wakamwambia siku ya saba kabla ya jua kuchwa; Ni kitu gani kilicho kitamu kuliko asali? Ni kitu gani kilicho na nguvu kuliko Simba? (Waamuzi 14:18)

Mf 61 SSBasi Wafilisti *wakamkamata,**Wakamng'oa macho yake wakamchukuwa**Wakamtelemsa mpaka Gaza*

Wakiwa wamemfunga kwa pingu za shaba, *wakamweka* ili asage ngano huko gerezani (Waamuzi 16:21).

Mf 80

SS

Kwa taya la punda

Malundo juu ya malundo

Kwa taya la punda

Nimeua watu 1,000 (Waamuzi 15:16).

Mf 81

Basi nyumba ile ilikuwa imejaa watu waume kwa wake; na wakuu wote wa Wafilisti walikuwa- mo humo, na juu ya dari palikuwa na watu 3,000 waume kwa wake waliokuwa wakitazama, wakati Samsoni alipocheza... Samsoni akasema, “Nife pamoja na Wafilisti” Ndipo akazisukuma zile nguzo kwa nguvu zake zote, lile jengo likaanguka juu ya viongozi na watu wote waliokuwamo mle ndani yake. *Hivyo akawaua watu wengi wakati wa kufa kwake kuliko siku za uhai wake* (Waamuzi 16: 27,30).

Mf 84

SS

...kwani tazama, utachukua mimba, nawe utamzaa mtoto mwanamume; na wembe usipite juu ya kichwa chake; maana mtoto huyo atakuwa mnadhiri wa Mungu tangu tumboni; *naye ataanza kuwaokoa Israeli na mikono ya Wafilisti* (Waamuzi 13:5)

Mf 85

SS

Naye akawa *mwamuzi wa Israeli katika siku za Wafilisti muda wa miaka ishirini* (Waamuzi 15:20).

...Naye alikuwa *mwamuzi wa Israeli muda wa miaka ishirini*
(Waamuzi 16: 31).

Mf 97

SS

Ndipo Samsoni na baba yake na mama: yake wakatelemkia Timna wakakafika mashamba ya mizabibu huko Timna; na tazama, mwanasimba aka- mngurumia

Roho ya BWANA ikamjilia kwa nguvu, naye akampasua kana kwamba anampasua mwana-mbuzi wala hakuwa na kitu cho chote mkononi mwake; lakini hakuwaambia baba yake na mama yake aliyoyafanya (Waamuzi 14:5-6).

Mf 102

SS

Naye akaona mfupa mbichi wa taya ya punda, akautwaa, akapiga watu elfu kwa mfupa huo. Samsoni akasema, Kwa taya ya punda chungu juu ya chungu, Kwa taya ya punda nimepiga watu elfu

(Waamuzi 15:15-16)

Mf 117

(16) Wewe wanichukia tu, wala hunipendi, wewe umewategea kitendawili hao wana wa watu wangu, nawe hukuniambia mimi. (17) Naye akalia mbele yake hizo siku saba wakati ulioendelea karamu yao, basi ikawa siku ya saba akamwambia, kwa sababu alikuwa akimsisitiza sana; naye akawaambia wale wana wa watu hicho kitendawili (Waamuzi 114:16-17).

Mf 118

SS

5. Tafadhali uniambie asili za nguvu zako nyingi (Waamuzi 16:6)

6. Tazama umenidhihaki na kuniambia uongo; sasa tafadhali, niambie, waweza kufungwa kwa kitu gani? (Waamuzi 16:10)

7. Hata sasa umenidhihaki, umeniambia maneno ya uongo; niambie sasa tafadhali, niambie, waweza kufungwa kwa kitu gani? (Waamuzi 16:13)

8. Wavezaje kusema nakupenda, na moyo wako hauko pamoja nami? Umenidhihaki mara hizi tatu, wala hukuniambia asili ya nguvu zako nyingi (Waamuzi 16:15).

Mf 134

SS

Samsoni akaenda, akakamata mbweha mia tatu, kisha akatwaa vienge vya moto akawafunga mbweha mkia kwa mkia kienge ya kila mikia mwili....akawaachia mbweha kati ya ngano ya Wafilisti (Waamuzi 15:4-5).

Mf 135

SS

Wafilisti wakamkamata, wakamng'oa macho, wakatelemka naye mpaka Gaza, wakamfunga kwa vifungo vya shaba, naye alikuwa akisaga ngano katika gereza (Waamuzi 16:21).

Mf 136

SS

Samsoni akamwita Bwana, akasema,
Ee Bwana Mungu, unikumbuke, nakuomba,
Ukanitie nguvu, nakuomba, mara hii tu,
Ee Mungu, ili nipate kujilipiza kisasi

Mf 137

SS

Samsoni akasema; na nife pamoja na hawa Wafilisti. Akainama kwa nguvu zake zote, ile nyumba ikawaangukia hao wakuu, na watu wote waliokuwa ndani yake. Basi wale watu aliowaua wakati wa kufa kwake walikuwa wengi kuliko wale aliowaua wakati wa uhai wake (Waamuzi 16:30).